

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Arobaini – Tarehe 4 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 38, Waziri Mkuu anaweza kuulizwa maswali na Mbunge yeote ambaye atazingatia masharti kuhusu maswali ya Bunge pamoja na mwongozo uliowekwa na Nyongeza ya 6 ya Kanuni hii. Maswali atakayoulizwa Waziri Mkuu, hayatakuwa na taarifa ya awali kama maswali yenye. Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu kitakuwa ni Siku ya Alhamisi kwa dakika 30, lakini chini ya kifungu kidogo cha (4) kinasema, Waziri Mkuu anaweza kutumia kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, kutoa taarifa au ufanuzi kuhusu suala lolote linalohusiana na shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma, kwa muda usiozidi dakika kumi ikifuatiwa na maswali kwa Wabunge kwa dakika 20 kuhusu taarifa yoyote na maswali mengine ya Serikali. Kwa hiyo, ninamuita Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa taarifa fupi kwa mujibu wa Kanuni uliyoleza sasa hivi. Taarifa hiyo ni matokeo ya mjadala wa Bajeti ya Uchukuzi, ambayo ilikuwa na mambo mengi. Nimeona nitumie fursa hii niweze kutoa ufanuzi wa mambo yafuatayo:-

Awali ya yote, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Uchukuzi na Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia kwa maandishi na kwa kuzungumza kwenye majadiliano ya Wizara hii ya Uchukuzi yanayoendelea hapa Bungeni. Michango yenu kwa kweli ni mizuri, ninawashukuruni sana kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimeona nitoe maelezo haya, kwa sababu yaliyojitokeza ni mambo ambayo yameonesha uzito na sisi Serikalini tukaona pengine ni vizuri katika kujaribu kusaidia Bunge lako katika kuendeleza mjadala huu, tuyaweke bayana mambo fulani fulani.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninataka kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mheshimiwa Rais aliamua kuunda Wizara mbili kutokana na uzito wa majukumu yaliyokuwa katika Wizara hiyo moja na hii ilitokana kwa sehemu kubwa na mazingatio ya maoni yallyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ndani ya Bunge hili kwa nyakati tofauti.

Kwa hiyo, uamuzi huo ulilenga kupunguza majukumu mengi yaliyokuwa yamebeebwa na Wizara ya Miundombinu kabla ya kutenganishwa na kupata Wizara mbili ikiwemo hii ya Uchukuzi. Lengo la kuundwa kwa Wizara ni kuimarisha utekelezaji wa Miradi ya Sekta ya Uchukuzi ikiwemo ya

usafiri, reli, anga, maji pamoja na barabara kwa upande sasa wa Wizara ya Ujenzi na kabla ya kutenganishwa wote mtakumbukwa vipaumbele vilivyowekwa zaidi kwenye ujenzi wa barabara na madaraja. Kwa hiyo, wakati tukiendelea na majadiliano ya Wizara ya Uchukuzi, ninaomba niruhusu nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuitisha makadirio ya Wizara ya Ujenzi, kwa sababu yamewezesha ujenzi wa barabara na madaraja kuendelea kwa kuzingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uchukuzi inahitaji uwekezaji wa mitaji mikubwa kwenye ujenzi wa reli, bandari na hata viwanja vya ndege. Vilevile uwekezaji kama huo unahitajika kwenye ununuzi na ukarabati wa ndege, injini za treni na mabehewa yake pamoja na mahitaji ya meli. Mahitaji hayo ni makubwa na ambayo Bajeti iliyotengwa haitoshelezi. Wizara hii kama ilivyo kwa Wizara zingine, inakabiliwa na ufinyu wa Bajeti. Hata hivyo, Serikali imekuwa siku zote inafanya kila jitihada kuhakikisha Wizara zinapata fedha za kutosheleza mahitaji. Kutokana na ufinyu wa Bajeti wa Wizara hii, jana, Serikali ililazimika kukutana na kuangalia uwezekano wa kuongeza bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kutokana na vyanzo mbalimbali. Kukutana kwa Serikali ilikuwa ni muhimu ili kuweza kujadili michango mingi mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge hili Tukufu, kwa mtazamo ambaa unawenza ukaimarisha mijadala na kwa maana hiyo maslahi kwa Watanzania. (*Makof*)

Kwa hiyo, baada ya Kamati ya Miundombinu kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kuishauri Serikali kuongeza bajeti hiyo kwa shilingi bilioni 95, jambo ambalo tuliliridhia na kulikubali, lakini hatukuweza kufikia kiwango hicho kama ilivyokuwa imeombwa. Kikao cha jana kimewezesha Serikali kufanikiwa kupata fedha hizo ambazo zitatumika kwenye maeneo matatu yafuatayo: Reli ya Kati, Kampuni ya Ndege Tanzania na Usafiri wa Majini yaani Meli katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kiasi hicho cha shilingi bilioni 95 ni kiasi ambacho Wizara ilikuwa imeji-commit au imejiahidi mbele ya Kamati kwamba, zikipatikana zitawezesha huduma za msingi katika maeneo hayo matatu kuweza kuendelea bila matatizo makubwa. (*Makof*)

Serikali inaanmini kabisa kwamba, pamoja na nyongeza hiyo, bado bajeti hiyo haikidhi mahitaji yote yallyopo kwa sasa. Hata hivyo, kwa kuzingatia kwamba, bajeti hii ni ya kwanza kwa Wizara tangu ilipoundwa Novemba, 2010 baada ya Uchaguzi Mkuu na kwa kuwa Sekta hii imepewa kipaumbele katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano, Serikali itahakikisha bajeti zijazo zinaipa Sekta hii kipaumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilioongelewa kwa hisia kali na Waheshimiwa Wabunge, wakati wa mjadala ni matatizo ya Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA). Serikali imesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge, na kwa sasa imeshawaagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai na Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa, kuanza uchunguzi mara moja ili kuiwezesha Kamati ya Bunge ya Mheshimiwa Peter Serukamba, iweze kutekeleza jukumu lake ipasavyo katika uchunguzi utakaofuatia. Ninataka kiliarifu Bunge lako kuwa, Serikali itatoa kila aina ya ushirikiano kwa Kamati hii kuhakikisha kwamba, jambo hili linashughulikiwa ipasavyo. (*Makof*)

Baada ya uchunguzi huo, Serikali itachukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu, kwa wote watakaobainika kuhusika kulihujumu shirika hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pia wamezungumzia suala linalohusu malipo ya pensheni kwa Wastaafu wa TAZARA kwa upande wa Tanzania, wanaodai kiasi cha shilingi bilioni 22. Suala hili liliamuliwa na Baraza la Mawaziri la TAZARA linalijumuisha Mawaziri husika kutoka nchi hizi mbili kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upande wa Tanzania na mwenye dhamana kama hiyo kwa upande wa Zambia, wafanye uhakiki wa madai haya kwa pande zote mbili. Wadhibiti hao wamewasilisha taarifa zao Serikalini kwa ajili ya kushughulikiwa. Kwa upande wa Tanzania na tayari Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandalila na utajadiliwa hivi karibuni na hatua stahiki zitachukuliwa.

Kwa hiyo, nilitaka nitumie nafasi hii kuwahakikishia Wafanyakazi wa TAZARA na Watanzania kwa ujumla kwamba, punde uamuzi huo wa Baraza utakapofanyika, hatua zote

zinazohusiana na malipo ya pensheni au mafao kwa wastaa fu hao zitachukuliwa bila kuchelewa. (*Makofî*)

Serikali imefanya kila linalowezekana ili kupata kiasi cha fedha kilichokuwa kimeombwa na Kamati ya Miundombinu pamoja na Serikali kukubali katika hali ngumu sana ya fedha tulionayo kama ilivyojitokeza kwenye majadiliano ya Bajeti ya Serikali katika Wizara mbalimbali zilizotangulia. Ninataka niwahakikisheni kuwa, Serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha Wizara zote zinapata Bajeti ya kutosheleza mahitaji yake. Tukumbuke kuwa mapato yetu bado ni madogo, tutaendelea kufanya kila liwezekanalo kuongeza mapato ya Serikali ili kuondokana na tatizo hili. Vilevile ninazitaka Wizara zote zitumie fedha walizotengewa kwa bajeti zao kwa malengo yaliyokusudiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa namna fedha hizi zitakavyowekwa katika bajeti, utatokana na ushauri nitakaokuwa nimepewa na ninadhani utawasilishwa katika nyakati tofauti hapa Bungeni, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba imekuwa *factored* katika Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ufanuzi wa masuala mengine yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge, utaendelea kutolewa na Waziri mwénye sektu pamoja na Naibu na Mawaziri wengine wanaohusika ili kuweza kuhitimisha hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa muda uliobaki sasa nipo tayari kuendelea kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kama ulivyoelekeza. Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofî*)

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Kama kawaida yetu, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani yupo; Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kumwuliza Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza Waziri Mkuu, kwa kauli yake ya awali aliyoitoa hapa leo, kufuatia mjadala wa jana wa Bunge, ninapenda sasa kumwuliza swali moja la msingi ambalo linagusa maslahi ya Watanzania walio wengi sana kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni zaidi ya mwezi mmoja tangu Waziri wa Fedha aliposoma Bajeti katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bajeti ambayo iliwapa Watanzania wengi matumaini ya kushusha bei ya mafuta ya *petrol* na *diesel*, lakini vile vile ilikusidia kupandisha bei ya mafuta ya taa; na kwa kuwa zimetolewa kauli mbalimbali zikiwemo kauli za *EWURA*, kauli za Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi, kauli ya Wizara ya Nishati na Madini na jana hatimaye *EWURA* waliweza kutoa bei elekezi ili itekelezwe na wafanyabiashara wanaofanya biashara ya mafuta; na kwa kuwa jana katika Jiji la Dar es Salaam, Jiji la Mwanza, Jiji la Mbeya, Jiji la Arusha na sehemu nyingine kadha wa kadha wafanyabiashara wa mafuta wamegomea agizo la *EWURA*; je, Waziri Mkuu unatupa kauli gani ya Serikali kuhusiana na sakata hili na ni nini hasa mnakusudia kifanywe na ni amri ipi sasa tuichukue na kama utakubali amri yako sasa iwe ndiyo amri rasmi ya Serikali kuhusu utekelezaji?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mbewe, maswali yake mengi mengi kwa pamoja kama ifuatavyo:-

SPIKA: Jibu tu mafuta tu na kauli ya Serikali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, tunacho chombo ambacho ndiyo kimepewa jukumu la kusimamia masuala ya udhibiti wa mafuta, yaani *EWURA*, kinaongozwa na sheria, kinaongozwa na taratibu. Kwa hiyo, tangazo lilitolewa jana ni kwa kuzingatia sheria iliyotungwa na Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni kweli na mimi nilipata hizo taarifa, lakini sisi tusingeliweza kuingilia kati maamuzi ambayo yalikuwa yamefanywa na chombo halali. Tulichowashauri ni kwamba, nendeni mkakae na wadau wote na jana wamekutana na leo wanakutana ili hatimaye

waweze kukubaliana ni namna gani wanawenza kumaliza mgogoro uliojitokeza. Kwa hiyo, hadi hapo nitakapopata taarifa ya mwisho sisi tutasubiri.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Waziri Mkuu, kwa majibu yake. Hoja ya msingi inabaki kwamba, EWURA wamekuwa na zaidi ya mwezi mmoja kushughulikia bei ya mafuta na kauli ya Serikali ilitolewa Bungeni. EWURA ni chombo ambacho kipo chini ya Serikali. Bajeti ya Serikali ilisomwa katika Bunge hilli mwezi Juni mapema kabisa; ni zaidi ya mwezi na nusu sasa, Taifa linakabiliwa na sintofahamu halisi ya mafuta. Leo Waziri Mkuu anatuambia ni chombo cha kisheria, lakini tunajua hakipo juu ya sheria kwa misingi ya kuwa juu ya Serikali.

Kwa maana hiyo, Waziri Mkuu atakiri kwamba kumekuwa kuna uzembe katika ku-manage tatizo zima la mafuta hadi sasa hivi kwani ni muda mrefu na bado kumeendelea kuwa na usumbufu na sintofahamu kubwa? (*Makof*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria, hayupo; hata Serikali tunalazimika kufuata sheria. Kwa hiyo, siwezi kufanya jambo ambalo ni kinyume cha sheria. Mmeitunga hapa, mnawajibika kufuata sheria ile kama mlivyoitunga. Sasa ni kweli kwamba, kauli ilitoka hapa Bungeni kuititia Waziri wa Fedha, lakini isingweza kutekelezwa mpaka ule Muswada wa *Finance Bill* uwe umekamilishwa na Rais ameweeka saini yake. Kwa hiyo, hiyo imechukua muda baada ya ile *Finance Act* kupatikana, utekelezaji kwa mujibu wa sheria hiyo ukafuata. Baada ya hapo ndiyo hatua hizi sasa ambazo unaziona zimefuatia katika utekelezaji wa yale tuliyokuwa tumeyasema. Asingweza kufanya vinginevyo kabla ya *Finance Act* kupatikana. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimemvumilia Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa sababu ya umuhimu wa swali lenyewe, lakini wengine mtauliza maswali mafupi.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa dhana ya Kilimo Kwanza itawezekana tu kutekelezwa hapa nchini kama Wananchi watapewa motisha katika mazao yao kwa maana ya kupata bei nzuri ya mazao wanayoyalima; na kwa kuwa katika hali isiyokuwa ya kawaida hivi majuzi Serikali iliamua kushusha bei elekezi kutoka shilingi 1,100 mpaka shilingi 800, bei ambayo ni ya kutupa, bei ambayo haimpi maslahi mkulima; na kwa kuwa sasa Serikali imesema kwamba inaingia kwenye utafiti wa kujua uhalali wa bei anayotakiwa kulipwa mkulima lakini wakati huo huo imeshashusha bei ya pamba; kwa nini Serikali isishikilie msimamo wake wa kusema kwamba bei ni shilingi ni 1,100 mpaka pale utafiti utakapokuwa umekamilika? (*Makof*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninaona hili suala limehama limekuwa ni la Serikali kwamba, sisi ndiyo tulipanga bei, sisi ndiyo tumeteremsha bei. Jambo hili siyo kweli, wadau wa pamba ndiyo mliokaa Mwanza na kwa vigezo vilivyokuwepo wakati huo, vilitokana na bei ya soko ya pamba, mkakubaliana kwamba bei hiyo sasa itakuwa shilingi 1,100. Mimi nilijaribu kulifuatilia sana hili kutaka kujua nani walikuwemo humo, nikaambiya vilikuwemo vyombo vyote pamoja na Chama cha Wakulima, ambao ndiyo wadau wakubwa.

Bei iliyopangwa ilitokana na mjadala uliojitokeza pale Mwanza. Baada ya pale kilichosemwa sasa ni kauli tu iliyotoka katika kuthibitisha mlichokuwa mmekubaliana. Sasa mwezi mmoja baadaye, bei ya pamba imeshuka na mkalazimika kwamba, kutokana na mazingira yaliyokuwepo, isingweza kuuzwa pamba zaidi ya shilingi 800. Sasa hili hamuwezi kusema ni letu, ni jambo tu la soko la dunia ndiyo limetufikisha pale, ndiyo maana sisi Serikalini tumeesema *okay, fine* tutakachowea kujitahidi ni kuangalia angalau bei isiendelee kushuka zaidi. Sisi tumeunda Kamati Ndogo, tujaribu kuona tunafanyaje ili *ku-protect* angalau hiyo bei isiendelee kushuka. Sasa nini kitafanyika baada ya pale; imani yangu ni kwamba, wadau hao hao mtarudi mkakae tena pale Mwanza, mlizungumze; tutakachokuwa tumefanikiwa kukipata, tutaki-filter katika hiyo bei mpya, kwa lengo la kuwezesha shughuli hiyo iweze kuendelea.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Kwa kuwa kauli ilitolewa na Waziri mwenye dhamana ya Kilimo humu humu Bungeni, kwa hiyo, moja kwa moja ilikuwa ni kauli ya Serikali. Sasa kwa kuwa nchi yoyote ile lazima ilinde wakulima wake; na kwa kuwa nchi zingine zinatumia utaratibu wa kuwapa *insurance* wanunuzi wake; Serikali inasema nini kama kweli tatizo la bei ya pamba ni la kidunia kama linavyotajwa ingawa bei imeshushwa bila utafiti?

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba hawa wakulima wa pamba kama kweli wanapata hasara na kuwa bei ya pamba imekuwa ikipanda mara kwa mara na sisi tunavyozungumza nina uhakika kwamba ikifika mwezi wa kumi bei ya pamba itapanda; Serikali itakubali kuwapa *insurance* hao wanunuzi ili waendelee kununua kwa bei ya shilingi 1,100 na kwa kuwa na wao wako tayari?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, bei ya pamba mwaka jana niliambiwa ilifikia shilingi 600 kwa kilo moja. Safari hii ndiyo mlipandisha mkafikisha 1,100. Serikali ilichofanya ni kusema yale tuliyokubaliana, *okay!* Sasa hoja ni kwamba, kwa nini Serikali isiwe na utaratibu wa *insurance*, sawa. Mimi ninachowenza kusema hapa ni kwamba, jamani tukubaliane tu kwamba mazao haya ambayo soko lake linatawaliwa na Soko la Dunia ni eneo ambalo linahitaji tukae tuliangalie tunafanyaje. Haiwezi kuwa kwa pamba peke yake, tunayo korosho, tunayo chai, tunayo kahawa na tumbaku; haya yote hatuna udhibiti wa bei zake. Mimi hoja yangu ya msingi ni kwamba, Serikali katika mipango yake ya miaka mitano, tujitahidi kuimarisha ujenzi wa viwanda vinavyotumia rasilimali hii hapa nchini kama namna nyngine ya kuwashakikisha kwamba mazao ya wakulima yatanunuliwa. Sasa hilo shauri la Mheshimiwa Mpina, siwezi kusema kwamba, nitalifanya sasa hivi, haiwezekani. Kwa hiyo, tutahitaji tukae chini tuliangalie tuone tutafanya nini kwa mazao yote na wala siyo pamba tu, mazao yote kwa ujumla.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Ninakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuliona jina langu. Ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja. Hivi karibuni Benki Kuu ya Tanzania imechapisha noti mpya na zikaanza kutumika na katika kutumika kwake tumegundua kuna pesa nyngi bandia zimekuwa zikitumika na kuleta usumbufu kwa Wananchi lakini noti hizi zimeonekana kuchoka haraka sana na Wananchi wanapozirudisha benki hasa Benki ya *NMB* zinakataliwa; nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili?

WAZIRI MKUU: Ninafikiri nijibu la mwisho basi. Ni kweli kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya Watanzania kwamba, noti hizi zinachakaa mapema na mimi nillipata. Tulichofanya na sisi tulimpelekea Gavana wa Benki Kuu, Profesa Ndulu na yeze akasema ameshapata taarifa kuhusu tatizo hili. Akaniambia, itabidi walifanyie uchunguzi kwa sababu wao wanaamini noti zile zina ubora unaotakiwa. Kwa hiyo, kama yapo matatizo hayo ndiyo alisema ngoja alifanyie kazi kwanza aone linatokana na nini; ni noti zipi ambazo zinaonekana kuwa na hilo tatizo, pengine kunaweza kupatikana majibu ambayo ni ya uhakika zaidi.

SPIKA: Ahsante. Ninaomba muwe na maswali mafupi kidogo, kwa sababu muda wenye ni mfupi.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hivi Wananchi tena wale wa pembezoni wadogo wadogo ndiyo wanaohangaika, wakienda kule wanaambiwa pesa hizi *NMB* hawawezi kupokea, wao wazipeleke Benki Kuu; Mheshimiwa Waziri Mkuu hawa Wananchi watahangaika bure na tungeliomba kauli ya Serikali itoke mapema kusudi watu hawa wasipate shida, kwa sababu pesa hizi tunapokwenda *kwenye ATM* ...

SPIKA: Umeeleweka.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, jambo hili tulishalifikisha Benki Kuu, acha walifanyie kazi. Tutaomba na hilo unalolisema walizingatie, watoe maelekezo ya nini kifanyike, lakini kama ni uchakavu wa noti hata noti hizi tulizokuwa tunazitumia kabla ya sasa nazo pia ziliwu zinachakaa. Mimi nimewahi kupewa nyngi tu nipeleke Benki Kuu kwa sababu zimekataliwa kwenye Mabenki. Kwa hiyo, kuna uchakavu lakini uchakavu unaouzungumza wewe ni kwa sababu inaonekana kama limechukua muda mfupi ndiyo maana mimi nikawa *concerned*, nikalipeleka kwa Gavana wa Benki Kuu.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Ahsante Mheshimiwa Spika. Katika Bunge la Tisa wakati wa m dororo wa uchumi, Kambi ya Upinzani ilipendekeza iundwe sheria ya kusimamia *Stimulus Package* ambayo iligharimu takriban shilingi triliioni 1.7. Moja ya sababu ya kupendekeza au pendekezo hilo ni hofu ya matumizi au usalama wa fedha hiyo wakati wa mchakato wa kutumika.

Katika Bunge la Kumi, Mkutano wa Tatoo, Mheshimiwa Waziri Mkuu uliulizwa swali na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto kuhusu Taarifa ya CAG ambapo ilikuwa ikihusu kiasi cha takriban shilingi bilioni 48 ambazo CAG alishindwa kupata maelezo yake ingawa taarifa hiyo ilikuwa ya muda...

SPIKA: Usituhutubie, Mheshimiwa Kafulila, usituhutubie tafadhalii.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Kidogo kidogo. (*Kicheko*)

SPIKA: Haya malizia.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Majibu hayakuweza kupatikana. Kikao ambacho kinaendelea sasa Mheshimiwa Leticia Nyerere, amejibiwa swali la msingi na Wizara ya Fedha ambapo alitaka kujuu ni makampuni gani na ni watu gani ambaa mpaka sasa imeshindikana kufahamika hata kwa CAG kuhusu fedha hizo takriban shilingi bilioni 48.

SPIKA: Wewe unataka kuuliza nini?

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Swali sasa. Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni kwa mwesenendo huu Serikali yako inadhihirisha hofu ya Wapinzani katika Bunge la Tisa ya kwamba fedha hizi huenda zimetumika vibaya na pengine ni uhusiano wa Serikali na baadhi ya hayo makampuni?

SPIKA: Swali lenyewe ni zuri lakini limenyooshwa.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, labda nimjibu tu Mheshimiwa Kafulila kwamba, basi vizuri ndugu yangu sisi tumesikia, tutajitahidi kufanya hayo unayopendekeza. Kwa sababu mimi ninavyoamini, jambo ulilifanya kwa nia njema, makampuni yanajulikana. Tutakachofanya ni kuleta tu taarifa hapa, kutoa kauli kueleza kilichotokea ni nini na makampuni gani yanahuksika ili kama kuna haja ya kuendeleza mjadala juu ya jambo hilo, liweze kufanyika.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nami ninapenda nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu uliwhi kuulizwa hapa Bungeni juu ya suala la kuwepo katika nchi yetu watu wenye uraia wa nchi mbili na ulimwagiza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na mwuliza swali wakafanye uchunguzi juu ya jambo hili. Lakini mpaka sasa imekuwa kimya.

Je, huoni kuwa ukimya huu utawapa fursa watu hawa ambaa wapo kinyume cha sheria kuja kuchangia katika mambo mengi muhimu ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya Katiba Mpya, kitu ambacho itakuwa siyo haki yao?

WAZIRI MKUU: Sina hakika, ninadhani anazungumzia suala la uraia wa sura mbili.

SPIKA: Mwanzo ule haukuelewka, ulisema watu walifanyaje?

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Uliulizwa swali hapa kuwepo kwa raia ndani ya nchi yetu, ambaa wana uraia wa nchi mbili hivi sasa na ukaagiza uchunguzi ufanywe. Ulimwagiza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ashirikiane na aliyeaalikuwa swali, ambaye alikuwa Mheshimiwa Mohamed Habibu Mnyaa. Wamefanya hiyo kazi, lakini mpaka sasa ni kimya.

Mheshimiwa Spika, je, huoni ukimya huu unaendelea kuwapa fursa watu hawa ambaa wapo kinyume cha sheria, kwa sababu huwezi kukaa katika nchi yetu uwe una uraia wa nchi mbili wakati hajipitishwa sheria hiyo na wanashiriki katika shughuli muhimu na watakuja kushiriki hata kutoa mapendekezo ya Katiba, kitu ambacho siyo haki yao?

SPIKA: Sasa tumekuelewa.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ninadhani Waziri wa Mambo ya Ndani amesikia jambo hili. Tutamsisitizia akamilishe hilo zoezi ili tuweze kubaini ni akina nani na hatua stahiki zichukuliwe.

SPIKA: Kwanza kabisa, ninaomba tukushukuru kwa majibu. Leo tumefanikiwa kuwa na watu wane, lakini tume-cover vyama vyote. Kwa hiyo, tunakushukuru sana na kwa taarifa uliyotutolea. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu kwa hatua inayofuata.

MASWALI YA KAWAIDA

Na. 368

Tatizo Sugu la Maji Mji Mdogo wa Mikumi

MHE. ABDULSALAAM S. AMER aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kumaliza tatizo sugu la maji Mji Mdogo wa Mikumi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Abdulsalaam Seleman Amer, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Mikumi upo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na unakadiria kuwa na watu wapataao 9,600. Ni kweli kuwa, Mji huu una tatizo kubwa la maji, ambapo hivi sasa huduma ya maji inasambazwa na Kamati ya Maji Mikumi, ambayo huduma yake ni ya kususua na Viongozi wa Kampuni hii wanaendesha Mradi wa Maji kinyume na taratibu na kusababisha mgogoro uliodumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kutohana na tatizo la muda mrefu la upatikanaji wa maji katika Mji Mdogo wa Mikumi, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, inatekeleza mradi wa kuchimba visima vya maji. Mtaalam Mshauri anaendelea kufanya usanifu wa miundombinu ya maji katika viji kumi vilivyochanguliwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, ukiwemo Mji Mdogo wa Mikumi. Katika bajeti ya mwaka 2011/2012, zimetengwa shilingi milioni 116.4 na kati ya hizo, shilingi milioni kumi zimetengwa kwa ajili ya Mji Mdogo wa Mikumi. Vijiji vingine ni Dumila, Lumango, Kiegea, Maguha, Msowero, Iwemba, Tunda, Kifinga, Zombo, Lubo, Chakwale na Kidedya

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ukikamilika utamaliza tatizo sugu la maji katika Mji Mdogo wa Mikumi.

MHE. ABDULSALAAM S. AMER: Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Katika sheria ya mji mdogo, tumeambiwa tuunde Bodi za Maji za Mji Midogo. Bodi imeundwa majina ambayo yapo kwenye Wizara yake, lakini mpaka leo majina hayajaidhinishwa. Je, lini au siku gani itakuwa majina haya yaweze kuidhinishwa ili nirudishe kwa wananchi wa Jimbo la Mikumi waweze kuunda Bodi yao ya Maji?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkoo, ni kweli Wananchi wa Mikumi kupitia Mkoo wao wa Mkoaa, wameleta mapendekezo kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, ambaye ni Waziri Mkoo aweze kuteua Bodi ya Maji katika Mji Midogo ikiwepo na Mji wa Mikumi.

Ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa jinsi alivyokuwa anaafuilia na ninafurahi kumjulisha kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkoo, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, tayari ameteua Bodi ya Maji ya Mikumi. Majina yameshapatikana yako Ofisini kwangu. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Bodi iliyoteuliwa ili kuweza kuboresha upatikanaji wa maji katika Mji wa Mikumi. (*Makofi*)

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Ninashuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuuliza swalii dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mkoaa wa Tabora unafanana kwa uhaba wa

maji kama Wilaya ya Mikumi. Je, Serikali ina mpango gani wa ahadi yake iliyotuhidi itatupa maji kutoka Ziwa Victoria yatakayopitia Nzega, Igunga, Tabora Manispaa, Urambo na Sikonge? Ahadi hii ilikuwa ya Mheshimiwa Rais ; je, Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani sasa kuanza kuitekeleza ahadi hiyo?

SPIKA: Mnajua Waheshiwa Wabunge, tumewavumilia sana kuuliza maswali tofauti kabisa na ya msingi. Sasa hapo ukijibowi nusu usilalamike. Bahati nzuri Naibu Waziri yupo. Msilizie maswali yanakwenda mbali kabisa na lile la msingi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, ninaona upo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kwanza, tumeshatoa ahadi kwamba, Serikali imeshaamua kupeleka maji Tabora kutoka Ziwa Victoria na sasa hivi kinachoendelea ni msanifu kuweza kupima na kuainisha njia ambayo itatumika ili maji hayo yaweze kupelekwa Tabora. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge, asiwe na wasi wasi, Serikali ikiahidi ina maana ni lazima itatekeleza. Sisi tutasimamia kuhakikisha kwamba, maji yanapatikana kutoka Ziwa Victoria.

Na. 369

Sekta ya Madini Kusaidiana na Sekta ya Kilimo Kuinua Uchumi Nchini

MHE. FATUMA A. MIKIDADI aliuliza:-

Kilimo pekee kama njia kuu ya uchumi kimeshindwa kukidhi mahitaji ya nchi na ongezeko la watu nchini :-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanua wigo wa uchumi kwa kutupia macho katika Sekta ya Madini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kilimo hakiwezi kuachiwa kama njia kuu ya uchumi na ni kweli kwamba, sekta zingine zinapaswa kuchangia, ikiwemo Sekta ya Madini. Serikali kwa kutambua hili, kwa upande wa madini, mwaka 1997 ilipitisha Sera ya Taifa ya Madini ili madini hayo yaweze kutoa mchango wake katika uchumi na Pato la Taifa. Sera hiyo imeleta mafanikio ya kiuchumi na kijamii, ikiwemo mchango kwenye Pato la Taifa kutoka asilimia 1.4 mwaka 1997 hadi asilimia 2.5 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na changamoto nyingi katika Sekta ya Madini zikiwemo, kiwango kidogo cha fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nyingine za uchumi, mchango mdogo katika Pato la Taifa, kasi ndogo ya uendelezaji uchimbaji mdogo; kiwango kidogo cha uongezaji thamani na uharibifu wa mazingira, Serikali ilipitisha Sera hiyo upya kwa lengo la kuihuisha ambapo mwaka 2009 ilipitisha Sera mpya ya Madini. Pamoja na malengo mengine, Sera hiyo inalenga kuimarisha fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nyingine za uchumi, kuboresha mazingira ya kiuchumi kuvutia uwekezaji; kuboresha mfumo wa sheria; kuimarisha uwezo wa Serikali katika kusimamia Sekta ya Madini, kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuhamasisha uongezaji thamani madini nchini. Malengo yote haya yanalenga kupanua wigo wa uchumi wa nchi kupitia Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria Mpya ya Madini 2010 na Sera ya 2009, umelenga wawekezaji wakubwa na wadogo. Utaratibu wa majadiliano unaendelea na wawekezaji walioingia mikataba kabla ya sheria hii ili na wao wafanye kazi zao, chini ya mfumo mpya wa Sheria ya Madini ya 2010. Aidha, ushiriki wa STAMICO katika miradi yote mikubwa ya madini, chini ya sheria mpya, umehimizwa kwa lengo la kusimamia maslahi ya Taifa. Kwa upande wa

uchimbaji mdogo, matarajio ni kuhimiza taratibu za kurasimisha ili uchimbaji huo uweze kufikiwa na mikopo ya taasisi za fedha, pamoja na kuboresha taalamu za teknolojia ya uchimbaji.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kutohana na uhaba wa mvua, zana duni za kilimo, uhaba wa pembejeo na ongezeko la watu, kilimo pekee kwa kweli hakikidhi haja. Ninashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kwamba; njia zenyewe za uchumi toka madini zinaendelezwa. Sasa hivi tunayo madini mengi nchini Tanzania, lakini kasi ya uchimbaji na upembezi wa madini hayo ni hafifu sana. Utaona kwamba...

SPIKA: Mheshimiwa, swali la nyongeza tu.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Je, Serikali sasa hivi ina mkakati gani wa kuongeza kasi ya uchimbaji na upembuzi wa madini nchini Tanzania ?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ninadhani amesema kasi ya utafiti, maana yake *exploration* ili kujua katika eneo la Tanzania tuna madini gani. Kazi hii inaendelea, inafanywa na Wakala wa Jiolojia wa Tanzania. Kama unavyo jua nchi yetu ni kubwa sana, kwa hiyo, baadhi ya maeneo ambayo yametengwa Wakala wa Jioloji, kazi hiyo inafanyika sasa hivi. Kimsingi ni kuboresha tu kwa kazi ambayo ilishafanywa zaidi ya miaka 50, 60 iliyopita na kuleta ile *assessment* ya *exploration* kwa mfumo wa kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yapo maeneo ambayo kazi hii imeanza na tunatarajia kwamba, hatuwezi tukamaliza nchi nzima kwa haraka lakini kwa maeneo mengine inafanywa na Wakala wa Jiolojia na kwa maeneo mengine inafanywa na wale ambao wanachukua leseni halafu wanaamua kufanya kazi za *exploration* na *prospecting* kwa kiwango cha miaka mitatu, minne, nao wanapata kubaini ni kiwango gani cha madini kilichopo katika maeneo wanayoombea leseni.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wizara imeonesha maeneo mbalimbali Tanzania na aina za madini ambayo yapo. Madhumuni makubwa ya kufanya hivyo ni kuwawezesha Watanzania waweze kumiliki rasilimali hizi. Kwa kuwa Watanzania hawa hawana utaalamu na hawana fedha za kujua hasa au za kuweza kufanya *exploration*, matokeo yake ni kwamba, wageni wanapokuja wanafanya *exploration* na Watanzania wanauza maeneo haya waliyopewa kwa bei ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haiwezi sasa kuwawezesha Watanzania kufanya hii *exploration* ili wajue thamani ya mali iliyopo kabla hawajauza mali waliyonayo ili waondokane na umaskini walionao?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye swali la msingi, suala la uchimbaji na suala la *exploration*, ndiyo funguo ya kujua tuna hazina gani, wapi na kwa kiwango gani. Sasa kulingana na kiwango kile cha uchimbaji unaokusudiwa kufanywa, kwa mfano, kwenye uchimbaji mkubwa wa migodi mikubwa, *exploration* huwa ni kazi ambayo inaendelea labda hata kwa miaka mitano, sita, kama ilivyo sasa hivi kule Ruangwa, kuna mgodi unaitwa Nambiranji, wamekuwa wanafanya *exploration* kwa muda wa kama miaka minne, mitano, lakini *exploration* hiyo ni kazi ya gharama kubwa, mpaka sasa hivi ninadhani wanakwenda kwenye dola milioni sita au saba.

Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tutengeneze utaratibu kwenye yale maeneo ambayo tunaweza tukabaini kwa uhakika kwamba, hapa pana *prospects* kubwa za madini kwa kiwango kikubwa. Serikali tumeshakusidia kufanya *exploration* kwa kuelekeza Wakala wa Jiolojia ili maeneo hayo kwanza yamilikiwe na STAMICO. Halafu STAMICO sasa kwa niaba ya Watanzania wote, iingie ubia na uendelezaji, kwa maana hiyo watakuwa na hisa na *free carried interest* na kadhalika, lakini kwa maeneo ambayo ni uchimbaji mdogomdogo, hilo linaweza likawa

gumu, kwa sababu *exploration* yenyewe inaweza ikawa gharama kubwa kuliko hata uchimbaji wenyewe.

Na. 370

Ujenzi wa Barabara ya Kisarawe – Maneromango na ile ya Mlandizi – Vikumburu

MHE. SELEMANI S. JAFO aliuliza:-

Barabara ya Kisarawe – Maneromango na ile ya Mlandizi – Vikumburu zimeainishwa kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM kutengenezwa:-

Je, ni lini ujenzi wa Barabara hizo utaanza rasmi ili Wananchi wa Wilaya ya Kisarawe wawewe kunufaika nazo kiuchumi kwa uwekezaji wa viwanda, kilimo na utalii kwenye Hifadhi ya Selous?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza llani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 kwa kujenga Barabara ya Kisarawe – Maneromango (km 54) kwa kiwango cha lami kwa awamu. Hadi kufikia 2010, kilomita 12.5 zimejengwa kwa kiwango cha lami katika Pugu na Mpuyani. Serikali itaendelea kutekeleza ahadi hiyo kwa kujenga barabara hiyo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika Barabara ya Mlandi – Vikumburu, Serikali ina mpango wa kujenga barabara kutoka Makofia – Mlandizi – Maneromango hadi Vikumburu, kwa kiwango cha lami kama ilivyoainishwa katika llani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010. Barabara hii imepangwa kuanza kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa juzi tu tumepitisha Bajeti ya Wizara ya Ujenzi; na kwa kuwa hivi sasa majibu yameonesha dhahiri kwamba barabara hii itajengwa kwa awamu; ni nini *commitment* ya Serikali kwamba kazi hiyo itaanza lini kwa ujenzi wa Kisarawe katika suala zima la awamu?

(ii) Kwa vile usoefu unaonesha kwamba wakandarasi wengi wanapokwenda kujenga ujenzi hata vibarua wanawachukua kutoka maeneo mengine. Je, Wizara inatamka nini juu ya wale Makandarasi ambao wanakwenda kufanya kazi za ujenzi wa barabara lakini wanawachukua vibarua kutoka maeneo mengine?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mhesihmiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Kwa Barabara ya Kisarawe – Maneromango, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, azma ya Serikali ni kumalizia zile kilometra 41.5 za changarawe zilizobaki kwa lami. Tumeanza kuifanyia upembuzi yakinifu kutoka Mpuyani hadi Maneromango na tumetenga pesa kwa ajili ya kazi hiyo ambayo imebakia kidogo, shilingi milioni 63.7 na baadaye itabidi tuanze kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna kipande cha Mlandizi hadi Maneromango na Maneromango hadi Vikumbulu; hizo tunesema tunaanza upembuzi yakinifu mwaka ujao wa fedha, lakini kwa sasa tumetenga pesa za matengenezo tu. Tumetenga pesa ya kutosha kabisa, shilingi milioni 319 na vilevile tuna kilometra mbili, hasa kati ya Maneromango na Mlandizi,

tumetenga shilingi milioni 47. Vilevile Maneromango – Vikumbulu, tumetenga pesa ya kutosha tu ya ukarabati wa hizo barabara.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba vibarua kwenye kampuni za ujenzi wanachukuliwa maeneo mengine. Serikali haiwezi kutoa kauli kwenye kazi ya kampuni binafsi, ambayo imepewa kazi ya ujenzi. Mimi ningeomba tu vijana wa maeneo hayo, wachangamkie tenda. Tusubiri sisi kutoa kauli kama Serikali ili wao wapewe kazi hata pale ambapo hawana *interest* na hizo kazi.

Na. 371

Huduma za Benki Katoro

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA aliuliza:-

Mji wa Katoro una wakazi zaidi ya 40,000 ambao wengi wao ni wafanyabiashara wanaohitaji huduma za kibenki ili wafanye kazi zao kwa tija bila hofu ya ujambazi ambao kwa sasa hulazimika kusafiri zaidi ya kilometra 45 mpaka Geita kufuata huduma hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha benki inafunguliwa Mji wa Katoro ili kuondoa usumbufu kwa Wananchi hao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango na inatambua umuhimu wa kuhakikisha benki zinafunguliwa ili kusogeza huduma za kibenki karibu na Wananchi hususan katika kuwezesha jamii husika kuwa na fursa ya kupata huduma za kibenki, ikiwemo kuwekeza amana (*deposits*) na pia kupata mikopo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi, biashara, kilimo pamoja na kuepuka kutembea mwendo mrefu kufuata huduma za kibenki.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo, Serikali imeweka Sera mbalimbali kama vile Sera ya Taifa inayolenga kuwafikia na kuwahudumia wateja wadogo wadogo (*National Micro-Finance Policy*), inayosimamiwa na Benki Kuu.

Serikali kupitia Benki Kuu, imetoa vigezo nafuu vyta uanzishwaji wa Benki za Wananchi (*Community Banks*) katika Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (*Licensing Authority*) za Mwaka 2008. Katika Kanuni hizo, Benki Kuu imeweka kiwango cha chini cha mtaji kwa ajili ya uanzishwaji wa Benki za Wananchi na Taasisi mbalimbali za kifedha, ambazo hutegemea kwa kiasi kikubwa hamasa na uwezo wa Wananchi katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ni jukumu la Viongozi wa Kisiasa na Kijamii pamoja na Taasisi mbalimbali, kuhamasisha Wananchi katika maeneo yao kuanzisha Benki za Wananchi (*Community Banks*), ikiwa ni mkakati wa kusogeza na kupeleka huduma za kibenki karibu na Wananchi hususan katika maeneo ambayo hayajafikiwa likiwemo eneo la Mji Mdogo wa Katoro.

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa jibu alilonipa Naibu Waziri, lakini ni kweli Serikali imeweka Sera muhimu, Kanuni pamoja na vigezo vyta kuanzisha Benki hizi; kigezo kimojawapo ni mtaji na mtaji huo bila ya kuwa na milioni 250, huwezi ukaanzisha Benki hizi za Wananchi. Kigezo hiki, kwa kweli ninakiona ni kikwazo kikubwa sana.

(i) Je, Serikali ipo tayari kuangalia uwezekano wa kupunguza kigezo hiki kutoka milioni 250 kwenda milioni 50 ili kuwawezesha Wananchi hawa kuweza kuanzisha benki hizi kwa urahisi? (*Makofii*)

(ii) Katika Jimbo la Busanda hasa Makao Makuu ya Jimbo ambapo ni Katoro, kuna uhitaji mkubwa sana wa huduma za kibenki. Ninauliza kwamba; je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuzishawishi benki zilizoko katika Wilaya ya Geita Mjini kuweza kufungua Matawi pia katika Mji wa Katoro ili kuwawezesha Wananchi hawa kuweza kupata huduma hizi kwa kipindi hiki ambacho hatujaanzisha Benki za Wananchi? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa mtaji wa kiasi cha shilingi milioni 250 ni mkubwa kwa Wananchi wenyewe kipato kidogo wa vijiji. Pia Serikali inatambua kuwa, Benki za Wananchi zina mchango mkubwa sana kwa Wananchi wa Viji vyeye kipato kidogo. Kwa kuzingatia ombi au pendeleko la Mheshimiwa Mbunge, Serikali itakaa pamoja na Benki Kuu, na kuangalia upya viwango vya fedha ambavyo vinapelekwa kwenye Serikali.

Hata hivyo, Serikali inashauri Wananchi wasio na uwezo, kuanzisha asasi za kifedha zitoazo huduma za kifedha kwa wateja wadogo wadogo kama vile *SACCOS, VICOBA* ili kuweza kusogea karibu zaidi huduma za kibenki zinazozingatia mazingira ya mahali husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kufuataia mageuzi ya Sekta ya Kifedha yaliyoanza mwaka 1991, Serikali ilijitoa katika uendeshaji wa shughuli za kibenki moja kwa moja na kuziachia benki zenyewe. Hata hivyo, Serikali inatambua umuhimu wa kuimarisha uchumi wa maeneo yote ya nchi ili kuweka mazingira yatakayovutia mabenki kuanzisha huduma za kibenki maeneo mbalimbali. Kwa mfano, Benki yetu ya *NMB Ltd*, imeweza kuanzisha matawi 139 katika nchi nzima; hii ni sawasawa na asilimia 80 ya Wilaya zote hapa nchini.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo lillikuwepo katika eneo la Busanda linawiana kabisa na tatizo ambalo linawakabili Wananchi wa eneo la Kilwa Kaskazini hasa eneo la Somanga na Kipatimo. Je, Serikali ipo tayari kukaa na Benki Kuu kubadilisha utaratibu uliopo sasa kutumia vyombo vya usafiri wa kusafirishia pesa kutoka maeneo ya benki na kupeleka katika maeneo ya vituo hivyo ili ATM ziweze kufunguliwa na zipunguze tatizo la mrundikano wa watu kwenda katika maeneo ya mbali kupata huduma?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, ninafikiri unafaa na sisi kama Serikali tutazingatia mapendeleko aliyyoyatoa.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa vile Wilaya ya Mbarali ina benki moja tu na Wilaya ile ni pana sana na hivyo kufanya Wananchi wapate tabu sana kupata huduma hiyo ya kibenki. Je, Serikali ipo tayari sasa kuanzisha benki nyingine Mji wa Chimala au Madibira?

SPIKA: Swalii lako jipya kabisa! Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu.

Msiulize maswali kwa sababu ya kuuliza tu! Sasa huyu hana habari kama litakuwa jibu namna hiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu. Msiahidi vitu ambavyo hamjavifanyia utafiti.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba njibuu swalii la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba, kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge kwamba na yeze anapenda Tawi la Benki lifunguliwe katika eneo lake ni swalii jipya lakini ninashauri kwamba, tungeonana halafu tuangalie. Kufuatana na majibu ambayo nimeyatoa

hana, tutaangalia uwezekano wa sehemu yake na yeye kupatiwa benki kwa utaratibu ambao nimeuleza hapa.

Na. 372

Kasoro za Usambazaji wa Walimu Mashulenii

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA aliuliza:-

Ripoti ya Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya MKUKUTA kwa kipindi cha miaka mitano inaonesha kuwa kulikuwa na kasoro za usambazaji wa walimu. Kwamba, mikoa tajiri ilikuwa na walimu wengi tofauti na mikoa masikini. Shule zilizo pembezoni pia zilikuwa na upungufu wa walimu ziklinganishwa na zile za mjini na kadhalika:-

- (a) Kasoro hizo zilisababishwa na nini?
- (b) Je, Serikali imejipanga vipi kuondoa kasoro hizo katika Awamu ya Pili ya MKUKUTA?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), hupanga walimu kulingana na idadi ya walimu wanaohitimu na kufaulu mafunzo katika ngazi mbalimbali, kwa kuzingatia mahitaji ya walimu kishule na kihalmashauri. Pamoja na utaratibu uliopo, bado kuna tofauti ya ikama ya walimu katika mikoa na kati ya shule za mjini na zile za pembezoni.

Tofauti iliyopo katika ikama ya walimu katika mikoa na shule haitokani na kasoro katika upangaji na usambazaji wa walimu. Sababu zinazochangia uwepo wa tofauti ya ikama ya walimu katika Mikoa, Halmashauri na Shule ni pamoja na:-

- (i) Mazingira magumu katika baadhi ya Mikoa, Halmashauri au Shule ilipo. Hii husababisha walimu kutoripoti au kuondoka mara baada ya kuripoti.
- (ii) Imani za kishirikina katika baadhi ya maeneo huwafanya walimu waondoke au wasiripoti.
- (iii) Uhamisho wa walimu hasa wale kike baada ya kuolewa na matatizo ya kifamilia au matatizo ya kiafya.

(b) Mheshimiwa Spika, ninaomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa, katika Awamu ya Pili ya MKUKUTA, Wizara yangu kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI, imeweka mikakati ya kupunguza tofauti ya ikama ya walimu hasa katika mazingira magumu kwa kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ili yaweze kuwavutia walimu kufanya kazi katika maeneo wanayopangiwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu na miundombinu.
- (ii) Kutoa posho maalum kwa walimu wanaopangwa katika maeneo yenye mazingira magumu.
- (iii) Kushirikiana na wadau wa maendeleo ya elimu katika kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

(iv) Kuongeza udahili wa wanafunzi wanaochukua programu za ualimu katika vyuo, vyuo vikuu vishiriki vya Serikali na vya binafsi.

Mheshimiwa Spika, ninatoa wito kwa wadau wote wa elimu, kushirikiana ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ili kupunguza tatizo la upungufu wa walimu lililopo katika mikoa, shule za mijini na vijijini. Pia, ninapenda kuwaagiza Maafisa Elimu wote wa Mikoa na Wilaya na Halmashauri zao husika na Wakurugenzi, kushirikiana kuwapanga walimu kulingana na mahitaji ya shule hususan shule za vijijini.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa katika jibu la msingi Naibu Waziri amekiri kwamba, kuna tofauti ya ikama ya walimu na kutoa sababu mbalimbali; lakini kwa usoefu nilionao kama mwalimu, imeonekana kwamba kuna baadhi ya Maafisa Elimu ambao siyo waaminifu, hutumia nafasi zao na kupanga walimu kwa manufaa yao binafsi; mfano ukabila, urafiki na undugu. Je, Naibu Waziri, atanihakikishajie kwamba, suala hili litafanyiwa uchunguzi na kukomeshwa, hususan katika Mkoa wa Singida?

(ii) Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna upungufu mkubwa wa walimu na inahitajika kupata walimu; je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kuwaajiri walimu ambao wako mitaani ambao Serikali iliwapa fursa ya kurudia mitihani yao na ambao wanakadirisha kuwa zaidi ya 2000 ili kuweza kupunguza tatizo hili la walimu hususan vijijini?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ikama ya walimu, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba, kazi ya Wizara au kazi ya Serikali Makao Makuu ni kupanga walimu na kuwasambaza kwenye Halmashauri husika. Kwa hiyo, Maafisa Elimu wa Sekondari na Maafisa Elimu wa Shule za Msingi wa Wilaya kwa Shule za Msingi na Sekondari, ndiyo wenyewe jukumu la kuwasambaza walimu kwenye shule huko mijini na vijijini kadiri ya upungufu wanaouona wao na ikama ilivyo. Sasa basi kama kuna Halmashauri ambazo zina upungufu wa walimu, tunaomba Wabunge pamoja na Maafisa Elimu wa Mikoa, tushirikiane, tukae pamoja na DEOs, tuweze kuwapanga walimu kutokana na ikama ilivyo. Taarifa zilizopo pale Wizarani ni kwamba, kila mwaka huwa tunapanga walimu kwenye Halmashauri. Sasa ni kazi ni ya DEOs kuwapeleka kule vijijini kutokana na sehemu husika. Anachosema Mheshimiwa Christowaja pale kwamba, baadhi ya Halmashauri unakuta vijijini kuna walimu wawili hata mmoja, lakini pale mjini Halmashauri ya Wilaya unakuta kuna walimu zaidi ya 30 kwenye shule; kwa kweli huu ni upungufu wa DEOs wenywewe.

Mheshimiwa Spika, ninataka kusema kwamba, wiki iliyopita mimi nilikuwa Morogoro kufungua kikao cha semina ya kazi ya REOs wote Tanzania na DEOs wote na niliagiza kwamba sasa watafute mfumo maalum wa kusambaza walimu vizuri, bila kufuata upendeleo, ukabila na hata udini, namna wanavyopanga. Mara nitakapogundua hilo, hata Waheshimiwa Wabunge nisaidieni, mkiona kuna DEO ambaye anapanga walimu kwa upendeleo, nipeni taarifa mapema nitachukua hatua za kisheria. (*Makof*)

Kuhusu swalii lingine la ajira kwa walimu ambao wako mitaani; hii lugha niseme tu kwamba hawajaajiriwa ni kweli kwamba, mwaka jana baada ya matokeo ya ualimu kutoka, kuna walimu ambao walipata *supplementary walifeli*, tukaagiza Baraza la Mitihani, tarehe 4 Aprili, walirudia mitihani zaidi ya walimu 2000 na sasa wamefanya, kwa hiyo, wapo kwenye orodha ya kuajiriwa pamoja na hawa wengine ambao tutawaajiri kwenye mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, Mheshimiwa uwe na amani tu kwamba, wataajiriwa wote. (*Makof*)

SPIKA: Swalii la nyongeza Mheshimiwa Mkosamali. Samahani Mheshimiwa Mkosamali, namwita Waziri wa TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kwanza, ningependa nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, kwa majibu yake mazuri. Pia nitoe ufanuzi juu ya upangaji wa walimu katika vituo mbalimbali na nini tunaweza kufanya kuhakikisha kwamba, hakuna upendeleo wala unyanyasaji wa aina yoyote katika kuwapangia walimu vituo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kueleza kwamba, katika Halmashauri zetu zote, tunayo Kamati ya Elimu, Afya na Maji, ambayo inasimamia masuala ya elimu pale Wilayani. Sisi Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani katika maeneo yetu. Ningependa kutoa wito tu kwamba, kwa kutumia Kamati yetu ya Elimu, Afya na Maji, pale ndipo mahali pa kuhoji utendaji wetu wa Idara ya Elimu na pale ndipo mahali pa kufanya marekebisho. Kwa sababu nchi yetu hii leo ina Halmashauri 133, zitazaliwa nyingine 30 hivi karibuni, tukisema kwamba TAMISEMI au Wizara ya Elimu tuwe tunafanya marekebisho katika Halmashauri hizo, tutafanya lakini itachukua muda mrefu katika mzunguko.

Kwa hiyo, ningemwomba sana Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum na Waheshimiwa Madiwani wote, tushirikiane na Madiwani wenzetu kuhakikisha kwamba, matatizo kama haya katika Halmashauri yetu hayatokei.

SPIKA: Kwa kuwa nilimwita Mheshimiwa Mkosamali, sina namna itabidi nimwite tu tena.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Nilitaka kuuliza tu kwa kifupi kwamba; kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ni moja ya Halmashauri zilizoko pembezoni mwa nchi; na walimu walioripoti toka mwezi wa kwanza hawajalipwa stahiki zao ikiwa ni pamoja na pesa za mizigo mpaka leo; je, Serikali haioni kwamba inataka walimu hawa wakimbie Wilayani Kibondo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kibondo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo linajitokeza hapa kuhusu hawa walimu ambao wanasma kwamba, hawajalipwa kama mwali mu alikwenda moja kwa moja kwenye Halmashauri aliyopangiwa, hiki kinachozungumzwa hapa hakitokei. Kama amepangwa kwenda Magu, akaondoka akaenda Kibondo au akaenda Siha, maana yake ni kwamba, sasa ataanza kwenda mlolongo mwingine tena mpya; hilo ni moja.

Sasa kwa vile Mheshimiwa Mbunge ana taarifa zaidi kuliko sisi hapa, sisi tunakuomba utupatio majina ya hao walimu ambao wamekwenda pale, tutakushughulikia sasa hivi ili tuweze kujua ni nini kilichotokea. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha, maswali pia yamekwisha, kwa hiyo, ninao wageni. Kwanza kabisa, nina mgeni maarufu sana ambaye ni mke wake mpendwa Mheshimiwa Eng. Rashid Mfutakamba, Naibu Waziri wa Uchukuzi, anaitwa Remmy Mziray Mfutakamba. Amekuja kushuhudia anavyosulubiwa mume wake hapa, siku akimwambia kule nyumbani nilikuwa na matatizo aweze kuelewa vizuri. (*Makofii*)

Wageni wengine ni wanafunzi ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo; kuna wanafunzi 65 na walimu kumi kutoka Shule ya Msingi ya Mazoezi Kigurunyembe kutoka Morogoro, wakiongozwa na Mwalimu Ayubu Fifi; Wanafunzi wa Kigurunyembe na walimu wasimame. Ahsante sana, karibuni sana na ninadhani mtapata elimu mliyokuwa mmeikusudia. (*Makofii*)

Kuna wanafunzi kumi kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri Dodoma; hawa wako wapi? Ninadhani watakuwa kwenye *basement* nafasi imekosekana.

Kuna wanachama 35 wa *club* ya wapinga rushwa inayofadhiliwa na TAKUKURU kutoka Shule ya Sekondari ya Central wakiongozwa na walimu wao. Sijawahi kusikia; wako wapi hao? Ninafikiri nao wamekosa nafasi, pengine mchana watapata nafasi maana hawa wanapinga rushwa kwa hiyo ni jambo zuri.

Wanafunzi 23 kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Johans Kilombero, Morogoro. Hawa wako wapi? Ninafikiri nao wamekosa nafasi wanaweza kuingia mchana.

Tuna wanafunzi 20 wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Mkoo wa Arusha, wapo kwa ajili ya kutembelea Bunge; hawa nao wako wapi? Ninafikiri pia nafasi haikutosha.

Tuna wanafunzi 30 wa Chuo Kikuu cha St. John's Dodoma, hawa majirani zetu mnakaribishwa wakati wote mnaweza kuwa karibu na sisi hapa. Ahsante sana, someni kwa bidii na mijenge hoja kumaliza matatizo yenu siyo vinginevyo. (*Makofii*)

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mohmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana, watakuwa na kikao katika Ukumbi wa *Basement*.

Leo pia tuna furaha na kuwapongeza wafuatao kwa siku ya kuzaliwa kwao; kwanza kabisa kuanzia Rais Obama wa Marekani, yupo hapa Mheshimiwa Eng. Stella naye kazaliwa leo, yupo Dkt. Kafumo wa Nishati na Madini pia amezaliwa leo. Kwa hiyo, ninawatachia heri na maisha mengine marefu mara mbili ya hayo mliyonayo sasa. Tunaendelea.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kuhusu mwongozo wako kwa jambo lillotokea mapema na 68(8) kuhusu taarifa kwa mjadala unaoendelea toka jana; kwa mujibu wa taarifa nzuri sana aliyotoa Mheshimiwa Waziri Mkuu leo asubuhi, ningependa kupata Mwongozo wako kwa maana vilevile ya kutoa taarifa; kwanza, *ni-declare interest* kwamba, mimi pia ni Mbunge wa Dar es Salaam na Diwani katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. (*Makofii*)

Pili, *ni-declare interest* kwamba, Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Dkt. Didas Massaburi ni ndugu yangu.

SPIKA: Mwongozo kuhusu nini sasa maana usinihutubie tena, unataka tufanye nini tuache kujadili au tufanye nini?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Nitoe taarifa kwa mjadala unaoendelea.

SPIKA: Kwamba nini sasa? Ninaomba muwe *brief*, kwa sababu tukijadili tena inakuwa haifai, unataka kusema nini.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Kwa sababu mjadala huu unaendelea, nilitaka kutoa taarifa kwa mjadala unaoendelea baada ya maelezo ya Waziri Mkuu na hasa kuhusu suala la Meya wa Jiji la Dar es Salaam.

SPIKA: Amefanya nini; kwamba tuache kujadili au vipi?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Hapana tuendelee kujadili lakini tukizingatia hiyo taarifa na ukweli ambaeo nilitaka kuutoa.

SPIKA: Mjadala ni mawazo ya Mbunge mmoja katika kujadili mjadala huu. Sasa siwezi kuzuia Wabunge ambaeo wako kwenye orodha yangu kwa sababu yoyote ile. Taarifa ya Waziri Mkuu, haimaanishi kwamba, msijadili; siyo maana yake hiyo ni kwamba, amewaongezea uelewa wa mambo yanayoendelea lakini siyo kwamba wasiendelee kujadili. Mheshimiwa Salim.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: Nimemaliza Mheshimiwa Waziri.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kuhusu kifungu cha 38 cha Kanuni. Wiki mbili zilizopita, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, aliomba mwongozo kuhusu utaratibu mzima wa kuuliza maswali kwa Waziri Mkuu na ukaahidi kwamba, utafuatilia na utatoa maelekezo. Nikwambie kwamba, Wabunge wako wanapata shida sana sasa hivi hasa katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, wanaamka mapema wanawahi kujiorodhesha, lakini hatimaye utakuta wale wallowahi siyo wanaopata fursa ya kuuliza; ninaomba mwongozo wako.

SPIKA: Sawa, tumesema kabisa utaratibu huu una matatizo kwa sababu nyingi tu, lakini tumesema tutaiangalia pamoja na wakati tutakapoangalia Kanuni siyo sasa hivi. Kama leo hii nimemwacha Mheshimiwa Regia, kwa sababu ye ye tayari ameongea mara tatu, nimemwacha Mheshimiwa Hamad Rashid, kwa sababu amepata nafasi mara moja, nimeamua kuchukua chama kimoja kimoja na ninafikiri nimefanya vizuri, kwa hiyo, tunaendelea. Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, mwongozo.

SPIKA: Aaah! Tumemaliza mwongozo sasa hatuwezi kuongozana mpaka mwisho. Katibu tuendelee.

HOJA YA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012
Wizara ya Uchukuzi (Reli, Bandari na Usafiri wa Majini)**

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tutajadili leo mpaka saa saba na robo. Waliochangia mara moja ni Mheshimiwa Donald Max, atafuatiwa na Mheshimiwa Shaffin Sumar; tuenze haya Mheshimiwa Max.

MHE. DONALD K. MAX: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniona. Awali ya yote, ninaomba niseme kwamba, hatukuja hapa kumhukumu Mheshimiwa Nundu, Waziri wa Uchukuzi, lakini ni machungu ambayo tunayo katika kulijenga Taifa hili.

Ninaomba nisirudie masuala au michango iliyotolewa na wenzangu Mheshimiwa Tizeba, Mheshimiwa Rage, Mheshimiwa Mama Hewa, Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Mbewe, wote mawazo yetu yaikuwa hayo na michango hiyo ndiyo nilitaka kuitoa jana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze Waziri Mkuu, kwa sababu hicho ndicho tulikuwa tukitifuta, Watanzania tunaumia na maumivu yetu ninafikiri leo Waziri Mkuu ametujibu hapa na mimi nilikuwa na imani kwamba Serikali yetu pesa ipo. Sasa kwa sababu pesa hiyo imepatikana, tunachotaka kumshauri Waziri wa Uchukuzi, tunaomba tubadiliike.

Tatizo kubwa linalotukabiri katika haya mashirika yetu ni ubadirifu na uaminifu kuwa mdogo, wachakachuaji wamo humo humo Wizarani na usimamizi ni mbovu. Sasa ninaomba nimshauri Mheshimiwa Waziri kuwa, mimi ninafikiri viro vitu vingine hata sisi tunaweza kusaidia. Humu ndani ya jengo letu hili, wataalam unao wengi wanatosha, watu wenye uelewa wapo na watu waliofanya kazi kwenye mashirika hayo wamo humu ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba tuweke utaratibu ywa kuwa tunaleta taarifa, kwa sababu tunapoidhinisha hizi pesa baadaye zinatusulubu sisi na wanaoumia wapo asilimia 70, humu ndani hata theluthi hatufiki. Kwa hiyo, ninaomba na sisi vilevile tuwe tunatafutwa tutoe ushauri wa bure, huhitaji kutulipa pesa, wewe tuombe ushauri. Kwa sababu haiwezekani, ukiniambia tumepeewa au zimekuja *engine* 79, leo zinafanya kazi *engine* 37, *engineers* wapo na wengine ni sisi hapa;

tumeendesha makampuni makubwa, sijawahi mimi kusimamisha gari hata mwaka mmoja, iweje wewe na *engine* 79 uniambie kwamba nusu yake zimesimama? Kama *engineers* wako hawafai watoke. (*Makofi*)

Hizi ajira zenu ningeomba Wizara hasa kwenye upande wa Serikali huku, *system* ya ajira kidogo ibadiliike; usimweke mtu akawa suga pale miaka 20 ni yule yule, kwa sababu watu wapo na Watanzania kwa uadilifu tunazidi hata nchi za jirani. Kwa hiyo, ningeliomba kila inapofika hata miezi mitatu hivi, tuwe tunapeana taarifa tumetoka wapi na tunakwenda wapi ili kwenye mawazo tusaidiane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara hii kwa sababu ilitokea kwenye Wizara ya Ujenzi, msifanye kazi peke yenu, ubinagsi upungue, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ni kitu kimoja. Katika kukabiliana na yale majukumu, Mheshimiwa Rais, aliliona hili akaona azigawe ziwe Wizara mbili kupunguza majukumu ya Waziri. Sasa mkileta ubinagsi, inatusumbua sisi.

Jimboni kwangu kule Geita, nimeshakwenda *TANROADS* mara mbili, gati linajengwa na Wizara ya Ujenzi, anayeshughulika na meli ni Wizara ya Uchukuzi, sasa utakuta kila mtu yuko kivyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikienda Wizara ya Ujenzi, lazima nijiamini kwamba na Uchukuzi salamu zangu wamezipata, Uchukuzi na Ujenzi ni kitu kimoja, kwa sababu hapa tunazungumzia Reli, Bandari, Anga, Barabara yote ni kitu kile kile. Kwa hiyo, ningewaomba sana Wizara yako na Wizara ya Ujenzi, kiwe kitu kimoja, kurushiana mpira haitatusaidia, kwa sababu hapa tunajaribu kurekebisha janga tulilonalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nisirudie wenzangu waliyoyasema, wote tuna machungu yale yale na wote jana tulitaka kupiga kelele, bahati mbaya muda ukatuishia, mimi sikuchangia jana na leo ni siku ya mwisho nimeona nitoe ushauri. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ninaomba uhame hiyo mashine; Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Waziri Mkuu kwa aliyoaongea leo, amenifanya hata sina la kuchangia. Lakini mimi nitasema machahe kidogo kwa sababu toka mwanzo nimekuja hapa kuwaunga mkono wenzangu wote waliochangia kuhusu matatizo ambayo yametukuta. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu leo amenikata miguu, Mungu ambariki, maana leo na mimi nisingejali, ningesema yale ambayo yangekuwepo kichwani mwangu.

Mheshimiwa Spika, nimefurahia sana kwa jinsi Serikali ilivyoamua kuongeza bajeti. Lakini nasikitika sana kwamba bajeti hii imeongezwa lakini Bandari ya Tanga imeachwa pembeni. Kuna Mjumbe mwenzangu jana aliongea kwamba katika Mikoa ambayo inatakiwa tuiangalie, ni Mikoa wa Tabora, watu wengi wameanzia pale. Ndege ya kwanza ilianza kutua pale. Nami napenda kuwaeleza wananchi au Watanzania wenzangu kwamba viongozi wengi wamesoma katika Shule za Sekondari za Tanga, kwa nini Mji wa Tanga unasahaulika?

Nimesema hivyo kwa sababu tumeona katika vipaumbele wamesema kwamba watajenga reli ya kutoka Tanga kuititia Arusha kwenda Musoma. Sasa reli hii itakamilika vipi kama hakutakuwa na Bandari Tanga? Katika Mikoa wa Tanga huu huu ndiyo Mikoa ambao wafanyabiashara wengi walikuwa wanategemea ili mizigo yao itoke upande wa Tanga kwenda Mpaka Afrika Mashariki, yaani Kenya na Uganda wote wangepitia katika Bandari ya Tanga. Lakini cha kushangaza kwenye bajeti hii Tanga haikutamkwa. Sasa Tanga unatoka Ndugu yangu Waziri, wewe mwenyewe umejisahau kwako, unashabikia sehemu nydingine. Kwa mfano, Dar es Salaam kunajengwa gati mbili, yaani Na. 1 na Na. 7 ili kupanua meli nydingi zije. Kwa nini tunang'ang'ania tu Bandari ya Dar es Salaam wakati kuna Bandari nydingine kama ya Mtwara na Tanga? Kwa nini hizi gati ambazo zinatakiwa zipelekwe tu Dar es Salaam zisiletwe Tanga? Kwani Tanga kunani? Yaani, tunataka tuige nyimbo za wasanii? Maana wasanii wamesema, "Tanga kunani"? Kwa hiyo, hata Bungeni hivyo! Inashangaza sana. (*Kicheko*)

Kwa kweli wala sikutarajia Wizara nyeti kama hii mnatoa bajeti inayolingana na watafiti wa Waganga wa Jadi. Kwa kweli Serikali iliangalie hili. Bajeti imetoa vipaumbele saba, lakini kati ya vipaumbele hivyo, Tanga imesahaulika. Kwa nini isahaule? Kwani hakuna wananchi? Ndiyo Miji mikongwe. Katika Miji, Tanzania ambayo ilikuwa na viwanda vikubwa ilikuwa ni Tanga na Dar es Salaam, lakini leo hii Tanga ndiyo inakuwa mji wa mwisho? Kwa hili ningesema sana leo, lakini kwa sababu wenzangu wallionitangulia wamesema, agenda ni hiyo hiyo, siwezi kuongeza ufundi katika hili ila tu kuna mengine ambayo yamejitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika makubaliano, Waziri alikuja mpaka Korogwe akasema kwamba Korogwe kutakuwa na Bandari ya nchi kavu, lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sioni Korogwe kwamba hii bandari ya nchi kavu itajengwaje na iko wapi na imepangiwa vipi. Sasa naomba na hili vilevile nipate maelekezo kwamba ile bandari ya nchi kavu ya Korogwe itatengenezwa namna gani? Kwa sababu ikitengenezwa bandari ya nchi kavu ya Korogwe ina maana Mikoa ya Kaskazini yote na nchi jirani tutakuwa wanahifadhi mizigo yao pale.

Leo hii kumetolewa vipaumbele vyta meli, meli zimetajwa kwa maziwa yote, lakini sijaona meli hapa inayotoka Tanga kwenda Pemba na kupitia Zanzibar kwani huku hakuna wananchi? Naomba Waziri aangalie na hili kwa sababu kila siku wanaopinduka na majahazi ni Tanga na Bagamoyo, kwani Tanga mmetuweka katika mafungu gani? Tunaomba sana kama mmeamua kugawa meli na mmasema mnatengeneza meli na kadhalika, wananchi wa Tanga nao wamechoka kufa na maji. Naomba mtuandalie na sisi tupate meli moja ambayo itakuwa inakwenda Pemba, Mombasa mpaka Zanzibar ili na wananchi wawe katika hali ya usalama. Kila siku tutapanda majahazi mpaka lini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mmezungumzia masuala ya viwanja vyta ndege. Nasikitika sana viwanja vingi vyta ndege mmeamua kwamba safari hii vinatengenezwa, lakini sijaona hapa uzio wa kiwanja cha ndege cha Tanga, kwani kile kiko nje ya Tanzania? Kama kipo, kwa nini na chenyewe kisitengenezewa uzio? Kwa sababu mji wa Tanga unakua, watu wanaamua tu kujijengea na kama wanajijengea hawaangalii hapa ni kiwanja cha ndege wala nini. Kama kweli mnataka kuviendeleza viwanja, basi kiendelezeni na kiwanja cha Tanga. Viwanja vidogo vidogo mmevisahau kabisa.

Kuna kiwanja Mombo ambacho viongozi wote Wakuu wa Nchi wanashuka pale, lakini hapa sioni. Kwani mnataka kuniambia viongozi wakija pale wapate vumbi? Kiwanja cha Same hapa sikioni, kwani hakuna watalii? Kuna Mbuga ya Wanyama ya Mkomazi watu wanashuka pale, lakini mnaviangalia viwanja ambavyo watu wanakwenda kuchimba madini tu, mwangalie na viwanja ambavyo watu wanakwenda kwenye utalii. Kuna milima ya Usambara kule watu wanakuja wanashuka, wanakwenda milimani lakini viwanja hivi hamtaki kuvitengeneza, mnatarajia nani akavitengeneze? (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu umenikata makali sana leo, maana leo ilikuwa niseme kiasi ambacho leo hata Mheshimiwa Spika labda ungeniambia nikae chini. Lakini inauma, kwani haya mambo yanayofanya ya reli, reli zilizokuwa hapa ni Reli ya Kati na Reli ya Tanga. Lakini nashangaa watu wanaweka vipaumbele kwa vitu ambavyo haviendani na matatizo ya wananchi.

Sehemu ya Reli ya Tanga ni sehemu ambayo ingesababisha hata hiyo barabara inayojengwa na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ingedumu. Lakini leo hii Reli ya Tanga kama hajafanya kazi, hiyo barabara itakayotengenezwa kwa shilingi triliuni moja itafanya kazi gani? Hakuna haja kwa sababu lengo la kutengeneza barabara ni kwamba barabara ziwe nzuri na lengo la kutengeneza reli ni kwamba reli iwe inabeba mizigo mizito, kwani kuna viwanda pale, kuna kiwanda cha Saruji, kuna Machungwa mengi, kuna matunda kutoka Lushoto watayapeleka wapi kama barabara yenye ndiyo hiyo na reli yenye ndiyo hiyo? Sasa hivi eneo la Mombo limekufa. Nimewahi kuomba hapa kwamba ile eneo la Mombo ambalo limekufa, basi watu wakasafishe, lakini sasa hivi limekuwa ni chaka la nyoka. Sasa tutakuwa tunafanya kazi ya kuwalinda wananchi au kuchunga nyoka?

Mheshimiwa Spika, lakini Waziri kama kweli wamekupa pesa ndogo, basi usisahau kwako Tanga, ukumbuke kwamba kule una wapigakura na ukumbuke kwamba kule ulikotoka wananchi wanakutegemea sana. Wewe umekaa nje ya nchi kwa sababu ya kulinda hadhi ya Tanzania ndio maana ukawa Rais wa Marubani wote duniani. Lakini sasa nashangaa sana.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa upande wa *UDA* nashukuru sana, umesema makubwa sana, la kama kitu kimeshaundiwa Tume na hii Tume ina watu makini, mimi nakubaliana na wewe. Sisi katika maisha yetu tulikuwa tunakaa sana Dar es Salaam tukiwa tunategemea sana *UDA*. Lakini kwa sababu Waziri Mkuu ameshaliongea na sisi tumeona kwamba ni la maana, mimi leo sioni haja nikisema kwamba siungi mkono hoja, mimi ninachodai ni kwamba nakubaliana kabisa na maneno waliyoongea wenzangu, lakini nataka nikuhakikishie kwamba mimi naunga hoja hii mkono kwa maneno ya Waziri Mkuu, lakini kama yatakuwa tofauti nitaondoa shilingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari kavu, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja mpaka Korogwe akaenda mpaka *Old Korogwe* akaangalia eneo la kukaa Bandari Kavu, mbona hapa kwenye kitabu chake hakuna? Nimesoma hapa, lakini mbona sioni? Kwani hii Bandari Kavu inataka kwenda wapi? Nimeona Bandari Kavu ya Shinyanga akitofautisha sehemu ya Bandari Kavu na mahali ambapo reli ya kwenda Rwanda ipo ni tofauti. Lakini pale reli iko karibu, Bandari Kavu ipo karibu, lakini kwenye kitabu chake hakuweka. Sasa unataka upeleke wapi? Wale wananchi ambaosisi tuliwaambia kule kwamba safari hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi inajenga Bandari Kavu, unataka tukawaambie nini?

Mheshimiwa Spika, sipendi kuongea sana, maana wenzangu walionitangulia wameongea makubwa sana, lakini nilitaka tu niikumbushe Serikali kwamba mimi sitatoa shilingi na ninaunga mkono hoja hii kwani nimeridhika na maneno aliyosema Waziri Mkuu. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Pudensiana Kikwembe.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika hii hoja.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli siko mbali sana na Waheshimiwa Wabunge kwani na mimi kwa moyo wangu nilikuwa na lengo la kupinga hoja hii. Lakini kutohana na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa sababu ninaiamini Serikali kwamba itatekeleza, sina tatizo na Wizara hii. Kwa niaba ya wananchi wa Mpanda na Katavi kwa ujumla pamoja na Rukwa ninawaeleza kwamba tupo hapa kuwawakilisha vyema kabisa japokuwa jana kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema kwamba anamsemea Waziri Mkuu. Waziri Mkuu ni Mbunge na ninafikiria anatimiza wajibu wake vizuri kabisa kwa wananchi wake Jimboni kwake na Mkoa wa Rukwa Katavi ,tupo Wabunge tunaoweza kuwawakilisha wananchi wetu vyema kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niendelee kwa kuongelea suala la hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 22 namba 37 kuna mkataba wa makubaliano baina ya Serikali ya Tanzania na Uganda kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya Tanga, Arusha, Musoma na Bandari za Mwambani, Musoma na Kampala kwamba ulisainiwa tarehe 29 Juni. Ninachofahamu kwa nchi ya Uganda Entebbe, ndio, kuna port. Sasa labda Serikali inataka kutuambia kwamba inataka kujenga upya kituo pale Kampala? Kama kulikuwa na hayo mazungumzo, yanaendeleaje? Wamefikia hatua gani? Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa aweze kulieleza hilo na kulitolea ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, pia katika ukurasa wa 43 namba 78 katika mpango wa muda mfupi wa uboreshaji wa huduma za reli za kati mwezi Mei, Wizara yake ilifanya mazungumzo na Benki ya Dunia kwa lengo la kupatiwa fedha za dharura za kutelekeza mpango wa kutelekeza huduma za reli. Mpango huu utajumuisha ukarabati wa miundombinu ya reli, ununuzi wa vichwa, treni na mabehewa. Taratibu za makubaliano kati ya dunia na Serikali zinatarajiwaa kukamilika kabla ya mwezi Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu hapa kwanza ameanza na neon, "katika mpango wa muda mfupi." Lakini ukiangalia katika hali halisi, reli zetu bado ni zile ambazo geji yake yake ni ya kizamani, mabehewa yake ni ya kizamani, vichwa ni vya kizamani kwa maana kwamba nina wasiwasi na hii sentensi ya kusema, "katika mpango wa muda mfupi wa uboreshaji wa huduma." Kwa sababu ni lazima vichwa na mabehewa yaagizwe.

Sasa inawezekana zoezi hili likawa ni la miaka miwili au mitatu au minne kwa sababu ni vitu ambavyo vimepitwa, ni vya muda mrefu, siyo kama tuna reli mpya kwamba tunakwenda tu kununua na kuleta zikaendelea kufanya kazi. Kwa hiyo, katika hili pia Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake naomba anipatie ufanuzi na majibu kwa niaba ya wananchi wa Mpanda.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba niongelee kuhusu suala la wananchi wa Mpanda, hususan wanaotumia reli ya kutoka Mpanda kwenda Tabora. Nashukuru kwanza Mheshimiwa Waziri umeweza kututengea angalau shilingi milioni 400 za marekebisho kutoka Mpanda mpaka Kaliua kwa sababu reli yetu ile ilikuwa ukipanda utafikiri umepanda barabara yenye makorogesheni kwa sababu unaruka mle ndani unadundadunda hata leo nimeota, nikafikiri niko kwenye treni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa kweli ulipatie kipaumbele suala hili hasa reli ya kutoka Mpanda kwenda Tabora. Wananchi wamekuwa wakiteseka pale *Station* Mpanda na hata Tabora, kwanza kwa kukosa kiunganishi kutoka Mpanda mpaka Dar es Salaam, Mpanda mpaka Mwanza. Lazima wafike Tabora pale wakae siku mbili au tatu au nne. Kipindi cha baridi wananchi wanapata taabu sana pale *station*, unakuta wametandika mifuko ya *sulphate*, wametandika Khanga na wamelala chini na watoto.

Naliongea hili kwa sababu usafiri wangu toka nasoma, toka nikiwa mtoto ambao nimetumia ni Reli ya Kat. Tulikuwa tunatua Tabora ndio tunaunganisha kwenda Mpanda. Wakati mwingineunalazimika kukaa pale siku mbili au tatu Tabora ukisubiri *connection* ya kwenda Mpanda. Ama unatoka Mpanda unalazimika kukaa pale siku mbili au tatu usubiri treli ya kutoka Kigoma au Mwanza ndio uunganishe kwenda Dar es Salaam. Tunaelewa kabisa Mkoa wetu hauna Hospitali za Rufaa, lazima watu wapite pale kwenda Bugando au kwenda Muhimbili. Kwa hiyo, wanateseka sana pale wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwanza atawasaidia wananchi wa Mpanda kwanza kwa kuongeza idadi ya mabehewa. Hatuna behewa la *first class* wala hatuna behewa la *second class*, mabehewa ya *third class* yako manne. Wananchi ni wengi, wanabebana mle ndani, wanabebea mizigo kichwani, kwa kweli inasikitisha sana, vichwa ni vibovu, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atupatie mabehewa ya kutosha na wala kusiwe na usumbufu kwamba mwananchi anatoka Mpimbwe anafika pale au anatoka Karema anafika pale Mpanda Mjini anakaa siku tatu pale *station* kusubiri tiketi ya Jumatano kwa sababu tuna treni mara tatu kwa wiki.

Kwa hiyo, siku pia ziongezwe ili ziweze *ku-match* na treni ya Mwanza pamoja na treni inayotoka Kigoma, na kama watu wa Kigoma wameweza kupewa treni, mabehewa yanayouganisha kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, kwa nini ishindikane behewa za kutoka Dar es Salaam au Mwanza moja kwa moja mpaka Mpanda? Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Waziri naomba alifanyie kazi na kunipatia majibu leo kwa niaba ya wananchi wa Mpanda kwamba unaowaongeza mabehewa na hawapati tena usumbufu pale Mpanda Mjini hata wanapokwenda Dar es Salaam ama Mwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niongelee katika suala la usafiri wa maji. Nashukuru sana kwamba fedha imetengwa na kiasi fulani kitakwenda kuboresha miundombinu katika maziwa yetu. Katika Ziwa Tanganyika meli zilikuwepo mbili, yaani *MV. Lihemba* na *MV. Mwongozo*. *MV. Mwongozo* haipo kabisa sasa hivi na hatujui ilikofia. *MV. Lihemba* ni mbovu kweli. Wananchi walioko kule ni wavuvi, kuna wafanyakishara wa kutoka Kongo, Burundi na Rwanda wanaingia kule, wanatumia boti, boti zinajaza ile lumbesa kabisa na wananchi wakiwemo humo ambayo ni hatari na matukio mbalimbali yamekuwa yakitokea kama vile hili lilitotkea la *Lake Nyasa* jana wananchi wamekuwa wakipoteza maisha na mali zao kwa kukosa usafiri wenye uhakika.

MV Lihemba kule inatembea mara mbili kwa mwezi. Mwananchi hawezi kusubiri kusafirisha mzigo wake eti mpaka meli itakapokuja na inapopita kule inakuwa na vituo maalum? Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba vituo viongezwe ile meli ifanyiwe marekebisho, kama sivyo tunahitaji meli mpya. Wananchi wa kule nao wana haki ya ku-enjoy maisha yao kwa kufanya biashara zao vizuri na wana haki ya kupata huduma na *security* ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, Ziwa Tanganyika linajulikana limepita kwenye Bonde la Ufa, kila dakika linabadiilika hali na uhakika, kwa hiyo, tunahitaji meli kubwa na mpya ambayo itawenza kusaidia wananchi wa kule ili waweze kufanya shughuli zao kwa ajili ya kujiletea pato katika familia zao. Vilevile namwomba Waziri arudishe baadhi ya vituo kwa mfano, kituo cha Msamba. Kituo cha Msamba ni kituo kikubwa lakini meli hauitui pale. Kuna wafanyabiashara wengi wa Samaki wanaotoka Burundi, Rwanda na Kongo. Kwa hiyo, tunaomba hicho Kituo kirudishwe.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuongelea suala la anga. Tumekuwa na viwanja vingi, tunashukuru hata kwetu Mpanda sasa hivi tuna uwanja wa ndege angalau itatusaidia. Lakini naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, nakumbuka mwaka 2007/2008 kama sikosei Mheshimiwa Waziri kwa kipindi hicho nilikuwa Beijing, alikuja Mheshimiwa Waziri Mama Nagu, Mheshimiwa Chenge na waliongozana na Rais.

Katika maongezi yake Mheshimiwa Rais aliongelea suala la kuanzisha ndege kutoka Tanzania mpaka Guangzhou kitu ambacho mimi nilifikiri na ninakiona mpaka sasa hivi kwamba ni cha msingi sana kwa sababu bidhaa nydingi zinazoingia Tanzania zinatokea Guangzhou. Mheshimiwa Mbobe ni shahidi kwa sababu naye amekuwa akienda Guangzhou mara kwa mara, kwa hiyo, anafahamu kabisa namna gani Guangzhou inafanya biashara vizuri na Tanzania.

Kwa hiyo, nafikiri katika huo mpango wa kuboresha usafiri wa anga, naomba tupate ndege moja kubwa ambayo itatoka Dar es Salaam moja kwa moja mpaka Guangzhou. Hiyo itasaidia sana katika kukuza uchumi badala ya kusema mtu atoke Guangzhou apite *Qatar and then arudi Dar es Salaam au atoke...*

SPIKA: Wewe mwenyewe inabidi ku-*declare interest*, ulikutana na Mbobe wapi? (*Kicheko*)

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, nilikutana na Mbobe Guangzhou, lakini alikuwa hanifahamu, kwani alikuwa amekwenda kuangalia namna gani ya ku-*design* sehemu yake ya biashara Dar es Salaam.

SPIKA: Wewe je?

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Japokuwa alikuwa hanifahamu kwa sababu nilikuwa...

SPIKA: Na wewe je?

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, mimi niko kule kwa muda mrefu sana nikwi nasoma.

SPIKA: Ahsante, endelea!

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba tu niseme kwamba sina tatizo na Wizara hii na kwa niaba ya wananchi wa Mpanda na Rukwa. Kama haya yote yatatimizwa na tutasikiliza kilio cha wananchi wa Mpanda, ninaunga mkono hotuba hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, nilisema atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, na Mheshimiwa James Lembeli pia atafuatia.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami naungana na wenzangu kuwapongeza Mawaziri wapya kabisa katika Wizara iliyoundwa upya. Ni kazi ngumu sana walijonayo.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema maneno yafuatayo: kwanza, katika miaka ya themanini *Air Tanzania* iliwahi kununua ndege moja mbovu kutoka kwa George H. Kitendo cha Ndege mbovu kufika hatua ya kwanza ilikuwa ni Mkurugenzi kuachishwa kazi haraka na Waziri akapoteza kazi. Hii *discipline* ndiyo itakayotusaidia kujenga hizi taasisi. Kama hatuchukui hatua za nidhamu kwa watu wanaozembea kwa makusudi, tutaendelea kuwa na matatizo haya, hata kama tuna fedha za kutosha za kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni *Air Tanzania* ilikwenda kukodi ndege mbovu mbovu ikaja hapa, għarama kubwa sana ikapotea. Lakini hakuna hatua iliyochukuliwa. Sasa mimi nasema hili ni tatizo moja ambalo lipo na ni lazima sasa tulikabili. Mimi nafikri Bunge lina nafasi nzuri kuitipia Kamati zake na Bunge zima kuwa-*discipline* watu ambao hawatekelezi wajibu wao. Tuisaidie Serikali katika hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba leo hapa tumezungumzia suala la *Air Tanzania*. ukisoma randama yao wanasema walikuwa na safari 28, sasa watafikia 78 wakati hakuna hata safari moja inayofanyika. Kinachofanyika ni nini? Mnakumbuka tulikuwa na semina pale Ubungo, tukizungumzia hali nzima ya mashirika ya umma na utendaji wetu wa kazi? Tukasema kama hakuna utaratibu wa *capitalisation* ya mashirika haya na tukafanya utaratibu wa kujuwa hasa *business plan* yake ikoje, tutakuwa tunakuja Bungeni tunaongeza fedha, lakini hakuna kinachoonekana. Leo tuna Shirika la Meli na Wachina, toka mwaka 1967 lina meli moja tu na leo ndiyo tunazungumzia kuunda meli ya pili. Toka mwaka 1967 na ni shirika linalofanya biashara. Sasa ingekuwa kuna *proper planning* ambayo ingetengenezwa mapema na *capitalisation* ikafanywa *proper* leo shirika lile ambalo linatengeneza faida tungkuwa na siyo chini ya meli nne au tano. Lakini tuna meli moja na sasa hivi wanazungumzia kutengeneza meli ya pili. Hatuna utaratibu wa kuendesha biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nakubali kabisa kwamba jambo la msingi kwanza tuamue kwamba, tunataka kufanya biashara au tunataka kufanya siasi? Tukitaka kufanya siasi tutazungumza hapa kwamba tumpe Waziri fedha akalete ndege mbili au tatu. Kama huajipanga vizuri hiso ndege hazitafanya kazi. Kwa hiyo, ni lazima kwanza tujipange kufanya biashara, hatua ya kwanza.

Kama tunataka Serikali ifanye biashara, iseme ni kwa asilimia ngapi inataka kufanya biashara. Mwekezaji anayekuja achukue asilimia ngapi? Watanzania wachukue asilimia ngapi? Huo ndio utaratibu. Matokeo yake ni nini? Leo Tanzania inataka kuzungumza na wawekezaji ili waweze kuwekeza, ukiwaliza, Serikali yenye nyile mna mpango wa kuwa na hisa ngapi katika hili? Hawajui! Watanzania watarithi vipi utajiri huu? Hawajui! Kwa hiyo, mwekezaji akija, kwa sababu nyinyi hamjajitarisha atachukua kila kitu, maana ye ye anafanya biashara, siyo mpumbavu. Atachukua kila kitu, tutabaki kulalamika tu hapa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachokiomba katika Serikali, hebu jipangeni. Jipangeni mseme mnataka nini ili tuje Bungeni tuseme jamani Waheshimiwa Wabunge tumejipanga katika kuwarithisha Watanzania Shirika la Ndege la Tanzania, asilimia 30 ni ya kwao. Tuna- *raise* vipi *funds* za Watanzania hao kurithi? Tunakwenda kwenye *capital market*, tunazungumza nao namna gani Watanzania watarithi *shares* zao? Pili, tunasema Serikali itakuwa na hisa hizi kutoptaka na *assets* walizonazo. Mwekezaji akija aingie kwa ubia huu, na *plan* yetu ya kufanya kazi ni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tatizo letu ni kwamba hatujui ni kipi tunachokitaka. Nenda kwenye madini, hali ni hiyo hiyo. Nenda katika sekta hali ni hiyo hiyo. Kwa hiyo tutakuja Bungeni hapa, tutalaumiana, leo Serikali imesema mnatoa fedha hiso, lakini ukisoma hii Randama ya Mheshimiwa Waziri, *is not realistic* kwamba una safari 28 za *Air Tanzania*, leo unasema safari 78. Kwa ndege gani? Hiso safari 28 ziko wapi? Kuna *experience* gani? Una *man power* imekaa pale inakula fedha tu. Kunahitajika kujipanga vizuri. Mimi naomba sana, sasa hivi tuna sheria ya *PPP*,

kakaeni kitako, mtazame hii mizigo mizito ya *infrastructure* ya usafiri, *solution* yake ni kutumia ile Sheria ya PPP tutapata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, ni aibu, mradi wa Songwe hapa, hili ni zaidi ya Bunge la Nane, hakuna *development programme*, kwa wenzetu imechukua miezi 18. Bunge la Nane, mimi nahesabu mradi wa Songwe, kila wakati tunabajeti mradi huo huo mmoja. Tumemaliza mwaka huu, na mwaka ujao utakuja tena vilevile. Sasa ukisoma humu viwanja hivi chungu nzima vimeandikwa hapa. Huyu shilingi bilioni moja, huyu shilingi bilioni tatu, mradi huo hasa unataka kiasi gani? Ili tuseme mara hii, jamani fedha zetu tulizonazo hebu tuelekee Tabora, tukamalize tatizo la Tabora, liondoke na iwe hadithi. Hivi kuna tatizo la Kigoma, hebu tukamalize tatizo la Kigoma limalizike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kwenda namna tukagawana Sungura mdogo. Huyu sungura mdogo hagaiwi vizuri tukashiba. Ningeelekeza mahali ambapo nina hakika *output* yake ni kubwa. Ukiniambia leo niende Kigoma nikafanye *gragging* ya Port ya Kigoma, nitengeneze *infrastructure* Kigoma najua mtaji utakaingia pale kutoka Congo ni mkubwa. Mtapata fedha za kuendeleza mahali pengine. *That is how you do it.* Sasa matokeo yake tunakuja hapa kila mtu anasema mimi nataka kibarabara hiki, huyu anataka hiki, faida yake huioni. Kwa hiyo, tunarudia kusema hizi *budget systems* zetu, utarudia mradi huo huo mmoja miaka kumi kwa sababu mara hii umepewa shilingi bilioni moja, mara hii umewekewa *token*, mara hii mfadhiri hakutokea. *That is the story we are having.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningeomba Serikali ijipange katika kutatua matatizo ya *infrastructure* katika nchi, na njia pekee ni kuishirikisha *private sector* na ili *private sector* ishiriki ni lazima sisi Watanzania tujjue kwamba tunawataka washiriki kwa kiwango gani? Bila hilo hamna kitu. Ndiyo maana tatarudi hapa Bungeni tutasema ooh, wanachukua raslimali zetu, wanaondoka, Watanzania wanaachwa maskini. Ni kweli wataachwa maskini.

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilikuwa namwuliza Waziri wa Madini hapa kwamba, sisi tunagaiwa viwanja nya maeneo ya dhahabu na kadhalika. Wenzetu wanakuja na fedha zao dola milioni tatu au nne wanafanya *exploration*. Wakitoka hapa wanakwenda kwenye *stock market* mradi walioununua kwa dola laki moja una-raise hundred and twenty million dollars kwa kupoteza shilingi milioni tano tu. Sasa tatizo lenyewe ni kwamba wewe mwenyewe hujui unachokitaka, wala hujui raslimali yako.

Kwa hiyo, ni lazima tufike mahali sasa tuamue kama Tanzania kwamba, Watanzania tunataka kuwarithisha utajiri wao kwa kiasi gani. Hivyo ndiyo tutafanikiwa. Ndiyo maana utaona *Kenya Airways* kuna asilimia za Wakenya, *investors* na kuna asilimia za Serikali, *and they are flying*. Wakenya waliamua kwamba Nairobi iwe *hub* ya Afrika, sisi *Air Tanzania* bado tunazungumzia tu kwamba tataruka hapo Comoro, tutazunguka wapi, lakini hasa *policy* yetu kama *Air Tanzania* ni nini? Hamna! Sasa mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri, haya ndiyo mambo ya kuyazingatia na kuyafanya kazi. Tutasaidiana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwombwa sana Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na fedha hizi alizoahidi Waziri Mkuu, na hizi ambazo zimepita bado mnahitajika mrudi kwenye Kamati ya Miundombinu mkakae kitako. Mimi naamini kabisa zitapatikana hata fedha nyingine mtakapozungumza na wahisani wengine kama *World Bank* na kadhalika kwa sababu hii fedha bado ni kidogo sana. Mje na kitu ambacho mtatuambia kwamba mwaka huu katika miezi 18 tunamaliza tatizo fulani ili mwakani tuzungumze lugha nyingine. Lakini tatarudi hapa tutazungumza *the same language* na maneno yatakuwa haya haya makali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mambo yangu mimi ni mawili tu. La kwanza ni nidhamu. Tuchukue utaratibu wa Benjadjid wa Algeria ambaye alikuwa na utaratibu kwamba ukituhumiwa kwa rushwa kwanza anakwambia Mheshimiwa pumzika, tunaendelea na uchunguzi tukimaliza uchunguzi utarudi kazini kama huna makosa. Kama una makosa unakwenda Mahakamani. Lakini sasa unamwacha mtu anatembea tu, anafanya anachotaka tu, halafu mnapiga hadithi. Hatuwezi kufika huko! Hili suala la nidhamu linazidi kuondoka, kila siku linadorora na hatufiki mahali. Kwa hiyo, mimi nafikiri hili ni la kwanza la kuzingatia.

Mheshimiwa Spika, la pili naiomba sana Serikali, miradi hii mikubwa tuliyonayo ya barabara, reli, lazima tufike mahali tuamue. Leo tunajenga barabara, bila ya reli hakuna barabara itakayodumu, kwa sababu hakuna barabara inayoweza kuchukua tani 3000, 4000. Hakuna! Kwa hiyo, utakuta umejenga barabara, kesho kutwa yamepita malori makubwa, utakuta imeshafanya milima na haipitiki tena. Inabidi utafute fedha tena za kutengeneza barabara uliyoitengeneza miaka miwili iliyopita nyuma, kwa sababu hakuna reli.

Kwa hiyo, kwangu mimi *priority number one* ningesema hapa tuelekezeni fedha kwenye reli. *Solve the problem ya railway!* Ndiyo inayobeba mizigo mingi, ndiyo inayochukua abiria wengi na hasa watu wa daraja la chini. Tuwe *focused!* We are not focused! Kwa hiyo, hata hizi fedha za reli unazopitaa hivi sasa unakwenda kutengeneza reli ile ile yenye *gauge* ndogo, bado matatizo yetu yako palepale. *Go to China kakope (borrowmoney)!* Go to the World Bank kakope, tengeneza reli. Hebu ondokeni hapa mkisema jamani kwanza reli, hadithi nyingine tuache. Tutafungua uchumi wa nchi hii, mapato yataongezeka, usafiri utaongezeka na watu wataondokana na shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fanya *dragging* ya Bandari ya Dar es Salaam, *TPA* wanazo fedha za kufanya *dragging* pale. Tumelizungumza hili la *dragging* ya *Port* ya Dar es Salaam kwa zaidi ya miaka 15. *Fifteen years* katika Bunge hili! Kenya wameamua juzi *two hundred million dollars* wame-calculate, wameshatengeneza Bandari wamemaliza, wanaendelea na kazi nyingine. Sisi we are just talking. Kafanye *dragging* ya *Port* ya Dar es Salaam, panua reli, utazame uchumi wa Tanzania kama haukufunguka. Lakini tumbaki na hadithi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba, hebu tuwe *focused*. Bahati nzuri juzi tumepitisha Mpango wa miaka mitano, lakini bado tunahitaji *kuu-narrow down*. Priority number one ni nini, nchi ifunguke? Wasukuma wanataka kusafirisha ng'ombe wao, pamba yao, waondokane na hizi shida. Tumbaku kule kwa Mzee Sitta itoke kwa njia ya reli gharama zake ni ndogo, bidhaa zetu zitapata bei nzuri. Bei ya bidhaa zetu inakuwa kubwa kwa sababu gharama za usafiri ni kubwa. Sasa tafuteni njia za kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Air Tanzania* wanazungumzia kununua ndege. Mimi nadhani wangefikiria kununua *air cargo*. Kama kuna *area* hajaguswa Tanzania ni usafirishaji wa mizigo kwa njia ya ndege. Ndege ya kwanza kabisa na hasara zao zingekwisha. Peleka nyama Congo, Burundi, yaani ni bidhaa tu, na ndege za tani 25, 35 ziko tele tu. Kaa, *plan these things*. Ndiyo maana nasema lazima kuwe na *corporate plan*. Hii ya kuja kutuambia tu utatengeneza ndege tatu, nne, tano, doesn't make any sense to me! Tuwe na *corporate plan* itakayowezesha *Air Tanzania*, investor aje ili tutumie raslimali hizi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Baada ya maneno mazuri ya Waziri Mkuu na haya niliyoyasema, utekelezaji ukifanywa, mimi nafikiri kuna matumaini mbele ya safari. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nilikuwa naangalia hapa watu wengine nikawa naona kama ni kundi, lakini sikupewa majina yao. Naambiwa ni Wajumbe wa Baraza la Vijana, Mkoa wa Mara wakiongozwa na Ndugu Fidelice Manyerere. Wako wapi hawa? Vijana hao ambaa ni Wajumbe wa Baraza, wako wapi? Aah, wengine wametoka. Haya vizuri! Ahsante sana na karibuni. (*Makofi*)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Kwanza naomba *ku-declare interest* kwamba mimi ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kwa vile maeneo mengi yameshazungumza na michango mingi imeishatoka kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, sitaki nirejee katika maeneo hayo, iwe katika ndege, reli au bandari. Mimi nataka nijikite zaidi kwa ndugu zangu wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*). Kule kwetu tunawaita 'Ngadu,' wale kaa ambaa wanaishi baharini na nchi kavu. Sasa hawa ni wadhibiti wa masuala hayo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mamlaka hii ilianzishwa kwa Sheria Na. 9 ya mwaka 2001. Ikaanza kufanya kazi zake Agosti, 2004 baada ya kutangazwa rasmi na *Government Notice No. 297* ya mwaka huo huo wa 2004. Mamlaka hii sheria zake zilipitishwa na Bunge na ilitakiwa ifanye kazi vizuri na jana katika hotuba ya Waziri tumemsikia kwamba anataka kufungua ofisi za mamlaka hii takribani katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nianze na usimamizi wa mamlaka hii katika usafiri wa maji kwa maana ya maziwa pamoja na bahari. Kwa mujibu wa tafiti na taarifa za *Indian Ocean Memorandum of Understanding (IOMOU)* inayoratibiwa nchini India katika Mji wa Goa. Taarifa hii ambayo waliiota mwaka 2008 na 2009 inaonyesha kwamba kati ya vyombo 100 ambavyo vinakuwepo katika eneo la majini, katika Tanzania vyombo 35 havina ukaguzi. Vyombo 35 haviko salama! Vyombo thelathini na tano havieleweki! Vyombo 35 hivi havina utambulisho! Yaani hata ile kujulikana kwamba hivi ni vyombo vya nchi fulani vinatembea katika maeneo yetu ya maji. Hapa inaonesha ni namna gani nchi yetu inavyopoteza mapato.

Mheshimiwa Spika, nydingi kati ya meli hizi ni za kigeni ambazo zinakuja katika bahari zetu na zinachukua zinachopenda. Wakati anachangia hotuba ya Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alitoa mfano wa Maldives, ni kwa namna gani nchi ile inaendesa uchumi wake kwa kupitia uvuvi tu. Leo kama kiwango kikubwa hiki cha meli zinakuja na kuondoka tu katika nchi yetu, hazieleweki zinafanya ninj? Zinakwenda wapi? Kwa kweli hapa tunapoteza mapato makubwa ya Serikali. Ni jukumu la wadhibiti hawa ambao wamepewa mamlaka na vyombo husika waweze kushughulikia suala la kuzikagua meli hizi.

Mheshimiwa Spika, katika meli 35 hizi, vimo na vyombo ambavyo tunavitumia kwa ajili ya usafiri wa abiria. Walivikagua na wakakuta makosa hayo. Kosa kubwa limekuja kuonekana pale meli hizi zinapotakiwa ziingle na kutoka Bandarini ambapo ni lazima zisajilliwe. Kuna malipo ambayo yanapaswa yafanywe pale. Kuna fomu pale inaitwa *ship clearance form* ambayo ni lazima ijawze kwa sababu ndiyo inawezesha kujua uwezo wa ile meli yenye na uzoefu wa crews.

Mheshimiwa Spika, hizi meli zinapopiga chenga kwenda pale kwa kweli maafa mengi huwa yanatokea. Wanapiga chenga siyo kwa sababu baadhi ya meli ni mbovu. No! Wanapiga chenga kwa sababu pale kuna malipo ambayo ni lazima Serikali iyapate. Sasa hapa wanapapiga chenga. Kuna fedha nydingi sana zinapotea hapa katika kitengo hiki. Mheshimiwa Waziri anataka kuwajengea *SUMATRA* Ofisi Wilayani, lakini kwanza akawatafatule fedha katika kitengo hiki. Fedha za hapa zitatosha kujenga ofisi zote za Wilaya katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, bado niko baharini. *SUMATRA* hawa hawa wamehudhuria katika Mikutano mingi ya kimataifa. Labda nitoe mfano wa Mikutano miwili. Kwanza, kuna ule Mkutano waliohudhuria Nairobi mwaka 2008 uliohusu ukomesaji wa maharamia na wizi wa kutumia silaha katika bahari yetu kuu, lakini vilevile katika maziwa yetu makuu. Jana hapa wakati tunachangia Wizara hi,i Mheshimiwa Abdulkarim Shah alitoa mfano wa namna gani kisiwa kile cha kwao kule kiliviyovamiwa na majambazi wa kutumia silaha. Sasa tunawaomba hawa wenzetu, huu uzoefu walioupata wasikae tu ofisini, hebu wajaribu kuangalia namna gani watapambana na hili suala. Mafunzo wameshayapata tayari na ili kuzifanya hizi bahari zetu na maeneo yetu ya maji yawe salama ni lazima huu uzoefu walloupata katika Mikutano hii hebu wautumie tuone.

Vile vile walihudhuria katika Mkutano mwingine ambao unaitwa *East African Community Mission* ambayo iliasisi *MRCC* uliofanyika Mwanza na ukafanyika na pale Kisumu. Kwa hiyo, wamepata mafunzo makubwa. Nashukuru kwamba wameanza kuchukua hatua, *Lake Tanganyika* kule wameamua kufungua Ofisi na vile vite kwa kushirkiana na *TPA* wameamua kuanzisha kitengo hiki pale Dar es Salaam ambacho kilizinduliwa na Mkurugenzi Mkuu wa *IMO*.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenda tu katika semina, jamani haitosaidia. Tunawaomba *SUMATRA* msionekane kama dhaifu. Mna nafasi kubwa ya kuhakikisha kwamba eneo la maji ya nchi yetu liko salama kwa kushirkiana na Taasisi nydingine Polisi, Jeshi, hebu tuone namna gani mnawenza kufanya kazi. Tunamsulubu Waziri katika baadhi ya mambo lakini kuna baadhi ya

mambo tumsifu. Kwa hiyo, tunaomba *SUMATRA* msaidieni Waziri katika hili na sisi tuko tayari kusaidiana na nyinyi. Sisi tuna tafiti chungu nzima. Nataka niwape siri moja ya *CUF*. Chama cha *CUF* hakilali usiku na mchana. Saa 24 kina-monitor katika dunia, kinaangalia namna gani mwaka 2015 tutakapokuja kuchukua nchi hii tutaweza kuiendeleza. Njooni kwetu, tuna *material* nyingi sisi. Prof. Lipumba yuko pale, Mwanauchumi wa Ulimwengu. Tuwaonyeshe, tuwape mambo yanavyokwenda.

MBUNGE FULANI: Kampeni hiyo!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Siyo kampeni.

Mheshimiwa Spika, vile vile sasa nataka nitoke baharini niende nchi kavu. *SUMATRA* ni wadhibiti wa usafiri wa nchi kavu. Wakati tunachangia hapa Wizara ya Mambo ya Ndani nilizingumzia sana suala la ajali za barabarani. Kwa kweli nilisikitika sana na baadhi ya wananchi walisikitika sana wakati wa *ku-sum up*, Waziri wa Mambo ya Ndani hakuzungumzia kabisa wala hakutaja hata neno moja kuhusiana na ajali za barabarani. Mimi nilitegemea kwamba kutokana na mchango ule wa Wabunge kwamba Waziri siku ile angelitamka kwamba Kikosi cha Barabarani anakivunja na anaandaa utaratibu mpya wa Kikosi cha Barabarani, lakini la kushangaza hakuzungumza chochote katika hilo.

Ninawaomba wenzangu wa *SUMATRA* kwamba hili suala ni jukumu lao na hapa kuna mapato makubwa ya nchi yanapotea. Sisi tunaona tu ajali, tunakaa tunapeleka salamu za rambirambi, lakini tunasahau kwamba nchi inaingia katika hasara. Mwaka 1994 Tanzania ilipoteza shilingi billioni 11 kwa ajili ya ajali za barabarani. Hizi tafiti sisi tunazo, nimewaambia hapa shilingi billioni 11 ambapo *National Insurance* ilitumia, shilingi billioni 15 kwa ajili ya kulipia *road accidents*, hebu tuangalie kutoka mwaka 1994 hadi leo ambapo ajali zimezidi mara kumi nchi yetu imepoteza kiasi gani? Ni fedha nyingi!

SUMATRA tokeni Ofisini, msikae maofisini. Mimi najua Waziri amezungumzia suala la kuwafungulia Ofisi katika Mawilaya, kule mtakwenda kubughudhiana na hawa wenye madaladala kwa ajili ya tiketi, hakuna kingine. Hebu tuleteeni mpango ambaeo na sisi tuuangalie kama Wabunge tukiona unafaa *take off* kwa hilo. Kama kuna sheria zinakwaza, zileteni, lakini kwa kweli kuendelea nchi kupoteza mapato namna hii tutakuwa hatuwartendei haki wananchi.

Nitazungumzia suala la *U-track* na leo nataka nilizingumze tena. Ule ni mzigo kwa raia. Yule mmiliki wa basi atakapoinunua ile *U-track* na kuifunga ile fedha hatalipa ye. Yeye ataongeza bei katika nauli na huu mzigo utamwangukia mwananchi. *U-track* yenyewe sasa ilivyo na mchezo, hawa makondakta wanaichukua ile *U-track*, ndani yake mle mna *chip*, ile *chip* anaitoa, anaiweka katika simu yake na analiacha. *Bus linatangulia* wale wanapo-*trace* wanakuta *Bus* liko Dar es Salaam, kumbe yule kondakta ameichukua ile *chip* ameweke katika simu, kapanda *Bus* la nyuma. *Bus* limeshapita Dodoma kuelekea Singida, unapoli-*trace* unaambiba *Bus* liko Morogoro. Kwa sababu ile *chip* iko ndani ya simu ya kondakta ambayo bado iko Morogoro. Sasa haisaidii kitu, ni mzigo tunataka kuwapa wananchi.

Nilimwambia Waziri wa Mambo ya Ndani, lile ni bomu ambalo amewekewa ndani ya mfuko wake. Nashukuru kwamba *SUMARTA* katika Kamati, wao walisema hawakuhusishwa na mpango ule. Japokuwa waliidanganya Kamati kwa kiasi fulani, lakini hili tutabanana huko huko katika Kamati, kwa sababu sahihi zao nimeziona katika *document* ya *U-track* na hili hawawezi wakabisha. Lakini hili tutabanana huko huko ndani ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ulikuwa ni huo. Kwa hayo, machache sijaweza kuunga mkono hoja. Kwanza mpaka niangalie mustakabali mzima wa Waziri atakavyoweza kuja kuleta majumuisho yake hapa. Ahsante.

SPIKA: Ahsante, nashukuru. Sasa namwita Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Felix Mkosamali ajiandae na Mheshimiwa Fatma Mikidadi pia.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu. Lakini sana sana namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kusimama kuchangia hoja ndani ya Bunge hili la Bajeti kwa mara ya tatu.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyopo mbele yetu kwangu mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Wilaya ya Kahama ambao ni wadau wakubwa kabisa wa sekta ya reli na ya anga kwa maana ya Shirika la Reli Tanzania na Shirika la Ndege, ni muhimu na ni wajibu wangu kwa kweli kuwasilisha maoni na matakwa ya wananchi wa eneo hilo. Lakini sio wananchi wa Kahama tu, nina hakika wananchi wa maeneo yote ambayo Reli ya Kati inapita kuanzia Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na wale wa Mpanda kwa Waziri Mkuu, Tanga, Arusha na Moshi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hotuba ya Waziri Mkuu asubuhi, ninapata kigugumizi cha kusema ninaunga mkono hoja au siungi mkono hoja, nitatoa uamuzi baada ya maeleo ya Waziri kutolewa. Katika mazingira ya sasa, nampongeza na kumsifu Waziri Mkuu kwa taarifa ambayo ameitoa ndani ya Bunge hili. Naamini Waziri Mkuu ni mtu makini. Hata wakati akitoa taarifa yake unaweza kuona usoni mwake kwamba jambo hili lilikuwa linamkera na limemgusa. Sasa kama nilivyo sema, nitasema naunga mkono hoja au siungi mkono baada ya kumsikiliza Waziri na kumwona usoni kwake kama yale atakayokuwa anayazungumza kweli Serikali itayatekeleza.

Mheshimiwa Spika, inaumiza sana kuona Shirika la Reli halifanyi kazi ipasavyo. Nakumbuka katika Bunge la Tisa wakati Serikali inaleta hoja ya kubinafsisha Shirika la Reli, Wabunge waliokuwa wengi walikataa katakata. Lakini kama ilivyo kawaida ya Serikali na wale walioongoza jitihada za kuwashawishi Wabunge wakubali, wengine bado wamo huku ndani, walikataa kwa kutoa sababu chungu nzima nyingine za kiutafiti kwamba wale jamaa wa India hawana uwezo.

Bunge lilitidhia na baada ya wiki mbili, tatu tukaanza kuona vichwa vya treni vya kwetu vinapelekwa India kwa kigezo cha kwenda kufanyiwa marekebisho na mabehewa pia. Leo namshangaa Waziri! Ukiangalia kitabu hiki, *cover* yake ni nzuri sana, imepambwa na picha nzuri, lakini hizi picha siyo halisi. Kuna picha ya *Air Tanzania* hapo. Nataka nimwulize Waziri, hii ndege iliyopigwa picha hapa, iko wapi? Kwa nini anaiweka kwenye *cover* ya hotuba yake? Huku ndani kuna meli, hii meli naona ya Mwanza sijui *MV Victoria*, hivi hii meli kwa jinsi inavyoonekana hapa ndivyo ilivyo leo hii? Jamani hawa Watanzania wanaotusikiliza tukizungumza humu si wanatushangaa?

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi pekee katika ukanda huu wa Afrika ambayo inatumia barabara kukuza uchumi wake. Duniani kote nchi zote zilizoendelea, usafiri wa reli ndiyo msingi wa uchumi wa nchi. Sasa hapa tumetengeneza fedha nyingi sana kuimarisha barabara zetu, lakini nikuhakikishie, hizi barabara hazitachukua miaka miwili mitatu zimekwisha. Angalia mitambo mizito, mikubwa, minene ya ajabu inayosafirishwa kutoka Dar es Salaam kwenda Shinyanga kwenye migodi.

Mambo haya yalitakiwa yasafirishwe kwa reli na sisi tunaona fahari kuyasafirisha kwa barabara. Ndugu zangu kule Wasukuma, Wanyamwezi sasa hivi wanatasafirisha ng'ombe kuja Dar es Salaam kwa malori. Hata ubinadamu hatuna kwa ile mifugo. Ukiiona jinsi wamebanana kwenye yale malori huwezi kuamini. Pamba ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na tumbaku inayotoka kwa Mzee Sitta inasafirishwa kwa malori. Sasa lini tutafikia hatua na sisi ya kusafirisha bidhaa zetu kwa reli?

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha ni kwamba kama miaka ya 1970, 1980 ambapo uchumi wa nchi hii ulikuwa duni na ulikuwa unakua kwa kiwango cha chini, bado treni iliweza kusafiri kila siku kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma na Mwanza. Leo tunapozungumza humu ndani ya Bunge kwamba uchumi wa nchi hii unakua kwa kasi ya asilimia sita, bado treni haitembe. Nilikutana na Mjerumani mmoja akaniambia, Watanzania ni watu wa ajabu sana. Wanasisia kitu ambacho hakipo na wanashangaa leo tunasema kwamba treni sijui ndogo na kadhalika. Ukienda Ujerumani bado wanaendelea kutumia baadhi ya reli zilizojengwa kabla ya

vita kuu ya kwanza ya dunia zilizojengwa miaka ya 1890 bado wanatumia. Sasa iliyopo haifanyi kazi, tunazungumzia kujenga sijui mtandao mwингine. Ni mambo ambayo mimi siyaelewii.

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Waziri hapa anasema bandari kavu ya wapi? Mimi natoka Kahama pale wanapodai kwamba ni bandari kavu hapaonyeshi dalili za bandari kavu. Yale majengo yaliyopo pale yamechakaa, yamekwisha. Stesheni ya Isaka sasa hivi, Isaka kwa Kinyamwezi au Kisukuma maana yake "Kichaka". Ukienda pale leo inadhihirisha wazi kwamba hapa ni kichaka. Miaka ya 1970, 1980 mimi nikienda shule pale mahali ilikuwa ni safi, leo hii ni makazi ya mbuzi, kondoo wasiokuwa na mwenyewe na vichaa. Uchumi wa wananchi wa Kahama sasa hivi umeathirika kwa kiwango kikubwa. Zamani wakisafirisha mizigo yao kwa treni mpaka Isaka, bei ya bidhaa ilikuwa chini, leo hakuna kitu, ndio maana nimesema napata kigugumizi niunge mkono au nisiunge mkono. Nikiunga mkono sasa hivi kabla ya wananchi wa Kahama hawajamsikiliza Waziri akielezea mipango thabiti ya kufanya Isaka bandari kavu hawatanielewa na mimi sitakubali. Mambo ya ajabu sana!

Mheshimiwa Spika, wanasema Isaka ni bandari kavu na kiungo cha kutoka Tanzania kwenda Rwanda na Burundi. Katika kitabu hiki wanasema wamekamilisha ujenzi wa *container terminal* Shinyanga. Hakujengwa Isaka, kimekwenda kujengwa Shinyanga. Sasa najiuliza, huyo aliyepanga ile *container terminal* isijengwe Isaka iende kujengwa Shinyanga, anaifahamu ramani ya nchi hii? Ina maana treni itatoka Dar es Salaam kwenda Rwanda kupakia mizigo? Itapita Isaka itakwenda Shinyanga halafu itarudi kinyumenyume ndiyo iende Rwanda?

Mheshimiwa Spika, matatizo ya nchi hii yanaanzia pale tu viongozi na watendaji ambaa wanapewaa mamlaka kuongoza Taasisi hizi hawana uzalendo. Mimi nataka niulize, jana nilikuwa naangalia kule alikokaa Katibu Mkuu, wakati Wabunge hapa wanazungumza kwa hisia, wao wanacheka na wana haki ya kucheka kwa sababu hawajali! Yapata kama miaka kama saba sijasikia Waziri sijui nani amepanda treni kutoka Dar es Salaam kwenye ziara, anakwenda Tabora, hapana. Hawapandi na wako kwenye magari yenyе viyoyozi. Kwa hiyo, hawajui adha wanayopata wananchi wa Kahama, Kagera, Kigoma kupanda mabasi kutoka kule kuja Dar es Salaam. Turejeshe moyo wa uzalendo na Mashirika mengi haya yatakwisha, yatakuwa kwa sababu waliopewa dhamana ya kuchagua nani aende kufanya kazi pale hao hao ndio wanachakachua, wanapeleka watu ambaa wanayamaliza Mashirika haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati *Air Tanzania* iko kwenye mawe unapeleka mtu ambaye ameweka Shirika lingine kwenye mawe eti akafufue. Turejeshe moyo wa uzalendo. Nikirejea kauli ya Waziri Mkuu asubuhi hii, nasema mimi namsubiri Waziri, vinginevyo nitakaa kimya. Ukiona mambo yanaharibika kwa kiasi hiki na watu wanafurahi, nchi hii ni yetu sote na kuna wakati huwa nafikiria labda Mwalimu Nyerere ametulaani, yote aliyokuwa akiyasema miaka ya 1960, 1970 na ya 1980 na tunaona fahari kuyarejea leo, utekelezaji hakuna. Watu wanaharibu, wanasema sheria. Kibaka kule barabarani akikwapua simu ya mtu, miaka kumi jela. Humu ndani tunawafahamu watu wanaharibu, wanakula fedha za Mashirika, hivi sheria ipi inayotumika kwa yule wa chini, hawa wa katikati na wa juu haiwagusi? Mtu anaharibu, anahujumu, taratibu zinatuwa; haiwezekani. Enzi zile za Mwalimu ukifanya kosa, bahati nzuri wewe Mama Makinda umefanya kazi wakati wa Mwalimu. Ilikuwa ukifanya kosa, ni pale pale. Sasa huu utaratibu wa sasa ni kwa maslahi ya nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sipendi kengele ya pili ilie wakati naendelea kuzungumza. Nina uchungu sana na kawaida yangu leo nimepozwa na kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu asubuhi, vinginevyo humu ndani palikuwa hapatoshi. Nina mambo mengi ambayo nimepewaa na wananchi wa Kahama, Mwanza na wapi niyaseme humu ndani kwa sababu mimi siogopi, nasema ukweli, lakini kwa kauli ya Waziri Mkuu naiheshimu ninakaa chini. Nashukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mimi nawaambia siku zote, someni Kanuni zenu, zina nafasi ya kufanya hayo yote mnayoyasema. Mnayo nafasi kubwa kabisu, sasa nyie mkianza kusema bila kutumia Kanuni wananchi watazitumia wapi? Ni ninyi wenye wenyewe ndiyo wenye uwemo. Mradi mtu unakuwa mkwelli, huna maslahi nyuma yake, hapo mambo yatakwenda. Lakini mtu anakuwa na maslahi halafu analeta hoja, haiwezekani. Kwa hiyo, ndiyo hivyo, kanuni zetu ziko wazi, zina nafasi nydingi sana. Kwa hiyo, naomba mztumie wakati wote.

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni sikuwatambulisha walioongozana na mke wa Mheshimiwa Mfutakamba, ni Madiwani na wanaongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Mashaka. Ahsante sana. Halafu pia ameongozana na Wajumbe wa Kamati ya Siasa ikiongozwa na Mwenyekiti, Ndugu Abdallah Kazwika na hao nao wasimame. Ahsante sana. Kwa hiyo, yule mama hakuwa peke yake, alikuwa na ujumbe wote huo. Karibuni sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mkosamali akifuatiwa na Mheshimiwa Mikidadi.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa naomba kutoa pole kwa wananchi wa Muhambo kwa sababu tumepatwa na msiba wa aliyekuwa Mbunge wa Kwanza wa Jimbo lile, Mheshimiwa Pius Mliliye kuptit Chama cha TANU. Kwa hiyo, naomba nitoe pole kwa wananchi wa Kibondo na nawaambia kwamba na mimi nitakuja kutoa pole zangu maana Mzee huyu alikuwa anatushauri sana hasa sisi Wabunge vijana. Baada ya pole hizo naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda wakati Waziri atakapokuja kujibu, nifahamu kuhusu hii ndege ya Mheshimiwa Rais maana tunasikia kuna ndege kubwa sana watu wanawenza wakacheza *basketball*, mipira na nini. Sasa tunataka tujue kama ndege hii ipo na kama ipo inatusaidia nini na kwanini isiuzwe ili kununua ndege nyingine? Maana haiwezekani tuwe na ndege ambayo inaweza ikatua kwenye viwanja vitatu halafu Shirika la Ndege lisiwe na ndege hata moja! Kwa hiyo, napenda kujua hii ndege inatusaidia nini? Maana ni kubwa sana, tunasikia hakuna ndege kubwa kama hii Afrika.

Mheshimiwa Spika, la pili, napenda kuzungumza kuhusu suala la uwajibikaji. Mwalimu Nyerere aliwahi kuzungumza kwamba ukiwa Ikulu ni mzigo mzito, watu wasililie kwenda Ikulu au kuwa Mawaziri. Leo Uingereza watu wakteuliwa kuwa Mawaziri wanaskitika. Ni masikitiko makubwa maana umepewa kazi kubwa na mzigo mkubwa na mzito. Kwa hiyo, na sisi Tanzania tunataka ukipewa Uwaziri siyo kwenda kufanya *party*. Ujue kabisa kwamba umepewa mzigo mkubwa, mzito, kwa sababu watu wanakuangalia wewe na hatuwezi tukakuonea huruma kwa sababu umekubali kuupokea huo mzigo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa kuna Mikataba ambayo imekuwa inaingiwa ambayo ndiyo inasababisha matatizo makubwa sana kwenye nchi hii. Hapa nina mkataba umeandikwa: "The United Republic of Tanzania Concession Agreement for Tanzania Railway Cooperation Concession Between Reli Assets Holding Company Limited and Tanzania Railway Limited."

Huu Mkataba ndiyo ulioingiwa baada ya *RITES* kuungana na Serikali na kutengeneza *TRL*. Baada ya kuungana ndiyo wakaingia Mkataba huu na *RAHCO* ili *RAHCO* iweze kumiliki na kusimamia raslimali za Shirika la Reli. Sasa Mkataba huu ukiuangalia ni mkataba ambaa ulikuwa ni mbovu na ulikuwa haulisaidii taifa hili. Ndiyo umetufikisha hapa, umesababisha *RITES* ishindwe kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Mkataba huu, inaonyesha tulikuwa na vichwa vya treni 117 lakini vichwa vilivypo sasa viko 32 baada ya hii Kampuni kupewa kuendesha Shirika hili. Sasa cha kushangaza ni kwamba watu walioingia mkataba huu wamewajibishwa namna gani? Ambao wamesababisha mabehewa haya yapotee tumewachukulia hatua gani? Tunaposema uwajibikaji ni kwamba Waziri tunasikia huko na mimi niliwahi kusoma kwenye baadhi ya magazeti tukasikia kwamba Mheshimiwa Magufuli anataka kuijuzulu na nini, baadaye ikapotea hivi hivi. Sikuelewa! Inawezakana yeze anakuwa mkali, anaeleza kwamba kama hamnipatii kiasi hiki mimi sifanyi kazi. Kwa hiyo, na hapa hatutaki Mawaziri ambaa wanatuletea bajeti ambayo haitoshi ambayo tutabaki tunaizungumza kwa siku mbili tatu.

Tunataka Mawaziri ambaa wanakwenda wanasema hii bajeti haifai kwa sababu wao kama Mawaziri wana-*collective responsibility*. Wana uwajibikaji wa pamoja kama Ibara ya 52 na 53 za Katiba zinavyosema. Lakini kama Waziri haukuliani, unajuzulu na kukataa. Siyo unakuja na kitu ambacho unaona hakiwezekani. Sasa leo wanakuja na bajeti hii, kiufupi ni kwamba haiwezi kututua matatizo haya. Nani aliwatuma wakubali? Lazima *individual responsibility* zifanyike. Kama

hukubaliani na Mawaziri wengine, jiuzulu. Kama hujuzulu maana ukija ndani ya Bunge inapaswa Wabunge wote tuungane tukujibishe, kwanini umekubali kuleta vitu ambavyo haviwezi kutekelezwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mkataba huu ulikuwa ni mbovu mno. Mkataba huu ukiusoma katika clause ya 14 unaiondoa *SUMATRA* katika kuisimamia *RITES*. Mkataba huu unamwondoa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kufuatili raslimali na mali za kampuni za *RITES*. Sasa nani anaingia mikataba hii, tutafika wapi Tanzania kwa kuingia mikataba ya namna hii? Hapa nina barua ya *demand notice* ambayo *TRL* waliwaandikia hawa *RAHCO*, tarehe 8 Septemba, 2009 kueleza kwamba wamevunja mkataba huu na kwamba wanadai walipwe *compensation*.

Hawa hawa wa *RITES* wanataka wadai *compensation* wakati wao tumewa... kwanza cha kuchangaza ni kwamba tulikuwa na *share* asilimia 49 wao *wana-share* asilimia 51 wakati wamekuta mabehewa tunayo ya kutosha, tuna raslimali za kutosha halafu sisi tunakuwa na *share* ndogo, wao wanakuwa na *share* kubwa. Hii ni mikataba ya namna gani? Siyo mikataba hii ambayo ilikuwa na mambo ya rushwa hii! Waziri aliyeingia mikataba huu kwanini hakujuzulu? Kwa sababu kama hawezi kufikia hatua ya kujuzulu watu waliofanya vitu hivi si tutaendelea? Tena nawashauri Waheshimiwa Wabunge tusiwe tunawaoneea huruma Mawaziri. Tusiwaonee huruma kabisa, wamepokea mzigo huu wakijua wana uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nchi hii kutokana na kutujibishana, watu wanaanza kuona huruma, ooh, tukimwajibisha Waziri aliyeshindwa kusimamia, aliyeingia mikataba huu itakuwaje? Tutakuwa tumempunguzia ulaji! Hapa hatuna mambo ya ulaji! Hapa tumekupa Wizara, simamia. Huwezi, jiuzulu aje mtu mwingine. Hata wakijuzulu kumi, sisi hatuna shida, wajuzulu tu, kwamba tumeomba hela hatujapewa, tokeni, mpaka tupate anayeweza, mbunifu wa kubuni vitu.

Kwa hiyo, kwa mikataba hii mibovu na *demand notice* hizi, mimi siwezi kuunga mkono hoja hii kwa sababu reli haiwezi ikarudi katika kiwango ambacho kinatakiwa. Reli hii tunayoiona imejengwa na Mjerumani mwaka 1905 imefika Tabora mwaka 1914 imefika Kigoma mwaka 1914. Sasa cha kushangaza ni kwamba leo wanakuja kwa mfano na hoja kwamba reli iunganishwe kutoka Isaka kwenda Burundi wakati umbali wa kutoka Isaka kwenda Burundi ni mara mbili ya umbali kutoka Kigoma kwenda Burundi. Kwa hiyo, bado ni matumizi ambayo siyo sahihi kwa raslimali zetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo napenda kuzungumza kutokana na muda ni suala la wafanyakazi. Baada ya mikataba hii kuingiwa mwaka 2007 wafanyakazi wengi walistaafishwa. Baada ya kustaafishwa, wengi wao walilipwa pesa, wale waliondelea wamepata matatizo makubwa sana kutokana na Shirika hili kuingia mikataba na kampuni hii mbovu ya *RITES*.

Kwa mfano, kuna mmoja amefanya kazi miaka 40, amelipwa shilingi milioni mbili baada ya kustaafu. Hicho ni kiwango gani? Tunaomba wafanyakazi hawa wafanyiwe kama wale wa *NBC* na Mashirika yaliyobinafishwa kana *NMB*. Baada ya matatizo haya kutokea, walilipwa vizuri. Leo wafanyakazi wanagoma, kinachowafanya wafanyakazi wagome kwenye Shirika hili la Reli ni kwa sababu ya masuala ya kifuta jasho. Leo hawajui hatma yao ni nini, wanaendelea kugoma. Naomba Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi tukakubaliana na mambo ya namna hii. Wafanyakazi wanafanya kazi, Serikali inaingia mikataba mibovu, inawatoa *SUMATRA*, inawatoa *CAG*, bado tunawapa mabehewa mengi. Ilifikia sehemu kampuni hii ya *RITES* ikastopisha mabehewa yake ikidai fidia, bado tunadai tulipwe.

Nataka pia Waziri wakati anatoa majibu yake, njue kabisa kwamba baada ya mkataba huu kuvunjika: Je, *RITES* tutawalipa pesa yoyote? Kama tutawalipa, ni kiasi gani ili tujué hapa? Isiwe kuna pesa nyingi tunataka tuwalipe hawa kwa sababu wameandika *demand notice* ya kudai pesa, tuwalipe pesa zetu wakati wao ndiyo wametusababishia hasara na wakati mkataba tulioingia japo ulikuwa na makosa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama mkataba ulikuwa na makosa, aliyeuingia pia lazima awajibishwe. Lakini pia wakati mabehewa mengi yameshindwa kufanya kazi, wafanyakazi Watanzania ndio ambao walifanya juhudzi za kufufua mabehewa hata haya mnayoyaona. Sasa leo kwanini wafanyakazi hawa hatujalali?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna mambo ya kusikitisha sana na mimi ningewashauri Wabunge wenzangu, najua bado hamjkwenda kwenye vikao vya *part caucus* na nini, naomba msibadilike. Hizi pesa zilizoletwa bado ni kidogo, haziwezi zikatatua tatizo la reli, haziwezi zikatatua matatizo ya Bandari, haziwezi na sisi tunataka tuwe na bandari ambazo ni makini. Tunataka tuwe na reli imara. Leo mngekuwa mnazungumza reli ya Kigoma ipite Kasulu, Kibondo iende mpaka Burundi ije iunganishe na hii ya Nyakanazi ili kuinua uchumi wa kanda ile, Kigoma ingekuwa kama Dubai.

Mheshimiwa Spika, naomba nisiunge mkono hoja hii. (*Makofii*)

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani petu leo. Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya leo ya kuwepo hapa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nianze kuchangia hoja yetu iliyopo hapa leo. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama walivyompongeza wenzangu kwamba kitendo cha kuongeza bajeti ya shilingi bilioni 95 kwa kweli kimewafurahisha wananchi na sisi sote tulipo hapa leo na kwa kweli mawazo yetu sasa hivi yamebadilika. Kwa hiyo, tunamshukuru Waziri Mkuu kwa kitendo hicho.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia hoja ilipo mezani petu leo. Suala la *TAZARA*, ATC, Reli ya Kati, *UDA* wenzangu wameshasema vya kutosha na Serikali ni siku nafikiri wameelewa, watajipanga vizuri na kwa kuzingatia kwamba Wizara hii ni mpya, basi naona wakikaa pamoja wanaweza kuleta mabadiliko fulani kama alivyochochuka hatua Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, kwa hayo wenzangu wamesema kikamilifu na siwezi kuongeza maana nitatoa utamu.

Mheshimiwa Spika, nije moja kwa moja sasa katika mchango wangu. Mimi nitachangia suala la bandari, reli na viwanja vya ndege. Nikianza na bandari, Tanzania tumebahatika kuwa na bandari halali ukiacha zile za panya, bandari halali 18. Ukiwa katika ukanda wa Pwani kuna bandari kumi; Ziwa Victoria kuna Bandari ya Musoma, Mwanza na Bukoba; Ziwa Tanganyika kuna Ujiji na Kigoma; Ziwa Nyasa *Mbaba Bay* Manda na Nyasa, nane hizo. Huu kwa kweli ni uchumi mkubwa Tanzania.

Uchumi huu ungeweza kuzalisha kiasi cha kutosha kwamba sisi Tanzania hatungekuwa na matatizo ya usafiri. Ndiyo maana katika vikao vile vya *SADC Mtwara Corridor* mwaka 1997 walikaa wakatafakari wakasema kwamba Tanzania kuna bandari na bandari hizi zinaweza kutusaidia sisi na nchi za nje zikiwemo Malawi, Zimbabwe, Zambia, Msumbiji na Afrika Kusini. Zingeweza kusaidia kwa makini kabisa bila wasiwasi, kwa sababu mpaka sasa watu wa Malawi wanallilia Bandari ya Mtwara na ukienda Mtwara utakuta *schedule* zao pale. Mtwara kuna majengo yao katika Bandari ya Mtwara, lakini sasa wanaipataje?

Kwa sababu kutoka Malawi mpaka Mtwara ni kilomita 948 lakini kutoka Malawi mpaka Dar es Salaam ni karibu kilomita zaidi ya 1600. Kwa hiyo mpaka sasa watu wa Malawi wanallilia bandari ya Mtwara lakini wataipataje?

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara baada ya kuongeza bajeti hii watusaidie kufufua bandari ya Mtwara. Bandari ya Mtwara ina kina kirefu, wanasema kwenda chini ni mita kumi kama kunakuwa na maji kupwa (*low tide*), maji yakijaa kunakuwa na mita kumi na nne hadi kumi na tano kina kwenda chini katika bandari ya Mtwara, katika *high tide*. Bandari ya Mtwara ina sifa zote, unaweza kuweka kontena elfu moja katika bandari ile. Sasa hivi ina eneo kubwa kabisa, ekari 1,700 tungeweza kuendelea kufanya biashara na nchi za *SADC* lakini tunafufuaje bandari ya Mtwara, Serikali inatusaidiaje?

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Mtwara ina eneo ekari 1,700 ambalo ni nchi kavu vilevile kutoka pale kwenda mbele zaidi, unaweza ukapanga mambo mengine. Bandari ya Mtwara unaweza kuweka meli kubwa mbili kwenye gati, unaweza kuweka meli sita za kimataifa. Sasa katika nyongeza hii ya pesa tunaomba Serikali itusaidie kupanua bandari ya Mtwara kwa sababu sasa hivi Mtwara kuna mambo mengi, kuna gesi, kuna *gypsum* kuna mambo chungu nzima ambayo bandari ya Mtwara ingeweza kubeba uzito huo.

Mheshimiwa Spika, bandari ya Lindi ni bandari kongwe ambayo ilianza tangu wakati wa ukoloni wa Ujerumani, ni bandari ambayo ilikuwa inawasaidia wananchi wa Mkoa wa Lindi kusafirisha bidhaa zao ikiwa ni pamoja na mbao, korosho, ufuta na kubeba watu. Wakoloni Wajerumani walijenga kwa makusudi ya kusafirisha madini na vilevile walitumia bandari ya Lindi kusafirisha vito mbalimbali kutoka Mkoa wa Lindi, kwa mfano waliweza kubeba *dinosaur* mwenye kilo themanini kutoka Tanzania, Lindi kumpeleka Ujerumani, walitumia bandari ya Lindi. Kwa hiyo, meli kubwa zilikuwa zinaweka pale nanga, lakini sasa bandari ya Lindi imejaa mchanga, bandari ya Lindi haifai, bandari ya Lindi sasa hivi inamomonyoka wanasema ina bomokabomoka, haina thamani yoyote na ndiyo maana asilimia sitini ya wananchi wa Lindi na Mtwara wanakwenda Dar es Salaam kwenda kufanya biashara ndogondogo kwa sababu bandari zetu zimekufa. Kwa hiyo, tunaomba katika eneo hili, tusaidiwe ili bandari ya Lindi iweze kufanya kazi.

Mhehsimiwa Spika, sasa hivi mfumuko wa bei umekuwa mkubwa, vitu ni ghali kutohana na kwamba usafiri wa bandari, meli hazipo, watu wanabeba bidhaa zao kwenye magari, vitu vichache ambavyo haviwezi kukidhi haja. Kwa hiyo, mfumuko wa bei unakuwa mrefu na watu Dar es Salaam wanazidi kuwa wengi kwa sababu hata sukari kilo kumi, hata mzigzo mdogo ni lazima mtu wa Lindi atoke Lindi aende Dar es Salaam, kwa hiyo Dar es Salaam kunakuwa watu wengi, tunaomba bandari ya Lindi tusaidiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari ya Kilwa, Mtwara *Corridor* walitaka kuendeleza vilevile Bandari ya Kilwa kwa sababu wanajua Kilwa ni Mji Mkongwe. Bandari ya Kilwa ni kati ya Bandari kubwa tano za Afrika Mashariki, enzi ya AD 900-1700 bandari ya Kilwa ilikuwepo. Kulikuwa na bandari ya Lamu, bandari ya Mogadishu, bandari ya Mombasa hizo zote za Kenya, kwa Tanzania ilikuwa Kilwa na Sofala ya Msambiji. Bandari hizo kuu tano Afrika Mashariki ni bandari kongwe zenye sifa ya pekee tangu enzi ya AD 900-1700.

Mheshimiwa Spika, katika bandari ya Kilwa, kuna utalii mwingu kabisa, kuna magofu ya Waarabu pale; watu wanakuja kwenye utalii wanatumia bandari ile, vita ya majimaji ilianzia Kilwa Kinjekitile, watu wanakuja pale. Kuna mapango kati ya mapango 21 ya Tanzania, pango la Kilwa, linaitwa pango la Mang'omes ni pango kuu katika Afrika, lilitumika wakati wa vita. Bandari ya Kilwa nayo muiangalie tusiachie hapo, ina manufaa yake, utalii, biashara, uchumi, mawasiliano na kadhalika, naomba tusaidiwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia masuala ya bandari, sasa naomba nizungumzie masuala ya reli, Mtwara *Corridor* walitaka kuendeleza reli ambayo inatoka Mtwara mpaka Mchuchuma, hii reli imeishiaje? Kwa sababu njia rahisi ya kutoa madini ya makaa ya mawe Mchuchuma, Chuma na Liganga, ni Mtwara. Unajenga *rail* mpya mpaka Mtwara kwa sababu Mtwara kuna bandari ambayo itabeba ile mizigo kupeleka mbele ya safari, naomba vilevile tuiangalle reli hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile reli hizi zamani tulipokuwa tunasoma tunasema reli ya Tanga, reli ya Dar es Salaam, Dodoma na kuendelea tulikuwa tunapanda wakati tunasoma shule, lakini pia kulikuwa na reli ambayo inatoka Mtwara kuja Mingoyo kuja Mtama mpaka Nachingwea wakati huo ilikuwa inabeba karanga na abiria. Hii reli *iling'olewa* Kusini, reli hii inaleta mazao mengi, tunaomba Serikali itusaidie kuiangalia upya reli hii kwa sababu bado tunaihitaji, mizigo ni mingi, ufuta, korosho. Sasa hivi kumeibuka suala la *gypsum* na *gypsum* ni mawe makubwa huwezi kuyapitisha katika lori kutoka Mkoa wa Lindi kwenda Dar es Salaam inabidi uingize aidha kwenye treni au uingize kwenye meli, kwa hiyo, tunaomba reli hii iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kusema ni suala la *airport*, Mkoa wa Lindi kuna *airport* kubwa kabisa. *Airport* ya Lindi ilijengwa wakati wa ukoloni mara tu baada ya vita ya pili, Mwingereza alipoingia Tanzania akajenga *airport* Lindi, *airport* ya Lindi ina *runway* sita, *airport* ya Lindi ina ukubwa wa pekee, iliweza kutumika katika ukombozi wa Afrika ya Kusini na Msambiji. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itusaidie. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge unaunga mkono hoja au? (*Kicheko*)

Sasa nitamwita Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza na Mheshimiwa Abdallah Mtutura naye ajiandaye na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi pia ajiandaye.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nami naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuamsha salama baada ya mapambano ya hoja humu ndani jana, watu hatukuamka na presha tumekuja vizuri, tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba sitaunga mkono hoja hii na naomba Wabunge tuwe na msimamo kama wa jana.

WABUNGE FULANI: Aaaaaaaah!

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Haya ni mawazo yangu.

SPIKA: Tatizo lako unajibu watu ambao hawakuhusu, wewe endelea tu.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, sawa. Mimi naomba Kambi ya Upinzani twende na mawazo ya Kiongozi wetu ndani ya Bunge kwamba sisi hatuwezi kula matapishi yetu, tunasema hatuungi mkono hoja na hatuungi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninazo sababu za msingi, leo hii Waziri Mkuu amekuja asubuhi na taarifa nzuri kwamba Serikali imekubali kuongeza shilingi bilioni 95 zilizoombwa na Kamati inayohusika na Wizara hii lakini mimi nimeona Waziri Mkuu amefanya hivyo ili kupooza munkari ya Wabunge ili tupitishe bajeti kuwaondolea fedheha Serikali kama tulivyofanya katika Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, ukifanya hesabu ndogo tena za haraka, Wizara hii bajeti iliyopewa katika bajeti hii ni shilingi bilioni 167.9 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, naomba uongeze hiyo shilingi bilioni 95 utapata shilingi bilioni 252.9 *roughly*. Katika hizo za maendeleo, kwanza Shirika hili ndege zake zinadaiwa shilingi bilioni 31 madeni ya matengenezo, Shirika hili linadaiwa na *RITES* zaidi ya shilingi bilioni 63.7 ikiwemo na yale malipo ya kuvunja mkataba lakini pia kuna madeni ya wastaafu ambayo ni shilingi bilioni 21.5. Mimi nimejaribu kufanya hesabu hapa nikaona ukizijumlisha hizo unapata shilingi bilioni 162.2 ukitoa katika hiyo idadi ya kwanza utabaki na shilingi bilioni 136.5.

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza kama siyo Waziri Mkuu kuja hapa kutulambisha pipi mdomoni ili tuweze kulegea, tuweze kupitisha hii bajeti, hizi shilingi bilioni 130.5 zitafanya nini? Zitatengeneza mabehewa, zitanunua ndege, zitatengeneza meli yetu ya MV. Victoria ambayo sasa imekuwa garasha, zitafanya nini kutookana na kilio cha Wabunge hapa? Ndiyo maana nasema Waziri Mkuu amekuja na hiyo taarifa ili kututuliza Wabunge ili tuanze kuamua mengineyo, ndiyo maana nilikuwa nasema kwamba kwa pamoja tungesimamia msimamo uleule, hii pesa haitoshi na hatutegemei mabadiliko yoyote katika kurekebisha miundombinu hii ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo na kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Waziri aliandika barua ya kuomba pesa kwa Waziri Mkuu kwa barua yake ya tarehe 27 April, 2011 yenye kumb. CA.98/386/1 na alieleza vizuri kwamba ili Shirika hili liweze kufanya vizuri, kwamba ili tuweze kuendeleza reli, reli peke yake amelombea hela ya

maendeleo shilingi bilioni 221.6. Sasa leo Wabunge tunasema kwamba kwa vile tumeongezewa shilingi bilioni 95 sasa tuamue vinginevyo. Mimi naona bado msimamo uwe palepale. Bado hakuna pesa ya kutosha kuweza kurekebisha miundombinu hii.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida sasa Serikali kuwa na ubabe na kushindwa kutusikiliza, mimi nimeshangaa leo ni chanzo kipi ambacho Serikali imeweza kupata shilingi bilioni 95. Jana ilikuja hoja hapa kwamba kuna vifungu viliongezwa katika Wizara ya Ujenzi, sawa ilikuwa imeshapitishwa kwenye bajeti sikatai, lakini hatuwezi kushindwa sisi Wabunge kutoa mawazo, kama kuna kifungu 4168 ambacho kilikuwa na pesa shilingi bilioni 358 hazina kazi, zinangojea watu waje, lakini mimi naamini kwamba bajeti inapopitishwa ni kwamba watu wameshajua watapewa pesa aidha kwa wafadhili, wanatuonesha katika randama, wakichomeka vifungu vya namna hii pesa hiyo tulikuwa tuna-*suggest* kwa nini isitolewe ikaenda kwa Waziri wa Uchukuzi kule, tukawa na uhakika wa kutengeneza meli, reli na mambo mengine? Tunajua imepita lakini yalikuwa ni mawazo ya Wabunge na mawazo hayakuwa na madhara yoyote, *was just suggestions (Makof)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu mikataba ya *RITES*. Naomba niongelee kuhusu reli kwa sababu watu wa Mkoa wetu wa Kagera tumeathirika sana kwa kuharibika kwa miundombinu hii, ndiyo maana kwa niaba ya watu wa Mkoa wa Kagera, kwanza mimi napenda kulaani kabisa watu waliosaini mkataba ule, walaaniwe kabisa na walegee. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mikataba hii imetuua na kutuumiza sisi wananchi wa Mkoa wa Kagera. Sasa hivi kutoka Bukoba Mjini ukiacha Karagwe, Ngara kuja Dar es Salaam ni zaidi ya shilingi elfu sitini.

SPIKA: Walegee namna gani? Tuendelee. (*Kicheko*)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, kama watu wanaumia na watu wanasaini mikataba ya namna hii ni lazima tuwaombee vibaya. Watu wa Kagera wanaumia, maisha yamekuwa magumu kutokana na usafirishaji. Nilichangia wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu nikasema nawasubiri, nashukuru Mungu amenipa nafasi hii, nijaribu kutetea watu wa Mkoa wangu ambaao kwao kwa kweli gharama za kuendesha maisha zimekuwa kubwa mno. Huwezi kujenga nyumba, mahitaji mengine, bidhaa zote zinasafirishwa kupitia njia ya barabara, gharama inakuwa karibu mara mbili zaidi ya bei ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, reli imekufa, meli yetu ya mizigo nimeisoma humu eti imeenda Kampala, MV Umoja ambayo ilikuwa inabeba mabehewa mengi. Serikali hii imeikimbiza, imeipelea Kampala sijui wapi, sijui inafanya kitu gani, imetufanya sisi watu wa Kagera tuumie. Naomba Waziri utuambie hiyo meli iko wapi, nilikupania wakati ule, utueleze kwa nini imetoka Kagera na imekwenda kuhudumia Waganda?

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuona ni jinsi gani Serikali hii inavyoharibu miundombinu, nenda pale Mwanza South, Mama Maria Hewa amesema jana kwamba mabehewa na eneo lote lile limeota kichaka kabisa mpaka mabehewa yamejaa majani na kadhalika. Sijui kama watu waliopo Serikalini wanaenda kukagua hii miundombinu na kuona jinsi gani mikataba hii inavyotufikisha mahali hapa.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye meli waliyotuonesha jana hapa, MV Victoria siyo meli hiyo ni uozo. Juzi hapa nimeenda kupakia gari langu dogo kwenda Mwanza, nilikuwa na safari ya dharura wakaniambia wanapakia moja na hii ni gari dogo tu. Meli ile haipakii mizigo sasa hivi, inapakia abiria nao kwa wasiwasi, leo mnatuambia kwamba tuna meli, hatuna meli katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, utashangaa Ziwa kubwa namna ile lina meli moja, meli zote, MV Serengeti, MV Kreliusi, MV Bukoba ilizama, hakuna kitu sasa hivi katika Ziwa lile. Watu wanalamizika sasa hivi kutumia usafiri wa barabara ambaao ni *risk* kwa ajali mnazoziona, ni mara chache meli kuzama, ni mara chache treni kugonga. Kwa hiyo, huu ni usafiri wa uhakika na wa bei nafuu kwa ajili ya walala hoi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia bajeti nzima hii sioni kama kweli kuna dhamira yoyote ile ya kuweza kuinua Shirika letu. Tunampa mzigo Waziri, tunasema Waziri ajiuzulu na yeye ni mgeni lakini kwa kweli wamekuingiza mkenge ndugu yangu, watu tupo hapa tunakusulubu ni haki yetu kwa sababu umeshikilia Wizara lakini wale waliokuwepo nyuma wawajibishwe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi kitu kinachonipa tabu ni jinsi gani watu wanatuharibia mambo halafu tunakaa kimya. Mheshimiwa Lembeli amesema Watendaji wanatucheka, wanatuona kama ni *the comedy* hapa, wanatu-joke tu. Tukishasema, tunapiga kelele wenzetu wanacheka wanakwenda kutuibia, wanaenda kuharibu mashirika na sisi tunakaa kimya. Kipindi cha Awamu ya Kwanza, Mwalimu Nyerere ulikuwa ukifanya hivyo anakufukiza hata nauli hakupi, unarudi nyumbani kwenu huko unaenda kuadhirika kama uliyotaka Watanzania waadhirike na ikibidi anakufuata kukuflisi, sasa leo hii mpaka hata mwezi jana nilisikia *Major General* Sarakikya alikuwa anashangaa utajiri wa Watumishi wa Umma katika nchi yetu. Mimi sisemi kwamba watu waishi maisha ya oyoy hapana, lakini kwa kweli tuwe wazalendo maana tamaa sasa zimekuwa tama, tumelifikisha Taifa letu hapa, hakuna uzalendo, sasa hivi hakuna mtu ambaye anataka kufanya watu kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sikubaliani na hoja hii, naomba Kambi ya Upinzani tusikubaliane wacha wengine wakubali, lakini najua hata wa CCM kuna wengine hapa wamekaakaa tu labda kuogopa Kamati za Siasa, lakini kwa kweli hatujaisaidia Wizara hii. Tuendelee na watafute fedha maana inavyoonekana kama hizi shilingi bilioni 95 zipozipo na nyagine wana vifungu labda. Mimi naona wana mahali ambapo wameweka fedha, kama shilingi bilioni 95 zinaweza kupatikana kwa Wabunge ku-*riot* ina maana tutakuwa tuna-*riot* kila siku wanaongeza vifungu, basi uwe ndio mtindo tufike hapa kila siku tugangamale, tuseme ovyo, tuwaambie Mawaziri wanyongwe ndio muende kuleta fedha. Zipo! Kifungu hiki kinatoka wapi, kuna mapato gani, kuna vyanzo gani huku vilivyofichwafichwa, vipo waongeze kama jinsi Waziri alivyosema wampe shilingi bilioni 221, ameeleza vizuri ndani ya barua yake mimi nimeisoma hapa kwamba jamani hiki na hiki siwezi kuisoma yote, kwa hiyo, tungempa nafasi.

SPIKA: Lakini hukusema mwaka huu alikuwa ameomba ngapi katika hizo.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mwaka huu katika hizo za reli yeye alikuwa ameomba shilingi bilioni 221.65 kwa ajili ya reli tu, yaani TRL, TAZARA, RAHCO jumla alikuwa ameomba hiyo peke yake. Kwa hiyo, ina maana alikuwa anajua sisi tungepona kama angepewa hiyo hela, sisi Kagera huko tusingekuja kukodolea macho. Tungejua kwamba sasa hapa ndio tunapona, watu wetu wanaishi vizuri na hata reli ya kutoka Tabora kwenda Mwanza sijui wamepeleka wapi? Hakuna! Sasa tunashangaa kama watu wanaweza kutufanya kazi namna hii na sisi Wabunge tunakaa hapa tunanyong'onyea, hatwezi kunyong'onyea tutaendelea kutounga mkono hoja hii ili waweze kutuongeza fedha na wahakikisha miundombinu hii imeimarika.

Mheshimiwa Spika, mimi nimekataa kusema mambo ya ndege kwa sababu ndege huko Kagera tunapanda *Precision Air*, walianza na ndege moja, wale ni wafanyabiashara, sijui Watanzania hawajui kufanya biashara, mimi sielewi, ndege moja *Precision Air*, leo wana *Boeing*, sasa tuna nyagine inaitwa 540 ndio tunapanda siku hizi tena wamepunguza na bei. Watu wa Kenya walivyoona 540 imekuja wameongeza na ndege nyagine inaitwa *East African Communications* ukifika pale wanakupa hiyo, wanakubembeleza ukienda Watanzania tunakodoa macho, tunatoa fedha zetu, tunawaajirisha watu wa Kenya mambo yote yanakuwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kwa kweli *consultation* ifanywe, Wabunge tuendelee kushikamana kuhusu hili, hakuna sababu ya kunyong'onyea kwa sababu Waziri Mkuu ametuletea pipi kutulambisha mdomoni tujilambelambe hapa, hapana na yeye tumkatalie, tunamheshimu, lakini tumkatalie kwamba kwa hili hapana tunataka ndege, tunataka ubaguzi ule ambaa umesemwa jana kwa wafanyakazi wa TAZARA uishe, siwezi kurudia hakujibu. Mambo machafu yaliyosemwa kule *International Airport* ya *Kilimanjaro*, hatukupata majibu, sasa tutaunga mkono vipi, Waziri Mkuu asituwekee pipi mdomoni na yeye arudi nyuma aangalie kwamba hapa hajatenda haki.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niishie hapo kwa kweli sitaunga mkono hoja, ahsante kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, kwanza ni-*declare interest*, mimi ni mmoja wa Wakurugenzi katika Bodi inayosimamia maendeleo ya bandari Tanzania. Vilevile ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nitoe pongezi kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, kwa usikivu wake wa hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na dhana kwamba kila jambo lifanywe mara moja kufumba na kufumbua kama anavyofanya Mwenyezi Mungu, hili haliwezekani. Serikali hii imepangiwa kuitumikia nchi yetu kwa miaka mitano. Tunapozungumzia maendeleo ya reli au bandari na usafiri wa anga, tunatarajia kwamba kima cha fedha ambacho kimepangwa basi kila mwaka Kitakuwa kinapangwa ili kuweza kutekeleza yale ambayo tumekusudia kuyafanya. Hatuwezi kuifufua reli yetu ambayo iko katika hali mbaya katika kipindi cha mwaka mmoja, hilo haliwezekani. Cha msingi tuendelee kuisii Serikali iendelee kupanga fedha za kutosha ili reli yetu iweze kufufuliwa na iweze kufanyakazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unapotaka kumsaidia mtu mwenye njaa kali huwezi kuanza kumpikia ugali mgumu, unampikia uji mwepesi akishakunywa anatalia baadaye ndipo umpikie ugali tena ugali laini siyo ugali wa watani zangu Wasukuma, kesho yake ndipo umpikie ugali mgumu. Hali ya reli iliyopo sasa hivi na *management* yetu tuliyonayo, nadhani busara iliyotumika na Serikali mimi naiunga mkono, zitolewe kiasi cha fedha tuanze kuifufua hatua kwa hatua. Leo ninaambiwa kwamba fedha zilizotengwa ni kidogo sana, jana tumezungumzia habari za barabara, juzi tumezungumzia habari za huduma za afya, bajeti ya maji nayo inakuja, Wabunge hawahawa watasema nayo fedha hazitoshi, upande wa Kazi fedha hazitoshi, tukazitoe wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema fedha zilizotengwa hazitoshi lakini bado tuisii Serikali iendelee kuangalia uwezekano wa kuongeza fedha mwaka hadi mwaka. Huyu ni mgonjwa tunayemfufua, cha msingi ni kwamba fedha zilizopo ziongezwe mwaka hadi mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumbani kwangu tuna bibi yetu mmoja anaitwa bibi Aliucha. Bibi huyu siku moja tumemtembelea alikuwa amepika chungu kimoja lakini wajukuu zake kila mmoja alikuwa na matarajio tofauti mmoja anasema anataka chai, mwingine anataka uji, mwingine anataka ugali lakini akasema wote nitawahudumia kwa chungu hikihiki kimoja. Maji yalipochemka mwenye chai akatengewa chai yake, maji yale yakakorogwa uji, ulipochemka mwenye uji akatoa, akapewa uji wake lakini maji ya mwisho yenyе uji yakapikwa ugali. Nataka kuisii Serikali kwamba mandhali tuna fedha kidogo basi tuzielekeze pale ambapo tutapata tija ya kutosha. Naomba nimuunge mkono sana tena kwa moyo thabitii Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa yale aliyoyazungumza yote yanastahili kuchukuliwa na Serikali.

(*Waziri alikatisha kati ya Kiti na Mzungumzaji*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri naomba ufuate utaratibu. Endelea alikuwa ananizuia nisikuone.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, yale mazungumzo aliyozungumza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, nayaunga mkono na nashangaa kwa nini huyu hajajinga na CCM mpaka sasa hivi kwa sababu mawazo yake ni ya Ki-CCM na huyu inabidi tumchukue, tumrudishe huku kundini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tuimarishe Bandari ya Dar es Salaam, chungu hiki kimoja kama tutakitumia vizuri, tukaimarisha Bandari ya Dar es Salaam, tusahau Mtwara mimi natoka Kanda ya Kusini, tuachane na Mtwara, tuachane na Tanga kwa sasa hivi mandhali sungura huyu ni mdogo tumuelekeze kwenye Bandari ya Dar es Salaam, tuelekeze kwenye ufufuaji na upanuaji wa *gage* ya Reli ya Kati vilevile tuimarishe Bandari ya Mwanza. Kasungura haka katuwezesha kuzalisha zaidi

ili tupate nguvu ya kujenga Bandari ya Tanga na Mtwara lakini leo kasungura haki tukisema tutakawanye baada ya miaka mitano hatutakuwa na kitu cha kueleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba Bandari ya Dar es Salaam ndio bandari pekee inayotoa faida sasa hivi. Katika Mashirika ya Umma, ni Shirika la Bandari peke yake ndilo linalotoa faida kubwa kuweza kuijendesha na kuwekeza. Basi ndugu zangu, watani zangu Wangoni huwa wanasema kwamba weka fedha mahali penye fedha. Naomba Serikali iwekeze sana kwenye bandari, iwekeze sana kwenye reli itatuwezesha kupata nguvu ya kuweza kufanya mambo mengine. Sasa hivi tukiwa na fikra kwamba fedha hizihizi tunakwenda Mwambani Tanga, fedha hizihizi twende sijui Kigoma baada ya miaka mitano tutakuwa hatuna cha kuwaeleza Watanzania kwamba tumefanya nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kama sitawapongeza wafanyakazi wote wa Bandari Tanzania kwa jinsi wanavyochapa kazi mpaka kuwa Shirika lenye nguvu linalotengeneza faida kubwa kuliko mashirika mengine yoyote Tanzania. Wafanyakazi hawa wanaongozwa na menejimenti, vilevile naomba nitoe pongezi kubwa sana kwa menejimenti ya Mamlaka ya Bandari chini ya Kiongozi wao, Mkurugenzi Mkuu Ndugu Mgawe. Bahati mbaya Ndugu Mgawe amebakiza sijui miaka miwili, mitatu kustaafu, sasa watu wazuri kama hawa badala ya kuwa na miaka midogo sasa hivi wanajandaa kustaafu maskini ya Mungu. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niwapongeze sana Bodi ya Bandari, mimi nikiwa mmojawapo, ndio tulioisimamia bandari mpaka inatengeneza faida kiasi hicho. Nimwombe tu Mheshimiwa Waziri, kwamba kuna baadhi ya mambo tumekuletea yenye lengo la kuongeza ufanisi katika bandari, yamekaa ofisini kwako muda mrefu sana kutoka enzi ya Mheshimiwa Kawambwa na wewe bado umeyarithi. Naomba uyatolee maamuzi aidha hapana au ndiyo, kuliko kukaa nayo, kwa kweli utavunja moyo katika utendaji wa Shirika letu la Bandari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nimuunge mkono Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kuhusu *ATCL*, tumelaumu hapa menejimenti, Bodi ya *ATCL* lakini hatujaangalia upande wa Serikali iliweza ku-treat namna gani Shirika hill? *ATCL*, walikuwa na Mpango Kazi wao (*Business Plan*) wa miaka mitano, Serikali imeshindwa kuisimamia/kuiwezesha *ATCL* ikaweza kutekeleza mpango ule. Leo moto ulipuke halafu tipeleke kikombe kimjakimoja kuzima moto ule, hauwezi kuzimika. Kwa hiyo, naomba kama kweli tumedhamiria kufufua *ATCL* basi mpango kazi utakaoandalila na hiyo *management* itakayoandalila tuisimamie na tuiwezeshe kikamilifu. Tukisema tipeleke fedha kidogokidogo zitaungua, tutapeleka zingine zitaungua na hakuna chochote ambacho kitawezu kukamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mpango kazi ni jambo muhimu sana ili Shirika liweze kuendelea vizuri. Tumesifia hapa *Business Plan* za wenzetu wa *Precision* zinakwenda vizuri lakini wao wanawekeza. Sasa utakuwa na Mpango Kazi ambao huwekezi fedha hauwezi kufanya kazi yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba niwasih wana CCM wenzangu ambao wako humu ndani ya nyumba tuunge mkono hoja hii kwa sababu mwelekeo wa Serikali, Serikali sikivu, ni nzuri na naamini kwa mwelekeo huu tulionyeshwa hapa asubuhi bajeti hii Wabunge wa CCM na wa Upinzani wataipitisha kwa hoja ya nguvu moja, nakushukuru sana. (*Makof*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nipaye kuchangia kidogo kwenye Wizara hii ya Uchukuzi japokuwa wenzangu waliotangulia wametandika sana tutao kotaokota tu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kuanza nitoe ushuhuda wangu kwa marehemu, nilimfahamu marehemu kabla hata hajaanza kuumwa, kwa kupata huduma zake wakati nasoma nikimaanisha *ATC*. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nillitumia *ATC* wakati nasoma Mtwara kwenye miaka 1990, *Boeing*, ilikuwa na huduma nzuri sana, *Fokker* ilikuwa na huduma nzuri, walikuwa wanatoa chakula lakini baadaye nikamaliza shule nikawa kwenye shughuli zangu za sanaa nasafiri Mtwara, Mwanza nikawa nazitumia ndege zilezile mara nikaona hawatoi tena chakula, wanatoa tu *sandwiches*,

mikate baadaye ikafuata mikate bila *blue band* nikaona sasa hapa kuna tatizo linakwenda kutokea kwa vielelezo vidogo tu. Mara nikaona wanatoa soda tu tena kwenye *glass* siyo kopo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, watu wengi wanajaribu kutetea, wanajaribu kusema *ATC* haikuwezeshwa na vitu kama hivyo. Mwaka 1977 *ATC* ilikuwa ina ndege mpya 11, ultaka iwezeshwe vipi? Miaka 34 iliyopita ilikuwa na ndege mpya 11 leo hii hakuna ndege hata moja, ni nani yuko jela na atatoka lini kwa kosa hilo? Nani amekwenda jela kwa kuhujumu mafanikio haya ya Taifa ya miaka 34 iliyopita ambapo tulikuwa na ndege 11, *brand new, Boeing* mbili 737, aina ile ya ndege mpaka nchi za nje sasa hivi wanatumia, Marekani wanatumia, wanachofanya kwa sababu ya utalaam wangu mdogo, nachojua ndege haizeeki bodi sana inazeeka injini, injini ndio ina masaa. Kwa hiyo, inakwenda injini ikifika masaa fulani wanavua injini wanabadilisha wanaweka injini mpya au injini yenye masaa ya kutosha ndege inaendelea kufanya kazi lakini sasa sisi hatuyaoni hata mabati labda haya mabati yametengenezewa majiko au yameuzwa kwenye chuma chakavu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ndege 11 miaka 34 iliyopita leo hii hatuna ndege tuna majengo, *asset*, tuna Wakurugenzi, tuna mabosi na kila kitu halafu hakuna mtu yuko jela. Mkurugenzi wa *ATC* huyu aliyepti, Mheshimiwa Mkapa, alimtoa kwenye *PPF* alimpiga chini, tunakuja kusikia Rais Kikwete kamchagua kuwa Mkurugenzi wa *ATC* wakati ambapo *ATC* ilikuwa inahitaji mtendaji makini kabisa ambaye hana doa huko nyuma, huyu Ndugu Mataka alikuwa na sifa gani ya ziada mpaka akapelekwa *ATC* kwenda kuimaliza/kuiua kabisa? Maana yeze nadhani angalau hata alikuta ndege za kukodi lakini wamempa Ukurugenzi kwa kadri inavyompendezza Rais, amekwenda kumaliza kabisa suala la *ATC*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wanasema tunasifia makampuni kama *Precision, Precision* sijui walianza na ndege ya watu wanenye lakini angalia leo walipofika tena sijui kama huyo mwanzilishi wa *Precision* amewahi kuitwa ndani ya Bunge hili kupongezwa kama walivyopongezwa wale vijana wetu waliofaulu kwenye Shule za Kata maana naye amefanya kitu kikubwa, anatakiwa aitwe ndani humu apongezwe kwa kufanya kitu ambacho Taifa limeshindwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, yeze kaanza na ndege ndogondogo mpaka sasa hivi ana ndege kubwa na Shirika lake *lime-nourish* kabisa. Kwa hiyo, hawa Watanzania nao tungewaita ili labda tuwape moyo ndani ya hili Bunge waendelee kutupa mawazo mengine ambayo tunawenza tukayatumia hata kwa mashirika yetu yanayoshindwa kama *ATC*. Kwa kifupi tunahitaji kufanya *overhaul*/ya kila kitu.

Mheshimiwa Spika, *the other day* nilisimama humu ndani nikauliza kwamba, je, Serikali inaweza kukubali kwamba Sera ya Ubinafsishaji imefeli? Nikapewa maeleo marefu na Mawaziri wawili bila kupewa majibu lakini huu hapa ni ushahidi mwingine kwamba Sera zetu za Ubinafsishaji zimeshindwa inabidi Watanzania tuenze upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilisoma kwenye gazeti, huyu Mataka anastaafu, anastaafu sijui ameambiwa hebu kaa pembeni, lakini anaaga kwenye gazeti. Anaulizwa mafanikio yake, anasema nimeleta nembo mpya, *logo* mpya ya kampuni na kuondoa ile ya makaburu badala ya kuleta ndege mpya analeta nembo mpya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito ndani ya Bunge lako kuanza kuirudisha *ATC*, tuenze kurudisha ile nembo ya zamani, nembo yenye historia ya uzalendo, hii nembo ya sasa hivi ni nyepesi, haina hata *corporate touch*, utafikiri nembo ya kibashara fulani, *ka-stationary* fulani. Kwa hiyo, kwa kuanza na *ATC* tuenze kurudisha *logo* kwanza, ni ya kizalendo itatukumbusha hata zile ndege 11 na tutakuwa na moyo zaidi wa kufanya kazi na kusogea mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tuangalie Bodi za Mashirika na Makampuni yetu kwa sababu nalo ni tatizo. *With all respect to our senior citizens* ambao wameitumikia nchi hii na Taifa kwa ujumla, lakini sasa mimi sioni umuhimu tena wa kuwapa ujumbe wa Bodi, Uenyekiti wa Bodi ma-*diplomats* wastaafu. *Diplomats* kazunguka Angola, Zambia sijui Senegal wapi kote kaiwakilisha nchi, umri wake wa kustaafu umefika unakuja hapa unaona umpooze, unampa Uwenyekiti au Ujumbe wa

Bodi. Majenerali, Mabrigedia wastaa fu wamelitumikia Jeshi miaka 35, heshima kubwa kwao, lakini tutafute namna nyingine za kuwapa ahsante utumishi hawa, tutafute namna nyingine za kuwashukuru au za kuwapoza, lakini sio kuwaweka kwenye Bodii, tena Bodii zinajaa watu, watu tisa, Bodii gani ina watu tisa, watu 12? Bodii watu wanee, watano vichwa makini vikae vipange mambo, mashirika yaende, makampuni yaende, hakuna zaidi ya hapo. Ndiyo kama nilivosema Serikali ifikirie njia nyingine ya kuwazawadia hawa *senior citizens* kwa kazi nzuri waliyofanya, lakini kwenye Bodii tuangalie kidogo watu wenye nguvu, watu wanaoweza kukimbia, watu wabunifu na sio lazima watoke Serikalini, watoke hata kwenye sekta binafasi kama vichwa vyao vinafanya kazi, ni Watanzania wetu na tunawajua, tuwasogeze, tuwaweke mle kwenye Bodii hata kama watakuwa ni vijana wenye miaka 26, kama kichwa chake kinafanya kazi, weka kwenye Bodii ili aisongeshe ATC mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia viwanja vya ndege wakati hatuna ndege za kutua kwenye hiyo viwanja pamoja na hayo lakini nishukuru kwa taarifa za uwanja wa Mbeya, Songwe tunaambiwa kwamba unaisha mwezi Disemba 2011, tunakabidhiwa au unaanza kazi. Mimi nasema hivi, inanifanya nisiamini kama kweli ule uwanja utaanza kazi mwezi wa kumi na mbili kwa sababu kutoka sasa hivi mpaka mwezi wa kumi na mbili ni miezi minne, lakini hatujasikia Serikali ikitoa mwongozo au mamlaka zinazohusika zitoe taratibu kwa wazabuni ambao wataendesha kama migahawa pale, maduka au hao watu wapo tayari au mnataka kuwatoa wapi? Kwa sababu wako Wanambeya pale wafanyabiashara ambao wako tayari, wanasubiri wapewe maelekezo kwamba watapataje mchakato wa kuendesha maduka pale kwenye *airport*. Hata kuendesha meza za kuuza magazeti, wako Wambeya ambao wanasubiri. Kwa hiyo, mnapotuambia kwamba mtatukabidhi *airport* mwezi wa kumi na mbili, wakati mpaka sasa hivi hatusikii, hatuoni hata mabango ya biashara yanayotayarisha mazingira ya biashara kwenye ule uwanja wa Songwe *International*, kwa kweli ndiyo maana badala ya kufurahi kwa sababu sasa hivi tulitakiwa tuwe tunafurahi, lakini tuna wasiwasii kwamba kweli huu uwanja Disemba utakwisha? Kwa sababu viashiria vya mwanzo vingekuwa ndiyo hiyo kwamba bwana Mwanambeya mmoja anasema kwamba niko *busy* kidogo pale najengajenga duka langu, niko *busy* pale naanda mgahawa na vitu kama hiyo. Katika suala la uwanja wa ndege wa Mbeya, naiomba Wizara ya Kilimo maana *the other day* nimemsikia Waziri wa Kilimo anazungumzia kilimo cha maua Mbeya, kwa hiyo, *now* tunaomba wafungue michakato ya kilimo cha maua kwa sababu tunaamini *airport* itakuja mwezi wa kumi na mbili mwaka huu (2011), hali kadhalika za kutua na ndege pia tunaamini zitakuwepo.

Mheshimiwa Spika, nataka niiguse kidogo *TAZARA* ingawa Mheshimiwa Zambi jana ameigusa kwa upana na dada yangu kule Angella aliigusa kwa upana, lakini kwa kuwa na mimi nilitumwa, lazima niiguse kidogo. *TAZARA* Mbeya kuna manung'uniko mengi, iko hoi kwanza *TAZARA* yenyewe, iko hoi kwa wizi, ubadhirifu na mipango mibovu, lakini wakati tunazungumzia mikopo kutoka China, misaada kutoka China, tuangalie kwanza manung'uniko yaliyokuwepo pale. Pale *TAZARA* Mbeya ninakowakilisha mimi, kuna manung'uniko makubwa sana ya mafao ya wale wazee pale, wanatembea huku na kule wanahangaika kila ofisi katika kutafuta haki zao. Bila kuondoa yale manung'uniko, hakuwezi kuwa na neema, hakuwezi kuwa na *future* njema. Tuondoe yale manung'uniko ya wale wazee walioitumikia *TAZARA* bila matatizo yoyote, halafu ndiyo tuangalie mikakati mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumaliza kabla sijasahau nizungumzie *Mbeya Dry Port*. Mheshimiwa Lembeli kazungumzia pale *Dry Port* ya Isaka nikataka nikate tamaa nisizungumzie, lakini wacha tu nizungumzie. Pale Mbeya lyunga kuna kituo cha mizigo kinaitwa *Malawi Cargo Center (MCC)*, kwa mujibu ya menejimenti ambayo nilishazungumza nayo mara kadhaa, waliniambia kwamba wao walishamaliza michakato yote wa kile kituo kuwa *dry port* mpaka hata jina nje wametoa kutoka *MCC* wameandika Mbeya *Dry Port* ikimaanisha kwamba walikuwa tayari kwa kuendesha ile Bandari ya nchi kavu. Watu wa Mbeya wanaisubiri, wafanyabiashara wa Mbeya wanaisubiri kwa sababu itasaidia kwanza wafanyabiashara wa Mbeya kuondokana na ukiritimba wa Bandari ya Dar es Salaam. Mtu anakuja Dar es Salaam anakaa mwaka mzima, pili, itasaidia hata *TAZARA* kupata biashara. Kama nilivosema kwenda China na kupata mikopo, halafu unakuja hapa mabehewa yanakaa, yanaliwa na kutu, yanakufa tena unakwenda kuomba mkopo India unarudi, haitasaidia kitu kama hatuna mipango ya biashara. Mpango mmojawapo

wa kuipa *TAZARA* biashara ni kuanzisha Mbeya *Dry Port* kwa sababu ile *dry port* itakuwa na uwezo wa kuhudumia zaidi ya *container* 25,000 kwa mujibu wa Menejimenti.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ile *dry port* inatoa ajira kwa watu 40 tu, lakini kwa mujibu wa Menejimenti itakapopata leseni na kuwa *fully operating* itakuwa na uwezo wa kutoa ajira kwa Wanambeya takribani 250. Kwa hiyo, hapo tutakuwa tumewasaidia wafanyabiashara na tumewasaidia Wanambeya kupata ajira katika ile sehemu na sehemu yenye wafanyakazi 200-250, kuna mama ntilie wangapi au mama lishe wangapi watakaokuwa wanatoa huduma za chakula hapo? Madereva wangapi watakao kuwa wanakuja pale? Kwa hiyo, kutakuwa kila siku pako *busy* kwa mzunguko wa watu takribani 800, 1000 kama sio 1500 ambaو watakuwa wanapokezana hela. Ni kitu ambacho tunakihitaji kwa sababu pia tutakuwa tunahudumia watu kutoka nchi za *SADC*, kwa maana hiyo wale watu wa nchi za *SADC* hawaji na hela zao *local*, wanakuja na dola. Mbeya hatuna hata *Bureau De Change*, sjui iko moja, hata ukienda hamna watu. Sasa bila dolari, uchumi utachangamka vipi na sisi tunataka tuwe na vyanzo vya dolari, *airport* inakuja, tunaomba *dry port* na vitu kama hivyo kwa sababu ni mkakati wetu wa dhati kuifanya Mbeya iwe Jiji kamili kama Majiji mengine yalivyo yanachangamka Mwanza, Arusha halikadhalika na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa leo naomba niishie hapa na siungi mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru sana kupata nafasi hii leo. Mwanzoni nilikuwa nimepanga niondoe jina kabisa kwa sababu...

(*Hapa kuna Mheshimiwa Alikatiza kati ya Kiti na Mzungumzaji*)

SPIKA: Mheshimiwa, hebu simama kidogo umwangalie yule anayeongea, halafu na mimi, umefanyaje? Umevuka, haya endelea Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Jana nilikuwa nimeomba niondoe jina langu kutokana na mjadala ulivyokuwa mkali hasa hizi salamu kutoka Mwitongo kwa Mheshimiwa Nundu pale, lakini nimeona na mimi nitoe mawazo yangu tu kutokana na hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nianze na Shirika la Reli, kwanza *ni-declare interest*, mke wangu anafanya kazi reli, lile Shirika ambalo linaelekea kufa, limekufa tu tuseme. Hata wakati likifanya kazi nilikuwa mimi ndiyo nahangaika kutoa nauli kila siku kwa sababu liliikuwa halifanyi chochote pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nchi zote duniani, Mheshimiwa Nundu anafahamu, yale *ma-giant countries* Marekani, Uingereza, Canada alikokuwa, Ujerumanu pamoja na maendeleo mazuri waliyonayo katika barabara na viwanja vya ndege, lakini bado reli ni muhimu kuliko kitu kingine chochote, hili analifahamu. Wanavyoendesha reli zao ama Mashirika la Umma ili yaendelee ku-survive anafahamu pia kwa nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zamani wakati mimi nakwenda kusoma Sengerema kule walikuwa wanapewa *warrant* na Serikali, unapewa *warrant*, unakwenda pale, Serikali ina uhakika kwamba Shirika litaendelea kuwepo, lakini tumekuwa na mashirika kama reli, watu hawajui anapanda nani, yanakuwa tu na watu wapo, eeh! Tatizo letu ni kutochukua *action*. Kama Wabunge jana tu wamechukua *action* kukataa hii bajeti toka asubuhi mpaka jioni, Serikali leo imekuja na hoja hapa kwamba inatoa shilingi bilioni 95, walikozitoa hawajasema. Hivi tukiwabana leo tukawaambia warudi baada ya siku tatu, watakuja na *one trillion* hapa, Shirika hili halitakuwa limeendelea? *Let us be serious*. Kwa siku mbili wamekuja na shilingi bilioni 95, tukiwapa siku tano, tutakuwa tumpata hela na shirika litakuwa linafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, shemeji yangu Mtutura pale alikuwa anazungumza nikasema niombe Mwongozo, nikasema wacha ninyamaze tu kwa sababu kaoa Kondoa yule, nimemsamehe tu. Jambo la msingi ni watu kuwa *serious* kwenye usimamizi wa mambo ya umma. Reli ile ilikuwa muhimu sana lakini leo haipo. Kwanza mimi siku moja walipoanza kuua magenge kwenye njia ya reli hii, nikajua reli itakufa. Si USA, si wapi reli yoyote ile lazima iwe na magenge njiani kwa ajili ya

kuhakikisha reli iko salama. Sisi tulipoanza kuua magenge na watu wamekaa kimya tu wanaangalia, reli inakufa tu hivi, wanazungumza maneno ya ajabu tu, tumekaa kusengenyana tu, reli inakufa, kazi yetu kukimbilia kwenye magazeti badala ya kuangalia mambo ya faida kwa wananchi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, halafu mnataka sisi tuje hapa tunyamaze, eti kwa sababu sisi ni Wabunge wa CCM, *no!* Sisi tunawatumikia wananchi. Tumepegawa kura na wananchi wa CCM na wasio wa CCM. Fufueni Shirika la Reli lile hata mke wangu arudi kazini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niente kidogo kwenye Shirika la Ndege, ukienda pale JF Keneddy pale New York, vinchi vidogo tu unakuta ndege zao zipo, Trinidad and Tobago wana Shirika la Ndege linakwenda mpaka Marekani pale, Haiti wana ndege, Cuba wana ndege, vinchi vidogovidogo tu hivi. Sasa linchi kubwa kama hili, tumeua Shirika la Ndege, tunasafiri kwa kutumia nini? Boti hazipo, ndege hakuna yamebaki mabasi tu, nayo mabasi yenye ni malori yanavunjwa yale maskania yanatengenezwa mabasi, watu wamenyamaza tu, haiwezekani! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana na sio kuomba *in such* kwa sababu Serikali ndiyo wajibu wake, kwa sababu kila siku tukisema naiomba Serikali, naiomba Serikali, ndiyo wajibu wa Serikali kuwatumikia wananchi wake. Kwa hiyo, mimi ningitaka Serikali ya Chama changu Chama cha Mapinduzi, fanyeni kila muvezalo mrudishe Shirika la Ndege. Leo tunaongeza uwanja pale Dar es Salaam, nilipita juzi, tunaongeza *ka-terminal* pale, ndege zenye we hatuna, zitakuwa zinatua ndege za nani pale? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kama tunaboresha viwanja vyetu, basi tutafute kila mbinu, turudishe Shirika letu la Ndege na hata wale waliosababisha Shirika hili kufikia hatua hii, hebu tuwatizame. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Dodoma hapa, uko katikati ya Mji, ndege ikikosea pale, watu wote *Area 'C'* pale, hapa *Airport* sijui kama watabaki. Kuna uwanja unajengwa kule Msalato, hebu Serikali ule uwanja, eneo hili hapa tupeni viwanja tujenge. Uwanja uko katikati ya Mji hivi, watoto wetu hawalali na ikitua ile ndege sijui ni *Foka* ni kelele tupu. Toeni ule uwanja, kamilisheni ule uwanja wa Msalato, pale tupeni viwanja hata Wabunge tunahitaji kweli kujenga Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nimalizie, nisisitize tu kidogo kuhusu hili suala la reli kwa kweli na nimeomba nilirudie hasa kwa mara ya pili. Mimi nasikitika sana kuona reli inakufa. Mbunge mmoja siku moja alisema hapa, akasema tukitaka kutafuta hela za kujenga reli tunaweza, za kuimarisha bandari zetu tunaweza kuzipata, hebu tutumie mawazo ya watu wanayoyatoa hata kama hatuwapendi, lakini tuchukue mawazo yao, tuchukue mawazo yao yatusaidie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuangalie ni jinsi gani tuimarishe reli yetu, Wanywamwezi wale, Waha wale, Wasukuma, tena mimi nilikuwa nasikia raha sana pamoja na kwamba, Mheshimiwa Spika uniwie radhi kidogo, tulikuwa tukiingia tukitoka Sengerema kwenye behewa moja, tulikuwa wanafunzi wakorofu sana kutoka Sengerema. Tukiingia pale, hakuna behewa letu mtu kupita, ilikuwa ni raha mustarehe, lakini reli imekufa. Nilikuwa namuwaza pale, mama mmoja alisema Mwanza South pale, sasa hakuna kitu na wote tupo tu.

Mheshimiwa Nundu kama mimi ningepewa hiyo Wizara ningekataa kabisa, ningesema Mheshimiwa Rais, naomba uniwie radhi sana, napenda sana kuwa Waziri *but I am sorry, I cant manage this Ministry, that is it.* Wewe umekubali, lazima na sisi tukuchakachue, tukueleze ukweli kwamba hii ndiyo Tanzania na hizi ndizo salamu kutoka Mwitongo kule kwa Baba wa Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kwa kweli mimi *to be sincere siwezi kuunga mkono hoja, kwa nini?* Kwanza hatujaambiwa hizi pesa zimetoka wapi, ningombaa tusogeze siku mbili mbele ili ziendelee kujaa ili baada ya hapo tutakuwa na uhakika reli yetu itatengenezwa, nashukuru. (*Makof*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, binafsi asubuhi wakati nasikiliza taarifa ya Waziri Mkuu, nilikuwa natarajia kwamba angesema tunasitisha zoezi, tunatoa muda ili kuweka mambo sawa lakini tafsiri imekuja tofauti, imekuja kuonesha kwamba waliozungumza Wabunge jana, majibu yake ni shilingi bilioni 95. Sio kweli! Yaliyozungumzwa jana ndiyo vilio vya Watanzania vya miaka 50, ambavyo haviwezi kutatuliwa na shilingi bilioni 95 ya ziada. Yaliyozungumzwa jana na yaliyoendelea kuzungumzwa leo asubuhi, ndiyo yanahitaji majibu kwa ajili ya hili Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nina maswali ambayo muda wote nakaa najiuliza, tarehe 9 Desemba, 2011 tunaenda kusheherekeea uhuru wa namna gani? Leo Mwalimu Nyerere angeweza kuamka kwa mara nyingine tena, angetutandika bakora, angetushangaa ni watu wa namna gani, ndege 11 hakuna kitu, reli za misaada zote, Ujerumanu reli ya kat, China ya TAZARA misaada hiyo, hakuna kitu, halafu leo unasema shilingi bilioni 95 ndiyo inaweza kutatua tatizo, si kweli na wala sio jibu sahihi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo ambayo inahusika kwa asilimia 100 ili kuweza kuleta faida kwa Taifa. Wizara hii ndiyo moja ya chanzo cha mapato cha Serikali tofauti na Wizara nyingine, Ujenzi tunajenga kama sehemu ya mawasiliano lakini Wizara ya Uchukuzi, ndege tunapata, tunatoa huduma wakati huohuo Serikali inapata ukiongeza na Bandari ndani yake lakini tafsiri ni tofauti. Wabunge tunakaa kabisa kwa pamoja, tunapongezana, jamani hatulitendei haki Taifa hili, hatuwatendei haki watu waliotupigia kura, tutafakari moyoni mwetu. Je, tulipanga kuwa hapa? Miaka 50 tulipanga tufikie hapa? Ndiyo vitu ambavyo tunahiji kufikiria. Tunahitaji kuwa watu wenye uchungu juu ya Taifa letu. Tunapokuwa tunagombea tunakuwa na maneno mazuri lakini kwenye utekelezaji tunakuwa ni watu tofauti. Kwenye utendaji hatuwi watu wenye ubinadamu. Hayo ndiyo mambo ambayo wengi yanatugusa.

Mheshimiwa Spika, labda tunapokuwa tunagombea tunakuwa na dhamira tofauti maana mwagine anagombea ili aende kupata fedha, mwagine anagombea ili aweze kusaidia watu. Kila mmoja ana dhamira yake ndani yake. Mwingine anagombea ili apate heshima lakini kama kweli unagombea kwa ajili ya nia moja ya kuwasaidia Watanzania hatuwezi tukapitisha hii bajeti. Hii bajeti siyo tu inahitaji bilioni, ni zaidi ya triliioni ndiyo ambayo ilihitajika tukae tuzungumze hapa. Bajeti hii ilitakiwa ije *i-reflect* miaka 50 ya Uhuru tulioipata. Bajeti *ina-reflect just* matarajio ya watu fulani, kuridhisha wanasiasa ili tuweze kupitisha bajeti hii, kwa mfumo huu tutafika? Lazima tuulizane, tutafika kwa mfumo huu?

Mheshimiwa Spika, wote mnafahamu kabisa Rais Kagame aliwahi kusema kama si utani alikuwa *serious* alimwambia Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete nipatie mimi niwe Waziri wa Bandari na Maliasili, nitalisha Tanzania pamoja na Rwanda. Hii ni dharau! Mnaweza mkafikiri ni utani lakini ni dharau. Anaongelea Uwaziri Tanzania ili alishe Tanzania pamoja na Rwanda nchi yake. Leo Mawaziri mnashindwa kumuuliza ni kwa nini alisema hivyo? Unaifikiri ni kwa sababu gani alisema hivyo? Kwa sababu anajua umuhimu wa bandari. Ameona bandarini kuna kitu pale. Ndiyo mienendo ambayo tumekuwa siku zote tunalalamika, utakuta vizuizi 29 toka Dar es Salaam mpaka unafika Kigali ina maana Tanzania nzima hatuaminiani. Unatoka hapa Kibaha kizuizi, Morogoro, Mikese pale kizuizi. vizuizi vingi lakini vyote *source* kuanzia kwenye bandari, maana yake Taifa zima hatuaminiani. Tutafika tunakokwenda? Tuulizane tutafika tunakokwenda? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, je, haya tunayoyaongea leo tunayaongea ili kuridhisha Watanzania? Kama ni kweli, ni kheri, nasema kweli ni kheri Bunge hili likavunja. Ni kheri likavunjwa tukarudi, Watanzania wachague watu wanaoweza kuwatumikia, hatuwezi tukawa tunapitisha vitu ambavyo tunajua kabisa hatuwatendei haki Watanzania. (*Makof*)

Waheshimiwa ninyi wenye uzalendo wa kweli, naamini kabisa wengi mnalijua hili ninalolisema, lakini kuna mahali tunasema hatuhitaji kuficha tena siri za Serikali ndiyo maana leo Wabunge wananyanya na kulipua siri za Serikali mbele ya umma. Tutafakari mara mbili, tujifikirie zaidi nini ambacho tunataka tukifiki. Tufifikirie vizazi vinavyokuja, ndiyo mambo ambayo tunahitaji kuyafanya kwa wakati uliopo.

Mheshimiwa Spika, mimi wakati nasoma seminari tuliwahi kuambiwa kitu kimoja mwanadamu yejote anafikia mahali anakata tamaa (*point of no infinity*). Hata kama amezaa mtoto na kila siku anampiga, ikiflikia mahali akasema sasa baba litakalokuwa na liwe maana yake ndiyo *point* ya kukata tamaa na kukataa tamaa kwa mwanadamu kukishafika mwisho wake hata umwambie maneno mazuri hawezu kukubali. Hata umfanyie jambo lolote zuri, hawezu kukubali. Ndiko ambako naona tunataka kulipeleka Taifa hili. Sasa Waheshimiwa Wabunge, je, mmeshawahi kuliona hilo? Wabunge wote na Majimbo yote ambayo tunatoka tunajua tuna changamoto mbalimbali lakini changamoto hii inaligusa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kujumuisha jioni aje na majumuisho ya kwamba kwanza tunataka hizi fedha walizozitoa siyo zipite kwa mdomo, ziwe kwenye vitabu kama ambavyo tulirudisha bajeti ya Nishati na Madini. Kwa hiyo, wawe wametuandikia, tusipitishe tu kwa sababu yamezungumzwa na Waziri Mkuu basi yapite. Tulikuwa tunazungumza na Wabunge wengine kila mmoja alikuwa anapigiwa simu kwa wakati wake akiulizwa kwamba wewe tulikuagiza uunge mkono hoja ili baadaye ipite, tunasaidia Taifa? Wanasema Wabunge tulikuwa nao, wanunung'unika pembedi, kwa sababu wengine wanasema mimi ni Mjumbe wa CC usirudie kusema maneno hayo. *Who are you kwenye Taifa hili?* Kuwa kwako mjumbe wa CC ndiyo kumkataza mwingine asiseme ukweli? Hatuwezi kwenda kwa mfumo huu. Hatuwezi kulifikisha Taifa kama tutaendelea kwa mwenendo huu.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni salamu kwenu. Kilio cha Watanzania wanyonge walioneseka kwa muda mrefu, sasa hivi tunasema *enough is enough*. Mbozi walivyokuwa wanantuma walijua kwamba tunatuma kiongozi ambaye anakwenda kuismamia Serikali, anakwenda kuwasemea wananchi wake ili Serikali ichukue hatua. Sasa kama Mawaziri mnasema kabisa hamwezi kutekeleza majukumu kwa sababu mna majukumu ya Majimbo muache tuteue Mawaziri nje ya Wabunge ili tuweze kuwawajibisha labda hiyo ndiyo inaweza ikafanya kazi lakini kwa sababu na ninyi wenyewe mnahusika na Majimbo, mnashindwa kutekeleza makujukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tatizo kubwa kwenye Idara nzima ya Reli, Idara nzima ya Bandari na Sekta nzima ya Ndege kwa maana ATCL ni Utawala tu. Kwa sababu hivi vyote vilikuwepo, kama visingekuwepo tingesema hili ni tatizo lingine lakini vilikuwepo, sasa vimekwenda wapi? Hilo ndilo swalii ambalo wote tunatakiwa tujilize. Vilikuwepo, ndege zilikuwepo 11, leo tuna sifuri. Reli tulijengewa, zote leo hazifanyi kazi. Wafanyakazi wanalamika, bandari ndiyo hiyo bado inasuasua pamoja na kwamba tunapata kidogo lakini nani wa kulaumiwa kama siyo Utawala?

Mheshimiwa Spika, baadaye tunasema kwamba tufuate Sheria. Sheria na yenyewe wakati mwingine ina makosa kwa sababu unapokuwa mtu wa kutegemea zaidi Sheria kwa masaa 24, kwa sababu Sheria ukipoteza karatasi moja huwezi kumfunga mtu. Hata leo tulikuwa tunawalamikia watu wa UDA, wale watu wa UDA kila mmoja anajua ushahidi kabisa, hawa watu wameiba, hawa wamechukua fedha ya Serikali, lakini watashindwa kuwafunga kwa sababu hatuwezi kuwakamata kwa ushahidi wa asilimia 100. Haya ni makosa makubwa sana katika Sheria. Sasa huu ndiyo mwenendo mzima ambao mimi nauona katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Wabunge wengi tumelalamika, tunachohitaji kuamua ni moja, tuwape muda, siyo kosa, siyo kwamba tunawahukumu, tuwape muda wa wiki moja, wiki mbili wakajipange upya walete bajeti itakayokidhi mahitaji ya Watanzania. Bajeti itakayokidhi maana halisi ya miaka 50. Tunataka siku ya tarehe 9, ndege iwe inaruka angani, angalau mpya kwa sababu mimi wakati tunasoma Uchumi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tunajua namna unavyoweza kurusha ndege. Ndege hununui kwa fedha yote. Unalipa 10% percent nyininge utakuwa unaendelea kulipa. Tunataka turushe hata ndege moja mpya, angalau na sisi tuwe kwa miaka 50 kwa maana siyo miaka 50 hakuna ndege, tutakuwa tunasherehekeea nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hivi ni vitu ambavyo tunahitaji kuvifanya. Taifa halihitaji laana ya kujitakia yenyewe kwa sababu sisi kwa maandiko yetu Biblia inasema "Laana yoyote huwa inakaa vizazi vinne na laana huwa inakaa kutokana na maamuzi mabaya wanaochukua watu walio wakubwa dhidi ya wengine". Kwa hiyo, kama kiongozi ukichukua maamuzi mabaya juu ya Taifa hili unaliangamiza Taifa lako, unajiangamiza wewe mwenyewe, unaangamiza na vizazi

vingine nyuma vinne, wote watakuja kulalamika baadaye, sasa tutaendelea hivi mpaka lini? Sasa kwa sababu hatuhitaji kufikia huko tunahitaji kuwa watu wa hatua siyo watu wa kuyumbayumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiachia hilo, Wizara yetu imeshindwa kuwa na ubunifu wa vyanzo vyta mapato kwa ujumla. Moja ya sehemu ambayo wameshindwa zaidi ni namna gani ya kutafuta vyanzo vyta mapato kwa ujumla. Leo katika Jimbo langu la Mbozi Magharibi eneo la Tunduma, Mawaziri wote wanalamika, Wabunge wengi wanalamika kwamba tukipita pale Tunduma, kuna msongamano wa magari makubwa kwenda nchi za jirani. Tunashindwa kupita pale Mheshimiwa Mbunge tusaidie, wakati wao wenyewe kama Serikali wanajua kabisa tunaweza kusaidia na tukafanya chanzo cha mapato tukianzisha bandari ya nchi kavu pale, ambapo magari yote yanayokwenda Congo, yanayokwenda South Africa, Botswana, Zimbabwe na nchi zingine za Malawi, yanaweza yakaa pale bandari ya nchi kavu yakalipia, Serikali ikapata mapato na tukaondoa foleni. Mnashindwa kugundua vyanzo vyta mapato vidogo kama hivi. Mnakwenda kuwekeza pale hektu 100 tu magari yanakaa pale, mambo yanakwenda vizuri. Kwa nini tunashindwa kugundua vitu kama hivi? Tunaleta mawazo lakini hayatiliwi maanani ni kwa sababu ninayeongea niko upinzani. Hapana mimi si mtu wa namna hiyo, tunahitaji Taifa Vyama baadaye, hicho ndicho kikubwa ambacho tunahitaji kukizungumza.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji vitu ambavyo vinakwenda na wakati na hili Mheshimiwa Waziri lazima uliweke maanani. Katika hizo fedha mlizitoa ambapo ninyi wenyewe mnajua, maana mimi najua asilimia kubwa itakuwa ni mikopo, namna ya kurudisha huu mkopo mnawenza mkaurudisha kupitia Tunduma kwa kuanzisha hii bandari ya nchi kavu. Sasa hili ni lazima mlifanye ili angalau hata miaka 50 watu waone kabisa kwamba kweli Serikali inachukua hatua yenye nia thabit ya kuwasaidia Watanzania wake. Sasa hili ningeomba kabisa na lenyewe mlilitile maanani na mlisikie kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala la bandari mimi nitapendekeza jambo moja. Kwa kuwa mpaka sasa hivi wote tunaonekana tumeshindwa, tunahitaji tufanye tafiti mpya. Tufanye *analysis* tujue ni namna gani tunaweza tukaikoa bandari kwa sababu mwenendo wa kubadilisha tu Menejimenti hautatusaidia lakini suala la *commitment* kwa Mawaziri na Viongozi waliopewa hiyo hatamu ni lazima liwepo kwamba Waziri atuambie leo jamani nikishindwa kutatua suala la bandari, msongamano wa mabehewa bandarini pamoja na magari ambayo yanakaa na kuoza, ndani ya mwaka mmoja niondolewe Uwaziri. Tukiwa tunasema tu kwamba jamani twende hivyo, maana hata Rais Kagame anapokuwa anakuteua kuwa Waziri wake huwa anakupa *condition* moja, je, utaweza na unapokwenda pale unamwambia kwamba mimi Mheshimiwa Rais katika haya masuala moja, mbili, tatu ndani ya miaka mitatu nitaweza, nikishindwa ninajiengua. Kwa sababu siyo dhambi kuijiengua, umeshindwa kutekeleza wajibu na ni uzalendo wa hali ya juu, ndicho tunakihitaji sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, mimi nachoweza kumwambia Mheshimiwa Waziri kama kweli wanashindwa tuleteni sisi hapa. Niletenei mimi muone kazi itakavyofanyika. Mnanipa miezi sita tu baada ya hapo watu mtaona matunda ya Taifa hili. Kila kitu kinawezeka, sisi tunajua. Kwa nini kishindikane? Nipeni mimi nguvu yangu inavyotofautiana na Nundu na Wasira vilevile kwa sababu mimi kidogo ni kijana, kazi inaweza kufanyika hapa. Hiyo ni moja ya pendekezo ambalo mimi ninatoa lazima mlisikie jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la reli. Suala la reli kwa kuwa tayari Mheshimiwa Waziri ameelleza kabisa miaka 50 hatujajenga reli hata kilomita moja, leo anayejenga reli Angola ni mtu binafsi, lakini kwa niaba ya Serikali ya Angola. Sisi nasi angalau bajeti yetu ionyeshe kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha hata kilomita mbili tu tunajenga ili tunapokwenda kuzitangaza watu waelewe kabisa kweli hawa watu wana nia thabit ya Taifa hili. Tutaeleweka, Watanzania wataona kabisa kwamba sisi tuna nia nzuri. Sasa ili tuweze kufanya hayo ni lazima tuwe na umoja na ushirikiano. Haya mawazo tunayoyatoa myashike, msiyapuuze tu, kwa sababu tunajua watu wengine wanafikiria labda sisi tunaongea utaniutani tu lakini ni mawazo thabit na yana uwezo wa kuliondoa Taifa hili katika hiki kipindi ambacho tunakipitia.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kuzungumza sana lakini nawaomba tuliyoyazungumza tuyashike lakini bajeti ya leo kwa kweli tuipe muda kidogo wakajipange upya. Nafikiri ni uzalendo zaidi. Tuipe nafasi, tukikubali kuipa nafasi hata mimi nitakuja na mtazamo tofauti lakini kama hatutaipa nafasi siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA : Ahsante sana, utapewa huo mzigo. (*Kicheko*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Kitu gani, muda mbona mfupi mno?

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Kuna kitu gani kimetokea, hebu jaribu Ole-Sendeka.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Ndiyo Mheshimiwa Spika, nina jambo ambalo nimetaka kuomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a) kwamba hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Mbunge aliyemaliza sasa hivi kuongea ni rafiki yangu na namheshimu sana lakini katika maelezo yake yote mengi na mazuri kuna jambo moja tu amelliingiza hapa ndani kwamba kuna Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wameitwa na Wajumbe wa CC na kupewa vitisho. Uhuru wa maoni ulioko Bungeni unatolewa na Ibara ya 100 ya Katiba ya nchi yetu na Chama cha Mapinduzi kinaheshimu uhuru wa maoni uliopo Bungeni. Siamini kama kuna Mbunge yejote wa Chama cha Mapinduzi aliyeitwa na Mjumbe wa Kamati Kuu. Kama Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba kuna vitisho vinavyotolewa na Mjumbe yejote wa Kamati Kuu alithibitishie Bunge au aondoe kauli hiyo kwa sababu Mjumbe wa Kamati Kuu kama Mjumbe tu hana Mamlaka yoyote ya kumwelekeza Mbunge yejote wa Chama cha Mapinduzi jambo lolote. Chama kwetu ni vikao na siyo mtu mmoja.

SPIKA: Nakubaliana na hilo lakini ameshasikia, tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa mujibu Kanuni ya 68(vii), naomba Mwongozo wako kuna jambo ambalo mimi limekuwa likinisumbua sana kichwani. Naomba nifanye reference kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano...

SPIKA: Kama ni siku zilizopita basi naomba ukae kwanza tuendelee. Ukae nitakuita baadaye kwanza nifanye kazi.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA: Naam!

SPIKA: Sitaki kumnyima nafasi yule ninayetaka kumwita sasa. Naomba ukae, Mheshimiwa Kafulila.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ambayo huenda nikawa mchangiaji wa mwisho kwa sababu nilikuwa nimekata tamaa.

SPIKA: Wewe changia tu.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, nina haki ya kushukuru.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia Sekta ya Uchukuzi tafsiri yake tunazungumzia uchumi wa Taifa na siku zote tangu niwe Mbunge huwa najuliza hivi haya mambo ambayo yameandikwa kwa mujibu wa tafiti hawa Mawaziri wetu huwa wanayasoma au huwa

yanahifadhiwa kwenye makabati tu? Nimesoma kwenye ripoti inaitwa *Poverty and Human Development* ya mwaka 2007 inaonyesha kwamba kama Tanzania ikitumia jiografia yake ya kupakana na nchi ambazo hazina kwa mfano sekta ya usafiri kwa maana ya kuwa na usafiri wa uhakika wa anga, kuwa na bandari, kuwa na reli ya uhakika, eneo hili peke yake ni eneo ambalo linaweza likatoa mchango mkubwa kwenye uchumi kuliko sekta zingine zote ikiwa ni pamoja na kilimo. Sekta pekee ambayo inaweza ikaongoza kwenye kukuza uchumi wa Taifa hili kuliko sekta yoyote ile ni sekta ya uchukuzi lakini ni sharti tuboreshe au tujenge bandari ya uhakika, tuwe na reli ya uhakika, tuwe na usafiri wa anga wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nilishtuka sana kuona Waziri analeta bajeti na kimsingi si Waziri, kuna Baraza la Mawaziri, kwa sababu hii bajeti ya Waziri mpaka imefika hapa tafsiri yake ni kwamba vichwa vyote, kikosi chote cha *Cabinet*, kilikaa kikafikiria mstari hadi mstari eti ikaridhika kwamba hii ndiyo bajeti ya Uchukuzi, tuwatendee haki Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, najua na umetungwa msemo hapa wa kasungara kadogo. Nchi tajiri hii hauwezi ukazungumza kasungura kadogo, ni mambo ya aibu. Ni nchi ya tatu kwa dhahabu Afrika unazungumza habari ya umaskini? Hioo misemo ni ya kimaskini kwenye nchi tajiri, haiwezekani! Tunahitaji tuboreshe bandari, tunahitaji tuboreshe reli, tukaboresha usafiri wa anga, tunaweza tukajenga uchumi huu kwa kiwango kikubwa kuliko sekta nyingine yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, kwenye *transport economy* wanazungumza kwamba usafiri wa reli ni nafuu mara kumi ya usafiri wa barabara kama viwango vya reli na barabara vitakuwa sawasawa. Hii ni *transport economy* ya kawaida kwamba ukiwa na reli yenye ubora ukalinganisha bei yake, ukalinganisha ghamama yake na barabara, ghamama ya kusafirisha kwa njia ya reli huwa inakuwa nafuu *ten times*, mara kumi ya barabara na wala sizungumzi hili kwa msingi wa kusema kwamba pengine tuondoe zile pesa za barabara za Magufuli halafu tuziweke tena huku hapana, mimi siendi huko.

Mheshimiwa Spika, hii nchi ina pesa tatizo ni jinsi ya kuzitumia. Maana wakati tunazungumza kutoa shilingi billioni 95, Waziri Mkuu anazungumza hapa Bungeni shilingi billioni 95 mpaka na jasho, CAG anatuambia kwamba mwaka uliopita tu misamaha ya kodi ilikuwa shilingi billioni 680, haieleweki! Haya ndiyo mambo ambayo yanafanya sisi wengine tusielewe kwamba hivi kweli hawa Mawaziri, hii *Cabinet* au kuna mamlaka inanyimwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, inawezeekana pengine tunawalaumu nyie, labda hamna mamlaka mengine! Tuambieni, kama kuna tatizo la madaraka, mtuambie. Kwa sababu, uwezo upo, rasilimali Taifa hili linazo, mnashindwaje! Mkiboresha reli ikawa nafuu, tafsiri yake ni kwamba, zaidi ya kutoa huduma ndani ya nchi lakini pia mmeongeza ushindani wa kibiashara na kupunguza nakisi ya kitu kinaitwa *Balance of Payment*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, Taifa letu tunazungumza kila siku kwamba, urari wa mapato dhidi ya mataifa mengine ni tatizo kwa sababu, hatuzalishi sana. Lakini kuzalisha sana sio lazima kuzalisha pamba tu na tumbaku! Sio lazima kuzalisha dhahabu tu na almasi! Hata huduma, huduma ni uzalishaji. Huduma ya reli ambayo inategemewa na nchi ambazo hazina bandari, kwa maana ya kwamba ukiboresha bandari mwisho wa siku mizigo ile itasafirishwa kwa njia ya reli, kwa hiyo, bandari na reli zikifanya kazi pamoja vinaweza vikalifanya Taifa hili lifaidike na ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *Comperative Advantage*, kwamba kwenye eneo hili tuna *best comparative advantage* ukilinganisha na mataifa mengine! Tutafanya biashara hii ya usafiri, tufaidike zaidi na mapato kutoka Rwanda, tufaidike zaidi na mapato kutoka Burundi, tufaidike zaidi na mapato kutoka Zambia, tufaidike zaidi na mapato kutoka Kongoo! Hawa watu wote wanaweza wakalipa pesa za kigeni! Huduma hii ya usafiri tukaitumia kukuza uchumi wetu! Huduma hii ya usafiri wa reli na bandari ikasaidia kuboresha kitu kinaitwa urari katika mapato kati ya Tanzania na Mataifa mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini najiuliza hii *Cabinet*, ina kama mwaka mmoja tu, inashindwa nini kama kweli wana dhamira, kufanya mambo ambayo yanaonekana? Mimi siamini hilo!

Mheshimiwa Spika, lazima kuna tatizo tu! Haiwezekani vitu nya namna hii vishindikane, haiwezekani! Leo unazungumza Tanzania kasungura kadogo, ndio sababu hatuna ndege, tuangalie kwenye ndege kidogo, kwenye reli kidogo! Nchi ya Rwanda, ukubwa wake ni pungufu ya Mkoa wa Kagera, kule Rwanda milima yao haina madini ni mawe; wana ndege tano! Tanzania, nchi yenye utajiri wa kila namna! Nchi yenye almasi, *uranium*, dhahabu kwa kiwango kikubwa, makaa ya mawe, gesi na kila kitu! Lakini tunashindwa kabisa kutoka hapa tulipo! Haiwezekani! Ni lazima kuna tatizo katika hii Serikali! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima kuna tatizo na wala haya siyazungumzi kama Mpinzani, nayazungumza kwa dhamira safi kabisa kwamba, hii *Cabinet* ina tatizo la jinsi ya kufanya mambo, kuna tatizo tu! Huwezi kuja na bajeti ya bilioni 167, zinapigwa kelele kidogo zinaongezwa 95! Halafu unasema hii Serikali ni siki!

Mheshimiwa Spika, ninavyoju Serikali siki huwa watu wakisema inasikia. Lakini Serikali kiziwi, watu wakipiga kelele ndio inasikia! Hii Serikali sio siki! Hapa Waheshimiwa Wabunge, tukikomaa, bila kujali itikadi zetu, tukakomaa tukawaambia nendeni, wiki moja mje na mpango wa kutanzua mgogoro wa reli tuwe na reli ya uhakika, mje na sio mpango tu mje na fedha za kutanzua tatizo la bandari, hawa watu fedha wanazo! Fedha zipo! Nyie tukomae tu hapa! Wataleta fedha tu. Kuna vitu vingi vinapachikwapachikwa kwenye bajeti humu na mifumo yetu ya bajeti ilivyo milovu wala sio rahisi kuona. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, juzi hapa tunaambiwa sekta ya ujenzi ya ndugu yangu Magufuli, kuna bilioni kama 300 zinasubiri kwamba ikitoea amekuja mwekezaji na pengine hana uwezo wa kutosha, tunaweza tukaongeza kidogo shughuli zikaendelea! Mimi sikatai, sasa kama Wizara nyingine zinakuwa na ziada za namna hiyo, halafu nyingine *deficit* nakisi kubwa kiasi hiki! Tatizo hapa ni nini? Hapa inaelekea kwamba, tatizo ni *competence* ya Waziri! Kwamba, simsifu Magufuli, sisemi kwamba nitoe sifa tu, lakini hapa inaelekea kwamba huyu Magufuli, ana uwezo mkubwa wa kudai bajeti yake kuliko Waziri wetu! Kwa sababu, katika *concept* ya kawaida wa uchukuzi angepata kiasi kikubwa! Pengine basi hata nusu! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Miaka Mitano unahitaji pengine tungkuwa na kama bilioni 470 kwa miradi ya maendeleo, kama bilioni 470. Ndio mpango ambao Mheshimiwa Rais, amezindua hivi karibuni, ndio mpango ambao tunaanza kuutekeleza! Sasa pengine Mheshimiwa Waziri Mkuu au kimsingi Serikali ingekuja na nyongeza ya kusema kwamba, sasa tumeongeza kwenye bajeti ya maendeleo kutoka 167 ina *shoot* mpaka 470, hapo tungekubaliana. Kwanza tungekubaliana kwa misingi ya kwamba, kiasi hicho kingetosha. Lakini zaidi, ndio mpango wenu ambao mmeupitisha! Au ndio mpango wetu ambao kama Bunge tuliupitisha.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, hatuwezi kuboresha maisha ya Watanzania kama tutabaki na mfumo, kama tutabaki na reli duni kiasi hiki. Kwa sisi kama wakazi wa Mkoa wa Kigoma ndio balaa kwa sababu, bado hata barabara ni tatizo! Tunajua kuna kiasi ambacho kinaendelea, lakini bado ni tatizo kwa sababu, haiwezi ikaisha leo wala keshokutwa. Watu wa Tabora, Mkoa ambao una historia ya Uhuru wa Taifa hili! Mkoa ambao hauwezi ukaandika sentensi mbili za Uhuru, ukauacha! Nenda kaangalie lami, nenda kaangalie reli, mgogoro! Tunafanya nini? Tunafanya nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kwa sababu naona kuna upepo unaelekea kubadiliha hapa. Niwaombe, sisi wa Upinzani hatusemi kwamba tuingie madarakani leo asubuhi au leo mchana, ahaha! Hii Serikali ni ya kwenu, iondoeni ingizeni kikosi kingine! Si ya kwenu! Mnaweza mkaamua tu, wala sisi hatuingii leo! Semeni tu kwamba, kama mmeshindwa tunawapa wiki moja, mkishindwa kuleta pesa ya kutosha ya takriban bilioni hizo 470 kwa ajili ya kutengeneza mpango wa miaka mitano, tunawaondoa tunaingiza wengine! Labda kama hiki chama hakina askari wengine wa kuchukua nafasi hizi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini hiki kikosi kimechoka! Hiki kikosi kimechoka na ndio maana unaona siku hizi kila siku magazeti watu wanachapa usingizi tu! Mawaziri wanachapa usingizi! Tunazungumza hapa, hawatekelezi! Sasa sio tu hawatekelezi, zamani walikuwa hawatekelezi lakini

wanatusikiliza, sasa hivi wameamua na kulala. Ni tatizo! Ningewaomba, hawa watu wamechoka! Juzi Waziri mmoja alikuwa amelala kiasi kwamba, mpaka anafukuza mbu kwenye miguu! CCM wabadalisheni, ingizeni kikosi kingine! Ni nyle hawahawa! Sisi tutawaondoa miaka mitano ikimalizika, hatuna ugomvi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwaambie tu, gharama ya kutokufanya maamuzi huwa ni kubwa sana pengine kuliko hata maamuzi ya kuibal! Kuna watu, kwenye Serikali wanaweza wakaamua tu kwamba aah, mimi nipo tu! Mradi siibi, basi siwezi kufungwa! Lakini kwenye dunia ya utawala ya leo, dunia ya uongozi ya leo, kutokufanya maamuzi peke yake! Unapaswa kuhojiwa kwa kutokufanya maamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sio kwamba tutawahoji tu walioiba lakini hata ambao hawafanyi maamuzi, kwa sababu kutokufanya maamuzi unaweza ukasababisha hasara kubwa sana. Hili shirika la ATC, sio hoja ya leo. Hii leo hoja ya watu wa UDA, sio hoja ya leo! Kuna barua mpaka za Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini mpaka watu wapige kelele ndio Serikali iamue! Halafu inasema ni sikivu! Hii Serikali ni kiziwi, ondoeni kikosi hiki chukueni vijana wengine, wawekeni pale tuwa-test na wao. Miaka mitano kama mtabadilisha mara saba, mtajjua. Lakini tunataka Serikali ambayo inawajibika! Hatuwezi tukawa na Serikali ambayo haiwajibiki, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo angalia kuna Wabunge wanasoma barua ya Waziri kwenda kwa Waziri Mkuu, tangu jana na Waziri wala hashtuki! Hiyo ni *failure of the State!* Yaani ni *failure* ya *State*. Katika mazingira ya kawaida mtu angeshtuka eeh! Yaani kuna barua ya Waziri! Ya maoni ya Waziri, kwenda kwa Waziri Mkuu, imevuja Wabunge wanainukuu! Waziri hashtuki! Anaona kawaida tu! Ooh! Itakwenda kweli nchi hii! Katika mazingira ya kawaida, tungekwishasikia saa hizi kwamba, ninyi ambao mnanukuu hiyo barua, hiyo barua mmeitoa wapi? Ikoje? Kwa sababu, naamini kwamba hii ni *Confidential/inatoka* kwa Wizara inakwenda kwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Aah haa, nina Mwongozo wa kwanza, pasifuate Miongozo mingine. Dokta Kigwangalla.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Utumie muda mfupi kwa sababu nina dakika mbili.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, *inshallah* nitajitahidi.

Mheshimiwa Spika, na-refer Kanuni ya 68 (7), ambayo inanipa wajibu wa kukuomba Mwongozo kama kuna jambo linanitatiza. Naomba ku-refer na kuomba Mwongozo kwa kutumia Ibara ya 63 ya Katiba, Fasili ya II, ambayo naomba niisome.

Mheshimiwa Spika, inasema: "Sehemu ya pili ya Bunge, itakuwa ndicho Chombo Kikuu cha Jamhuri ya Muungano, ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii." Ukienda mbele, Ibara hiyo ya 63 (c)...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, nina dakika moja, sina muda! Unataka kusemaj?

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, inasema kwamba...

SPIKA: Wewe mwenyewe unataka kusema nini? Hiyo Katiba, tunajjua!

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, kwa (c) inaongelea kuhusu wajibu wa Bunge, katika kujadili Mikataba. Sasa hapa, nimeona kuna Mikataba kama mitatu katika Wizara hii ya Uchukuzi, ambayo imekuwa inajadiliwa na ambayo tayari iko *thought*. Wa kwanza ni Mkataba baina ya Serikali na *RITES*, wa pili ni Mkataba wa UDA na wa tatu ni ule Mkataba baina ya Serikali na Shirika la *CADCO*, liko kwenye Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, sasa nikashindwa kuelewa, hii Mikataba iliflikishwa Bungeni ikajadiliwa na ikapitishwa na Bunge, ili kutoa *go-ahead* ya kwenda kuitekeleza au la na kama la, je, huu ni ukiukwaji wa Katiba au la? Nashindwa kuelewa kwa sababu nimekuwa nikifuatilia naona Mikataba ya *RICHMOND*, ya *DOWANS*, ya Madini na yote ni Mikataba ya hovyo!

Mheshimiwa Spika, sasa je, hii Mikataba inawajibika kupita Bungeni au haiwajibiki kuptitishwa Bungeni? Naomba Mwongozo wako.

SPIKA: Haya, ahsante. Mwongozo utapewa baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, hatuna matangazo mengine. Nasitisha shughuli za Bunge, mpaka saa 10.00 jioni.

(*Saa 07.15 mchana, Bunge lilitungwa mpaka saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. GOODLUCY J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Omari Nundu, Waziri na Mheshimiwa Athumanji Mfutakamba, Naibu Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Nawapongeza pia viongozi wa Wizara kwa jitihada kubwa wanazofanya kujenga na kukarabatiwa miundombinu ya reli, bandari na viwanja vya ndege ambavyo kwa sehemu kubwa ni chakavu sana. Nina uhakika kuwa tukishirikiana na kuelimisha jamii umuhimu wa miundombinu hiyo na kutengewa fedha za kutosha kujenga upya.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu Viwanja vya Ndege. Katika Kitabu cha Maendeleo, Kifungu 1003, Kasma 4209 uwanja wa ndege wa Mwanza nimeona kuwa zimetengwa Sh.17,529,380,000/= kwa mujibu wa Kanuni ya 61(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2007, natamka kuwa nina maslahi na jambo hili. Ninavyokumbuka mwaka 2007/2008 Serikali ilipokea kiasi cha US\$12,000,000.00 toka Kuwait Fund na Sh. 7,130,000,000.00 toka TCRA. CAG alitoa hoja kadhaa juu ya matumizi ya fedha hizo ambazo zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza. Naomba kujulishwa kazi iliyotekelizwa kwa kutumia fedha hizo kwani sijaona mabadiliko makubwa tokea fedha hizo zitolewe.

Mheshimiwa Spika, nimeona kuwa karibu kila kiwanja cha ndege kinachomilikiwa na Serikali kimetengewa fedha katika bajeti hii. Hii husababisha kutokuwepo mradi mmoja utakaotekelizwa na kukamilika kwa dhati mfano, Songwe Airport ambayo ilianza siku nyingi na kwa kutambua umuhimu wake kwa uchumi wa Taifa ingepewa kipaumbele na hivyo kutengewa fedha za kutosha kukamilisha ujenzi wake. Nashauri kuwa utaratibu huu utumike miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kuhusu reli. Reli ni moja kati ya mihimili muhimu ya Taifa letu. Kwa kutambua umuhimu huo nashauri yafuatayo yafanyike ili kuwa na njia ya reli yenye kuaminika.

(a) Reli ya Dar es Salaam – Kigoma na Tabora – Mwanza zijengwe upya kwa geji ya Kimataifa.

(b) Reli ya Tanga – Mnyusi – Arusha ijengwa upya. Aidha, ahadi ya siku nyingi sana ya kujenga reli ya Arusha – Musoma itekelizwe.

(c) Ijengwe reli toka Shinyanga hadi Bukoba na Kampala ili kuwa na njia ya uhakika ya kusafirisha mizigo na abiria toka maeneo hayo.

(d) Reli ya TAZARA iboreshwe ili ihudumie Mikoa ya Nyanda za Kusini kwani Zambia ina njia mbadala kuptitia Msumbiji. Vile vile ijengwe reli toka Makambako hadi Songea - Mbambabaya.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa reli ikitengwa hudumu zaidi ya barabara na pia uwezo wake ni mkubwa kuliko barabara. Tutoe kipaumbele kwa reli.

Mheshimiwa Spika, nne, ni kuhusu usafiri wa anga. ATCL Taifa letu limekuwa likipoteza fedha nyingi sana kwenda nchi zenye mashirika ya ndege yanayotoa huduma nchini. Serikali imewekeza fedha nyingi sana kwenye Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwa ajili ya ununuzi, ujenzi wa miundombinu na uendeshaji wa kampuni. Hata hivyo, kampuni hiyo bado haitoi huduma kwa sababu ya ubadhirifu. Nashauri yafuatayo:-

(i) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iwekeze na kufufua kampuni hiyo. Kampuni hiyo ikifanya kazi kwa ufanisi itaongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini na pia kuongeza idadi ya mizigo inayosafirishwa kwenda nje hususan mboga, matunda na maua.

(ii) Bodi na Menejimenti iteuliwe na kupewa malengo yenyenye motisha penye nafaka na adhabu wakishindwa.

Mheshimiwa Spika, huduma za *precisionair*. Kampuni hii sasa hivi hutoa huduma kwa ukiritimba kwani haina ushindani wa dhati. Kwa sababu hiyo imekuwa na kawaida ya kutozingatia ratiba yake ya ndege kutua na kuondoka. Nashauri kuwa mdhibiti wa sekta achukue hatua za kufuatilia utendaji wa Kampuni hii na kuchukua hatua ili wajirekebishe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, usafiri wa wananchi wa Mwambao wa Ziwa Tanganyika ni usafiri wa meli. Katika ziwa hilo kuna meli ya kihistoria nayo ni ile ya MV. Lyemba, meli nyingine ni ile iitwayo Mwongozo.

Mheshimiwa Spika, je, kuna mpango gani wa kuongeza meli za kisasa na ngapi na kukarabati hizi za zamani ili kupunguza msongamano na matatizo ya wana Kigoma na Rukwa ikiwa ni utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga bandari sehemu zote zinaposimama yaani kila kituo ili kuepusha ajali wakati wa abiria kuingia na kushuka? Pamoja na kuliangalia jambo hili naomba Kilando kama kituo chenyeh watu wengi kipewe kipaumbele kwani pia hulima mpunga kwa wingi na mhogo unaokuwa kuelekea katika nchi ya Zambia.

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga ni kiwanja kisichokidhi kwa aina yoyote iitwayo kiwanja cha ndege, magari, baiskeli, pikipiki na watu, mifugo vyote hupitia humo. Kiwanja hicho kimeharibika vya kutosha. Je, kuna mpango gani wa kujenga kiwanja kipyatikatika mji wa Sumbawanga?

Mheshimiwa Spika, najua kuna hali ngumu ya kifedha katika Serikali yetu lakini niiombe Serikali yako katika matengenezo yatakayofanyika, niiombe Serikali ituwekee uzio katika kiwanja chetu kuepuwa uharibifu wa kiwanja hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya wafanyakazi wanaoishi mikoani wa Shirika hilo hasa la ndege walivyochoka pengine kwa hali ngumu ya maisha, wawezeshwe na si hivyo tu katika kusimamia mapato ili kampuni zetu zisizidi kuzorota lazima wakubwa wa mashirika haya wawajibishwe mara kwa mara ili wasijisahau.

Mheshimiwa Spika, tulitumainishwa kuwa utakapomalizika ujenzi wa mkongo wa *optic fibre*, bei za simu za mkononi zitapungua. Je, ni sababu gani hadi sasa bado bei hazijapungua?

Mheshimiwa Spika, hakuna jambo jema litakalowafurahisha Watanzania wengi walio maskini kama mtaimarisha njia na usafiri wa Reli.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali itulie sana kutafuta ni jinsi gani inavyoweza kuboresha Wizara hii ya Uchukuzi kwani hapa ndipo hazina ya Mtanzania ilipo.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Serikali haitaona umuhimu wa Wizara hii, basi ni kutuacha Watanzania kama watoto yatima waliotupwa porini na kuishi bila matumaini.

Mheshimiwa Spika, nchi ya India baada ya kugundua kama wao ni maskini waliazimia kila Wilaya kuweka usafiri wa treni hivyo kumfanya mwananchi wa India angalau kupata unafuu katika maisha japokuwa nchi ile ina watu wengi. Je, Serikali haiwezi kutafuta njia kama hiyo ili kumpunguzia makali Mtanzania wa kawaida ambaye anashindwa kupanda hata *bus* kwa nauki kuwa juu.

Mheshimiwa Spika, hii ni pamoja na kuboresha kituo cha Kilando, Nkasi, Namanyere, Rukwa ili kuboresha maisha bora kwa kila Mtanzania pamoja na Kabwe ili kuamsha kasi mpya kwa wana Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. AHMED J. NGWALI: Mheshimiwa Spika, *SUMATRA* ndio yenyе dhamana na vyombo vyote vya baharini lakini kwa bahati mbaya *SUMATRA* wameshindwa kabisa kusimamia vyombo hivyo, hii inatokana na ukweli kwamba ajali za majini zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku na kujenga hofu kwa abiria na mali zao.

Mheshimiwa Spika, ushahidi unaonesha katika miezi ya Juni na Julai kila mwaka ndio miezi inayotokea ajali nyingi kuliko miezi yoyote baharini. Hivyo, tunaiomba Serikali ifanye jitihada za makusudi katika kuhakikisha ajali hizo zinapungua.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya hali ya hewa katika miezi hiyo ndio chanzo cha ajali hizo, hivyo ,operesheni maalum iandaliwe na *SUMATRA* katika miezi hii ili kuweza kutambua vile vyombo ambavyo havina uwezo wa kusafirisha abiria visipewe idhini hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni kawaida ya *SUMATRA* kufanya ukaguzi wa vyombo vya baharini baada ya ajali kutokea, naiomba ibadilishe mfumo wake na ifanye ukaguzi kabla shughuli za vyombo hivyo havijaanza shughuli zake. Naamini ukaguzi ukifanywa mapema utapunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni jambo la kawaida kwa vyombo vya baharini kuongeza bei kiholela, ulangizi wa kupindukia wa tiketi za vyombo hivyo, lakini inashangaza *SUMATRA* kama msimamizi wa taasisi hiyo wamenyamaza kimya na hawana habari na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya baharini huwa vinajaza abiria kupindukia lakini hakuna hata mtu mmoja wa *SUMATRA* ambaye anafanya ukaguzi kabla meli au boti kuondoka. *Passenger manifest list* ambazo makampuni ya vyombo baharini yanazipeleka sio sahihi na hupelekeva vyombo hivyo kujaza abiria kinyume na uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, uchakavu wa vyombo vya baharini ni kikwazo kikubwa kwa wasafiri wa majini, mara nyingi vyombo husimama majini na kupelekeva abiria kupata usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa utekelezaji uliotukuka na ufanisi wa maendeleo ya nchi yetu naiomba Serikali isimamie shughuli zote za kimaendeleo ya nchi hii ili wananchi wake walio na busara waweze kuamini na kukubali utekelezaji uliotukuka wa Serikali. Serikali iliyio makini inahitaji kusikiliza mawazo ya wananchi wake na kuyafanya kazi. Ahsante

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi inabeba dhima kubwa ya kuchangia maendeleo ya Taifa kukiwa na mtandao mzuri wa mawasiliano. Barabara, usafiri wa reli, usafiri wa majini, usafiri wa anga, simu, fax na sasa intaneti.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa njia za uhakika za usafiri ndani ya nchi kunarahisisha sana usafirishaji wa idadi kubwa ya watu na kiasi kikubwa cha bidhaa kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine. Vile vile katika hili mbali ya kuokoa muda lakini lina mchang'o mkubwa katika kushusha gharama za biashara na hatimaye bidhaa. Suala hili linasaidia sana kuwepo kwa maingiliano ya watu katika jamii na hivyo kufanya watu wa upande mmoja kujifunza kutoka kwa watu wa upande mwininge. Kwa ujumla mtandao huu wa mawasiliano unaotokana na uchukuzi unaongeza tija kwa kiwango kikubwa, iwe ni kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya uchukuzi bado Tanzania ina matatizo makubwa ya mawasiliano ya barabarani, ardhini kwa maana ya usafiri na usafirishaji. Sehemu kubwa ya mtandao wa barabara uko katika hali mbaya kabisa. Kielelezo cha ubovu wa barabara zetu si kitu kigeni kabisa kwa wakazi wa miji yetu na ndio kukawa na tatizo la kufanya baadhi ya mikoa inayozalisha bidhaa mbalimbali kukosa uchukuzi wa kuhamisha biashara na bidhaa zao kupeleka sehemu nyingine jambo ambalo linarejesha nyuma juhudzi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna njia kuu tatu za reli. Ya kwanza, ni njia ya Reli ya Kati ambayo imeanzia Dar es Salaam hadi Kigoma na ambayo ina tawi lilioanzia Tabora hadi Mwanza. Vilevile tuna reli ya pili iliyoanzia Tanga hadi Moshi na Arusha yakiwemo matawi moja linaloanzia Korogwe hadi Dar es Salaam na lingine limeanzia Kahe (Mkoani Kilimanjaro) hadi Taveta mpakani mwa Kenya na Tanzania. Reli ya tatu ni ile ya TAZARA inayoanzia Dar es Salaam hadi Tunduma mpakani mwa Tanzania na Zambia.

Mheshimiwa Spika, reli hizi zilijengwa na wakoloni wa Kijerumanji kati ya mwaka 1896 -1905 wakiwa na lengo la kusafirishia mazao kama vile kahawa, pamba na katani kufikia kwenye bandari za Tanga na Dar es Salaam. Hatimaye wakoloni wa Kiingereza nao walizitumia kwa malengo hayo hayo ya usafirishaji wa mazao. Kudidimia kwa kilimo cha mazao ya biashara baada ya uhuru na kuwepo kwa barabara zinazounganisha Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Dar es Salaam kumepunguza kwa kiasi kikubwa, umashuhuri wa Reli ya Tanga. Ili umaarufu wake urejee itabidi juhudzi kubwa zichukuliwe kwa kuongeza wingi wa mizigo inayohitaji kufikishwa bandarini Tanga.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kwamba kuhuishwa kwa shughuli za kilimo na biashara katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga yenye kutatua mchang'o mkubwa katika kufanikisha hili, katika hili mchang'o mkubwa zaidi utatokana na kufanikisha juhudzi za kuhakikisha kuwa bidhaa za Uganda na pengine Rwanda zinazosafirishwa kupitia reli hii kwenda na kutokea bandarini Tanga, ili suala hili lifanikiwe ni lazima lijengwe Tawi la Reli litakalounganisha mikoa niliyoitaja.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa Reli ya TAZARA iliyojengwa mwaka 1970 – 1975, kwa msaada kutoka China na kwa ushirikiano wa Tanzania na Zambia. Reli hii ilijengwa kwa kuzingatia zaidi hali ya kisiasa iliyojengwa kusini mwa Afrika katika miaka ya sabini kuliko mahitaji ya kiuchumi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika usafiri wa majini bado Serikali imedorora jambo ambalo laiti kama si watu wenye uwezo wa kuwekeza basi Watanzania wangekuwa hawana uwezo wa kusafiri kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine, jambo ambalo ni aibu kwa nchi ambayo inajigamba kwamba inaendelea kutawala kwa kipindi cha miaka hamsini sasa ambayo ni nusu karne nzima sasa.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa baharini ni dhaifu kiasi ambacho mwananchi analazimika kulala sehemu asiyotarajia kutokana na ukosefu wa usafiri katika bandari zetu na kwa yule

atakayebahatika kupata usafiri anaweza akalanguliwa kwa kuuziwa tiketi ya Sh. 20,000/= kwa 40,000/= na hili hutokana na wamiliki wa vyombo hivyo, watendaji wao kuwauzia tiketi watu ambao hawana nia ya kusafiri jambo ambalo linakwenda kinyume na sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa usafiri wa Anga Tanzania imekumbwa na kadhia na aibu kubwa ya kutomiliki hata angalau ndege moja jambo ambalo hata baadhi ya viongozi wanaokuja hapa Dodoma wanakodi ndege toka kwa mashirika binafsi kwa bei ambazo hazilingani na umaskini tulionao Watanzania.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa anga ni jambo la lazima kwa Watanzania, tunasema kwamba nchi yetu ni kubwa kuliko Kenya na Uganda kuliko Zambia kuliko Rwanda, kuliko Burundi kuliko Ethiopia na wengi wao tumewatangulia kupata uhuru tuangalie nchi hizo nilizozitaja zina idadi gani ya ndege katika nchi zao tuijulize basi kuna maana gani ya kuwekewa Wizara hii ya uchukuzi na inafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, imefikia hatua Mtanzania anapokuwa na safari yake ya kutaka kusafiri ndani ya nchi kwa kutumia ndege afanye mpango wa kupatiwa tiketi wiki moja nyuma kabla ya safari yake. Sasa ni kwamba wasafiri wa ndege wapo kutoka sehemu moja ya nchi kwenda nyingine lakini kwa dharau wanayofanyiwa Watanzania, Serikali inaishia kutoa ahadi ambazo hazina utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakosa pato katika sekta ya uchukuzi kutokana na kuamini tu kwamba walio na thamani ya kupanda ndege ni watalii tu na sio Watanzania jambo ambalo ni la dharau ya hali ya juu kwa Watanzania ambao wana uwezo wa kupanda ndege hata kuliko hao wanaokuja kwa njia za kitalii lakini lengo lao ni kuja kuzipotosha jamii na sio kufanya utalii kama wanavyodai. Kwa taarifa hii naomba Watanzania wajiangalie sana juu ya vizazi vyetu vilivyopo na vijavyo.

MHE. ZAHRA ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndege ni utambulisho wa nchi, hivyo ni vizuri Wizara kujitahidi kuhakikisha kuwa ndege zetu zinarudi katika hali ya kuridhisha na kuweza kufanya kazi zake, kulipa wafanyakazi zaidi ya 180 na posho ni mzigo kwa Serikali na ni matumizi mabaya ya pesa za Serikali, pesa ambazo ni kodi ya wavuja jasho.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wimbi kubwa la wezi katika bandari zetu, jambo ambalo linakuwa siku hadi siku. Suala ambalo linawavunja moyo wafanyabiashara wetu, je, Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha jambo hili la aibu linakomeshwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia katika Wizara hii iliyowasilishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo ambayo tegemeo la uchumi wa Watanzania lakini haina pesa za kutosha, kilichobaki tunatafuta mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Ndege viwanja ni muhimu sana hasa Viwanja vya Songwe huko Mbeya, *KIA* na hata cha Mwanza. Ni lazima tuamue sasa kujenga viwanja bora na imara hasa uwanja wa ndege wa Mwanza. Kwa kuwa tunaingia katika shirikisho la Afrika Mashariki, uwanja huu utakuwa ndio kivutio kikuu cha wasafiri toka katika jumuiya hii. Bila shaka ni lazima mji huu utakuwa, hivi hatuoni tabu kuwa na kiwanja kama kilichopo. Ujenzi wa uwanja huu umekuwa ni hadithi kwa muda mrefu. Pia viwanja bila ndege ni mchosho tu.

Mheshimiwa Spika, Meli zetu ni chakavu sana, kiasi ambacho zingine zimepitwa na muda kama Meli ya Liemba, *MV Victoria* na nyingezeo meli hizi zimepitwa na wakati, hivi mpaka zilete madhara kama *MV Bukoba* na tuishie kujenga minara ya kumbukumbu. Serikali ina mpango gani

wa muda mfupi kuandaa meli mbadala ya Liemba kwani usafiri sasa wa Ziwa Tanganyika ni utata mtupu. Ni vema meli hizi zikapatiwa meli haraka ili kuja epuka ajali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari. Pamoja na bandari katika upokeaji na upakiaji mizigo, pia ni usafiri wa abiria pia, hivi naomba kuuliza pale bandarini, Dar es Salaam ambapo wanasaferia wananchi, ndani ya miaka 50 bado ukaguzi ni wa kikoloni (kupekuliwa) hasa kuna sababu gani ya kumfungulisha mtu sanduku anapokuwa akisafiri toka Dar es Salaam kwenda Zanzibar, tena mbele za watu bila kujali jinsia zao. Mfano, mama anaweza kukaguliwa sanduku lake na askari wa kiume, mbele ya foleni iliyo mchanganyiko wake kwa waume. Huu ni udhalilishaji. Hivi kuna ugumu gani kufunga mitambo ya kisasa ya ukaguzi, kama ambayo inafungwa katika viwanja vya ndege na hata hapa Bungeni. Tuone haya na tujisikie vibaya kwa udhalilishaji huu. Sasa ni wakati muafaka ndani ya miaka 50 ya Uhuru kuondokana na aibu hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupekuliwa huko lakini watokao visiwani, hulazimika kupanda ngazi ambazo ni ndefu sana, lakini tujue kuna wasafiri wazee, watoto na hata akinamama wenye watoto wadogo, ni bora tukaangalia upya jengo hili, pamoja na watumiaji hawa ambaa nimewataja hapo juu. Pamoja na hayo, kuna usumbufu mkubwa kwa wafanyakazi dhidi ya wasafiri. Tanzania bara na Zanzibar ni nchi moja, lakini hata kama umebeba 7V nchi 14 tu, wafanyakazi wa bandari watakutoza Sh. 6,500/= au zaidi ya hapo. Huu si uungwana hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, reli ni kitu cha muhimu sana, hasa katika usafiri na kusafirisha mizigo mikubwa, tunashuhudia kabisa barabara zetu zinavyoharibika kwa kuchukua mizigo mizito ambayo ingechukuliwa na reli. Pia usafiri wa treni kwa abiria ni muhimu sana na ni rahisi na ni usafiri wa watu wa hali ya chini na watu wa kawaida. Tunaitaka Serikali kuangalia upya reli zetu hasa reli iendayo Kigoma, Mpanda pamoja na Mwanza. Kigoma maisha yanakuwa juu sana sababu bidhaa zinasafirishwa kwa gari, ambapo barabara ni mbaya, matokeo bidhaa kupanda bei sana. Reli ya Mpanda ingeweza kusafirisha shehena za mahindi na bidhaa nyinginezo na ungekuwa msaada mkubwa pia kwa wakulima na hata watakoahuduma ya mahindi kwa unga, bei ingekuwa chini kulingana na uchukuzi wa reli. Watu hawa wanabeba mahindi kwa maroli, na ndio maana bei ya mahindi iko juu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya hewa. Naiomba Wizara iimarishe Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma. Kwani chuo hiki majengo yake ni machache, madarasa pia hata mabweni. Ni vizuri sana tukachukua hatua ya kukiweka chuo hiki. Wataalam wetu wasome na kupata ujuzi wa hali ya juu. Ahsante.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na matatizo sugu ya sekta ya uchukuzi nchini kama ifuatavyo:-

- (a) Shirika la Reli nchini limedhoofika vibaya na hivyo kudumaza shughuli za usafirishaji wa watu na bidhaa hivyo kuathiri uchumi wa Taifa.
- (b) Shirika la Ndege (ATC) liko katika hatua ya kufilisika na kufa kabisa.
- (c) Huduma za meli na bandari ni duni kiasi kwamba athari zake kwa uchumi wa nchi hii haisemeki.

Mheshimiwa Spika, imani yangu ni kwamba Serikali kuitia Wizara ya Uchukuzi ichukue hatua madhubuti na za haraka kuinusuru nchi yetu kuondokana na jinamizi hili la kujikongoja na kuonyesha dalili za kufa na badala yake zichukuliwe hatua za kuwekeza zaidi katika sekta hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, Taifa la Tanzania limejaliwa kuwa na rasilimali za kutosha ambazo ni pamoja na Rasilimali Watu, Rasilimali za Madini, Rasilimali za Mbuga za Wanyamapori, Rasilimali ya Bahari na Maziwa na Ardhi.

Mheshimiwa Spika, rasilimali zote nilizotaja hapo juu zina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Rasilimali watu ndio inayozitawala rasilimali zingine zilizosalia na kwa mantiki hiyo kutokana na rasilimali watu tunapata wasafiri na wasafirishaji na ndio wanaotoa fedha kama nauli na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Rasilimali watu ina mchango katika sekta ya Madini na kwa maana hiyo uimarishaji wa huduma ya reli ikiwa ni pamoja na kujenga mfumo mpya wa reli unaoendana na viwango vya Kimataifa na hatimaye kuwa na treni zinazoendeshwa kwa nguvu za umeme.

Wakati Taifa letu linajielekeza katika kuvutia wawekezaji zaidi kutoka nchi za nje. Kwa mfano, uchimbaji wa makaa ya mawe na chuma huko Liganga na Mchuchuma, Serikali ione uwezekano wa kujenga njia ya reli kupitia maeneo tajwa hapo juu kuanzia bandari ya Mtwara, reli hii itasaidia sana pia kwa maendeleo ya ukanda huo wa Kusini mwa Tanzania ambako kuna utajiri wa Gesi, Urani na mazao ya Korosho, ufuta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, siku za baadaye Serikali iongeze kasi katika kuratibu uharakishwaji wa ujenzi wa reli ya kutoka Isaka kwenda nchi za Rwanda na Burundi itakayopitia pia katika Jimbo letu la Mbogwe, uwepo wa reli hii utakuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa ndege mpya kwa ajili ya Shirika la Ndege Tanzania na pia ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya Dar es Salaam, Mbeya, Kilimanjaro na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Mwanza upewe kipaumbele kwani bandari duniani kote zimekuwa na michango mikubwa katika uchumi wa Mataifa mbalimbali duniani hususan katika biashara za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke katika mipango yake ya maendeleo ununuzi wa meli mpya za abiria baharini na katika maziwa makuu na meli za kusafirishia mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, narejea pia kusisitiza juu ya umuhimu mkubwa wa kuwekeza zaidi katika sekta ya uchukuzi nchini kwa upande wa Serikali. Kwani bila Serikali kuwa makini na kuwekeza kwa nguvu zaidi hasa kwenye reli ni dhahiri Taifa letu litakuwa linaachwa nyuma katika zama hizi za karne ya ishirini na moja.

Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano hasa reli ni muhimu katika sekta ya ulinzi na usalama wa Taifa. Sote tunakumbuka kwa namna ya pekee reli ya kati na ile ya TAZARA jinsi zilivyosaidia katika harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika na vita katи ya nchi yetu na nchi ya Uganda na kwa majanga mbalimbali yakiwemo wakimbizi na maafa ya mafuriko.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iipatie fedha zaidi Wizara hii ya Uchukuzi vinginevyo tutakuwa tunaigiza tu kwamba tunataka kuinua uchumi wa nchi hii.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwamba Shirika la Ndege (ATC) limekuwa, ni jambo la kulitafakari sana ni kwa nini Shirika hili linakuwa ukizingatia kwamba lilikuwa likifanya kazi na likizalisha sana, ajabu ni kwa nini lishindwe kuijendesha.

Mheshimiwa Spika, yafaa tujifunze kwa nchi nyingine ni vipi wao wanaweza kuanzisha na kutoa mashirika yao kama hili la kwetu na kwamba wenzetu wanaendelea. Jambo ambalo naliona hapa kwetu, ni tatizo la kutokuwa na utaratibu wa uwajibikaji kwa watendaji wetu lakini pia aliyepewa nafasi kujihalishia kufanya kila apendacho bila kujali kwamba yeze yupo pale kama milanzi na msimamizi wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la ATC yafaa kabisa kwa namna yoyote hata kama ni kwa kuingia ubia na watu binafsi lakini lifufuliwe ili angalau tuweze kulinda ile pitcha halisi ya nchi yetu ya kwamba tunazo ndege zinazomilikiwa na sisi wenyele lakini pia kuendelea kuvutia baadhi ya watalii ambaa baadhi yao wanapofika hapa nchini huwa na hamu ya kutembelea maeneo mbalimbali ya nchi yetu kwa urahisi lakini pia kukidhi haja yao ya kuona vivutio mbalimbali ikiwemo wanyama pamoja na Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa majini. Usafiri wa maboti pamoja na meli hapa nchini ni katika usafiri ambao unatumiwa na wananchi wengi sana katika harakati zao za maisha, lakini inatia shaka kwamba vyombo hivi (meli na maboti) vinavyoonekana kwamba vina umuhimu wa lazima kwa hapa kwetu kutumika ili kusaidia kupunguza usumbufu, tatizo la Serikali ni kwamba hakuna utaratibu wa ukaguzi kwa vyombo hivyo jambo ambalo linasababisha vifo kwa wananchi ambao hutumia vyombo hivyo nya majini katika safari zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, *Tanzania Port Authority (TPA)* ni shirika lenye mamlaka ya kusimamia, kukuza na kuinua uchumi wa nchi yetu. Kwa kupitia *TPA*, bandari zilizopo ndani ya nchi yetu zinaweza kuzidi kulingizia Taifa mapato mengi zaidi kulinganisha na hali ya sasa. Bandari zetu hivi sasa zinatishia hali ya biashara kwa watu wanaotumia bandari zetu hasa ile ya Dar es Salaam kutoptaka na wizi wa bidhaa katika bandari hizo.

Mheshimiwa Spika, kama hatutaangalia na kuchukua hatua za makusudi za kudhibiti hali hii ya wizi bandarini, tunaweza kupoteza mapato mengi kwa kukosa wafanyabiashara ambao wataendelea kutumia bandari yetu. Wizi unaofanywa wa vifaa nya magari na baadhi ya bidhaa nyingine inawapa hasara kubwa wafanyabiashara ambao kila siku wanatozwa ushuru na *TRA* lakini mizigo yao inapotea ndani ya mazingira ya bandari yetu eneo ambalo lina ulinzi muda wote, jambo ambalo linawatia hasara wafanyabiashara ambao kila wakati hutegemea zaidi kupata faida na sio hasara, sambamba na hilo, mizigo pia hukaa muda mrefu bandarini jambo linalopelekeea mrundikano wa bidhaa (makontena) na hapo ndipo wizi unapotokea, hata wezi wenye wanaopata maficho kwa mrundikano huo mkubwa wa bidhaa.

Mheshimiwa Spika, hata utaratibu wa kutozwa ushuru kwa bidhaa zinazoingia bandarini, haueleweki kwani maofisa wa *TRA* na wenye bidhaa hupatana bei za bidhaa na sio kwamba kwa kontena la futi fulani lenye bidhaa za aina fulani ni kiasi fulani cha ushuru jambo hili linafanywa kama kwamba watu wako mnadani. Naishauri Serikali iusimamie utaratibu huu na marekebisho yafanyike na yawe wazi na yanayoleweka ili mfanyabiashara awe anaelewa kwamba nikichukua bidhaa ya aina fulani katika kontena la ukubwa fulani basi nitatakiwa kulipa kiasi fulani, kwani utaratibu uliopo unatia shaka ya kuwepo harufu ya rushwa kubwa kwa watendaji wanaopokea toka kwa baadhi ya wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wote kwa kazi nzuri na ngumu ya kusimamia na kuendeleza njia kuu zetu za uchukuzi. Zote zina changamoto zilizo wazi zenye kuhitaji umakini wa uzalendo mkubwa katika kuzisimamia na kuziendeleza au kuziendesha.

Mheshimiwa Spika, langu kubwa liko katika usafiri wa ndege na hasa *ATCL*. Athari za kutokuwa na usafiri wa ndege wa uhakika ni kubwa kwa uchumi wetu wa nchi.

Mheshimiwa Spika, utalii ni sehemu moja inaathirika. Mfano *KQ* inabeba *Monopoly* ya ku-*attract* watalii kwa misingi ya usafiri wa uhakika kuja Afrika Mashariki. Hili liko katika uwezo wetu kulibadili kama tuna nia ya dharti.

Mheshimiwa Spika, kazi iliyokuwa inaonekana imeanza pale Kipawa, kwa mfano, kuzungushia uzio na kadhalika inaonekana imesimama. Ni nini maelezo ya kazi ya upanuzi au ujenzi wa *phase* hiyo ya III. Tukizingatia umuhimu wa Julius Nyerere kuwa *Hub*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ndege tatu na ziko matengenezioni? Je, sasa hivi ziko karibu kukamilika. Zikikamilika na kurudi, je, tuna watendaji wa kutosha kuzihudumia (*Engineers, Technicians*, pamoja na kutambua uwepo wa wafanyakazi wa shirika ambao wanaendelea kulipwa wakati hazipo ni muhimu, pia kuhakikisha mafunzo *specific* kwa ndege

tunazozitumia yanafanyika kwa watendaji, tusijeleta ndege ndio tukute tunahitaji watu *with skills* za kuzihudumia.

Mheshimiwa Spika, mipango yote ya upanuzi wa viwanja vya ndege na ununuzi au ukodishaji wa ndege mbalimbali kwa maana ya kusaidia usafiri wa ndege uendane na matayarisho ya dhati au endelevu na ya kudumu ya wafanyakazi wa ngazi zote. Hata upanuzi wa kiwanja cha Julius Nyerere utahitaji uwepo wa wafanyakazi na ndege za kutosha ili ufanye kazi vizuri na uwe na manufaa.

Mheshimiwa Spika, kuwe na mpango wa dhati kabambe wa kufufua *ATCL* kama dharura. Kwa mfano, mnaweza kuhakikisha tuna ndege mbili za 773 *Das* 300 kwa sasa na *support* zake ziwe zinafanya kazi kwa mpango chanya *full capacity* wakati mipango mingine inaendelea. Ndege zinazotengenezwa ziwe na uwezo wa kuendesha ndani na nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu bila kusita kubadili Bodi na *Management* iliyofikisha *ATCL* hapa au katika hali hii bila kuchelewa. Nashauri kuwe na mikakati ya dhati *based on the performance contract* ya kuwezesha kuwa na *Hub* ya Julius Nyerere *Airport*. Kama ni lazima basi pesa ya barabara ikatwe ipelekwe kwa ndege baada ya kuhakikisha tuko *serious* na hili ili lifanikiwe.

Mheshimiwa Spika, bado hakuna mkakati wa kuridhisha kuhakikisha reli ya Dar es Salaam – Kigoma inafanya kazi kikamilifu. Naomba tena kama kuna uwezekano wa kuhakikisha fedha za barabara zinakatwa na zinakwenda kwenye sekta ya reli kwa kuanzia ile ya kati.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *TAZARA* irekebishwe ili nafasi ya *MD* ipokezane baina ya nchi hizi mbili.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai anayoendelea kutupa na kutuwezesha kuwa hai leo hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa masikitiko yangu kwa Serikali kwa kuititia Wizara hii, kwa kweli sijui ni kwa kiasi gani Serikali imepuuza sana uchukuzi katika nchi hii ya wakulima. Bila uchukuzi hakuna maendeleo yatakayoonekana kama tunavyotegemea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu reli. Reli ya kati imekuwa kichocheo kikubwa sana kwa ukuaji wa uchumi hapo zamani, lakini sasa kuzorota kwa reli kumeleta adha na kuperomoka sana kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Pia kumekuwa na upitishaji wa mizigo mikubwa na mizito kuititia barabara badala ya reli na hii imekuwa chanzo cha ajali za barabarani na uharibifu mkubwa wa barabara. Ni muda muafaka sasa wa kuifufua reli ya kati kwani kuna madhara kwa kuikosa reli hii.

Mheshimiwa Spika, ipo mipango ya kujenga reli ya Musoma-Tanga na kupanua bandari ya Musoma kwa ajili ya kuhudumia nchi za maziwa makuu na Sudani ya Kusini (JUBA). Ujenzi wa reli hii bado umekaa sana sana kisiasa, bado hazijaonekana dalili za kutia matumaini kabisa kwa utekelezaji wa ujenzi wa reli hii na upanuzi wa bandari ya Musoma.

Mheshimiwa Spika, ni muda mzuri sasa kuwajulisha wananchi wa maeneo ambayo reli itapita ili kuwaandaa kuachia maeneo yatakayopita reli hiyo mapema ili kuepuka usumbu na migogoro ya fidia ambayo inaweza kujitokeza wakati wa utekelezaji. Hili likizingatiwa litawezesha sana utekelezaji wa haraka bila migogoro.

Mheshimiwa Spika, Bandari zetu hasa ya Tanga na Mtwara ni kichocheo cha uchumi wa Tanzania lakini zimeachwa au kuendeshwa kwa kiwango kidogo sana na hii imepelekea mrundikano wa shehena katika bandari ya Dar es Salaam, upotevu wa mizigo na ucheleweshaji wa kupakua na kupakia shehena za nchi na nchi jirani zinazohudumia na bandari zetu. Ucheleweshaji na mrundikano wa shehena ya mizigo bandarini umepelekea kukimbiwa na watumiaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, bado kuna uhitaji mkubwa sana wa kujenga bandari kavu (*Dry ports*) na kuimarisha zilizopo ili kupunguza shehena na kusaidia ufanisi wa shughuli za bandari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Viwanja vya Ndege. Kumekuwa na ujenzi wa viwanja vidogo vya ndege ambavyo vipo migodini vinavyopelekea mashaka kwa wananchi kwani yatendekayo katika viwanja hivyo yamekuwa na aina fulani ya usiri. Ni vizuri sasa kutumia viwanja vya ndege vilivyopo na kuviimarisha kabla ya kuruhusu vidogo vidogo vinavyojengwa migodini ili kuwe na uwazi na ukusanyaji mzuri wa mapato.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa ya mipakani kama vile Mkoa wa Mara (Musoma) katika eneo la Nyasusura.

Mheshimiwa Spika, eneo hili lilitengwa maalum kwa ujenzi wa kiwanja kikubwa cha ndege, kwa ajili ya mizigo na abiria tangu 1967. Lakini hadi leo hakuna dalili za ujenzi wa kiwanja hicho ambacho tayari eneo lipo na halihitaji kulipa fidia. Ujenzi wa kiwanja hiki utasaidia kusafirisha minofu ya samaki nje ya nchi na pia mizigo.

Mheshimiwa Spika, Musoma kuna Viwanda vya Kusindika Minofu ya Samaki ambayo huuzwa nje ya nchi kwa kupitia viwanja vya ndege vya Kenya.

Mheshimiwa Spika, bado viwanja vya ndege vya Mwanza, Mbeya na maeneo ya nchi vinahitaji sana kuboreshwa ili kuvutia mashirika mengi ya ndege kufanya safari za ndani na kutoa huduma za usafiri nchini na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, bado hali ya kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam hakipo tena katika hadhi ya Kimataifa, bidii inatakiwa kurudisha hadhi ya kiwanja hiki ili pia kiwavutie abiria wengi kutumia Kiwanja cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Ndege (ATCL). Inatia aibu kwa nchi ya vivutio vya utalii vinavyotegemea watalii kutoka nje ya nchi na hatuna Shirika la Ndege la kuwaleta watalii kutoka nje na kuwarudisha na pia kutoa huduma za Anga (usafiri) ndani ya nchi. Sasa ni muda muafaka wa kukopa na kulifufua Shirika la Ndege kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii kiuchumi. Shirika la Ndege lisiwe la abiria tu bali pia mizigo ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka kuendeleza utalii na kukuza uchumi basi sasa tufufue Shirika letu la Ndege.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Waziri wa Uchukuzi pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuiendeleza vizuri Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda niishauri Serikali kwamba tuanze na kuimarisha miundombinu ya reli ili tupunguze usumbufu wa usafiri wa wananchi wetu pamoja na mizigo. Tukifanikiwa kushughulikia reli na ikaanza kufanya kazi, basi barabara zetu zatabakia kuwa salama kwani mizigo inayopitishwa ni mikubwa mno na inaharibu barabara zetu. Ni vema Wizara hii ikapewa pesa za kutosha ili iweze kufanya kazi kabla ya barabara zetu zisizidi kubomoka kwa kuitishwa mizigo mizito inayozidi viwango vya kuitishwa kwenye barabara.

Mheshimiwa Spika, nashauri magari yanayopitishwa kwenye mizani yanapozidi uzito, basi yasilipishwe faini na baadaye yakaruhusiwa kuendelea na safari. Ni vema yakazuiwa na kutakiwa kupunguza mizigo na baadaye ndio yaruhusiwe kuendelea na safari zake.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Serikali ikatae mauzaji ya hisa za UDA. Hisa hizi zimeuzwa kwa bei rahisi sana, iweje mali za Uda ni nyingi sana na ziuzwe kwa bei ndogo namna hii. Na hizo fedha ziingizwe kwenye *account* ya mtu binafsi na zisiingizwe kwenye *account* inayohusika. Inavyoonekana mauzaji haya yana udanganyifu mkubwa, naomba Serikali iingilie katika na pafanywe uchunguzi wa kutosha ili ujulikane ukweli wa mauzaji haya ya hisa za UDA.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni vyombo vyoma bharini. Kwa kiwango kikubwa vyombo vyetu vyoma bharini ni vibovu sana na vinahatarisha maisha ya abiria ambao ni wananchi wa Tanzania na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali yangu iweze kuwa imara katika kukagua vyombo hivi mara kwa mara ili kuondosha maafa yanayojiteza mara kwa mara hasa katika vyombo (boti) ziendazo safari zake toka Dar es Salaam – Unguja – Pemba.

Mheshimiwa Spika, pili, ni usafiri wa anga. Kwa kuwa utambulisho wa nchi yoyote katika dunia hii kwa upande wa usafiri wa anga ni kuwa na ndege zake ambazo zinatambulisha jina la nchi. Mfano Air Tanzania, Ethiopian Air, Kenya Airways na kadhalika. Nasikitika kuona kwamba Tanzania ambayo ni nchi kubwa kuliko nchi zote za East Africa na Afrika kutokuwa na ndege yake wenyewe. Hii ni aibu kubwa kwa nchi yetu ya Tanzania kutokuwa na ndege yake inayotambulisha Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kurejesha huduma ya ndege yenyenye Nembo ya Tanzania ili uchumi wetu uweze kuimarisha na pia kuweza kuthaminiwa na nchi nyingine. Imekuwa Shirika halifanyi kazi na badala yake kuleta mzozo kwa wafanyakazi wa shirika hili? Serikali ifanye kila jitihada zitafutwe fedha japo za mkopo ili inunuliwe ndege mpya ya Air Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, Wizara hii haijajipanga vizuri. Pesa ilizopewa katika bajeti hii ni ndogo sana. Tunapoteza uchumi na fursa kuu za kujiletea maendeleo kwa mfano, Bandari zetu za Dar es Salaam na Tanga tutazifunga au zitabaki kuhudumia wateja wa ndani tu. wateja wote wa DRC, Uganda, Rwanda, Burundi na kadhalika watahama Kenya wanaboresha reli yao inakuwa na *Standard gauge* ili iweze kubeba mizigo mikubwa na kwa kasi na usalama zaidi. Nani ataendelea kupita Dar es Salaam? Sasa tuna ndege za binafsi na za watu kutoka nje ya nchi, *Precision*, 540, na kadhalika. Air Tanzania iko *ICU*.

Mheshimiwa Spika, ukipitisha mizigo wako bandari ya Dar es Salaam, uwe tayari kusubiri wiki kadhaa kabla ya kuutua, uwe tayari kulipa *storage* na pengine hata mizigo unaweza kuibwa au kudokolewa. Wizara hii inahitaji mipango madhubuti ili kuleta kasi mpya katika kukuza uchumi wetu. Ijipange upya.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Naibu Waziri na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri katika kuboresha sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo kuhusu uendelezaji wa uwanja wa ndege wa Mtwara hasa eneo la kungojelea abiria. Ni lini hasa ukarabati wa jengo la abiria utakamilika kwani sasa ni zaidi ya miaka mitano ukarabati huo haujakamilika na abiria wanatumia hanga la jeshi ambalo kwa kweli halina hadhi.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege wa Mtwara unahitaji kuwekewa taa ili uweze kutoa huduma masaa 24 hasa ukizingatia kukua kwa shughuli za uchumi Mkoo wa Mtwara hasa shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi kwenye bahari kuu ambao unatumia usafiri wa helkopta kwenda na kurudi kwenye kambi zao huko bharini.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu ni lini *VIP* mpya kwenye kiwanja cha Julius K. Nyerere itaanza kutumika kwani iliyopo sasa haina hadhi (eneo ni dogo sana kwa viongozi wa Kitaifa kama Rais, Makamu na Waziri Mkuu kutumia eneo moja na viongozi wengine wa Kitaifa suala ambalo halifanyiki katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata ufanuzi kwa nini kuna tofauti ya idadi ya miruko ya ndege na idadi ya abiria baina ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya viwanja vya ndege inaonesha idadi ya safari za ndege ziliongezeka kwa 13% kutoka safari za ndege 117,245 mwaka 2009/2010 hadi kufikia safari za ndege 132,584 mwaka 2010/2011. Mamlaka ya usafiri wa anga Tanzania inaonesha safari za ndege ziliongezeka kwa 8.5% kutoka safari 170,777 mwaka 2009/2010 hadi safari za ndege 185,278 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa abiria Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*) inaonesha idadi ya abiria iliongezeka kwa asilimia 10.3 kutoka abiria 2,054,499 mwaka 2009/2010 na kufikia abiria 2,265,658 mamlaka ya usafiri wa Anga Tanzania (*TCAA*) inasema abiria walotumia usafiri wa anga waliongezeka kwa 9% kutoka abiria 3,082,254 2009/2010 hadi 3,358,499 mwaka 2010/2011. Tofauti hii inatokana na nini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii kwa kuanzia reli ya kat. Nadhani sasa Serikali ijpange kufufua reli hii ili kuwezesha wananchi wa mikoa yote ya reli ya kat kupata usafiri wenye nafuu na pia kuweza kusafirisha mazao na bidhaa zingine. Napenda kutoa ushauri kwa Serikali kuwa ni vema Serikali yetu isimamie moja kwa moja uendeshaji wa reli ya kat.

Mheshimiwa Spika, tuangalie jinsi gani Serikali inaweza ikaingia ubia na nchi zingine kama China ambayo ilionyesha juhudhi zake wakati wa ujenzi wa reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu haina uwezo wa kutosha kufufua njia zetu za usafiri ikiwemo reli, njia ya anga na kadhalika, tuongee na Serikali za nchi nyngine, naamini tunawenza kupata nchi ambayo itakuwa tayari kushirikiana na sisi ili tuweze kutatua matatizo yetu katika eneo hili na maeneo mengineyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja iliyotolewa mbele yetu na Wizara ya Uchukuzi. Kat. ya Wizara ambazo utendaji wake unakabiliwa na changamoto nyngi sana na hivyo wanapaswa kuongeza kasi ili kuleta matunda yanayotegemewa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa majini ni muhimu sana ukawa wa uhakika kwa maana ya vyombo vinavyotumika na ratiba ya usafiri iliyo ya uhakika kwani ni usumbu mkubwa kwa abiria anayetegemea usafiri wa meli kuambiwa hamna usafiri na hivyo kulazimika kuvunja safari kwani mwananchi anakuwa hana njia mbadala kama ilivyo kwa usafiri wa nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, usafiri uliokuwa wa uhakika kwa wananchi wa Jimbo langu la Kalambo wa mwambao wa Ziwa Tanganyika kwa maana ya Mji Mdogo wa Kasanga, Vijiji vya Miuzi, Kapele Kasisi, Karitalamba, Kilewani, Chipwa, Kipanga, Samazi na vijiji vingi vilivyo Jimbo la Nkasi vimekuwa vikitegemea kwa miaka mingi usafiri wa meli za *MV Mwongozo* na meli Kongwe kuliko zote kubwa duniani ambayo bado inafanya kazi ya *MV Liemba*. Kwa bahati mbaya sana meli ya *MV Mwongozo* haifanyi kazi na meli pekee inayofanya kazi ya *MV Liemba* imepunguza safari zake kutoka safari mbili kwa wiki na kwa sasa safari mbili kwa mwezi mzima.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaleta usumbu mkubwa kwa watumiaji (abiria) na kwa usafirishaji wa mizigo. Naiomba Serikali ihakikishe ile ratiba ya zamani irudishwe na ikiwezekana ratiba iongezwe kwani fursa za kiuchumi kwa maana ya mizigo ya kwenda na kutoka nchi jirani ya Zambia, Burundi, Kongo na DRC.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwa kupertia Wizara hii kuhakikisha kwamba ile mikoa iliyominikoa kama ya Rukwa vinajengwa viwanja ili mikoa hii nayo iweze kwenda na kasi ya maendeleo na mikoa mingine. Eneo la kujenga uwanja mpya limetengwa kwa muda mrefu sasa, Wizara ifuatilie eneo hilo lillilo nje kidogo ya Manispaa ya Sumbawanga.

MHE. ABDULSALAAM S. AMER: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Maombi yangu kwa Waziri kuhusu maeneo ya *railway* yaliyopo katika Mji mdogo wa Mikumi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nyumba (kambi) zilizopo katika Mji Mdogo wa Mikumi zimechakaa na kuna wananchi wamekaa kwa muda mrefu. Wananchi hao wanatozwa kodi kila mwezi lakini hakuna ukarabati unaofanyika katika nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, maombi yangu kwa Waziri kwani hizo nyumba ziwe zikarabatiwe au wauziwe wakazi wanaoishi kwa muda mrefu katika nyumba hizo toka enzi za *East Africa Community (EAC)*.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba Wizara iwkodishe Halmashauri ya Mji Mdogo wa Mikumi sehemu ya godauni na kwa ajili ya kupakia magari yanayosongamana pembezoni mwa barabara kuu iendayo Iringa – Zambia.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ipo tayari kufuata masharti yote ya ukodishaji eneo hilo ili kuondoa msongamano wa magari ili zisiletu usumbu na kuharibu barabara na kuepusha ajali zinazotoka hasa usiku.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri azingatie maombi yangu kwa niaba ya wananchi wa Mji mdogo wa Mikumi ili uweze kukodishiwa Halmashauri hiyo katika kuongeza kipato cha Halmashauri ya Mji Mdogo wa Mikumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MAHMOUD HASSAN MGIMWA: Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mikakati mizuri katika kutekeleza Sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nachangia hotuba hii kwa masikitiko makubwa, kwani haioneshi nia ya kweli ya kutaka kusaidia sekta hii ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, sijaona dhamira ya kweli ya Serikali kutaka kusaidia usafiri wa reli, wala usafiri wa ndege (Anga), wala usafiri wa maji pamoja na nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, mazingira yaliyopo katika Wizara ya Uchukuzi hainishawishi kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, Serikali inashindwa namna ya kuamua kujenga Uwanja wa Ndege wa Nduli ambao ni muhimu sana kwa uchumi wa watu wa Iringa ambako kuna mbuga kubwa sana ya wanyama na kitega uchumi kikubwa kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, natamka wazi siungi mkono hoja mpaka Serikali ionyeshe dhamira ya kweli ya kuwasaidia Watanzania kwa kuongeza bajeti ili kuongeza ufanisi katika sekta ya uchukuzi.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kupata nafasi ya kuchangia angalau kwa maandishi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nasema siungi mkono hoja ya bajeti hii mpaka hapo nitakapopata majibu nitakayoyasema hapa chini.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga tumekuwa tukitegemea usafiri wa reli kwa muda mrefu sana sasa kupata hii Barabara ya lami isiwe sababu ya kuona kwamba hatuna matatizo ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango huu mzuri wa kujenga *ICD* Shinyanga, sioni itafanya kazi gani iwapo miundombinu ya reli haijawa sawa, tunawanyima haki wananchi wa nchi hii walio na kipato cha chini ambao hawawezi kusafiri kwa barabara, lakini bado kuna maeneo mengi yanavopitiva na reli hawana barabara kwa ajili ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili inayonifanya nisiunge mkono hoja hii ni suala la uwanka wa ndege wa Shinyanga uliopo Ibadakuli.

Mheshimiwa Spika, sijaona sehemu yoyote inayogusa uwanja huu, hivi kweli pamoja na kwamba uwanja wetu ni mdogo, ina maana matengenezo yoyote hapo hayatakiwi? Au Serikali inataka hata hivo ndege moja ya *Precision* navo ishindwe kutua Shinyanga?

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ya kutosha kuhusu reli ya katiba na uwania wa ndege wa Shinyanga. Absante

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli. Maendeleo yoyote ya nchi hayawezi kupatikana bila kuwa na *network* ya usafiri hususan reli. Kwa kuwa katika bajeti hii Serikali haijaonesha nia thabiti ya kuwekeza au kutenga fedha kutaka kufufua reli zilizotelekezwa baada ya kubinafsishwa kwa *RITES*, mfano, reli ya kati ambayo ilikuwa ni kiungo kikubwa sana cha biashara kati ya nchi yetu na nchi za Rwanda, Burundi, Congo na DRC ambazo ni *land locked countries*. Reli ya kati kwa mfano, ni muhimu sana kwa kusafirisha mizigo kwenda nchi nilizozitaja hapo juu. Serikali imekuwa ikipoteza mapato makubwa sana kwa kukosa kusafirisha mizigo kwenda katika nchi hizo ambazo hazina niia ya maji hivyo kuteqemea usafiri wa reli.

Mheshimiwa Spika, reli ya Singida – Dodoma imekufa bila maelezo lakini ilikuwa ni reli ambayo ni muhimu sana kwa kusafirisha mifugo kama ng'ombe, mbuzi na kuku kwa ajili ya nyama kwa wakazi wa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Mazao kama vile mafuta ya alizeti na asali nayo yalikuwa yakisafirishwa kwa kutumia reli hii. Kwa nini Serikali bado inasuasua kuifufua reli hii ya Singida – Dodoma pamoja na reli ya kati?

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa anga. Ni alibu kwa Taifa kusherehekea miaka 50 ya uhuru kwa mbwembwe na bashasha bila ya kuwa na ndege yake hata moja. Hivi tunasherehekea nini kama hata kile kinachotutambulisha Watanzania nje ya nchi kama ndege hatuna? Tunapotangaza kukamilisha kujenga viwanja vyta ndege kwa kutegemea ndege za kukodi tunamaanisha ninj?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uzoefu umeonesha kwamba mashirika mengi ya umma ikiwemo *ATCL* yamekuwa yakihujumiwa ni wakati wa Serikali sasa kutafuta mbia yaani *Local Investors*, mwekezaji wa ndani ashirikiane na Serikali kuwekeza katika Shirika la Ndege ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na umakini kama iliyofanya Kenya, kwa Kenya Airways. Kenya Airways inamiliikiwa na wazawa (wawekezaji) pamoja na Serikali na wote tu mashahidi jinsi shirika hilo linavyofanya kazi na kuzalisha kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *TICTS*. Pamoja na Serikali kuingia mkataba wenye utata na *TICTS* na kuendelea kuisifia, naitaka Serikali ifanye uchambuzi yakinifu kuhusu kampuni hiyo yenye harufu ya kifisadi na kuona kilichopo, maana *TICTS* si kweli kwamba wamefanya kazi kwa ufanisi kama ilivvoainishwa bali inaonekana kuna watu nyuma wanaoibeba kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara husika iwasiliane na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Mashirika ya Umma ili ione jinsi *TCTS* walivyoshindwa kufanya kazi yao na kushindwa kuongeza pato la bandari yetu ya Dar es Salaam ili kuiiridhisha kwa haya ninavovasema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la UDA. Usafiri Dar es Salaam ni muhimu sana katika kuleta ufanisi na kuongeza pato la Taifa. Kama walivyochangia Wabunge wote waliozungumza kuhusu suala la UDA, naishauri Serikali kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu kwa wahusika wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kuhujumu Shirika la UDA, likiwepo pia suala la kuua *unallocated shares* kwa Kampuni ya *Simion Limited* bila kufuata taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, nashauri na nawaunga mkono wachangiaji waliosema kwamba, Waziri Mkuu achukue maamuzi magumu ya kuivunja Halmashauri ya Dar es Salaam ili suala hilo la *UDA* lifanyiwe kazi kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa nasema siungi mkono hoja. Shukrani kwa ujenzi wa Uwanja wa Ndege, Mpanda.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusuasua kwa ujenzi wa bandari Karema, Ziwa Tanganyika inunuliwe meli mpya na reli ya Dar es Salaam, Tabora Mpanda iimarishwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho siungi mkono hoja.

MHE. NASSIB S. OMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kuhusu UDA. Ubadhirifu wa hali ya juu umefanyika katika Shirika hili. Wahusika wote hawakuwajibika wakiwemo:- Wizara yenyewe, Halmashauri ya Jiji, Hazina na Menejimenti ya UDA.

Mheshimiwa Spika, hatua za haraka hazikuchukuliwa laiti Wizara ingechukua hatua za haraka, aibu hii isingekuwa imetokea. Lazima hatua zote za haraka zichukuliwe ili wahusika wachunguzwe na vyombo vya umma.

Mheshimiwa Spika, pili, ni Shirika la *ATCL*. Shirika hili pia limekumbwa na ubadhirifu wa hali ya juu. Ndege zimepelekwa matengenezo na gharama zake kuongezeka mara dufu, ukilinganisha na gharama za mwanzo. Pia mahesabu ya Shirika hayajakaguliwa na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, yote haya yanachangia katika kuficha siri za watendaji.

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza kuwa hatua za *Ukaguzi* wa Mahesabu zichukuliwe. Pia wale wote waliohusika na ubadhirifu wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu Mkurugenzi Mkuu wa Hali ya Hewa. Mkurugenzi huyu anakaimu kwa muda mrefu, lakini hadi leo hatua za kumthibitisha hazijachukuliwa. Naomba Waziri atueleze kwa nini Mkurugenzi huyu hajathibitishwa hadi leo.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, kiujuila nampongeza Mheshimiwa Waziri yeye binafsi pamoja na Naibu Waziri kwa kazi yao ya kushughulikia matatizo ya Wizara ya Uchukuzi. Baada ya maelezo haya, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni umuhimu wa kuweka wazi matatizo ya mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Uchukuzi. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kila shirika la uchukuzi, (ndege, reli, meli na kadhalika) kinachozungumzwa ni matatizo na haja ya kuyaimarisha. Ni vizuri, lakini kinachohitajika ni uchambuzi wa kina kuhusu yafuatayo:-

- Sababu ya kuwepo matatizo;
- Aina ya matatizo; na
- Uchambuzi unasemaje juu ya matatizo hayo.

Je, matatizo hayo yapi yanahusiana na sababu zifuatazo:-

- *Managerial Competence;*
- *Financial capabilities;*

- *Technical competence;*
- *Capitalisation issues;*
- *Marketing factors; and*
- *Capacity utilization?*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba kabla ya Serikali kufanya maamuzi ya kuwekeza fedha zaidi ni lazima kwanza iwe na majibu ya maswali hayo sita (6) hapo juu.

Mheshimiwa Spika, pili, ni haja ya nchi kuwa *Credit Rated (Sovereign Rating (Credit), uwekezaji mkubwa nchini hasa katika miundombinu, viwanda, reli na kadhalika, tunahitaji kwanza nchi yetu ikubalike Kimataifa na masoko ya mitaji (*capital markets*) kwa njia ya *sovereign credit rating*. Mpaka leo Tanzania haijawa *rated* na ndiyo maana wawekezaji wakubwa wanasita kuwekeza Tanzania kwa kukosa taarifa za *ratings* za nchi hii. Nashauri Serikali ichague (*International Credit Rators (Moodys, standard and poor or fisher)* ili wafanye kazi hiyo na kutoweka katika nchi zilizo *rated*. Baada ya hapo *we can borrow from international capital markets by issuing sovereign bonds*.*

Mheshimiwa Spika, tatu, ni upanuzi na uboreshaji wa Viwanja vya Ndege vya Nduli (Iringa) na Kiwanja cha Njombe. Mikoa ya Iringa na Mbeya ni sehemu maalum ya uwekezaji kuhusu makaa ya mawe na madini mengine na Serikali itawekeza katika reli ya kutoka Mtwara-Songea-Mchuchuma na Liganga kwenye migodi ya makaa ya mawe. Kwa bahati mbaya viwanja vya ndege kuzunguka eneo hilo havijengwi wala kukarabatiwa. Je, uwekezaji kwa kutarajia watalam na watalii kwenda maeneo hayo wasafiri kwa magari kutoka Dar es Salaam?

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa maandalizi ya hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi ni Wizara nyeti kati ya Wizara zilizopo, kwani kwa kupitia Wizara hii maendeleo ya haraka yanaweza kupatikana nchini Tanzania. Najuliza kulikoni, Wabunge wengi wamesema, Kamati imeshauri lakini sioni mikakatai ya makusudi inayowekwa ili kuboresha utendaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Tanzania imezungukwa na nchi kama Uganda, Rwanda, Burundi na DRC Congo ambazo zote ni *land locked*. Njia ya wao kupata mizigo au kusafirisha mizigo kwenda nje na kupitia Tanzania. Njia rahisi yenye gharama nafuu inayoweza kusafirisha mizigo mingi, mikubwa na mizigo bila uharibifu ni njia ya reli. Uksafirisha kwa barabara unachakaza barabara na ni ghali.

Mheshimiwa Spika, ili kuinua uchumi wa Tanzania kwa haraka itabidi tukubali tutoe fedha za kutosha tujenge reli mpya ya viwango vya kisasa kutoka Dar es Salaam-Kigoma-Mwanza-Bukoba. Pamoja na reli lazima tuwekeze na kupanua bandari zilizo nchini na barabara husika ili kwa kupitia *network* hii ya bandari, barabara, reli tuweze kuvutia biashara ndani na nje katika nchi jirani. Kwa nini Serikali haionekani kuweka nguvu, mikakati ya uhakika na bajeti ya kutosha ili kuchochaea maendeleo ya haraka yanayoweza kupatikana Tanzania?

Mheshimiwa Spika, huduma ya Mamlaka ya Hali ya Hewa ni huduma muhimu sana. Kwa kipindi cha takriban kuanzia mwaka 1992 dunia nzima imepitia mikataba ya Kimataifa na mikutano mikubwa (*COP – COP16*) ili kujadili tatizo la mabadiliko ya tabia nchi yanayoathiri hali ya hewa. Mabadiliko haya yamesababisha vimbunga, mafuriko, ukame, majira kubadilika matetemeko na ongezeko la joto duniani. Tumeshuhudia Japan, hapa Tanzania kuna kumeguka kwa ardhi (*land slide*), visiwa viwili vimezama, upepo umeongezeka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, je, ningependa kujuu mamlaka ya hali ya hewa imejiandaaje kukabili mabadiliko haya ya hali ya hewa? Je, usalama wa Watanzania ukoje au unalindwaje? Je, Mamlaka ya Hali ya Hewa wamepewaa mitambo ya kisasa yenye kutumia teknolojia ya kisasa ili waweze kutoa tahadhari kwa Watanzania (*early warning systems*) ili waweze kujandaa na vimbunga, mafuriko yanayoweza kutokea? Nauliza Tanzania imejiandaaje kuboresha teknolojia ya mitambo ya Mamlaka ya Hali ya Hewa? Wakulima wamechanganyikiwa hajui lini walime, lini

wapande kwani majira yamebalika sana. Ni lini sasa Mamlaka ya Hali ya Hewa itaanza kutoa utabiri wa hali ya hewa wa muda mrefu ili kuwasaidia wakulima?

Mheshimiwa Spika, usafiri katika Ziwa Victoria ulikuwa mzuri, kulikuwa na meli zilizokuwa zinasafirisha watu na mizigo kwenda Musoma, Mwanza, Ukerewe, Bukoba na vile vile ziliweza kwenda Uganda na Kenya. Hivyo, nchi yetu ilipata mapato makubwa kutokana na huduma hizi.

Mheshimiwa Spika, hadi leo huduma zote hizi karibu zilikuwa hazipo. *MV* Bukoba ilizama na watu wapatao elfu moja hivi miaka zaidi ya kumi iliyopita. *MV* Victoria imezeeka na imechakaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kwa kutambua umuhimu wa huduma hii alitoa ahadi kuwa watu wa Ziwa Victoria watanunuliwa meli kubwa. Mbona sioni fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hii? Jamani hawa Watanzania wanateseka, je, ni lini Wizara hii itanunua hii meli?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AGGREY D.J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Omari Rashid Nundu kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii. Nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Mhandisi Athuman Rashid Mfutakamba kwa msaada mkubwa anaompatia Mheshimiwa Waziri na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, wenzetu wa *Meteorological Department*, wawe wanatutahadharisha mapema kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa. Aidha, elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi mpaka hapo Shirika la (*MSL*) Huduma za Meli halitapewa fedha za kuliendesha ili wananchi wa Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na wanachi wa Ludewa wapewe fursa nzuri ya kiusafiri.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Huduma za Meli lipewe fedha za kujidoresha. Serikali kupitia *TCAA* imeruhusu *Precisionair* kutoa huduma za *ground handling* ili ishindane na *Swissport* ambayo hufanya shughuli za *ground handling* pekee. Ili kuepusha athari za *vertical integration*, nashauri Serikali iamuru kampuni hiyo iende Kampuni tanzu ili kutenganisha huduma za usafiri kutoka zile za *ground handling*.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninayo masikitiko makubwa jinsi Wizara hii ilivyoshindwa kabisa kuendesha sekta ya uchukuzi. Mashirika mengi yamekuwa au yameshindwa. Tulikuwa na usafiri wa reli (*TRC*) limehindwa kujidoresha. Reli ya *TAZARA* nayo ina matumaini madogo ya kujidoresha. Tulikuwa na Shirika la Ndege nalo limekuwa. Kwa ujumla hakuna uadilifu wa kutosha juu ya usimamizi wa mashirika yetu.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko makubwa sana yanahitajika ili kuyanusuru mashirika haya ya umma. Lipo tatizo katika nchi hii, ambalo kama halitasahihishwa kamwe, hatutapa mafanikio. Nalo ni kuwafumbia macho viongozi wa mashirika haya ya umma wanaoyafilisi lakini hakuna hatua inayochukuliwa. Hakuna woga katika kuiba fedha za umma kwa sababu wana uhakika Serikali haitawachukulia hatua. Nchi hii haiwezi kuendelea. Tubadilike.

Mheshimiwa Spika, nataka kuona wale wote walioshiriki kuyaua mashirika yetu yote nchi hii, wachukuliwe hatua ili liwe fundisho kwa viongozi wengine. Kama hatakuwa na hatua zozote

zitakazochukuliwa basi nchi hii tutakuwa tumetweka rehani. Aidha, ufuatiliaji huu uendane pia na kuachana kabisa na usiri wa mikataba mbalimbali inayofanywa na Serikali, pindi mashirika yetu yanapobinafsishwa. Uchumi usipoimarika nchi hii haitatawalika vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunapoteza uchumi wa nchi kwa kutosimamia miradi mingi ya usafirishaji na uchukuzi. Tumejaliwa bandari, lakini nako ulaji mwinci mapato kidogo, naomba tuangalie vizuri bandari zetu ili ziweze kuwa chachu ya mapato ya Taifa. Kamwe nchi hii uchumi hautakua kama mchezo huu wa kulindana hautakomeshwa nchi hii, hataimarika kiuchumi hata kidogo, tuache huruma, tujali masilahi ya wengi.

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono hoja hii kama majibu ya msingi hayatatolewa.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nilichangia bajeti hii kwa kuongea nilijikita zaidi katika sekta ya reli pamoja na masuala ya wafanyakazi. Aidha, napenda kutoa maelezo ya ziada kuhusiana na sekta ya uchukuzi hususan, meli za mwambao, viwanja vya ndege, utabiri wa hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kulifkiria kwa kina suala la ufufuaji wa meli za mwambao. Natambua kila jambo jema lina madhara yake. Maboresho ya barabara zetu nchini yalifanya meli za mwambao kuonekana hazina faida tena kutokana na ukweli kwamba zinachukua muda mrefu kusafiri kwenda maeneo husika. Lakini hivi sasa *potential* ya ongezeko la shughuli za kiuchumi na biashara kule Mtwara, Lindi, Tanga na Bagamoyo, litailazimu Serikali kufikiria uwezekano wa kufufua usafiri wa meli za mwambao. Hivi viwanda vya mbolea, simenti na vinginevyo vitakapoalisha bidhaa zake kule Mtwara, lazima uwepo usafiri wa majini wa ndani utakaotumika kusambaza bidhaa hizo katika sehemu mbali mbali. Isitoshe, usafiri wa mwambao unaongeza *options* za usafiri kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni viwanja vya ndege. Naipongeza Serikali kwa kuendelea na juhudu zake za kuboresha viwanja vya ndege nchini. Hakika viwanja vinapoboreshwa, soko la abiria wanaosafiri kwa ndege linaongezeka. Tumejionea wenyewe kule Bukoba, baada ya kupanua kiwanja cha ndege leo hii *Precision Air* wanapeleka ndege kubwa mara mbili na mara nyingi inakuwa imejaa (*full capacity*). Hivyo, ni imani yangu Serikali ikiendelea kupanua viwanja vingine vya ndege, usafiri wa anga utaongezeka zaidi.

Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake atueleze Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe utamalizika lini? Maana zimeshakuwepo *deadlines* nyingi za kumalizika uwanja huo. Vile vile, ningependa Mheshimiwa Waziri atueleze *VIP* mpya ya uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam itaanza lini kutumika? Maana inaonekana kukamilika muda mrefu lakini haitumiki. Vile vile, pamoja na juhudu mnazofanya kutafuta fedha za ujenzi wa *Terminal III* ya uwanja wa ndege wa Julius Nyerere, nashauri muangalie namna ya kuboresha huduma katika *terminal II*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni utabiri wa hali ya hewa, hususan kompyuta maalum ya kuboresha utabiri wa Idara ya Hali ya Hewa. Nakumbuka Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara ya Uchukuzi katika ziara yake, alitoa maelekzo Idara ya Hali ya Hewa ipate kompyuta maalumu ya kuboresha utabiri wao wa hali ya hewa ili angalau tuwe na uhakika wa hali ya mvua ambaa utasaidia sana wakulima wetu kujipanga katika kilimo chao. Je, Wizara imeweka bajeti kwa ajili ya ununuzi wa kompyuta hiyo? Hii ni muhimu sana na ya haraka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii, siungi mkono bajeti hii hadi hapo nitakapopata maelezo ya kuridhisha.

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kumrudishia Mwenyezi Mungu sifa na utukufu kwa kunijalia kupata nafasi ya kuchangia kwenye bajeti hii ya uchukuzi ambayo ina matatizo ya msingi lukuki.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie suala la uchukuzi wa anga. Hii ni kashfa na aibu sana kwa wananchi wazalendo wa Tanzania. Sasa inakuwaje shirika hili liliokuwa linakwenda vizuri sana tena ilikuwa na marubani (*Pilots*) mahiri katika Jumuiya ya Madola. Lakini cha ajabu shirika hili liliingiliwa na ufisadi wa kiaina likaanza kudidimia. Inasemekana *Board Members* hao hao ndio walikuwa pia *Board Members wa Precision Air*. Hawa wakapendelea na kuweka mkazo kwenye kuendeleza *Precision Air on the expense of ATC and later ATCL*. Jambo hili likaachiwa hadi kuua kabisa *National Carrier!! Ah! Jamani*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba *ATCL* ifufuliwe kwa maslahi ya Watanzania wa sasa, kesho na vizazi vijavyo. Ili iweze kufanikiwa Mashirika yanayohusika na huduma hii kama *TANAPA* na wazalendo wa Tanzania wapewe nafasi ya kununua hisa katika shirika hili fedha itapatikana bila matatizo yoyote. Mbona Watanzania wanunuua hisa *CRDB, NMB*, na hata hilo Shirika la *Precision* lenyewe, kazi hii ifanyike haraka sana.

Mheshimiwa Spika, huzuni nydingine ni juu ya uendeshaji wa bandari, kusema kweli tumekuwa kama watu wajinga wasio na mweleko wowote. Hivi inakuwaje bandari ya Dar es Salaam haina ulinzi na ulinzi halali wa nchi menejimenti yenye ndio inayohalalisha wizi wa kutisha huko bandarini utafikiria kuwa nchi hii haina Serikali wala mwenyewe. Vitu mbalimbali vinavyopita hapo bandarini hasa magari kufika salama kwa mwenye mali ni nadra kwani utakuta magari mengi yameiwiwa vitu muhimu, kama viti, *radio, spare kit tool*, matair na kadhalika na huwezi kudai la sivyo unafanyiwa visa.

Mheshimiwa Spika, kuna *TRA* hawa pia wana mtandao wao wa kifisadi wa kutoza ushuru wapendavyo, madaraka yao ni makubwa mno. Mfano, sasa wamepangisha kwa watu wao kukusanya kodi ya kutunza magari yakingojea kuchukuliwa na wenye magari, kodi ziko juu sana na cha kusikitisha zaidi ni kuwa wanatoza kwa kukadiria katika US\$ ambapo ni *constant \$1 = 1,600* za Kitanzania iwe iko chini au vinginevyo. Haya mambo yanafanya katika Jamhuri ya Tanzania kama vile hakuna utawala wa sheria. Tabia hii ya wizi inakomaa sana, inapaswa ivunjwe na kutafutiwa dawa sawia ya kutatua matatizo hayana ipatikane haraka.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ninalopenda kulizungumzia, ni suala la usafirishaji wa binadamu katika majiji hasa Jiji la Dar es Salaam. Hili sakata la uchukuzi wa wanafunzi na Watanzania maskini ni huzuni kubwa sana. Hivi kweli Serikali ya CCM imeshindwa kupata ni jinsi gani au kupata utatuzi wa kuwasafirisha watu katika hali ya utu. Hadhi ya watu kubadilishwa kuwa kama mizigo hii haifai hata kidogo, hivi kwa nini tunafanya hivi?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, Serikali ifanye kwa vitendo huo usafiri wa magari yaendayo kasi na yawe muafaka kwa kupanda na kushuka kwa hali inayofaa yasiwe yale ya juu ambayo ni shida sana kwa watu wazima kupanda kwa heshima. Uchukuzi pia uangalie vizuri hizi *parking system*.

Mheshimiwa Spika, hizi *parking system* zinakusanya fedha nydingi na kuzipeleka kwa mtu mmoja ambaye hajawekeza chochote kwenye miundo mbinu ya hizo *parking*.

Mheshimiwa Spika, hivi kuna nini, kwa nini hizo fedha zisikusanywe na halmashauri zenyewe kwa matumizi mazuri ya kuendesha usafirishaji, kama kuweka *parking metre* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, nipendekeze kuwa katika Wizara hii kuna watu wengi wameonekana kuhujumu Mashirika yake kama, Reli ya Kati na *TAZARA, UDA*, meli, viwanja vy a ndege na kadhalika. Wote na wengine watafutwe na kufunguliwa mashtaka wakiwa ndani ya jela. Lakini si hivyo tu hatua kali zichukuliwe kama kuwafilisi na kutaifisha mali zao walizochuma kwa ufisadi. Hii itakuwa mfano mzuri na onyo sahihi kwa wale wote ambao wako njiani kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Naibu Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Mfutakamba, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uwanja wa Ndege wa Singida. Napenda kuipongeza Serikali kwa kukarabati Uwanja wa Ndege wa Singida pamoja na kuupanua. Kulingana na ukubwa wa kiwanja hiki ndege ndogo za abiria zinaweza kutumia kiwanja hiki lakini zinashindwa tu kwa sababu ya *running way* haina lami, kwa kuwa ulikuwa mpango wa Serikali miaka mitano iliyopita ni kitu gani kimekwamisha mpango huu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali inipe majibu kazi ya kuweka lami *running way* ya uwanja wa Singida fedha zitatengwa lini. Mheshimiwa Nundu Waziri ama Mheshimiwa Mfutakamba, Naibu Waziri wakati wanajibu hoja za Wabunge kesho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Reli ya Dodoma hadi Singida Mjini. Nasikitika kusema kuwa kauli ya Serikali ya kuimarisha reli ya kati pamoja na ya Singida haitekelezeki. Ninapenda kujua usafiri wa reli ya Dodoma hadi Singida itaanza lini kwani ilikuwa inategemewa sana na wananchi kwani ilikuwa inachukua abiria wengi hata bei ya nauli ilikuwa inaridhisha.

Mheshimiwa Spika, nasubiri maelezo ya Serikali hapo kesho, Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze na wananchi wa Singida wasikie. Ni ukweli usiofichika usafiri wa reli ulikuwa unasaidia sana kusafirisha mizigo pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vituo vya waangalizi wa reli ya Dodoma hadi Singida kurudishiwa. Napenda kuikumbusha Serikali kuwa waangalizi wa reli ya Dodoma hadi Singida walikuwa wanasaidia sana kwa kutoa taarifa endapo kuna tatizo lolote kwenye njia hiyo ya reli hasa masika pia watu wengi nia mbaya wanapoweka vitu vya hatari mfano mawe au machuma mazito na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali watakaporudisha usafiri wa reli basi na hawa waangalizi warudishwe kwenye vituo vyao. Waziri atoe kauli wakati anajibu hoja au Naibu Waziri ili nisiwasumbue kwenye vifungu au kutoa shilingi kwenye mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa UDA kuimarishwa. Nasikitika kusema kuwa, kukosekana kwa usafiri wa UDA wananchi wa Dar es Salaam na nchi tunapata tabu sana. Nasema hivi kwa sababu wametoa nafasi daladala aina ya (kipanya) kuzidi sana Dar es Salaam na vinasumbua sana kwani havifuati sheria za barabara, mfano, wanaacha njia na kupita pembeni mwa barabara. Naomba usafiri huu uimarishwe na wasipewe wawekezaji, Serikali isimamie yenye. Nasubiri maelezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nitaunga mkono hoja baada ya maelezo ya Waziri.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ijjelekeze kuimarisha kampuni ya reli. Kwa kuwa barabara ina mfuko wake wa *Road Toll*, nashauri na reli iwe na Mfuko kama huo ili kuwa na uhakika wa matengenezo na iwe na uwezo wa kujipangia kila mwezi tutarekebisha au kuweka reli mpya kilomita kadhaa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ijiwekee mkakati huo, naamini kwa mkakati huo tunaweza tukaboresha reli zetu, kama inavyofanya Wizara ya Ujenzi kwa barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhanah Wataala* kwa rehma na neema zake nyingi anazoendelea kunineemesha, *Alhamdu Lillah*.

Mheshimiwa Spika, sekta ya Uchukuzi ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani ikiwemo nchi yetu nzuri ya Tanzania, ndio maana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akaiundia Wizara yake yenyewe. Pamoja na Mheshimiwa Rais kuiundia Wizara yake peke yake Sekta ya Uchukuzi, akawapa kazi ya kuiongoza Wizara hiyo Ma- engineer Wasomi, mahiri, wachapakazi, wazalendo, weledi na zaidi ya yote wenye uchungu, huruma na mapenzi ya dhati kwa wananchi wa nchi hii. Hao ni Mheshimiwa Waziri Omar Rashid Nundu (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba (Mb), lakini pia Katibu Mkuu Engineer Omar Chombo. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa weledi wake wa kuwapa nafasi ya kuiongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ni kuwa karibu sana katika usimamizi wa Wizara hii ili kulinda heshima zao katika ufanisi wa kazi lakini pia heshima ya Mheshimiwa aliyewaamini kuwapa nafasi hiyo. Binafsi nina imani sana na Waziri na Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, kuwa na usafiri wa anga katika nchi (*National Flag Carrier*) ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yoyote duniani na ni utambulisho na fahari ya nchi husika nje ya nchi. ATC au ATCL kama ilivyoitwa baada ya kubinafsishwa imekuwa ni kinyume na matarajio yetu. Badala ya kuwa fahari ya nchi yetu, imekuwa aibu na fedheha kwa nchi yetu. Nini tatizo la aibu hii i.e. ATCL kufa/kufilisika?

Mheshimiwa Spika, tatizo ninaloliona mimi ni kutokuwa na utaratibu wa kuwajibisha wale wanaopewa dhamana ya kuendesha mashirika yetu. Kuongoza maana yake ni kujenga! Badala ya mtu anayepewa dhamana kujenga, anafanya tofauti, kazi yake inakuwa kuharibu aidha kwa uzembe, kutowajibika au kwa ubinasi tu na mamlaka zilizo juu yao badala ya kuwajibisha kwa kuwapa adhabu ili iwe onyo kwa wengine, wanawapa kazi nzuri zaidi! Nini tutategemea? Bila shaka ni kurithisha uzembe huo kwa watendaji wengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima iwe na *formular*, tena iwe wazi na nyepesi tu. Aidha, mtu akifanya vizuri apongezwe au akifanya uzembe, wizi, ubadhirifu aadhibiwe! Hapo ndio itakuwa tunajenga *discipline* kazini na kazi ya kujenga nchi ndio itafanyika. Bila Nidhamu hakuna utendaji na nidhamu sio kupiga magoti, bali nidhamu ni ufanisi katika kazi. Kupiga magoti ni daraja la chini ya nidhamu na mara nyingine inakuwa ni ya kinafiki.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli lau usafirishaji kwa reli ni muhimu sana kwa kuinua uchumi ya nchi yetu. Reli inakuwa na maisha marefu (*longlife*) na pia inachukua abiria au mizigo mingi kwa wakati mmoja. Hivyo usafiri wa reli ni nafuu sana na watu wa vipato tofauti wanautegemea sana usafiri huu.

Mheshimiwa Spika, reli pia ni usafiri wa salama zaidi kuliko mabasi na malori. Usafiri wa reli ukiboreshwaa utaongeza mzunguko wa biashara, utakuza vipato vya wananchi, utapunguza mfumuko wa bei za bidhaa, utaongeza utalii wa ndani na utakuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ya *SUMATRA* haifanyi kazi stahili iliyopangiwa na Taifa kuifanya badala yake imekuwa ikishirkiana na wamiliki wa vyombo vya usafiri hasa wa majini ili vyombo vibovu vifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha wiki tatu tu zilizopita, ajali nne za vyombo vya majini zimetokea na *SUMATRA* hajatoa taarifa yoyote. MV Serengeti ikitoka Unguja kwenda Pemba imepotea na kwenda Tanga! Jahazi likitoka Bagamoyo kwenda Unguja limezana na watu sita (6) wamekuwa. Boti zinazofanya safari kati ya Dar es Salaam na Unguja nyingi zimechoka na hazina *repair*. Mara kwa mara zinazima *engine* katikati ya mkondo na baya zaidi *crews* hata taarifa hawatooi kwa wasafiri na husababisha hofu kubwa. Hii si dharura, ni kawaida kuzimika na zinakaa zaidi ya saa moja zikiwa zimo majini bila ya mwelekeo, *SUMATRA* hata habari hawana mbali ya upandishwaji kiholela wa nauli na uzzidishwaji wa abiria na mizigo. Ni wakati wa kuchukua hatua sasa!

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninayo mengi ya kuzungumza lakini ni wazi Serikali yetu imekuwa siku na leo hii Mheshimiwa Waziri Mkuu katika taarifa yake asubuhi ametoa majibu ya kilio cha Wabunge na wananchi. Ameonyesha Serikali imesikia na hatua mbalimbali imezichukua hadi hata kupata pesa za kuongeza bajeti hii na hata kuunda Tume ya Uchunguzi wa Ubadhirifu katika Mashirika yaliyoko chini ya Wizara hii. Nampongeza Waziri Mkuu, naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika si leo wala siku za hivi karibuni bajeti za Serikali zitakuwa na fedha nyingi za kutosha kila tarajio. Fedha ni rasilimali adimu (*scarce resource*) hata Marekani na Ulaya bado wana shida ya pesa ya kutosha kukidhi mahitaji yao yote. Kikubwa ni namna gani rasilimali hii adimu itatumika kwa kutekeleza vipaumbele vya Wizara hii vya Serikali na kuleta tija. Katika Wizara hii ya Uchukuzi, naionomba Serikali iliendelee kufanya kazi kijamaajamaa sasa tuko kwenye mfumo wa kibepari (*capitalism economy*).

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya Umma sasa yaendeshwe kwa malengo na Wizara iamu ni miradi ipi au Shirika lipi litakalofufuliwa kwa kupewa rasilimali za kutosha ikiwepo rasilimali watu ya uhakika ili shirika hili liweze kufufuka na liendelee kwa tija na faida (*Yaani to sort out once and for all*). Yaani kuanzia sasa Bodi na Menejimenti za Mashirika haya zipewe malengo na Serikali ihakikishe yanafikiwa bila visingizio vyovoyote. Kwa kufanya hivi basi tutasonga mbele, reli, ndege, na usafirishaji vitaboreka na kutegemewa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nashauri kilio cha wafanyakazi wa *KDCO* na *ANS – KADCO* kurejeshwa *TA*A na *TCAA* na kulipwa mishahara iliyolingana na wenzao chini ya utaratibu wa Kiserikali ufanyike haraka. Wafanyakazi hawa wasiteswe/kufukuzwa na kutishwa na uongozi wa *KADCO* kwa kudai haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, *KIA* isibinafsishwe tena bila maandalizi ya uwazi na makini yenye kuhakikisha maslahi ya Taifa yanatekelezwa/yanalindwa.

Mheshimiwa Spika, ufanyike mkakati wa makusudi kushusha gharama mbalimbali zinazohusu Mashirika ya Ndege na abiria ili kuvutia mashirika mengi ya ndege kuja *KIA* na kuleta abiria.

Mheshimiwa Spika, Kenya wanapanua viwanja vyao na wana mpango wa miaka 30 wa kuboresha mifumo yao ya usafiri wa ndege kwa malengo maalum. Jomo Kenyatta wanawekeza zaidi ya 500 milioni. Serikali haraka ione mpango wa Kenya na nchi nyingine za jirani na iandae *Counter strategy* kwa faida ya Tanzania. Mkakati wa makusudi wa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu reli, Serikali itoe tamko na kauli kuhusiana na Reli ya Tanga – Moshi – Arusha na Moshi Voi. Reli hii inaendelea kufa na vyuma vyake vingi vinaporwa. Tukumbuke kuwa hata kama reli kwa maana ya mataruma ni chakavu ni vema kuweka mpango wa makusudi wa kulinda mfumo mzima wa reli hii ili sipotee kabisa. Kabla ya kujenga reli mpya, ni vema tukafufua kwanza reli zetu zilizoteketezwa.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukupongeza kushika nafasi ya Uwaziri katika Wizara hii. Aidha, nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Mfutakamba, kwa kazi nzuri sana na hususan umahiri wake wa kujibu maswali hapa Bungeni. Aidha, nampongeze Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanja vya ndege, tatizo kubwa katika viwanja hususan cha *KIA* ni kukosa huduma nyingi kwa lugha nyingine “*activeness*” pengine kutokana na sisi wenywewe kukosa ndege zetu na pia gharama zetu pengine kuwa kubwa na ukosefu wa *ku-market resources* (mlima/mbuga/utalii) wengi hushukia Kenya, hulipa fedha zote huko na kuja na magari nchini, ndio maana *Airport* zetu hazichangamki. Je, Wizara ina taarifa kuwa Kenya eti wana sera mpya ya kujenga *Airport* katika kila Mkoa, hivyo wanajenga *Airpot* ya Kimataifa karibu na Holili, *several kilometres from KIA?* Ukweli kabisa kutokana walivyo *dynamic we are going to see funeral* ya *KIA*.

Pamoja na uchafu wote uliogubika ubinafsishaji wa *KIA* na ambao Serikali imefumbia macho, je na hili la *Airport* jirani tunalifumbia macho? Wameanza nadhani wanakaribia kumaliza *feasibility study*, tuzibe ufa kabla haujaanguka ukuta.

Mheshimiwa Spika, *Arusha Airport* lini itapanuliwa ndege kubwa zitue ilhali nafasi ipo? Fedha ngapi zimetolewa hadi leo kwa ukarabati? Tukiunda Tume kuchunguza, tutavumbua mengi. Kumbukeni Arusha ndiyo *centre* ya utalii Kaskazini. Ikiwa Waarabu wamejenga uwanja wa Ndege Loliondo unaotua ndege kubwa sisi Arusha tunashindwa nini ilhali wataalam na viongozi tunao Arusha.

Mheshimiwa Spika, *VIP* Dar es Salaam imekuwa ngonjera. Tangu isemekane imekamilika na tunao ushahidi vifaa vyote viko tayari. *What are we waiting for?* Huu mwendo wa kobe mpaka lini Tanzania?

Mheshimiwa Spika, najua na natambua kazi kubwa inayofanywa katika Wizara, lakini kwa kweli kama walivosema wengi hata viji-nchi vilivyokuwa na vita miaka mingi wana ndege, sisi hatuna aibu? Aibu gani hii? Kabla ya kununua ndege, ondoa wote tuanze upya ili uozo wote utoke. Bodii iwe mpya. Wataalamu wapo hawana kazi. Wengine wamekimbia nchi. Tuko nyuma yako. Kabla ya Disemba jitahidini tuwe na ndege yetu. Miaka 50 iendane na ufufuo wa ndege.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa *ATCL* waliopo wanaendelea kulipwa mshahara bila kazi, eti wanasubiri malipo ya mafao yao, jamani muda wote wanaolipwa fedha hizo hazitoshi mafao yao? Naomba suala hili liangaliwe ili tutakapoanza tuanze upya.

Mheshimiwa Spika, bodi yenyе mafanikio ni ya watu wachache. *Ethiopian Airways*, Bodii ina *Chief Pilot*, Mwakilishi wa Wizara husika na mfanyabiashara mwenye uzoefu wa usafiri wa anga, *fullstop*, mafanikio tunayaona. Hebu na sisi tuache kuwapa watu wengi tena marafiki, tuangalie kazi. *My brother I'm confident together with knowledgeable Deputy Mfutakamba you can do this*, tutawa-support.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, baada ya kupata kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuiongezea Wizara ya Uchukuzi kiasi cha Sh.95 billioni kwenye bajeti yake ya mwaka 2011/2012, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi huo mzuri na naiunga mkono 100, hotuba hiyo ya Wizara ya Uchukuzi. Hata hivyo, napenda kuchangia kwenye maaeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, usafiri. Duniani kote hasa katika nchi zilizoendelea usafiri ni eneo ambalo linapewa umuhimu mkubwa. Hii ni kwa sababu kuwa na usafiri wa uhakika kunapunguza kasi ya umaskini, kuokoa muda wa watu kufanya shughuli mbalimbali za uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu kadri idadi ya watu inavyoendelea kuongezeka haswa kwenye Majiji kama vile Dar es Salaam, Arusha na Mwanza mahitaji ya usafiri pia yanakuwa makubwa zaidi. Katika nchi ya Uarabuni yaani Dubai wao wameamua kupunguza kero ya usafiri kwa kubuni njia nyininge ya treni za umeme zinazopita chini ya ardhi. Njia hii ya usafiri ni muafaka mkubwa sana hata kwa nchi yetu ya Tanzania. Hii ni kwa sababu inarahisisha watu kufika kwa haraka, inaondoa kero ya misongamano mikubwa ya magari barabarani. Naishauri Serikali ianze sasa kufikiri na kubuni njia hii ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, bandari. Katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Serikali iliahidi kuboresha huduma za uchukuzi katika bandari za Mwambao. Naipongeza sana Serikali ya CCM kwa kufikia uamuzi huu. Hata hivyo, napenda kuomba Serikali itoe kipaumbele kuendeleza bandari zilizopo Mikoa ya Lindi na Mtwara yaani Mtwara/Dar es Salaam na Lindi/Mafia. Kuboresha bandari hizi kutasaidia sana kuiendeleza Mikoa hii ambayo mara nyingi tumekuwa tukiitafsiri kwamba iko nyuma kimaendeleo. Vilevile itasaidia kupunguza kasi ya umaskini kwa kuongeza wigo wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, kuna fursa ambayo bado hajatumika ipasavyo lakini ni fursa ya utajiri mkubwa sana kwa raia wetu. Hii ni upatikanaji wa malighafi za *Gypsum*, mafuta, mkaa, mawe na chokaa za kutengeneza *cement*. Malighafi hizi zinachochea kuwepo kwa viwanda vikubwa na vinachochea mahitaji ya usafiri wa kubeba mizigo mikubwa ambayo kama bandari zetu zingeweza kuimariswa basi ingerahisisha kusafirishwa bila kutumia barabara zetu ili zisichakazwe. Maendeleo yaliyopo Mtwara na Lindi yameanza kuchukuliwa hatua. Ni vema sasa maendeleo haya yaende sambamba na uboreshaji wa bandari hizi ili kurahisisha uinuaji wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli. Namshukuru Waziri Mkuu kwa uamuzi wa kuongeza fedha kwa bajeti hii. Kilio chetu cha muda mrefu cha kufufua reli na kuwekeza katika reli labda sasa kitapata mwenyewe. Serikali iweke katika *priority list* reli, viwanja vyatia ndege na kadhalika basi viendane na kutenga fedha mahsus za kuboresha uchukuzi kwa njia ya reli.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya karakana za reli, ni vema akapatikana mwekezaji mwenye uwezo na ujuzi aendeshe kama sehemu ya biashara ila isiuze. Karakana ya Tazara hali mbaya sana, ni gofu kutokana na kutotengwa pesa za kutosha za kuendesha karakana. Bora sasa karakana hii iendeshwe kwa ubia, badala ya watu binafsi kutengeneza vipuri vyao hapo.

Mheshimiwa Spika, fedha za *road toll* na reli nayo ipate gawiwo kwani wao ni wachangiaji wakubwa. Reli ikiboreka itasaidia uchukuzi katika maeneo ambayo barabara haziko, lakini pia itawenza kubeba mizigo mizito na kusaidia sana kuepusha uharibifu wa barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, viwanja vyatia ndege. Viwanja hivi sasa viendeshwe kibiashara, wapewe uhuru wa kukopa ili waweze kuendesha shughuli zao, waruhusiwe kusimamia ujenzi wa viwanja vingine vipyta katika maeneo ambayo ujenzi wake utaleta tija na kuinua uchumi wa nchi. Wawekezaji waingie ubia na Serikali wasiachwe peke yao. Mkazo uwekwe katika kufundisha waongoza ndege, *ground handless* na *Engineers* ili viwanja vitakavyojengwa Watanzania waweze kuviedesha tusije tukategemea nchi jirani (kwa ajira). Ule mpango wa kujenga *runway* nyingine *KIA* imekuwaje? Haijengwi tena? Vile viwanja 10 vilivyo fanyiwa *study* na kukubalika vijengwe, vitajengwa kweli katika hali hii ya ukwasi? Maslahi ya wafanyakazi yaboreshwe.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa maziwa na ujenzi wa magati. Bado wananchi kando ya Ziwa wana hali ngumu ya usafiri. Meli zote za maziwa zimechoka, ni vema wawekezaji watafutwe ili waweze kutengeneza eneo la chelezo. Tutoe *incentives* kwa usafirishaji wa meli mpya hata vipandevipande kwa njia ya barabara ni ngumu. Meli zinazosafiri kwenye maziwa ziko katika hali mbaya tuhakikishe kila muda ziwe zinakaguliwa.

Mheshimiwa Spika, ukiritimba mkubwa wa kutoa mizigo Swissport na Bandarini – Dar es Salaam. Nashauri Swissport iongeze muda kidogo wa *storage* badala ya siku nne (4) ziwe siku 10. Ukiritimba wa utoaji mizigo Swissport na bandarini unakatisha tamaa. *Procedures* ni ndefu sana. Watendaji nao hawana hata mvuto na muda wa kushughulika au kusaidia watoa mizigo. Bandari yetu inashuka thamani kwa vile watoa huduma hawako *creative*. Kenya wanajenga bandari yao ya Lamu sisi Mafia inatushinda. Serikali itoe pesa za kutosha ili miundombinu ya reli na bandari na viwanja vyatia ndege iweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, vyuo vyatia anga, reli na hali ya hewa viboreshwe kwa kuvipatia wakufunzi na vifaa, viendeshwe kibiashara. Wakati umefika shughuli hii ya kuboresha ifanyiwe. Chuo cha Reli Morogoro, kilisaidia sana kusomesha vijana wetu ila kiko katika hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa bahari. Ugaguzi wa vyombo vyatia usafiri wa bahari ufanyiwe. Siku hizi meli nyingi toka Zanzibar huzimika au kushika moto katikati ya bahari. Ufuatilaji wa karibu unahitajika ili udhibiti na usalama wa usafiri uwepo.

Mheshimiwa Spika, ATC. Ipatiwe mtaji wa kutosha ili ifufuliwe, wafanyakazi wa ziada wasiokidhi kiwango wastaafishwe. Ipatikane *management* inayokwenda kwa wakati. Bodii takayochaguliwa iwe ni bodi nzuri yenyewe mwelekeo, inajua masuala ya usafiri wa anga. Nini kinaendelea Songwe Airport?

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Kutokana na umuhimu wa Wizara hii na bajeti inayopendekezwa haina tija na hivyo Serikali ione haja ya kuongeza fedha na ielimishe mambo muhimu yatakayotekelawa.

Mheshimiwa Spika, bajeti inaonyesha wazi namna itakavyoweza kurudisha hali ya Shirika la Ndege la Taifa (ATC), kurudisha Shirika la UDA na mali zake zote Serikalini, kurudisha hadhi ya Shirika la TRL na kuboresha miundombinu na watumishi wake. Kurudisha hadhi ya Shirika la reli ya TAZARA na kurekebisha sheria na mafao ya wafanyakazi kwa upande wa Tanzania. Kurudisha hadhi ya vivuko kama Ukerewe, Ludewa, Kyela, Kigoma, Rukwa, Mwanza, Kilombero na kadhalika ambavyo viko katika hali mbaya na kutishia maisha ya watumiaji wa vivuko vilivyopo. Wizara ya Uchukuzi ikiboresha na kusimamiwa vizuri itakuwa na mchango mkubwa katika kuinua uchumi wa Taifa katika nyanja za utalii, usafirishaji wa mizigo na kuitangaza nchi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero na Ulanga imetenganishwa na mto mkubwa wa Kilombero ambapo ni jana tu tumepitisha bajeti ya ujenzi ambayo imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa daraja ambalo litakuwa na thamani ya shilingi 50 bilioni. Hivyo basi daraja hilo litajengwa kwa miaka mingi ijayo mpaka liishe. Kwa kuwa daraja hilo halitatumika miaka ya hivi karibuni. Hivyo kwa sasa wananchi wa Kilombero na Ulanga wanatasifiri kwa Pantoni.

Mheshimiwa Spika, Pantoni iliyopo Mto Kilombero ni mbovu na mara kwa mara inaharibika. Hapo nyuma iliyokuwepo ilizama na kuua watu na iliyopo sasa inahatarisha maisha ya wananchi. Hivyo, Serikali iharakishe kupeleka kivuko imara ili kunusuru uchumi na maisha ya wananchi. Viongozi lazima wawe na uthubutu wa kuwajibishana ili kuokoa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha, ahsante.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kufunga mwezi huu Mtukufu nami nichangie machache.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi ni Wizara nyeti mno kwa kuwa Wizara inasimamia sekta kama vile reli, Bandari, usafiri wa majini na Shirika la Ndege la Taifa. Imetengewa Shilingi bilioni 69 kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 167 kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Uchukuzi imetengewa jumla ya shilingi bilioni 236 (167+ 69) hii inaonesha ni mtaji wa Shirika la Ndege la Taifa (ATC) kama ilivyoombwa peke yake. Shirika la Ndege, Shirika la Reli na Shirika la Usafiri Majini (MSCL) hayajatengewa fedha za kuwezesha kuyafufua mashirika hayo ili yaanze kazi mara moja kwa ufanisi na faida kwa baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa usimamizi wa Wizara unaonekana dhaifu, nianze na usafiri wa reli, ni chombo ambacho kwa Mikoa yetu ya Bara umewarahisishia sana wananchi wa Mikoa ya Singida, Arusha, Manyara na Dodoma kwenda maeneo ya Dar es Salaam na Mwanza, Kigoma na kubeba mizigo bila tatizo lakini kwa sasa reli inaonyesha kuyumba. Tanzania tunavyo vyanzo vya mapato na umaskini tunautaka wenyewe lakini uchumi tunao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Shirika la Ndege lina maeneo mengi ya viwanja vya ndege ili ziweze kutua na kwa kuwa shirika halina habari na viwanja hivyo kwa kuvifuatilia wao wana hesabu tu. Mfano katika Wilaya ya Kondoa kuna Kiwanja cha Ndege kimetelekezwa na kufika kutengenezwa na Kolea Kolea na kushirkiana na Halmashauri ya Wilaya hivyo kukikarabati na ndege hizo kutua hapo na mlinzi amejiriwa na Halmashauri na kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Shirika imesahau kabisa kama Wilaya ya Kondoa nayo ina wananchi wenye mahitaji ya kutumia ndege, sasa naomba Waziri anieleze kiwanja kile ni cha

Shirika la Ndege au ni cha Halmashauri ya Wanakondo ilii Wilaya iwe inatoza ushuru na kujipatia mapato.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii kwani haijajali maslahi ya nchi hii.

MHE. ASAA OTHMAN HAMAD: Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba heshima ya Taifa lolote ni kumudu kuuendeleza uchumi wake. Tanzania, Bandari, Reli, Anga, Maziwa na Mito, ni utajiri mkubwa kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, bandarini, watamyeyusha Waziri wakati Waziri ana heshima yake hapa nchini na nje ya nchi, jina lake linaheshimika, aache kuwatazama kwa karibu hao sio. Watendaji wa Bandari awapangue wote, watamweka pabaya!

Mheshimiwa Spika, UDA, Meya na Wakurugenzi wote waondolewe. Mji wa Dar es Salaam sasa ni aibu Kitaifa. Aibu! Fedha inayopotezwa kwa wafanyakazi kukosa kufika kazini, wanafunzi kushindwa kufika mashulenii kutokana na msongamano wa magari, ni wizi mtupu! Hii ni changamoto kwa Wizara!

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, Bandari ni lango la biashara duniani kote, ni njia kuu ya uchumi, hakuna nchi yenye bahari – bandari wananchi wake wakawa maskini. Bandari ya Lindi, ni muhimu kwa maendeleo ya nchi. Ilikuwa inasafirisha bidhaa na kupokea mzigo kutoka Ughaibuni moja kwa moja bila kutegemea Dar es Salaam. Ilikuwa inahudumia mashamba ya Mkonge, Ufuta, Karanga na kadhalika. Pamoja na mpango wa kuboresha bandari ya Lindi lakini hatujaona Fungu la fedha lillotengwa kwa ajili ya bandari ya Lindi

Mheshimiwa Spika, Reli ya Nachingwea, Waingereza waliona umuhimu wa Reli ya Nachingwea hadi Mtwara. Reli iliyojengwa baada ya Vita Kuu ya Pili iliyohudumia mashamba 25 ya Karanga Nachingwea *Groundnuts Scheme*, imeng'olewa bila maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, meli katika mwambao wa Lindi, Mtwara, Dar es Salaam na Tanga. Tulikuwa na meli ambazo zilikuwa zinatoa huduma katika Pwani ya nchi. Kukosekana kwa usafiri wa gherama nafuu kama meli na reli kunawenza kuongeza mfumuko wa bei katika nchi. Serikali ione umuhimu wa kuboresha huduma ya meli katika ukanda wa Pwani wa nchi yetu.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa nami naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati ilipokuwa inafanya kazi ipasavyo ilikuwa inasaidia sana Watanzania hasa wa Mpanda, Mwanza, Kigoma na Tabora kuweza kusafiri kwa gherama nafuu. Leo hii hali ya Watanzania ni mbaya kufuatana na mfumuko wa bei lakini moja ya sababu ni kukosekana kwa usafiri wa reli wenye gherama nafuu. Hata kiuchumi tumeathirika sana baada ya kukosa reli kwani Tumbaku ingeweza kusafirishwa kwa gherama nafuu na hivyo bei ya Tumbaku ingeweza kuongezeka hali kadhalika na zao la Pamba pia lingeweza kunufaisha wakulima. Pia hata pembejeo zingeweza kusafirishwa kwa gherama nafuu na mkulima angenufaika na hilo. Nashauri Serikali ielekeze nguvu zaidi kufufua Reli ya Kati lakini pia reli hii ya zamani itumike kusaidia kutengeneza reli mpya, kwa kuitumia reli ya zamani itapunguza gherama ya usafirishaji wa vyuma vya ujenzi wa reli mpya.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Reli Tabora na Morogoro. Vyuo hivi vilianzishwa ili kuwasomesha wafanyakazi wa Shirika na Vyuo hivi viliendelezwa hadi Shirika liliopoingia ubia na RITES ya India, hata hivyo Vyuo hivyo havikubinafsishwa na hadi leo haviendelezwi wala hatujui ni nani anasimamia uendeshwaji wa Vyuo hivyo. Mitaala iliyopo ni ya kufundisha Udereva wa Treni, *Station Master*, Guards na kadhalika na Shirika halajirii tena wafanyakazi wapya, je, hao wachache wanaosoma waende kufanya kazi wapi au na wao waungane na wasomi wengine kurandaranda mitaani? Nashauri reli ifufuliwe na wale wote ambaa wamesoma Vyuo vya Reli waajiriwe.

Mheshimiwa Spika, pia kuna wastaa fu wa *EAC Railways* ambao hadi sasa hawajalipwa mafao yao, naomba Serikali ilipe haki zao haraka. Naomba majibu wakati wa majumuisho ya hotuba leo.

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege Tabora. Nashauri kama inawezekana Uwanja wa Ndege wa Tabora upelekwe/usogezwe mbali na mahali ulipo kwa sasa kwa sababu baada ya miaka 30 ijayo Kiwanja cha Ndege kitakuwa kero kwani kitakuwa kimezungukwa na makazi ya watu. Tupate eneo kubwa zaidi na mbali na hapo kilipo ili tutoe nafasi kwa upanuzi wa Mkoa wa Tabora. Hali ya Kiwanja cha Tabora kinahitaji uwekezaji mkubwa zaidi, miaka ijayo tuwekeze lakini tuwe na uhakika mbele ya safari isije ikawa kero kwa sababu kwa sasa ni karibu sana na maeneo ya makazi.

Mheshimiwa Spika, historia inatusuta kwa sababu kiwanja hiki cha ndege kilijengwa na Mjerumani na ni kiwanja cha kwanza kwa ukubwa chini ya Jangwa la Sahara kwa wakati huo na ndio kilikuwa Kiwanja cha Kimataifa. Kiwanja hicho mwaka 1975 kulikuwepo na Kampuni kutoka Kenya ambayo ilikuwa inakipanua ili kuendelea kuwa cha Kimataifa. Hata hivyo, mwaka 1977 kulitokea vita vya kumwondo Idi Amin alipoivamia Tanzania. Hivyo mkandarasi huyo aliondoka na mpaka leo kuna masalia ya mitambo yake hapo uwanjani. Mpaka leo kiwanja hiki hakijapewa kipaumbele cha kuendelezwa. Leo hii hakuna ndege inayotua Tabora, hii ni adhabu kwa wakazi wa Tabora na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna faida nyingi za kuwa na kiwanja cha ndege cha kimataifa Tabora kwa sababu utalii utaongezeka ambapo kwa sasa watalii wote wanapitia Arusha. Pia kuna wanunuzi wa Tumbaku nao wangeweza kutumia kiwanja cha ndege cha Tabora na kutuongezea mapato kwani ni haki yetu kupata mapato kupitia wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, *SUMATRA* wanafanya kazi nzuri lakini sasa wameanzisha tabia ya kuwabughudhi wenye magari binafsi lakini makubwa yenye uwezo wa kupakia watu saba (7) hapa imekuwa dili ya kupata fedha kwa sababu mwenye gari kubwa hata kama anaitumia mwenyewe bila kufanya biashara *SUMATRA* wanamkamata na kumtoza faini kwa nguvu au mpaka apewe rushwa ndio wanamwachia.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii adimu na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji katika hoja hii muhimu katika maendeleo ya nchi yetu na inayogusa maisha ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kulivunja Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) na kuliunda upya kwani kwa sasa Shirika hilo kinadharia lipo lakini kwa vitendo halipo, limeshindwa kuijendesha na jitihada zote zilizofanywa ili kulifufua zimeshindikana. Hivyo basi ni wakati muafaka kuliunda upya.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itumie fursa aliyotujalia Mwenyezi Mungu ya Bahari ambayo kama tutaimarisha bandari zetu za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara zitatupatia mapato makubwa zaidi na kuinua uchumi wetu. Aidha, Serikali iharakishe ujenzi wa bandari mpya za Bagamoyo na Mwambani Tanga ili Sekta ya Uchukuzi izidi kuimarka zaidi.

Mheshimiwa Spika, huduma za uchukuzi katika nchi yetu zinaelekeea kubaya kutokana na msongamano katika Miji yetu mikubwa hivyo jitihada za kupunguza msongamano ni jambo la lazima ili kunusuru uدوروري wa uchumi wetu. Aidha, kutengeneza barabara ndogondogo hususan katika Jiji la Dar es Salaam kutasaidia sana kupunguza msongamano huo. Ahsante.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa Bandari ya Nchi Kavu katika eneo la Tunduma. Katika eneo la Tunduma ambapo ni mpakani mwa Tanzania na Zambia, ni eneo lenye msongamano mkubwa wa magari makubwa (ya mizigo) yaendayo nchi za jirani za Zambia, Malawi, Congo, Zimbabwe, Botswana na South Africa yamekuwa yakiegsha maeneo mbalimbali ya wananchi katikati ya Tunduma hivyo kuhatarisha hali ya usalama kwa raia na kukosresha Serikali mapato ambayo yangeweza kukusanywa kwa magari hayo kuegesha maeneo yatakayojengwa na Serikali kama Bandari ya Nchi Kavu wakati yakisubiri kukaguliwa na

kuendelea na safari. Hivyo basi kama Serikali ipo tayari inaweza kupanga pesa za ujenzi wa Bandari hiyo kwa lengo la kupata chanzo kipya cha mapato nchini.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, napenda kutoa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa anga, pamoja na kuwa usafiri wa anga hapa ndani unaotolewa na ndege za *Precion Air, Coast Travel na Fly 540* pamoja na kadhalika, bei ya usafiri wa ndege iko juu sana kama tiketi ya ndege (*one way*) KIA – Dar es Salaam ni shilingi 340,000 mpaka 370,000. Nashauri Serikali iweke taratibu ya kuthibiti nauli za ndege.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa watalii kuja Tanzania. Kwa kukosekana kwa *National Airline* ya kutoka Tanzania kwenda katika nchi ambazo ni soko kuu la watalii wetu Amerika ya Kaskazini, Ulaya ya Kati, America, Canada, Ujeruman na kadhalika na kutokuwa na "*Code Sharing Agreement*" nchi imekuwa inakosa 60% ya mapato kutoka kwa watalii hao, fedha hizo zinalipwa kwa ndege za nchi za nje, hii katika misingi ya kiuchumi ni *leakage*. Ushauri wangu, Serikali ifanye taratibu za haraka za kuwa na *National Flag Carrier* itakayofanya *code sharing* na mashirika mengine ya ndege.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa reli, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuwepo kwa mtandao wa reli imara, itafanya barabara zetu zidumu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa jumla. Kwa vile bajeti hii ni ndogo, nashauri isipitishwe badala yake Serikali ikae upya, bajeti iongozwe, hata kwa mkopo utakaolipwa kwa miaka 60!

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo ya reli, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Songwe, Mbeya, usafiri wa ndege, bandari na usafiri wa mabasi.

Mheshimiwa Spika, reli zetu zimechakaa sana, huduma ni mbovu. Reli ya *TAZARA*, ni kitu gani ambacho kimesababisha kushuka kwa ufanisi wake? Mwanzoni ilikuwa ikibeba abiria kwa usafi na huduma bora; sasa hivi zimekuwa zikiishia kubeba mizigo tu na wakati zamani abiria wengi walikuwa wanatumia reli hii ya *TAZARA* kutokana na huduma bora, bei nafuu na usalama. Maelezo ya kuhusu reli hii ya *TAZARA* yatolewe maana pia ilisaidia Mkoa mingi jirani.

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, Mkao wa Mbeya, kwa nini umechukua muda mrefu kukamilika? Umekuwa ukisusua na imekuwa ni hadithi ya Abunuwas, kwa nini? Maelezo ya kina yatolewe. Maelezo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi katika kitabu chake ukurasa wa 29 hayatoshelezi. Tukumbuke kuwa Mbeya ni *gateway* ya Mikoa na nchi nyingi za jirani, hivyo Mikoa na nchi jirani nyingi zitautumia pia kuongeza pato la Taifa/Mkao. Kwa nini gharama za utengenezaji uwanja huo zinaongezeka kila mwaka bila mafanikio ya kumalizika kwa ujenzi huo?

Mheshimiwa Spika, kwa nini hadi leo Tanzania haina usafiri wa anga kwa maana ya ndege ya Taifa? Kwa nini Shirika la ATC lipo na wakati halina hata ndege? Linafanya nini na *line-operate* vipi? Ni aibu kwa Taifa kwamba nchi yetu haina ndege hata moja, nemo yetu ya Taifa inapotea. Kuwa na ndege ya Taifa ndio kioo cha Taifa ndani na nje ya nchi. Serikali iunde upya kabisa Shirika hili na kuwezesha kuwa na ndege. Ikiwezekana hata iingie ubia na mwekezaji mwingine ili tu kuiletea nchi yetu heshima na nembo ya Taifa kuendelea kuwepo. Ukitaka kwenda Mbeya mfano inabidi uchukue mabasi ambayo yanachukua masaa kumi na mbili njiani. Ukitaka kusafiri nje ya nchi hadi upitie Nairobi nchi nyingine kwa ajili ya *connection* ya *Flight!* Hii ni aibu kubwa. Hatuna *National Carrier*, usafiri wa anga peke yake tungejipanga vizuri tungeweza sana kuinua uchumi wa nchi yetu kupitia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa mabasi imekuwa ni kero kwa mabasi ya Mikoani, ni machafu hususan ya Mbeya, huduma ni mbovu sana na hazilingani na nauli wanayotoza ambayo haiku *consistence*. *SUMATRA* inafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa nini bandarini mizigo huwa inachelewa na kuna ukiritimba sana usio na tija? Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina pia katika hili.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, kuna wafanyakazi wa reli zaidi ya 2,300, Kigoma ambao wanadai kifuta jasho chao toka kwa *TRC*, liliokuwa Shirika la Reli kwenda *TRL*, Kampuni ya Reli kwa muda mrefu sana hali inayowakatisha tamaa, lakini pia hawajui watalipwa lini. Sasa basi namwomba Waziri anieleze ni lini na kwa utaratibu upi watu hawa watalipwa kifuta jasho chao hasa ukizingatia kadri siku zinavyozidi kuongezeka ghamama za maisha zinaongezeka na wakati huohuo thamani ya pesa yetu inazidi kushuka.

Mheshimiwa Spika, kipindi Wizara hii ikiongozwa na Mheshimiwa Kawambwa tuliona Serikali ikitoa mipango ya kuboresha Reli ya Kati kwa kuongeza unene wa reli ili Garimoshi liweze kupita kwa kasi zaidi ya hii ili yopo sasa. Cha kusikitisha zaidi ni kwamba hakuna kilichofanyika mpaka sasa hali inayowafanya Watanzania wa Kigoma na kwingineko kuona kwamba mipango yetu mingi ni ya kwenye makaratsi na maneno tu lakini utekelezaji haupo. Hivyo basi kwa niaba ya Wanakigoma na Watanzania wote, tunasema tumechoka na hatutaki maneno bali utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, namwomba Waziri atueleze ni mikakati gani ya makusudi na ya haraka sana lakini pia ya ukweli ambayo imewekwa ili kuinusuru Reli ya Kati sambamba na bandari muhimu ya Kigoma.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndege la *ATCL*, nchi yetu ni kati ya nchi inayokua sana kuhusiana na biashara ya utalii na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza sio muda mrefu tutakuwa tuna-export mazao/maua mengi sana kwenda nje ya nchi. Kwa sasa hivi wenzetu wa nchi za Afrika Mashariki tayari wanazo ndege zao. Ni jambo la aibu mtalii anataka kuja Tanzania unamwambia njoo na *Kenya Airways*, hii ni aibu! Serikali imekuwa ikihamasisha mashirika makubwa kama *British Airways*, *Turkish*, *KLM* na kadhalika, ni jambo zuri lakini je, wakishatua Dar es Salaam au *KIA*, watasafirije bila kupata *local connection*? Je, akiwa anataka kwenda Mtwara au *KIA* kutoka Dar es Salaam si ingekuwa vizuri kutumia ndege yetu ya Taifa *ATCL*? Kwa kuwa kati ya hasara na kudondoka kwa *ATCL* ni madeni Shirika hili linayodaiwa, je, mpaka kufikia leo *ATCL* inadaiwa dola ngapi kwa kukodisha ndege ya *Airbus*? Je, Serikali haioni ni busara kuirudisha ndege ile ambayo inakodishwa kwa zaidi ya dola 300 kwa mwezi na fedha hizo zikatumika kwa ndege ya bei nafuu kama *Boeing* ambayo itakuwa ni rahisi zaidi sababu hatuhitaji *training* kubwa kwa *Ma-Captain*, Wahudumu, *Ma-Engineer*.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Reli, ni jambo la kusikitisha nchi kama Tanzania hatuna usafiri wa uhakika. Reli ndiyo ingekuwa kinga nzuri kwa barabara zetu kwa kusafirishia mizigo mizito na ni bei ya nafuu zaidi. Je, Serikali imeflikia wapi katika mchakato wa kuhakikisha reli (usafiri wa treni) unafanya kazi?

Mheshimiwa Spika, nashauri, kwanza, kama watatafutwa wawekezaji wa kuziendesha reli zetu, ni bora isipewe Kampuni moja, wapewe wawekezaji tofauti, wa Reli ya Kati na Reli ya Kaskazini mwininge. Hii itaboresha usafiri kwa sababu wataweza kutoa huduma hiyo, tumeshuhudia Kampuni ya *RITES* ilishindwa kuhudumia Reli ya Kati na ilikuwa njia moja tu. Pili, mwekezaji atakayepewa *tender* hii basi kwa mpango wa muda mrefu ziwepo njia mbili, treni moja inatoka Moshi nyngine inatoka Dar es Salaam zinapishana njiani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari, ni jambo la kusikitisha mizigo ikipitishwa Mombasa inatoka haraka sana lakini ikipitia Tanzania inachukua muda mrefu na kuna usumbufu sana. Je, tatizo ni nini? Serikali haioni tunakwamisha wafanyabiashara wa Kimataifa kuja kuwekeza Tanzania?

Mheshimiwa Spika, karakana iliyopo KIA (*Kilimanjaro International Airport*), ni kwa nini Karakana hii haitumiki? Ni kubwa inaweza kutumika kwa kutengeneza ndege, kupiga rangi na kadhalika, ilijengwa ili ifanye nini?

Mheshimiwa Spika, uwanja mdogo wa *Moshi Airport*. Uwanja ule upo *very strategic* kwa ajili ya watalii na kadhalika lakini uwanja ule umesahaulika kabisa. Je, kuna mkakati gani wa kuufufua Uwanja wa Moshi.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu ujenzi wa reli ya Dar – Isaka – Kiize – Msongati – Kigali, ushauri na jitihada za pamoja za Wizara husika Rwanda, Burundi na Tanzania

Mheshimiwa Spika, reli inayotarajiwa kujengwa yenyewe upana wa mm 1435, jitihada za utafutaji fedha *Exim Bank China* zihusise Mawaziri wa Uchukuzi wa Rwanda, Burundi na Tanzania. Serikali ya China inaweza kutoa mkopo wa bei (riba) nafuu kuliko kwingine kote duniani. Hata Marekani sasa inakopa China (PRC). Jitihada nyine zinaweza kufanya na Mawaziri husika kila mmoja kivyake ila ni vema wakaarifiana ili kuleta ufanisi, tija na zisije zikawachanganya wakopeshaji/wafadhibili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Uchukuzi ya mwaka 2011/2012. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ya kusimamia na kuendeleza sekta ya uchukuzi ambayo ni moja ya mihimili ya kuinua uchumi wa nchi yetu. Wananchi wengi wamefarijika kuona kwamba bajeti hii inalenga kuimarisha na kuboresha miundombinu katika Bandari zetu pamoja na miundombinu ya Reli, Viwanja vya Ndege na mfumo wa kusafirisha mafuta ghafi na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, bajeti hii imezingatia kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi ambayo imeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha nchi ina miundombinu ya usafiri ya kutosha, salama, yenyewe ubora, ufanisi na yenyewe gharama nafuu, ili kumuwezesha mkulima kusafirisha mazao yake toka shambani na pia kupata pembejeo kwa bei nafuu kwa lengo la kuleta maendeleo na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, Reli na Bandari zetu ni vyanzo vizuri vya mapato ya Taifa. Hivyo inatakiwa Serikali iweke mipango ya makusudi na kutenga fedha za kutosha kuboresha sekta hizo ili ziweze kuzalisha zaidi. Umuhimu wa miundombinu na usafiri wa Reli unatambuliwa na kila mwananchi. Mikoa ambayo imebahatiwa kuwa na Reli imenufaika sana kwa sababu wanarahisishiwa kupata pembejeo za kufanikisha kilimo bora na pia mazao yao yanafika sokoni kwa wakati kwani gharama za usafiri huu ni nafuu sana na huweza kubeba mizigo mizito na mingi ukilinganisha na aina nyine ya usafirishaji. Taifa pia linakuwa na uhakika wa kupata fedha za ndani na za kigeni kutookana na Reli hii kutumiwa kusafirisha mizigo ya nchi za jirani hasa zile za Afrika Mashariki kama Uganda, Burundi, Rwanda na DRC na Zambia, Afrika Kusini na Namibia kwa upande wa reli ya TAZARA. Aidha, Reli yetu ikiboreshwa na kutumiwa ipasavyo, itapunguza uharibifu wa barabara na kuokoa fedha za ukarabati wa mara kwa mara kwa mizigo mizito itasafirishwa kwa kutumia njia ya reli badala ya barabara.

Mheshimiwa Spika, nichukue pia fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa Kampuni Miliki ya Rasilimali za Reli (*RAHCO*) na Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kazi kubwa waliyofanya wakati wa mafuriko yaliyotokea Wilaya ya Kilosa ambayo yaliharibu sana miundombinu ya reli. Kazi hii imefanyika kwa utaalamu, ujuzi na ushirikiano mkubwa na imechukua muda mfupi kuliko ilivyotegemewa. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, viwanja vyetu vya ndege kwa sasa hivi vingi viko katika hali mbaya sana. Nashukuru na nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa matengenezo yanayoendelea sasa katika Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere na pia ujenzi wa jengo la Watu Mashuhuri (*VIP Lounge*) katika kiwanja hiki. Hii itaongeza sana hadhi (*image*) ya nchi yetu kwa wagensi wanaoingia na kutoka.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, nashauri Serikali itupie macho Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ambacho kwa kweli kinapitisha wageni wengi, watalii kutoka nje, hali yake hairidhishi hata kidogo. Pamoja na mipango mizuri ya kukarabati viwanja vya ndege Mikoani kama kiwanja cha ndege cha Mpanda, Mafia, Bukoba na Kigoma, Serikali pia iangalie mji wa Dodoma unavyokua kwa kasi. Kiwanja kilichopo kimepitwa na wakati na ni kidogo sana kana kwamba ndege kubwa haziwezi kutua hivyo kijengwe kiwanja ambacho kitakidhi na kuendana na kukua kwa Mji wa Dodoma. Serikali iangalie namna ya kukarabati kiwanja cha ndege cha Mbeya ili nacho kiweze kurahisisha usafiri wa kutoka Kusini. Naamini kwa hali nzuri ya hewa ya Mbeya kungekuwa na kiwanja cha kuaminika cha ndege, wawekezaji wengi wangefungua mashamba ya maua, viazi, ndizi, mpunga na mazao mengi yanayostawi katika Mikoa ya Kusini. Mazao haya yangeweza kuuzwa nje ya nchi na kuipatia Serikali pesa za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo, nashauri kuwepo na mpango wa kushirkiana na Sekta Binafsi (*PPP*) kuendesha baadhi ya miundombinu hii kwa mikataba itakayonufaisha pande zote. Kwa mfano, katika uchakavu wa reli, Serikali ijikite kutengeneza na kuboresha miundombinu na kutafuta wawekezaji amba o watafanya shughuli za usafirishaji amba o watakuwa na mabehewa yao, vichwa vya treni na wafanyakazi wao. Katika uendeshaji huu, Serikali itapata mrahaba kufuatana na mkataba. Pia itaondokana na gharama za manunuzi ya vitendea kazi hivyo ambavyo vinagharimu pesa nyingi sana za kigeni na za ndani na pia itaondokana na jukumu la kutunza wafanyakazi amba o kama mwendeshaji akilyumba basi linakuwa jukumu la Serikali.

Mheshimiwa Spika, bandari ni sekta nyingine inayochangia katika pato la Taifa. Kwa sasa hivi bandari ya Dar es Salaam inaelekea kulemewa na mizigo wakati bandari zetu nyingine hazitumiwi kikamilifu. Naiomba Serikali iweke mikakati ya kupunguza msongamano wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam na kutoa fursa kwa bandari ya Tanga na Mtwara kutumika kikamilifu. Kwa mfano, Serikali inaweza kuamua na kupitisha sheria kwamba baadhi ya bidhaa zinazopitia bandari ya Dar es Salaam zipitie bandari ya Tanga na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa sasa hivi ina upungufu mkubwa wa nishati ya uhakika. Nashauri Serikali iboreshe miundombinu ya kusafirisha gesi asilia inayotoka Songsongo kuangalia uwezekano wa kuitumia kuzalisha umeme utakaopunguza tatizo sugu liliopo kwa sasa hivi. Ni vyema pia kujenga na kuboresha miundombinu ya reli kwa maeneo yale ambayo yanasemekana kuna mkaa wa mawe, mkaa huu pia unaweza kwa kiasi kikubwa kusaidia katika kupunguza tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nianze sasa na kilio cha wananchi wa Jimbo la Kibaha vijijini kuhusu maendeleo. Watu wa kule wamenituma nisisahau msemo wao unaosema "Kilio na Mwana". Pamoja na kwamba Jimbo la Kibaha Vijijini liko karibu sana na Mji wa Dar es Salaam, maisha ya wananchi wa Jimbo hili yako chini sana katika nyanja zote. Uboreshaji wa sekta ya uchukuzi inaweza kufungua nafasi kubwa ya kuendeleza Jimbo lile na pia kupunguza msongamano wa watu wanaokimbilia Dar es Salaam kwa kufikiri kwamba maisha mazuri yanapatikana Mjini. Kufungua nyanja za biashara na kuhamishia shughuli nyingine katika Jimbo hili itasaidia pia kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya haraka si kwa Jimbo hili tu bali hata kwa Majimbo mengine ya jirani kama Chalinze, Bagamoyo, Kibaha Vijijini, Kisarawe, Mkuranga na hata Morogoro Vijijini. Reli ya Tanzania inapita katika Jimbo la Kibaha Vijijini na inategemewa na wananchi katika usafiri, ajira na biashara kwa maana pale Stesheni ya Ruvu, treni huunganisha mabehewa ya kwenda Bara na pia kutoka Bara kuja bandarini Dar es Salaam. Kwa makusudi kabisa na kwa umuhimu wa stesheni ya Reli ya Ruvu (*Ruvu junction*), Serikali ingeboresha na kujenga/kupanua stesheni hii ili kufungua mwanya wa mapato zaidi kwa wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini, Mkoa wa Pwani na Mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Spika, bandari kavu ni eneo lingine linaloweza kutegemewa kufungua mianya ya uchumi katika Jimbo la Kibaha vijijini. Pamoja na mikakati ya kupunguza msongamano wa mizigo inayointingia katika bandari ya Dar es Salaam, napendekeza Serikali katika kushirkisha sekta binafsi iangalie uwezekano wa kutumia Mji Mdogo wa Mlandizi amba o bado una maeneo makubwa ya ardhi ambayo hayajavamiwa na wananchi, kujenga bandari kavu au kijiji cha kuegeshea magari yote yanayoingizwa hapa nchini yawe ya *transit* au ya kuuza hapahapa nchini

kama ilivyo katika Mji wa Sharjah kule Dubai. Kwa kufanya hivi, Serikali itakuwa imesaidia katika kukuza maendeleo ya Mkoa wa Pwani, itapunguza msongamano wa sehemu za kuegesha magari zilizoko kila mtaa wa Dar es Salaam, itaongeza huduma ya kutoa mizigo kwa haraka zaidi na pia kupunguza msongamano wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam, kukuza uchumi wa Mkoa pamoja na kutoa ajira kwa vijana wa Mkoa wa Pwani na hata Mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivi Serikali itakuwa imeharakisha maendeleo ya Jimbo lile kwani mzunguko wa shughuli za watu kama biashara, mahoteli, nyumba za kulala wageni, maofisi na makazi, yote haya yatasaidia Mji huu kukua kwa haraka kiuchumi, huduma za jamii zitapatikana kwa urahisi na pato la Taifa litaongezeka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wake kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara iandae mpango mkakati wa kufufua na kuendeleza reli, bandari na viwanja vya ndege ili njia hizi kuu za uchukuzi na usafiri ziweze kuchangia katika uchumi na pato la Taifa, lakini pia kupunguza kero ya usafiri na uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege wa Dodoma uhamishwe nje ya mji na kujengwa kama *International Airport* kuwezesha Makao Makuu na katikati ya nchi kuwa na usafiri wa anga wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, mpango mkakati wa reli uandaliwe na kila Makao Makuu ya Mkoa ifikiwe na reli.

Mheshimiwa Spika, bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara zipanuliwe na kupatiwa vitendea kazi vya kuaminika na kutosha ili kuongeza ufanisi wa bandari hizi.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara kwa hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu na kwa usalama wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ametupa Tanzania bahati ya kipekee kijiografia kwa kuzungukwa na nchi nane na bahari ya Hindi upande wa Mashariki, hali ambayo inatupa fursa ya kufanya biashara na nchi hizo, lakini hatujatumia fursa hiyo vizuri. Je, Serikali ina mkakati gani wa dhati wa kuhakikisha kwamba Reli za Kati na Tazara, bandari zetu na Shirika la Ndege Tanzania (ATC) zinafanya kazi vizuri mapema iwezekanavyo ili kukuza uchumi wa nchi hii na usalama wa Taifa?

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011 -2015), hautamki lolote kuhusu kupanua/ujenzi wa viwanja vya ndege vya Nduli (Iringa) na Njombe (Mkoa mpya). Je, kuna mpango gani wa kupanua/kujenga viwanja hivyo ukizingatia kwamba Mikoa hii inazalisha mazao mengi ikiwa ni pamoja na mbogamboga, matunda, maua na kadhalika pamoja na utalii katika Milima ya Kitulo na Mbuga za wanyama za Ruaha?

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Uchukuzi katika mambo makubwa matatu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuchangia kwa kuanzia na upande wa viwanja vya ndege. Nimeona kwenye miradi ya maendeleo ya Wizara Mikoa kadhaa imepatiwa fedha kwa ajili ya kutengeneza viwanja vyao au kufanya marekebisho viwanja hivyo. Nina masikitiko sana ninapoona uwanja wa ndege wa Mkoa wa Shinyanga hauko kwenye *list* ya viwanja vilivyopata fedha bajeti hii ya mwaka 2011/2012. Pamoja na kutoa almasi na dhahabu kwa wingi, Mkoa huu unapuuzwa katika kupewa maendeleo. Kiwanja kile cha Shinyanga hakina hata kipande cha

lami, kutokea barabara kuu iendayo Mwanza mpaka *Airport*, ni vumbi tupu. Kwa nini Mkao ambao una rasilimali nyeti na nyingi kiasi hiki unakuwa unasahafulika namna hii? Kwa nini watu wanaokwenda Shinyanga watue Mwanza kwanza ndio wapande magari yao kwenda Shinyanga na wakati wangeweza kushuka moja kwa moja hapa Shinyanga? Naomba sasa Waziri anipe majibu ya kuridhisha kuwa ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa uwanja huo kwa kiwango cha lami na kupunguza adha wanayoipata wananchi na wafanyabiashara wanaokwenda na kutoka Mkoani Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba niende katika Shirika la Reli yaani (*TRL*). Ni ukweli usiopingika kuwa sasa hivi Tanzania hatuna tena Shirika la Reli bali ni ubabaishaji mtupu. Tumejionea wenyewe tumeingia mkataba na Wahindi, tumeuvunja wenyewe sasa tunawalipa *billions of money* kwa ajili ya uzembe wetu.

Mheshimiwa Spika, hakuna usafiri wa watu maskini kama ilivyokuwa Shirika la Reli Tanzania. Nikiwa mionganoni mwao nimepanda sana treni miaka hiyo ya nyuma kabla ya kubinafsishwa. Tatizo hapa ni nini lakini? Hivi kweli nchi hii inakwenda wapi jamani? Mashirika yote ya umma yamekufa hata kama yapo yanaelekeea kufa hivi karibuni. Watu waliokuwa wanaitegemea treni ya katii kwenda Mpanda, Kigoma na Mwanza na hasa walioko kwenye *vi-station* ambavyo viko porini wanafanyakaje kwa sasa? Naomba Wizara itoe ufumbuzi wa tatizo hili kwani Watanzania wengi sana wanapata shida na wafanyakazi wengi wamekosa ajira.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo treni ya mizigo sasa haiendi kwa wakati, kwani nina ushahidi kuna mfanyabiashara mmoja wa Kigoma, leo ni siku ya 21 behewa halijafika Kigoma sasa kama kuna *perishable items* nani anaingia hiyo hasara? Naomba nipatiwe majibu yanayoridhisha katika hili.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba nizungumzie sasa upanuzi wa uwanja wa ndege wa Julius Kambarage Nyerere (*J/NA*). Upanuzi wa uwanja huu mimi sina shaka kabisa. Kinachonipa shida hapa ni suala ambalo linawanyima usingizi wananchi ambao wanakaa kando ya uwanja huu Kata ya Kipunguni.

Mheshimiwa Spika, tokea Serikali iamue kupanua uwanja huu, kuna wananchi mpaka leo wameshindwa kuendelea na ujenzi, kukopa wala kuuza maeneo yao kwa sababu wanatakiwa kuhama lakini hawajalipwa fidia. Wananchi hawa wamekuwa maskini sasa kwani hawawezi kufanya kitu chochote, Serikali imewaambia wahame lakini haitaki kuwalipa fidia mpaka leo. Hawapati wapangaji wala hawakopesheki. Sasa hawa watu wataishi maisha gani? Tatizo ni nini linalofanya Serikali au Wizara isiwali pe fidia wakatoka hapo wakaendelea na maisha yao ya kila siku? Naomba nipatiwe jibu ni lini Serikali itawalipa wananchi hawa wa Kipunguni?

Mheshimiwa Spika, nne, nizungumzie bandari ya Dar es Salaam. Bandari hii imekuwa ikitumika nchini na nchi jirani kusafirishia mizigo na kupokea mizigo. Bandari hii ya Dar es Salaam ninavyoona mie inaelekeea siko kwani imekuwa na ubabaishaji mtupu. Kumekuwa na wizi wa mizigo inapofika bandari ya Dar es Salaam. Magari yamekuwa yakitolewa vifaa vingine na kufanya wenye magari kuingia hasara mara mbili. Hii tabia imeota sugu katika bandari hii kwani naona hakuna ufumbuzi wa jambo hili kadri siku zinavyokwenda. Naomba Serikali au Wizara iliangalie suala hili kwani linakatisha tamaa wafanyabiashara wanaotumia bandari hii kwani inapoteza sifa ya kuwa bandari salama.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali au Wizara iangalie pia suala la upakuzi wa makontena bandarini kwani unasuasua na kufanya mlundikano wa meli baharini zikisubiri kupakua. Naomba nipatiwe majibu Serikali ina mpango gani kuiwezesha bandari hii kufanya kazi zake kiufundi zaidi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu Uwanja wa Ndege wa Songwe. Ujenzi wa *Run way* ya ndege ni sawa kabisa na ujenzi wa barabara ya

lami. *Base* yake hujengwa na kifusi, mawe pamoja na *fill* ya jiwe liliilosagwa. Cha ajabu ni kuwa pale uwanjani hakuna *crasher* ya kusaga mawe. Hivyo kandarasi ameweka *fill* ya sementi ya pozolana badala ya *fill* ya mawe yaliyosagwa. Sasa hivi hiyo *base* imeonesha nyufa hata kabla lami hajawekwa. Naomba maelezo ya kina kuhusu jambo hili. Je, bei ya ujenzi imebadilika baada ya kupindisha *specifications* namna hii? Je, uwanja huu ukikamilika utahimili ndege zilizokusudiwa?

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri kwa kupewa Wizara tayari imekufa kwani muda huu aliokuwa nao hatuwezi kumlaumu.

Mheshimiwa Spika, kwanza katika matengenezo wamesema mengi lakini shida ya viwanja vya ndege ni matengenezo. Cha kushangaza kiwanja cha ndege Mombo hakipo katika orodha ya marekebisho ya viwanja. Wakati viongozi wakuu na watalii wanatumia kiwanja hicho cha Mombo.

Mheshimiwa Spika, karakana ya reli ilikuwepo Tanga ni kwa nini ilihamishiwa Kilimanjaro?

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa reli ingesaidia sana msongamano wa barabarani na kuharibika kwa barabara. Katika ufumbuzi wa msongamano, ni lini bandari ya Tanga itaanza kujengwa ili kuondoa msongamano wa Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na wizi ndani ya bandari je, Serikali imejpanga vipi ili kuondoa tatizo la wizi ndani ya bandari?

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii isilaumiwe kwani viongozi wote ni wageni walioharibu sio wao.

Mheshimiwa Spika, reli ianzishwe mara moja, bandari ya nchi kavu ya Korogwe itaanza kujengwa lini?,

Mheshimiwa Spika, *SUMATRA* haifanyi kazi kwa sababu ajali za barabarani zinaongezeka, hakuna chochote.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Nundu na Naibu Waziri Mfutakamba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Ludewa tunahitaji Kiwanja cha Ndege au *Air Strip* kwa ajili ya uwekezaji wa Mchuchuma na Liganga, lini tutapewa?

Mheshimiwa Spika, lini Shirika letu la Ndege litaanza kazi? Kwa nini tunatumia *KQ* na *South African Airways*, tubinafsish, tutumie utaratibu wa *PPP*, tuuze *Shares*, *ATC* ianze kazi. Kwa nini halifanyi kazi? Lini litaanza?

Mheshimiwa Spika, reli Makambako je, ratiba ya reli inayopita Makambako ikoje?

Mheshimiwa Spika, je Tanzania tunamiliki meli (*Sheep*)? If the answer is no, why? Lini tutakuwa na meli yetu?

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hotuba yako ya Wizara ya Uchukuzi asilimia 100 kwa 100.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati. Tabora ni Mkoa ambao unategemea sana usafiri wa reli lakini kwa kutokujali sababu za kiuchumi, karakana iliyokuwepo Tabora, karakana kuu ilihamishiwa Morogoro bila ya kuzingatia hali halisi ya kuwa Tabora ni njia panda ya Tabora – Mwanza; Tabora – Kigoma; Tabora – Dodoma – Morogoro – Dar es Salaam na Tabora – Kalima – Mpanda. Hali ya karakana Tabora ni mbaya sana, haina wafanyakazi wa kutosha, kwa hiyo, iko haja ya kuongeza wafanyakazi na kuboresha majengo ya karakana. Nashukuru Waziri na Naibu Waziri tayari

wametembelea na kuona haja ya kuboresha karakana hiyo ili iweze kutoa mchango mkubwa katika kukarabati injini za treni na mabehewa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Reli. Chuo hiki hakifanyi kazi yake vizuri. Nina imani Chuo hiki kinaweza kusaidia kuboresha Menejimenti na watumishi wengine kama vile Ma-T.T, Madereva Magari, *Station Master* na kadhalika. Nakumbuka wakati wa *East Africa Railways*, Chuo hiki kilithaminiwa sana lakini cha kushangaza Watanzania wenyewe hatukijali au kwa kuwa kipo Tabora?

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndege ATCL halifai hata kidogo hasa Maafisa wanaoiji Maafisa Masoko au Mkurugenzi wa Masoko na utawala wa juu haufai kabisa. Tafadhali rekebisha uozo huu. Kwa bahati mimi niliwahi kuwa mfanyakazi wa *East African Airways* lakini sjawahi kuona uongozi mbovu kama huu wa *ATCL*. Tafadhali namwomba Mheshimiwa Waziri afanye mabadiliko bila ya kuona haya wala huruma.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege. Napenda kumpongeza angalau kwa kutukumbuka kwa kutapatia fedha za ujenzi wa uwanja wetu wa Tabora. Wakati umefika sasa kufikiria ujenzi wa *Terminal* na kuhakikisha uwanja wa Tabora unapata hadhi ya kuwezesha ndege hata usiku kutua. Taarifa nilizonazo, ndege nyingi za nje zinapita Tabora katika anga yake lakini ikitokea tatizo, uwanja wa Tabora hautoshi, kwa hiyo, ujenzi wa uwanja wa kisasa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja ya Waziri, ahsante.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, huwezi hata mara moja ukapata tija ukiimarsisha Bandari ya Mtwara ukiwa na lengo la kupata biashara kuititia *Mtwara Corridor (SADC)* bila ya kuimarsisha Bandari ya Mbambabay. Hakuna juhudhi zozote za kuimarsisha wala kujenga bandari ya Mbambabay. Hapa tunaendelea kuota ndoto tu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kila siku watu wanakuwa katika Ziwa Nyasa kwa kuzama. Hii inatokana na kukosekana kwa meli za uhakika katika Ziwa hilo. Mheshimiwa Rais ameahidi kutoa meli moja yenye uwezo wa kubeba abiria 400. Katika hotuba hii haijagusia ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ziwa lote la Nyasa hakuna bandari yoyote ya kisasa kuanzia Ifuogi Port hadi Mbambabay. Hakuna hata ahadi tu katika hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kuwa siungi mkono hotuba hii ya bajeti.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uhai alionijalia tena siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru na wewe pia kwa nafasi hii lakini nimshukuru Waziri wa Uchukuzi, Naibu wake na Timu yake yote kwa taarifa na mpango kazi wao.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuchangia kwa maandishi juu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba miundombinu ya reli, bandari na *ATCL* pamoja na sekta ya barabara ndio uti wa mgongo wa uchumi kama sekta hizi zingekuwa hai. Kwa muda mrefu sasa sekta hizi zimekuwa zinafanya kazi kwa kiwango cha chini sana, *TPA*, reli nayo ilikuwa inakaribia kufa kabisa lakini *ATCL* ndio imekufa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wizara inahitaji nguvu zaidi na fedha za ziada, kurekebisha kina cha bandari, kupanua reli (Kati na *TAZARA*) na kununua ndege mpya za kutosha lakini kuboresha Menejimenti na uwajibikaji wenye uadilifu wa hali ya juu, ukiwijali wafanyakazi wa sekta hizo kwa kuboresha mishahara na posho zao mbalimbali lakini kulipa madeni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, natoa rai yangu kuwa Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Mawasiliano kuuletea Mkoja wa Rukwa maendeleo. Wizara ya Ujenzi inapo jenga barabara, Wizara ya Mawasiliano inapoboresha mawasiliano basi na Wizara ya Uchukuzi aidha inapo jenga bandari ya Kasanga basi ifikirie kujenga reli kutoka Kasanga iunganishwe na reli ya

TAZARA pale Tunduma (inawezekana) lakini pia uwanja wa ndege wa Sumbawanga uweze kuboreshwa ili sekta hizi za barabara (uchukuzi) reli, bandari na usafiri wa anga ukikamilika na kufanya kazi vizuri itakuwa ukombozi kiuchumi, kijamii, kimaendeleo kwa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika sekta hii ya uchukuzi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, reli zetu zimebaki zilezile tu yaani reli ya Kati na TAZARA. Sasa tuna miaka 50 ya Uhuru. Ni reli pekee ndiyo inaweza kuchukua mizigo mingi na kusafirisha watu kwa uwingu zaidi na bei nafuu. Mikoa ya Ruvuma na Rukwa ni Mikoa yenye rasilimali kubwa sana ya madini, ardhi nzuri hivyo kuwa na mazao mengi ya kilimo. Ni vyema ikaweka mipango ya kufikisha reli Sumbawanga na kujenga reli toka Makambako kwenda Songea - Mbinga na Songea Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa ujenzi wa reli toka Mtwara - Songea - Mbinga - Mbambabay upewe kipaumbele sasa. Ningefurahi kuona angalau upembuzi wa mradi umeanza katika mwaka huu. Katika bajeti ijayo itakuwa vyema kuona hii imetafsiriwa katika bajeti na ujenzi kuanza.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Uwanja wa Songwe Mbeya. Pongezi kwa ahadi ya kukamilisha December 2011. Naomba sasa viwanja vya Songea na Njombe viboreshwe ili vitumike kupeleka wasafiri na bidhaa.

Mheshimiwa Spika, ombi maalum, la kwanza, Mji wa Mbinga hauna uwanja wa ndege, uchumi ni mkubwa, Halmashauri imekwishatenga eneo, tunaomba wataalamu waje wakague na kwa pamoja mshirikiane kuona tunapata kiwanja cha ndege. La pili, uwanja wa Songea hakuna ndege za abiria zinazotua. Namwomba Mheshimiwa Waziri ashawishi kampuni za ndege zifike Songea.

Mheshimiwa Spika, kwa vile sasa tunao uhakika wa kuanza kutumika kwa kiwanja cha kimataifa cha Songwe - Mbeya, naombwa Serikali iboreshe viwanja vifuatavyo ili wakulima wa maeneo haya waweze kusafirisha mazao kama maua na matunda na pia kuwezesha watu kusafiri. Viwanja hivyo ni Kiwanja cha Songea, Kiwanja cha Njahe, Kiwanja cha Iringa, Kiwanja cha Mbinga (Tarajiwa) na Kiwanja cha Tunduru. Hii itasaidia kukifanya kiwanja cha Mbeya kiwe *busy* wakati wote.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia uzima nilionao. Naomba pia nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na shukrani hizo, nampongeza Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Nundu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mfutakamba, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri inayofanyika na Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja hii ya Wizara ya Uchukuzi ni kuhusu kucheleweshwa kwa malipo ya fidia kwa wananchi wa Ikumbi ambao walihamishwa miaka mitatu iliopita ili kupisha ujenzi wa nyumba eneo linalotazamana na uwanja wa ndege. Je, lini Serikali itawalipa wananchi wa Ikumbi mafao yao?

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege wa Songwe umewazuia wananchi wanaoishi Kijiji cha Iwejere (Ikambi Mtoni) ambao mahitaji yao makubwa yako Songwe viwandani. Serikali mwaka jana ilahidi kwamba itawajengea barabara lakini mpaka sasa barabara hiyo haljajengwa na watoto wanaotoka kitongoji cha Iwejere wanashindwa kabisa kupita ili waweze kwenda shulenii lakini wanapita njia ndefu na hata kucheleva kwenda au kufika shulenii. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu suali hili.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya kumaliza ujenzi wa Kiwanja cha ndege cha Songwe imekuwa ikitolewa mara kwa mara lakini bado ahadi hizo haziteketezwi. Je, Serikali inatoa ahadi gani tena kuhusu kumalizia uwanja wa Songwe?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba sijafanya utafiti wa ubora wa ujenzi wa kiwanja lakini kuna haja Serikali kufanya utafiti licha ya kwamba kuna Mshauri katika ujenzi wote wa kiwanja.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. MESHACK J. OPULKWA: Mheshimiwa Spika, Shirika la Reli limekuwa likisusua kwa muda mrefu sasa. Imefikia wakati sasa Shirika hili livunjwe kabisa na watafutwe wazawa wa kuliendesha. Uzoefu umeonyesha kwamba wawekezaji wageni wameshindwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye matumaini hasa kwa Tanga, Mungu ajalie ifanikiwe kutekelezeka. Kwani sasa hivi tunachojali ni maendeleo kwa wananchi bila kuangalia itikadi zao.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe mchango wangu:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina tatizo kubwa la mawasiliano ya ardhini kwa maana ya usafiri na usafirishaji. Mtandao wa reli uliopo mbali ya kwamba ni chakavu, pia hauko kimkakati, pamoja na tuhuma za uongozi mbaya unaosimamia mamlaka za reli zilizoko nchini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina njia kuu za reli tatu. Kuna Reli ya Kati inayoanzia Dar es Salaam hadi Kigoma na ambayo ina tawi linaloanzia Tabora hadi Mwanza. Kuna reli ya Tanga inayoanzia Tanga hadi Moshi na Arusha na pia kuna na matawi, moja linaloanzia Korogwe hadi Dar es Salaam na lingine linaloanzia Kahe (Mkoani Kilimanjaro) hadi Taveta mpakani mwa Kenya na Tanzania. Reli ya tatu ni ile ya *TAZARA* inayoanzia Dar es Salaam hadi Tunduma mpakani mwa Tanzania na Zambia.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa katika sekta ya reli kwa kweli rushwa, ubadhirifu na kutojali ndani ya Serikali vimetoa mchango mkubwa katika kusababisha hali mbaya katika sekta hii ya ardhini ambayo tunaishuhudia hivi sasa. Hali hii tuliyonayo sasa hivi ni kufa kwa kilimo cha kibiashara katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Aidha, kutokuwa na nia thabiti ya kupanua fursa za kibiashara na nchi ya Uganda kumeididimiza kabisa reli ya Tanga. Sasa hivi kuna matumaini makubwa kuwa kwa kipindi hiki ambapo Waziri yupo ndani ya Wizara hii na hotuba hii nzuri iliyopanga mikakati mizuri Tanga itafufuka.

Mheshimiwa Spika, uzembe wa kutoikarabati kikamilifu Reli ya Kati baada ya mvua za El-nino za 1998 umesababisha reli kusimama kutoa huduma kwa kipindi kirefu toka mwaka 2010 baada ya mvua kubwa iliyopiga katika Wilaya ya kilosa. Aidha, ubinafsishaji usio makini wa uendeshaji wa Shirika la Reli umeliongezea matatizo na kudidimiza ufanisi wa Shirika hilo na kuathiri kwa klasi kikubwa juhudzi za wananchi za kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye bandari kwani inanihu sana. Ni nchi chache duniani zenye jiografia nzuri kama Tanzania lakini haziko katika matumizi ya jiografia hiyo. Tanzania ina ufukwe wa bahari upatao kilometra 1,424 na ndani yake kuna bandari za Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Zanzibar kwa upande wa Mashariki. Upande wa Kaskazini, Kaskazini Magharibi, Magharibi na Kusini Magharibi inapakanwa na Mataifa ya Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Zambia na Malawi. Haya yote ni mataifa ambayo hayakujaliwa milango ya bahari, hivyo ni tegemezi kwa mataifa ya jirani ya Tanzania na Msumbiji kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, huduma mbovu bandarini na mtandao mbovu wa njia za reli na barabara ni mambo ambayo yamesababisha nchi jirani zisizo na bandari kutopendelea

kuendelea kutumia bandari zetu kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano Malawi na Zambia ziko karibu zaidi na bandari ya Mtwara kuliko zilivyo karibu na bandari ya Dar es Salaam, hata hivyo zinapoamua kusafirisha bidhaa zake kuititia Tanzania inalazimika kutumia bandari ya Dar es Salaam kwa sababu mawasiliano ya barabara na reli ni rahisi zaidi. Hali kadhalika Uganda iko karibu zaidi na bandari ya Tanga kuliko ilivyo karibu na bandari ya Dar es Salaam, lakini ni rahisi zaidi kuitishia bidhaa zake Dar es Salaam kutokana na reli ya Tanga kufa.

Mheshimiwa Spika, najua mikakati ya Mheshimiwa Waziri ni mizuri sana na inaigusa Tanga kwa kiasi kikubwa, naomba kwa heshima na taadhima, Tanga ipewe kipaumbele, tuenze na Tanga ujenzi wa Bandari na ufufuaji wa reli, ni muhimu sana kwa wakazi wa Mkoa wa Tanga, itaongeza pato la wakazi, Mkoa na Taifa kwa ujumla.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake lakini napenda kuchangia katika usafiri wa anga, usafiri wa baharini na usafiri wa reli.

Mheshimiwa Spika, maendeleo katika nchi yoyote duniani yanategemea sana usafiri. Usafiri ndio unaoingiza wafanyabiashara, watalii na bidhaa za ndani na nje. Maeneo haya bado Serikali haijatoa kipaumbele na hivyo kukosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa anga. Tanzania katika miaka mingi sana imekosa mapato kwa kukosa ndege za usafiri, tunashindwa hata na nchi maskini sana kama Ethiopia. Napenda Mheshimiwa Waziri aangalie vyema kabisa muundo wa kampuni ya ATC ili kuboreshwa zaidi na kuweza kusaidia Taifa. Hii nii aibu kubwa sana kwa Serikali yetu kutokuwa na ndege hata moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa baharini, kwa kweli hauendi sambamba na mahitaji ya Watanzania na hivyo kuzorotesha maendeleo ya Taifa letu. Kama Serikali inajikita zaidi kununua meli za usafiri, basi fedha nyangi zingepatikana la muhimu sasa ni kubuni njia nzuri za kuondoa usumbufu.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya usafiri baharini haviko katika viwango, ni vibovu na hivyo kusababisha ajali kwa raia wa Tanzania. Meli zinakaguliwa lakini wanavipasisha bila ya viwango kwa mfano Meli ya *Flying Horse*, meli hii ni chafu, mbovu na haifai kuchukua abiria, ni vyema kabisa SUMATRA wafanye kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu reli, ni usafiri muhimu katika Taifa lolote duniani. Reli inarahisisha kusafirisha mazao na mizigo mbalimbali na kurahisisha upatikanaji wa maendeleo Tanzania. Tafadhalii namwomba Waziri aangailie mambo haya matatu na ayaboreshe ili kuliingizia Taifa mapato. Mambo yenye ni kama nilivoyataja usafiri wa reli, usafiri wa anga na usafiri wa majini. Kama haya yatapewa kipaumbele, uchumi wa Tanzania utakua kwa kasi.

MHE. DKT. SEIF SELEMAN RASHID: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu, mwungi wa rehema katika baraka zake na kupata fursa ya kuchangia leo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri yenye lengo la kuongeza kasi ya usafirishaji wa bidhaa na watu kwa wingi zaidi na ikiwezekana uwe wa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya usafiri ndani ya Jiji la Dar es Salaam ni kubwa mno na wakati umefika kwa Serikali kufikiria njia mpya ya usafiri ili kupunguza msongamano kwa kuanzisha usafiri wa mabasi ya juu yanayopita kwenye kamba/waya yaani (*cable trans system*). Naamini usafiri huu utakuwa ni ukombozi kwa Jiji la Dar es Salaam kwa kuanzisha njia za (*cable trans*) katika njia kuu kuingia na kutoka katika Jiji. Bila ya shaka yoyote ni vyema kuanza kufanya kisichowezekana ili kuthibitisha uwezo wa kimaendeleo katika karne ya 21. Kama Chile waliweza kujenga *underground highway* zenye urefu wa zaidi ya km 20, naamini sisi tutaweza kuwa kutumia nguvu zetu za kifedha na nguvukazi kwa kushirikisha Jeshi letu, kikosi cha Nyumbu na bila ya shaka kupata ufadhili na mikopo kutoka ndani na wadau wa maendeleo, mradi huu utakaobadili sura ya Jiji letu utawezekana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuanza kufanya vitu vya kisasa zaidi kwa kuanza kujenga reli mpya yenye uwezo wa kubeba mizigo na abiria wengi kwa muda mfupi zaidi. Huu ni wakati wa kuanza kufanya vitu tofauti na utaratibu uliopo wa kusubiri wageni na kuthamini wawekezaji uchwara ambao nguvu kazi hutumia Watanzania. Ni lazima tukubali mwelekeo wa utendaji kazi ili sisi wenyewe tuthubutu kufanya vyetu wenyewe na tuamini kwamba tunawenza. Tununue vitendea kazi, tukabidhi kikosi cha Jeshi ili kwa nidhamu yake, uwezo wa kitaalamu wa Jeshi letu ambao waliweza kukarabati Reli ya Kati pale Kilosa kwa kasi kubwa sana, inawezekana tuenze kufanya yetu sisi wenyewe. Nashauri Jeshi letu liunde kikosi cha kiufundi na nguvukazi ili iwe rasmi kwa kazi zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, utawala wa chombo hiki cha reli utazamwe upya ili baada ya uboreshaji huu ni muhimu kama utaendeshwa kwa ubia na Watanzania wengi zaidi ili faida ya maendeleo hayo ubakie nchini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuongeza nguvu zake ili kuona ATC inafanya kazi kwa maslahi ya Watanzania. Wakati umefika wa kufukuza kazi wote wasiozalisha ili mizigo ya watendaji wabovu ndani ya Serikali sasa ipungue kwa haraka na bila ya huruma au mapenzi ya kubebana kusiko na tija. Naamini Watanzania tutaweza kwa vile tuliweza sana kwa ujenzi wa mambo mengi ya kustahili sifa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Tulipoletewa Bajeti hii kuipitisha tulipata wakati mgumu sana, hasa kutokana na mwelekeo wa Bajeti kwa Wizara hii. Kwa kweli pesa hazitoshi kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina majukumu makubwa sana sababu kubwa ni kwamba mashirika yote yaliyopo chini ya Wizara hii yapo hoi, yana migogoro mikubwa sana. Ninaomba nipatiwe ufumbuzi wa kutatuliwa kwa haya mashirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Ndege Tanzania (ATC) nasikia uchungu sana ninapoona nchi ndogo kama Rwanda sasa wana ndege tano za nchi yao. Sisi Tanzania tuna ndege moja tu ni aibu, aibu kwa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili linalokabiliwa na changamoto kubwa sana ikiwemo madeni makubwa yakiwemo mishahara ya wafanyakazi na stahili mbalimbali pia matengenezo ya ndege zetu ukisoma ukurasa wa 10 utaona mionganoni mwa wadai hawa ni *Celtic Capital Corporation* na kampuni ya Ndege ya Afrika Kusini. Tayari Mahakama imeamuliwa kukamata mali za ATCL. Aibu hii tutaiweka wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atakapokuwa anajibu hoja mbalimbali za Wabunge ningemba na mimi nipatiwe majibu ya maswli yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, kuna ndege ya Boeing iliyopata ajali katika kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Je, Serikali ina mpango wowote wa kuifanya matengenezo au ndio imetelekezwa na je, uchunguzi wa ajali ile ulibainisha chanzo ni nini?

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kujua kuwa inasemekana kuwa kuna taarifa kuwa ofisi ya mwakilishi wa Tanzania kwenye Shirika la Usafiri Tanzania kwenye Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) kule Mentareal imetungwa je, maslahi ya Tanzania yatalindwa na nani? Ikiwa Mheshimiwa Waziri ulikuwa huko huoni kwamba sasa ulikuwa muda muafaka wa kuimarisha ofisi hiyo badala ya kuifunga?

Mheshimiwa Spika, je, nini mkakati wa Serikali wa kuhamasisha wadau mbalimbali kuchangia mfuko wa mafunzo ili kupunguza uhaba wa wataalamu wa sekta ya usafiri wa anga?

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanja nya ndege, ukisoma katika ukurasa wa 17 katika kitabu cha hotuba ya Waziri utakuta miradi ya ujenzi wa viwanja nya ndege. Nimejaribu kuangalia Bajeti ya viwanja hivyo ni ndogo sana nafikiri ndio sababu ya kususua kwa matengenezo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini ningeomba kujua hatima ya kiwanja cha ndege cha Nduli Iringa na Njombe kwa kuwa kutokamiliwa kwa viwanja hivyo kuna sababisha Mkoa wa Iringa kukosa mapato ya pesa za kigeni kwa sababu tuna hifadhi ya mbuga za wanyama ambayo ilituwezesha kutembelewa na watalii kutategemea sana na ukamilifu wa viwanja hivyo tunaiomba Serikali itoe majibu kwa hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchukua fursa hii kuishauri Serikali juu ya ujazaji wa meli ya Mv. Liemba na Muongozo, meli hizi zimechoka lakini zinapakia watu na mizigo mingi hali ambayo ni hatarishi, naiomba Serikali ichukue hatua madhubuti ya kuinusuru hali hii.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni reli, mchakato wa reli ni mgumu sana. Kwanza kabisa treni ina usumbu mkubwa. Moja stesheni ya Kigoma mwaka 1963 lipewe zawadi ya usafi kama *the best kept station* lakini *station* hii kwa sasa hali yake ni mbaya, majani mpaka shingoni, maji yamechanganyika na udongo kuna tope baya hali ambayo ni sifa mbaya kwa nchi kama Tanzania yenye tatriban miaka 50 ya Uhuru!

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni mchakato wa kupata tiketi, wenzetu wa Dar es Salaam wanapata tiketi mwezi mmoja au wiki mbili mpaka moja kabla ya safari lakini kwa kinyume watu wanapata taabu, wanakata tiketi siku ya safari hali ambayo inapelekea wananchi wadamke saa kumi za usiku ili wapange foleni na wakati mwingine wanakosa kabisa hata hizo tiketi pamoja na kupanga foleni lakini cha kusikitisha zaidi ni kwamba zinakuwa zinapatikana kwa bei ya kuruka. Je, Serikali ni lini itarudisha hali ya zamani ili wananchi waweze kukata tiketi siku mbili au tatu kabla?

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu mende na panya kwenye chombo cha usafiri, hili nalo limekuwa tatizo sugu na ni aibu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni kuchanganya mizigo na watu kwa nini kusiwe na utaratibu wa mizigo kukaa sehemu yake na abiria sehemu yake lakini mizigo inajaa mpaka rohoni hakuna hata pakupita. Je, Mheshimiwa Waziri unatoa kauli gani juu ya mizigo hiyo mingi inayofanywa abiria washindwe kupita, Mheshimiwa Waziri tunaomba utoe kauli juu ya kero hii kama kweli Serikali yako ni sikiu la sivyo nakamata shilingi kwenye mshahara wako!

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha!

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Uchukuzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi ni Wizara mama katika uchumi wa Taifa letu. Hatuwezi kusema tunaweza kuendelea kiuchumi wakati miundombinu kama reli, bandari na anga haviko vizuri.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ione umuhimu wa pekee wa watoto mapacha wa barabara ambazo zimefikia katika hatua nzuri katika Wizara ya Miundombinu kwa kuwa pacha wa barabara ni pamoja na reli, anga na bandari, na hivi vyote kwa pamoja vikue katika hali nzuri nchi yetu itaweza kufanya vizuri zirudi katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, eneo la usafirishaji wa meli, pamoja na kwamba barabara tumefikia kiwango kizuri hususan barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mtwara ukiachilia mbali kipande kilichobaki cha kilomita 60 cha Ndunu – Somanga lakini upo umuhimu mkubwa kwa Serikali kufufua usafiri wa meli uliokuwa unafanywa huko nyuma kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara,

meli ni mkombozi kwa wananchi wa Mtwara, bei zake zipo juu sana, mara mbili ya bei ya bidhaa husika pahala pengine, hii inawaumiza sana wananchi wa Mtwara na hivyo kuwafanya waendelee kuwa nyuma kimaendeleo, ni vema Serikali ikatafuta namna ya kama siyo kuwa na meli ya Serikali kwa kuwa tumeshindwa basi kutafuta wabia amba wakileta meli itasaidia usafiri wa kawaida kwa wananchi na pia usafirishaji wa mizigo kibashara itakuwa kwa urahisi kwa mizigo mikubwa hasa vifaa vya ujenzi, batu, saruji, misumari, *gypsum* na kadhalika, hivi vikisafirishwa kwa meli ni dhahiri kuwa bei zake zitapungua kuliko ilivyo sasa ambapo wafanyabiashara wanasafirisha bidaa zao kwa malori.

Mheshimiwa Spika, eneo la reli, kwa miongo kadhaa tumeshuhudia usafiri wa reli umekuwa kero kubwa sana, si jambo jema sana kuona upande mwengine wa Tanzania hauna tatizo kabisa la usafiri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wana barabara safi na nzuri wakati upande mwengine kama mikoa ya Kanda ya Kati hadi Kigoma hawana kabisa usafiri wa kuaminika, ni Watanzania wenzetu ni vizuri wakapatiwa huduma ya usafiri ya uhakika kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, reli nayo ikiimashwa uchumi wa nchi yetu pia utakuwa umeimarika. Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akifunga Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi, alisitisita sana ufunjaji wa nyuki na uvunaji wa asali kama chanzo kimojawapo cha mapato kitakachowezwa kuwainua wananchi, najiuliza kama endapo wananchi wa Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga na Kigoma wakiweza kuvuna mapipa ya asali watasafirisha kwa mabasi? Hapana, reli iwe kipaumbele kwa mikoa hiyo ili mazao yao yote yaweze kusafirishwa kwa urahisi.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuongeza Bajeti shilingi bilioni 95 ili zisaidae ujenzi wa Reli, *ATCL*, Bandari na Meli.

Naomba nichangie maeneo yafuatayo, kwanza tufufue reli za zamani kuchochea kasi ya ukuaji wa kiuchumi, reli za Dar es Salaam – Tabora – Mwanza, Dar es Salaam – Tabora – Kigoma, Dar es Salaam – Tabora – Mpanda na reli za Dar es Salaam – Tanga, Dar es Salaam Korogwe – Moshi. Reli hizi zitasaidia usafirishaji wa mazao ya kiuchumi utapunguza gharama za bidhaa kwa usafirishaji kwa njia ya reli ni nafuu kuliko barabara. Pia usafiri wa abiria, kukarabatiwa kwa reli hizi kutasaidia kumpunguzia ukali wa nauzi za mabasi na ndege.

Mheshimiwa Spika, *ATCL*, Shirika hili linunuliwe ndege lakini ieleweweke tatizo kubwa katika shirika hili ni la kimenejimenti. Tutafute watu wenyewe uzoefu na mambo ya usafiri wa ndege. Tujuulize inakuaje *Precision Air* inafanya vizuri wakati *ATCL* inashindwa kukiendesha?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO: Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa nzuri ya Bajeti ya Wizara hii, napendekeza mambo yafuatayo yafanyiwe kazi:-

Mheshimiwa Spika, kuendeleza juhudzi za kuimashwa reli. Kuimashwa reli kutasaidia mambo mengi yakiwemo ya kuwasafirisha wananchi wengi zaidi, kusafirisha mizigo mingi ambayo kwa kiasi kikubwa kinatoka bandarini Dar es Salaam. Hili litasaidia kupunguza foleni iliyoko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Reli za *TAZARA* na za Kati na Tanga zikiimashwa zitasaidia sana suala la kuwasafirisha wananchi na mizigo toka Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuimashwa *ATC* na viwanja vya ndege, juhudzi zaidi zifanyike katika kuimashwa maeneo hayo. Huduma ya ndege ni muhimu sana hasa kwa Mkoa wa Kigoma amba unapakana na nchi jirani za *DRC* na Burundi ambazo zinautegemea sana Mkoa wa Kigoma katika kuingiza bidhaa mbalimbali kwa matumizi yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa bandari ya nchi kavu (*Inland Dry Port*) katika mji wa Chalinze. Naomba sana ujenzi wa eneo hilo ufanyike mapema kwani kwa kufanya hilo kutasaidia sana kupunguza foleni mjini Dar es Salaam hasa kwa mizigo iendayo Bara na Tanga.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongozi. Kuhusu suala la utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam ni kupindi kirefu kumekuwa na malalamiko kwa wananchi wanaopita bandarini hasa kutokea Zanzibar kulipishwa kodi ya *wharfage* kwa mizigo ya mikononi pesa nydingi tu, hivyo hilo ni tatizo la kodi, ninaamini mizigo inayopaswa kutozwa kodi ile mizigo mikubwa na mingi. Hivyo naishauri Wizara kupitia *TPA* kulisimamia suala hili na kulirekebisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uwanja wa ndege ni muda mrefu eneo la kusafiria abiria limekuwa halina *air condition* na kusababisha joto kwa abiria na tatizo hilo lipo kwa muda wa miaka mingi tu. Hivyo naishauri Wizara ilishughulikie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la UDA, inavyoonekana uingiaji wa mkataba wa ubia katika kulikodisha Shirika hili lilikuwa lina mizengwe kuanzia ngazi ya Bodi na *management*, naishauri Serikali kulishughulikia suala hili kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya usafiri, ninavyoelewa huduma ya usafiri inategemeana sana hapa nchini, kwa huduma ya usafiri wa reli, usafiri wa anga na usafiri wa barabarani, aidha, katika utoaji wa huduma ni lazima kila sekta itegemeane na mwenzewi katika kutoa huduma na kuongeza Pato la Taifa. Hivyo inavyoonekana kuna matatizo katika sekta hiyo, je, ni kwa nini Serikali haianzishi mfuko wa pamoja wa *Railways Infrastructure Fund* ambao utawezesha kusaidia matengenezo ya njia za reli, matengenezo ya mabehewa, mawasiliano na kadhalika, aidha, naamini ukianzishwa mfuko huu huduma ya usafiri itaboreka sana hasa kwa utoaji huduma kwa wananchi kwa uhakika pamoja na mapato kwa watu. Hivyo naishauri Serikali kuanzisha mfuko huu hasa kwa kuwa suala hili mchakato wa ripoti ulianzishwa hapo awali na Shirika hodhi la *RAHCO*.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Hali ya Hewa, ninakumbuka wakati Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alipofanya ziara ya kikazi katika Wizara ya Uchukuzi, alipokea taarifa ya kukosekana kwa rada kubwa mbili ambazo zikipatikana Mamlaka ya Hali ya Hewa itaweza kupokea na kutoa taarifa kwa wakati wa namna ya mabadiliko ya hali ya hewa. Sasa je, Wizara imeweza kununua rada hizo na kama imenunua imezfunga wapi na lini zimeanza kazi?

Mheshimiwa Spika, madereva na makondakta wa mabasi pamoja na daladala, imekuwa ni kero hapa Tanzania kwa madereva wa vyombo hivyo ambao wanakuwa hawana vazi rasmi la udereva na muda mwengine vivazi vyao vinakuwa vichafu na viraka kuleta karaha kwa abiria. Hivyo naishauri Wizara kuwataka madereva, makondakta kuvala sare rasmi kwa gharama zao na kwa wale ambao watabainika kutotii amri hiyo atozwe faini, pamoja na kusimamishwa kuendesha gari.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote chini ya Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, uchukuzi ni sekta muhimu sana katika maendeleo ya nchi kwa sababu baada ya kulima na kuvuna mtu anapaswa apeleke bidhaa kwenye soko. Uchukuzi waweza kubeba mizigo mkubwa ni reli lakini vilevile reli ni kimbilio la wengi kwa uchukuzi na usafiri. Reli yetu imechoka na mabehewa halikadhalika. Uwekezaji haukizingatia umuhimu wa kuwa na wataalam wetu ndani ya *management* wenye uwezo wa kupinga au kutoa maamuzi. Tuna wataalam wengi sana wenye uwezo mzuri, tatizo la reli lilikuwa ni miundombinu iliyochoakaa.

Mimi nimekulia kwenye reli kwani baba yangu alikuwa mfanyakazi wa reli aliyefikia ngazi ya Meneja ya Kanda kwa hiyo nimeona reli ikiwa katika hali nzuri na ilivyoanza kusuasua. Nidhamu ya kazi ilitoweka na Serikali ilipuuza ushauri ilitolewa, wale walikuwa wafanyakazi wa *East Africa Community* walishindwa kufanyakazi katika mazingira yasiyo na nidhamu na yaliyojaa ubadhilifu.

Mheshimiwa Spika, naamini bado Watanzania wenyewe uwezo mkubwa sana na ninavyoona watapewa ushirikiano na Serikali kwa hali na mali naamini wanaweza kuendesha Shirika hilo. Serikali ijaribu hilo.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote yenyewe maendeleo inahitaji usafiri wa ndege ili kupunguza muda wa safari na kuokoa muda unaoweza kutumika kwa shughuli za ujenzi wa Taifa badala ya kutumia saa sita unaweza kutumia saa tatu, kwa nini Serikali isichukue mkakati wa kulifufua shirika hilo, mimi naamini pamoja na matatizo mengi hasa ya mtaji mdogo pia kuna hujuma kwa maslahi ya watu binafsi. Matatizo mengine ni Serikali kukabidhi watumishi/viongozi ambaao siyo waadilifu ambaao baada ya kuharibu mahali pamoja wanahamishwa pengine, hili linachangia kwa kiwango kikubwa kushindwa kwa shirika hilo, wafanyakazi wamekuwa wanalamika kwa muda mrefu bila kusikilizwa. Kampuni ya *Precision* au *Kenya Airways* ni wazawa hao hao waliweza kuendesha, hivyo ni lazima Serikali iangalile siyo tu mtu wa nje ni nani anakuja bali hata wa ndani chini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la UDA ni aibu kubwa na ni kengele ya kuiamsha Serikali, hatujui ni wapi tena wizi wa kikubwa kama huu umetokea. Mimi nikiwa mmoja wa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam tumeangalia nyaraka zote ambazo tumezipata bila kujali itikadi za vyama tumeshtushwa na jinsi hali ya rushwa na ubadhilifu iliyokithiri kuweza kuagiza fedha za Shirika kulipwa kwenye akaunti yake binafsi, lakini vilevile kuweza kuza Kampuni/Shirika bila woga wowote. Lakini hili limetokea toka mwaka 2009, tulikuwa wapi hadi 2011? Lakini ni viyi watu watatu waliweza kuitisha maamuzi ya kukabidhi kampuni bila kuitisha kwenye Kamati ya Uongozi wa Jiji wala Kamati ya Madiwani ya Jiji?

Mheshimiwa Spika, dalili zote zinaonyesha kwamba kuna uwezekano mkubwa wa rushwa iliyopita na ni lazima tujulize kila hatua ilipita bila rushwa.

Mheshimiwa Spika, mali za UDA zipo hatarini kutoweka, mimi ningeomba cha kwanza kabisa kuweka amri pingamizi ili mali yoyote ya UDA isiweze kuuzwa au kubadilishwa umiliki. Wote waliohusika Serikali ichukue hatu za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwashitaki za kurejesha mali zote za UDA kwenye kampuni na kuwalipisha wote waliohusika warejeshe mali za kampuni.

Mheshimiwa Spika, tulibaini pia kuna nyaraka nyingi ikiwa pamoja na *MEMARTS* zimebalishwa, naomba hili Serikali liliangalie.

Mheshimiwa Spika, lakini pia mali nyingi za Jiji ikiwemo *DDC* Kariakoo na sehemu nyingi zipo kwenye ujisadi mkubwa tuchunguze.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi juu ya ucheleweshwaji wa makusudi katika kupakua makontena pindi meli zinapofika bandarini.

Mheshimiwa Spika, imedaiwa kuwa baadhi ya watumishi wa bandari wamekuwa wakipokea rushwa na kuchupisha meli bila kufuata foleni kwa meli zilizowahi kutia nanga, kwamba meli inayopelekwa mbele, imekuwa ikitoa rushwa kwa dola laki moja na kupakuliwa makontena kwa haraka na meli ambazo hazina fedha hizo ya hongo hucheleweshwa kupakuliwa kontena hata kama zitawahi kufika bandari.

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ikiwaumiza wafanyabiashara hasa wazawa kwa kuendelea kulipa gharama ya dola 70 kwa siku kwa kontena zao zinakaa muda mrefu kwenye meli bila kupakuliwa hivyo gharama zote wanabeba wenye makontena.

Mheshimiwa Spika, hali hii pia imeanza kuwa kero hata kwa wenye meli ambao hawana uwezo wa kuhonga dola laki moja ili meli zao zichupishwe na kuwahi kupakua makontena na wengi wameanza kukimbilia Bandari ya Dar es Salaam na kukimbilia Bandari za jirani ili kukwepa adha hiyo.

Mheshimiwa Spika, kitendo hicho kitafanya bandari yetu kukosa mapato, kwa watu kuanza kukimbiza meli zao na kwenda kutia nanga na kushusha mizigo kwenye bandari zingine.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hasa baada ya maelezo ya kina yaliyotolewa na Waziri Mkuu kutoa kauli ya kuongeza kwenye Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi shilingi bilioni 95, fedha hizo ambazo zimegawanywa katika huduma ya reli, ndege na meli. Naishukuru sana Serikali kwa usikivu huo, nashauri sasa fedha hiyo isimamiwe vizuri na mgawanyo huu uendane na utekelezaji wa dhati.

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza uletwaji wa ndege *Airbus A320* iliyopo Ufaransa tangu Julai, 2009 inayodaiwa dola milioni 3.0 jie haraka, pia ndege *Dash 8 - Q 300* iliyopelekwa *South Africa* kwa ajili ya matengenezo ambapo tunaambiwa imekamilika *ATCL* inatakiwa kulipa dola za Kimarekani 700,000, ni vizuri pesa hizo zikatumika kwa pamoja na kulipa dola za Kimarekani 24.72 ambazo ni za gharama ya matengenezo na tozo, pia ili kuimarishe *ATCL* iipeleke ndege yake ya tatu kwenye matengenezo *Dash 8 Q 300*.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto nyingi zinazoihusu *ATCL*, Serikali na *ATCL* izisimamie na izitafutie ufumbuzi ili mwakani tukija hapa yake yaliyoombwa na Wabunge yaonekane na yapate ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uwanja wa Ndege Mwanza, Serikali ilishatoa ahadi ya kupanua kiwanja hicho naomba Serikali inihakikishie kwa dhati ni lini kiwanja hicho kitaanza ujenzi wa kupanuliwa, imetengewa shilingi ngapi na kandarasi ni nani? Hii ni kutokana na ahadi za mara kwa mara ambazo tumekuwa tukizisikia humu ndani leo nataka kujua hayo.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni yangu kuhusu hotuba ya Waziri ya Uchukuzi, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu aliyoiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ipasavyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imeomba Bunge Tukufu la Tanzania, liidhinishe jumla ya shilingi 237,563,802,000; kati ya fedha hizo shilingi 69,585,672,000 ni kwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 167,978,130,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi 95,000,000,000 za ndani wakati fedha za nje ambazo sio za kutumainia sana kwani inawezekana zisipatikane ni shilingi 72,978,130,000.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha fedha ni kidogo sana na hakitoshi kabisa kufufua Shirika letu la Ndege la *ATC*, Shirika la Reli ambalo kwa hivi sasa linahitajika sana kusafirisha abiria pamoja na mizigo kwa gharama nafuu. Pia hazitoshi kabisa kuboresha usafiri wa majini ambao unadorora.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ambayo ni mpya iliundwa mwaka jana tu mwezi Novemba, 2010, inahitaji kupata kipaumbele kwa kutengewa kiasi cha fedha za kutosha. Serikali iwe na nia thabit ya kufufua Shirika la *ATC* na Reli. Huu ni mradi unaohitaji shilingi bilioni za fedha na watendaji walio makini, wawajibike kwa hali ya juu ambao kwa vyovoyote hawawezi kufanya ubadhifuru wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kiwango hicho cha fedha hakiwezi kwa hali yoyote kufanikisha maendeleo ya Wizara hii ya Uchukuzi, ili kuondoa adha za usafiri ambazo wananchi wanazipata wanapotaka kusafiri.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi 182 wa *ATC* wanaoendelea kulipwa na Shirika la *ATC*, Serikali inakiuka usemi usemao kwamba Asiyefanya kazi na asile! Inakuwaje mtu apate mshahara bila ya kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, endapo taaluma zao zinahitajika sana basi ni vema wafanyakazi hao wakahamishiwa katika Wizara nyingine hii ni kama Serikali naona kwamba wanataaluma hao huenda wakahamia katika nchi za jirani na hivyo Serikali kuwapoteza. Nashauri wapewe haki zao na wabakie wachache sana katika kulifufua Shirika.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nawakilisha hoja na siungi mkono.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana na kushangaza kwa kiasi kikubwa ikiwa watu wazima na wenyewe akili timamu wamekaa kwa muda mrefu kupanga Bajeti ambayo wanajua kuwa haiwezi kukidhi hata robo ya mahitaji ya Wizara wanayoisimamia. Hii inaonesha dhahiri kuwa hakuna *seriousness* katika utendaji wa kazi. Pia suala la kuwajibika halipo katika jamii yetu. Kwa msingi huu siungi mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya kushangaza sana katika nchi hii ambayo yanatia aibu sana Serikali yetu. Mambo haya yanaweza kuwa kikwazo cha maendeleo toka karne hii ya 21 hadi karne na karne iwapo tutaendelea kuyalea! Suala la utapeli wa viongozi wa Mashirika ya Umma ni kikwazo kikubwa cha maendeleo katika nchi hii. Suala la ubinasi, uchoyo, tamaa na roho mbaya katika nchi hii ndilo limeua Mashirika yetu ya Umma! Fikiria *ATCL & RTC* yamekuwa kwa sababu ya tamaa ya viongozi wetu! Huu ni unafiki na usaliti. Kamwe vitu hivi kwa kiasi kikubwa haviwezi kuvumiliwa! Katika kuchangia hoja hii napenda kuiuliza Wizara husika maswali yafuatayo:-

Kwa nini Shirika hili limekuwa?, je, walioliua hili wamechukuliwa hatua gani? Je, kuna mwelekeo wa kuanzisha shirika lingine badala ya UDA? Ni sababu zipi zilizopelekea Shirika letu lisikue ingawa lilianzishwa wakati ambao haukuwepo ushindani wa kibashara? Serikali inatoa kauli gani ya uhakika kwa Watanzania juu ya reli zetu zilizojengwa na Mwalimu J. K. Nyerere? Je, usafiri wa gari moshi utaanza lini hapa nchini kuelekea mikoa ambayo inapitiwa na reli hizo? Je, Waziri haoni kuwa kuzitelekeza reli hizo ni kusaliti juhudhi za Watanzania ambao walijitoa mhanga kujinga reli yao? Je, Waziri hana mbinu yoyote mpya katika Wizara husika?

Je, kwa nini bandari zetu zinaendeshwa kwa hasara? Je, ni sababu zipi zilizopelekea watu binasi hususan wahindi wapewe kibali cha kuhifadhi makontena ya mizigo inayoagizwa nje ya nchi? Ina maana Serikali ilishindwa kabisa kutafuta eneo la kuhifadhi makontena hayo badala ya kuwapatia watu binasi fursa hii? Waziri na watendaji wake hawaoni kuwa huo ni ufinyu wa fikra kuiweka mizigo ya wafanyabiashara mikononi mwa wahindi? Ni sababu zipi zinazopelekea makontena yanayohifadhiwa na wahindi yanaliipiwa gharama kubwa ukilinganisha na yale yanayohifadhiwa bandarini? Kuna fikra hapa?

Je, *TPA* inalinufaishaje Taifa la Tanzania? Je, kama shirika hili halililetei Taifa faida kwa nini lisivunjwe kwa manufaa ya umma? Waziri anasema nini juu ya uvujaji wa fedha unaofanywa na *management* ya *TPA*? Ina maana Waziri hajui kuwa *TPA* rushwa imekithiri? Je, bodi ya *TPA* inalitumikia ipasavyo Taifa au inatumikia matumbo yao? *TPA* kwa nini imeshindwa kujiedhesha kibashara? Kwa nini itegemee ruzuku toka Serikalini? Je, kuna fikra hapo?

Je, kituo hiki kinamnufaisha nani? Ina maana Serikali imeshindwa kukiendesha? Je, mwekezaji uchwara wa kituo hiki analipa kodi halali Serikalini? Ipi ni kauli ya uhakika ya Waziri juu ya unyonyaji unaofanywa katika kituo hiki cha mabasi?

Kwa nini *ATCL* imekufa? Kwa nini ndege za *ATCL* haziruki? Kwa nini Waziri asiwajibike juu ya hili? Ni hatua zipi zimechukuliwa za makusudi za kulinusuru Shirika hili? Je, wahuju mu wa Shirika hili wanafahamika? Kama wanafahamika ni hatua zipi wamechukuliwa za kisheria? Ndege mbouvu tatu za *ATCL* zitaanza kuruka lini? *ATCL* itarudisha lini nauji za wateja wake waliokuwa wamechukua tiketi za Dar es Salaam – Mwanza – Dar es Salaam au Dar es Salaam – Kigoma?

Je, viwanja vyetu vya ndege vinajiedhesha kwa faida? Kama ni ndiyo, ni kwa kiasi gani? Kama ni hapana ni kwa nini? Je, Serikali itapanua lini uwanja wa ndege wa Magena Wilayani Tarime ili uwanufaishe watalii wanaotoka Kenya na kuingia Tarime? Je, Serikali itapanua na kujenga lini Uwanja wa Ndege wa Musoma? Upanuzi wa uwanja wa ndege wa J. K. Nyerere utaanza lini na utakamilika lini? Upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza utaanza na kukamilika lini?

Je, TAZARA inajijendesha kwa faida au inajijendesha kwa hasara? Waziri amechukua hatua zipo mahususi za kutatua mgogoro unaoiandama TAZARA? Je, ni kweli kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAZARA lazima atoke Zambia? Kama ndiyo ni kwa nini na Waziri umelionaje suala hilo?

Mheshimiwa Spika, hitimisho, *resign* kwa kiingereza ina maana ya *to be ready to accept or endure, accept as inevitable*. Tafsiri isiyo rasmi ni kuwa tayari kukubali na kustahimili, kukubali kuwa jambo fulani ni lazima liwe, halizulilki.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa kwa ufinyu huu wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, Waziri hawezি kukwepa lawama. Aidha, alilikubali Bajeti kwa uoga. Mwalimu Nyerere anasema nini juu ya uoga, namnukuu; "Kukubali kufanywa vikaragosi vya viongozi ni dallili ya woga, si dalili ya heshima! Na woga na heshima ni vitu viwili mbalimbali. Maadili mema yanatutaka tuwaheshimu viongozi wetu, madhali wanajitahidi kutimiza wajibu wao. Maadili mema hayatudai tuwaogope viongozi wetu. Na viongozi makini hupenda kupata heshima ya wananchi wenzao, lakini hawapendi kuogopwa. Kuogopwa ni sifa na ada ya madikteta, viongozi halisi hawapendi kuishiriki. Kujenga mazoea ya kutii viongozi hata katika mambo haramu ni dallili ya woga, ni kukaribisha udikteta."

Waziri wa Wizara ni muoga. Anaogopa kivuli chake! Namshauri kuwa ikiwa hawezি kuucheza muziki wa ATCL, Bandari, Reli, TAZARA, TPA lakini hasa hasa ATCL, Bandari na Reli ajiuzuru kwa manufaa ya umma! Achukue hatua kali kwa waliohujumu mashirika yote hayo.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze na kusema kwa Wizara hii ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa Taifa, kwa sababu ni Wizara inayosimamia vyombo muhimu vya usafiri ambavyo vingeweza kutumika vyema licha ya wananchi kufaidi sana lakini hata Serikali ingefaidika zaidi katika kupata mapato ya shilingi na fedha za kigeni.

Msheshimiwa Spika, usafiri wa reli ni muhimu sana kwa wananchi wa kipato cha chini haswa walioko pembezoni mwa nchi. Lakini usafiri wa treni umekuwa unadorora siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, jambo hilo hilo limeikumba usafiri wa ndege ambao hadi sasa Serikali ya Tanzania haina ndege hata moja huku wafanyakazi wakiwa ofisini bila kufanyakazi na wakiwa wanalipwa mishahara.

Mheshimiwa Spika, huu ni mzigo mkubwa na aibu kubwa kwa Taifa letu. Naishauri Serikali kutumia njia yoyote ile ili kupata fedha kwa ajili ya kuimarisha usafiri wa reli na anga ili kuipatia Serikali fedha na wananchi wa Tanzania kujivunia kusafiri kwa ndege za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nzungumzie suala la uuzwaji wa Shirika la UDA lenye assets zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 10.9 kwa shilingi bilioni 1.2 .

Mheshimiwa Spika, huu ni utapeli mkubwa na naishauri Serikali kufuatilia jambo hili kwa makini ili kunusuru Shirika la UDA.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, napenda kuanza hotuba hii kwa kutoa mchango wangu moja kwa moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujua endapo Serikali inatambua kuwa kuna reli itokayo Dodoma hadi Singida, kwani naona hotuba hii haijagusa kabisa reli hiyo, wakati usafirishaji kwa njia hiyo ulisimama kwa muda mrefu sasa. Je, Serikali inaelewa ni kiasi gani cha mwanguko wa uchumi umeshuka tangu reli hiyo iache kutumika kwani biashara zote zimesimama zilizokuwa zinapitia kwenye reli hiyo? Naomba nijulishwe kuna utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, naomba nifafanuliwe, Kasma 4207 ni fedha kiasi gani na za nini? Kwani sieliewi kabisa na siamini macho yangu kwamba ni fedha za *Singida Airport*, mimi naamini kabisa kwamba Serikali inataka kwamba Mkoa wa Singida tuna mpango wa kujenga kiwanja kikubwa kwa kushirikiana na wawekezaji toka Dubai ili kurahisisha usafiri wa mizigo ya kwenda nchi jirani kwa kupunguza *route* ya Dar es Salaam (Bandari kavu). Hivyo tunahitaji kuungwa mkono kwa hali na mali toka Serikalini kwani ni kitega uchumi cha Taifa na si Singida peke yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huduma za uchukuzi hutegemeana hakuna namna yoyote ambayo sekta moja yaani bandari, reli au usafiri wa anga inaweza kujitosheleza yenewe katika kuinua uchumi wa nchi isipokuwa kwa umoja wao (*Interlink*). Je, Serikali haioni haja ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Reli (*Railway Infrastructure Fund*) kwa kuzingatia maelekezo ya sheria iliyoanzishwa Kampuni Hodhi ya Rasilimali Reli (*RAHCO*) ya mwaka 2007. Kwani mfuko ungewezesha sekta ya reli kupata fedha kwa ajili ya matengeneza ya njia ya reli, madaraja na mawasiliano na hivyo kuweza kuchangia ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka msongamano wa magari makubwa ambayo huwa ni kero katika Jiji la Dar es Salaam na hata nafasi iliyoko bandarini kuwa ndogo. Je, Serikali haioni kwamba ni vema sasa wakatumia reli kutoa makontena kwenye meli na kuyashusha Kisarawe au Ruvu. Ni magari makubwa yote yaendayo mikoani na nchi jirani wachukulie Kisarawe au Wami? Bali pale bandarini iwe mizigo midogo tu ya Dar es Salaam ama ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, mwisho nitashukuru sana kupata majibu kwa uhakika. Nasikitika kuwa nashindwa kuunga mkono hoja, kwani Singida wamenitura nisiunge hoja kama hakuna jibu la kufufuliwa kwa reli ya Dodoma – Singida, nkipata jibu nitaunga mkono hoja. Najua mna changamoto nydingi, kwanza Bajeti yenu ni ndogo mahitaji mengi sijui itakuwaje. Nawaombea kwa Mungu. Ahsante.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu na pili wananchi wa Jimbo la Babati Vijiini. Napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Babati Vijiini kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimwa Mizengo Kayanda Peter Pinda kwa kazi nzuri wanaofanya kuleta mabadiliko katika nchi yetu kiuchumi. Wengi hawaoni kazi kubwa iliyofanywa na wanabaki kulalamika. Kwa wanaoona miaka mitano ile ya nyuma na leo, kuna mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri Mheshimiwa Omari Nundu na Naibu Waziri Mheshimiwa Athumanji Mfutakamba kwa kuwa na dira (*vision*) ya kubadilisha sekta ya uchukuzi Tanzania. Tatizo kubwa ni ufinyu wa Bajeti. Naomba nitoe ushauri kwa Serikali, Mashirika karibu yote ya umma yanafanya vibaya kwa sababu ya uongozi mbaya ya *management*. Tubadilike na kuweka viongozi na *management* ambayo itafanyakazi kwa uadilifu na walipwe kutokana na faida ya Shirika itayopata. Kama kutakuwa na hasara, ichunguzwe na kama ni hasara inayotokana na masuala yasiokuwa ndani ya uwezo wao (majanga ya Kitaifa, kudorora kwa uchumi duniani na *natural disasters*) lakini kama ni hasara kutokana na gharama kubwa ya uendeshaji na faida ndogo basi wawajibishwe. Kila robo mwaka (*quarter*) ripoti zifike katika ofisi za ukaguzi na umma ujulishwe mapema. Mtumishi na kiongozi akiharibu au kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi sehemu moja asihamishiwe katika shirika lingine au bodi nydinge. Watakaobinika kutumia vibaya madaraka yao wakati wa utumishi na kuleta hasara pia washitakiwe bila huruma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia sehemu ya usafiri wa anga kwanza Serikali iangalie namna ya kuboresha na kurudisha usafiri wa anga (*ATC*). *Management* mpya ipatikane, tupate hata ndege nne za kukodi na pia ndege za shirika zirudishwe ili zifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana na tunashauri kama mashirika binafsi yanaweza kupata faida na kukua hata mashirika ya umma yanaweza. Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, tunashauri uwanja huu sasa usibinafsishwe, uwe chini ya *management* makini na ya kitaalam. Ni aibu ndege zinazotumia uwanja huo ni chache na kilometra chache, Nairobi – *Jomo Kenyatta International Airport* ni ajabu kuona ndege nydingi zinatumia uwanja huo, Watanzania wanaoishi Kanda ya Kaskazini husafiri nchi za nje kutoka Nairobi. Mizigo mingi ya mazao ya maua, matunda, mboga zinapitia Nairobi. Huduma nydinge muhimu *KIA*

zimedorora, *cafteria* ni ghali na hakuna huduma nzuri, pale pale nje vibanda vinatoa huduma nzuri na rahisi zaidi. Tutafute mtaalam atushauri namna ya kuboresha uwanja huo wa Kimataifa ili tuongeze kipato cha uwanja.

Mheshimiwa Spika, Serikali na pia adha ya usafirishaji mazao yetu na pia utalii Kanda ya Kaskazini ukue. Watalii wengi sasa wanatumia Nairobi na Mombasa, Tanzania ingefaidi hata siku moja mtalii anapofika na kulala Nairobi au Mombasa ni hasara yetu. Tunaomba mjaribu Watanzania wanaweza. Pia tunaomba na kuishauri Serikali iangalie kwa huruma wananchi wa Babati Vijijini na Mjini kwa kuikarabati *Air Strip* ya *Mamire*, ni *Airstrip* pekee jirani na Makao Makuu ya Mkoa, ilikuwa inatumika kwa utalii, ndege za kupiga dawa ya mashabani na muhimu kuliko yote kutumika kama *Rescue Strip* kwa *flying doctors*. Huweza kuokoa maisha ya wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, mwisho ndiyo itakayokuwa hatua ya mwanzo kupata uwanja wa uharaka Mkoani Manyara. Kwa upande wa usafiri wa magari ya abiria, tunashauri Wizara ijithadi kutoa maelekezo kwa *SUMATRA* na vyombo vingine kufuata sheria. Gari ya abiria 35 hupakia abiria 60 hadi 70 na ya 60 inapakia hadi abiria 90. Mbali na mizigo kujazwa ndani ya maeneo ya abiria ajali nydingi hutokana na *overload* na hata gari ndogo za Noah hupakia abiria hadi kwenye buti. Pia magari ya mizigo (*hu-overload*), hupakia kupita uwezo wake. Utaona fuso kupakia hadi tani 12 magari ya mnadani hupakia abiria na mizigo na ndipo wananchi kupoteza maisha pindi ajali inapotokea. Pia katika sekta hiyo hiyo bado mizigo inapakiwa kwa rumbesa au gunia yenye vilemba. Sheria ipo lakini haifuatwi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sheria, *SUMATRA* na *traffic police* husumbua sana magari ya binafsi yenye namba za mfano ambayo yana uwezo wa kubeba watu saba au zaidi (*saloon, station wagon, suv's*) wanadai yakatiwe leseni ya *SUMATRA* na kufanya hivyo pia lazima ulipie leseni na mapato *TRA* ya biashara kama namba ni za njano yaani *private car* (gari binafsi) kwa nini yalazimke kukata leseni ya *SUMATRA* na kulipia *TRA*, ni mwanya mkubwa wa rushwa. *SUMATRA* inatakiwa iwe *regulatory authority* na yenye kusaidia kuboresha usafirishaji na si kuwa kero na yenye nia ya kujikusanya kipato ya kibiashara kama *Traffic* na *SUMATRA* wameshindwa kufuatilia wenye magari ya abiria wasiwayanyaye wenye magari ya binafsi. Pia vijijini nauli hali hazizingatiwi, wenye magari ya abiria hujipangia. Tunashauri kila mwaka itoe taarifa kwa wananchi juu ya nauli halali na pia magari ya abiria yanayokiuka *route* na kutofika vituo vyake wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli. Naishauri Serikali kabla ya kuanza ujenzi wa reli mpya, reli zilizopo ya Kati na ile ya *TAZARA* pamoja na ya Tanga – Moshi – Arusha zingeendalea kutumika ili kupunguza adha ya usafiri wa abiria na mizigo. Reli ya Tanga – Moshi – Arusha, Serikali ingeangalia namna ya kuboresha huduma ambayo sasa imesimama, huduma hiyo ingerudishwa kupunguza gharama ya usafirishaji wa mali kutoka Bandari ya Tanga, Saruji na mazao mengine kutoka Tanga kuja Moshi na Arusha, pia mazao na bidhaa kutoka Arusha na Moshi kwenda Tanga. Muhimu itapunguza bei ya bidhaa kama Saruji, mafuta ya petroli na *diesel*, na mafuta ya taa pamoja na Kiwanda cha Saruji kupata madini ya *gypsum* kutoka Makanya kwa bei nafuu pamoja na kusaidia sekta ya mkonge.

Pia treni ya abiria ingesaidia, hata kwa mwendo mdogo kupunguza tatizo la abiria kupandishiwa nauli hasa kipindi cha sikukuu na wanafunzi pindi ya kufunga na kufunga shule. Hii pia ni mawazo yangu kwa Reli ya Kati, Serikali ingepokea ushauri wa kuongeza *engine* nne mpya na mabogi ya abiria ya madaraja yote pamoja na ya mizigo na mafuta. Ingepunguza bei ya bidhaa kwa eneo la Kanda ya Kati na Ziwa. Hata kama treni hizo zitaenda kwa mwendo wa pole, bidhaa hufika kwa gharama nafuu ni muhimu pia mazao kama pamba, tumbaku, kahawa na mazao mengine yangesafirishwa kwa bei nafuu na kuongeza bei ya mwisho kwa mkulima kuwa kubwa, bei ya mafuta kupungua Kanda ya Ziwa kwa kusafirisha kwa *bulk*. Pia mabogi ya abiria yaboreshwe yenye huduma ya chakula, malazi na huduma nyingine muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa sekta ya bandari Serikali iangalie namna ya kuboresha huduma ya bandari, kero mbalimbali na gharama kubwa inayotozwa na ucheleweshwaji wa kutoa mizigo kutoka bandarini, huwasababisha kutumia bandari za nchi jirani. Pia wizi wa mizigo kutoka bandari zetu ni tatizo sugu, mizigo mingi huibowi na kuwa hasara.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ingeangalia mfumo wa kutoa mizigo haraka kwa kushirikisha na *TRA*. Mfumo huo unasababisha mrundikano wa mizigo na wenyenye mizigo kuchajiwaa *damage charges*.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuandaa Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete kwa ziara ambayo ameifanya hivi karibuni Mkoani Mtwara, ziara ambayo imeleta matumaini makubwa sana kwa wananchi wa Mkoa huu na Mikoa ya Kusini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hii Mheshimiwa Rais alipata nafasi ya kutembelea Bandari ya Mtwara na kufanya kikao na uongozi wa Kampuni ya *OPHIL* ambayo ndio wawekezaji walioanza kufanya kazi, katika mazungumzo hayo wawekezaji hawa wapo tayari kupanua eneo la bandari ili wafanyabiashara wa mazao mbalimbali hasa korosho wapate eneo la kutia nanga meli za mizigo.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kampuni hii imeonyesha nia ya kuchukua maeneo upande wa pili wa bahari kwa maana ya Msanga Mkoo hali ambayo Serikali inabidi kuwa makini katika eneo hilo kwani kuna wakazi na mashamba pia, ni vema ikaeleweka hatma ya wananchi hao na mali zao.

Mheshimiwa Sika, hali kadhalika Serikali tayari imeonesha mpango wa kuanza ujenzi wa reli toka Mtwara – Mchuchuma Liganga. Natoa pongeza kubwa sana jinsi ambavyo Serikali inakuwa na kasi katika kupanga mipango ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ushauri wangu katika maandalizi haya ni vema ukafanyika kwa umakini mkubwa hasa katika njia ambayo reli hii itapita kwani kasi ya ujenzi wa nyumba za makazi na maeneo ya kilimo ni kubwa sana hivyo kama *survey* itafanyika mapema wananchi waelekezwe vya kutosha kutotumia maeneo hayo kwa kazi yoyote ili kuepuka kero za kulipa fidia mara mbili. Hivyo Serikali naiomba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutenga fedha za kutosha za fidia kwa wale watakaoathirika na zoezi hili ili waweze kulipwa kabla kazi hajaanza, hali kadhalika katika wale watakaoatahirika katika upanuzi wa barabara.

Mheshimiwas Spika, mwisho, naishukuru sana Serikali kwa kuanzisha vituo vya mawasiliano katika maeneo mbalimbali ukiwemo Mkoa wa Mtwara na Wilaya ya Masasi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba yake. Mchango wangu uelekee upande wa bandari. *TAG* zilizopo bandarini hazitendewi haki kwa kucheleweshwa kufanyiwa ukarabati wa kina kwa sababu *TAG* hizi zinasaidia nchi nzima hata Zanzibar ilipotokea kuzama meli ya *FATIH*. *TAG* hizo ndizo zilizokuja na kufanya uokoaji kwa upande wa Zanzibar tunashukuru sana. Naiomba Wizara iangalie kwa kina *TAG* hizi ili zisiuzwe kwa ajili ya matengenezo madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, pindi *TAG* inapokwenda matengenezoni wafanya kazi husika ndio waende kwenye matengenezo hayo na sio wachukuliwe kutoka sehemu nyingine kama ofisini kwa sababu wahusika wakuu na wanaoyajua matatizo ya chombo ni wale wanaokitumia kila siku hii pia itawapa motisha wafanyakazi kuzidi kuipenda na kujali kazi yao.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara izilinde *TAG* zetu pia na wafanyakazi wetu kwa sababu unatuingizia sehemu kubwa ya mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, bandari ni kiunganishi kikubwa cha wageni wa ndani na nje ya nchi, naiomba Wizara iongeze ulinzi katika bandari kwani ulinzi wa uchunguzi wa vitu vya hatari upo hafifu na dhaifu sana, pia wachukuzi waangiliwe sana ili kupunguza idadi ya vibaka bandarini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoitoa leo asubuhi ya kuongeza Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMMED: Mheshimiwa Spika, Tanzania ina rasilimali nzuri walizojaaliwa na Mungu lakini matumizi yake ni mashaka. Tanzania ina bahari, bandari nyngi tu na reli tulizorithi kwa wakoloni, lakini matumizi ni mabaya mno.

Mheshimiwa Spika, ili nchi iendelee katika uchumi wake ni muhimu kuwa na ndege/shirika la ndege ambalo litawasaidia kiuchumi kwa njia mbalimbali kama biashara, watalii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, uundaji upya wa Shirika la Ndege, nanukuu; "Wizara inaendelea na tathmini ya kutafuta mwekezaji binafsi kwa kushirikiana na Serikali katika kuunda upya Shirika la Ndege," mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hapo mwanzo shirika liliwa na mshirika wake wakalikimbia, hawajaweza hii inatokana na *management*, umangimeza na ubadhifru wa Shirika la ATCL. Kutokana na hali hii Rais aliwapa fedha ya kulifufua Shirika hili lakini badala ya fedha kutumia katika ufufuaji, fedha hii illumiwa kwa mambo mengine yakiwemo ununuzi wa magari.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *Kenya Airways* na *Precision Air* wameanza kwa ndege kidogo tu na hivi sasa wanakwenda nchi mbalimbali, *Precision* imeongeza mbawa zake na kufunga milango ya kwenda Comoro, Asia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na utekelezaji wa shughuli za ndege ni mbaya, siasa nyngi imekuwa ndio njia ya kuendesha shirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inunue ndege nyngine mpya na sio kununua mitumba ya ndege, itakuwa ni matatizo kwani ndege zote zitakuwa ni mbovu na fedha kupotea.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi 182 ambaao wanalipwa bila ya kufanya kazi ni vyema wakasitishwa mpaka pale ndege zitapopatikana, la sivyo Serikali itaendelea kupata hasara, kwani fedha hizi zichangwe na kupatikana nafuu ya kufanya shughuli nyngine au hata kuwa ni kiongezeo cha ununuzi wa ndege.

Mheshimiwa Spika, Bodi iliyopo nayo ni tatizo, ni vyema ikavunjwa na kuchaguliwa wale ambaao wenye uchungu wa mall na wananchi na nchi hii, na sio wale ambaao *heart* nafsi.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikatoa nafasi na kuwapa Wizara hii fedha ya kutosha ili ikafanye kazi vizuri badala ya kuwapa mashaka kwa Wabunge na wananchi.

Msheshimiwa Spika, reli ni uti wa mgongo wa nchi na safari kwa wanyonge na ni muendelezo mzuri wa uchumi wa nchi. Tanzania katika kuijendeaza kimaendeleo reli ni chaguo la mwanzo, huwasaidia wanyonge katika safari zao na huwa ni za uhakika kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na hata wale wanaoishi karibu na njia za reli huwa ni moja katika kuijendeaza wao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ukoloni, Wajerumani na Waingereza walizitumia reli Tanzania kama ni kitega uchumi wa nchi hii kwa kusafirisha bidhaa na kuwapa wananchi walio chini kusafiri kwa urahisi zaidi. Reli ziliwa zinafanya kazi zake vizuri na kupunguza gharama na shughuli za wananchi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikafanya ifanyavyo kutengeneza njia za reli ambazo hivi sasa wananchi nao wanazihujumu kwa kutoa vyuma na kuvuza kwa wanunuzi wa vyuma chakavu, huu nao ni ubadhirifu, shirika litazidi kudidimia.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe makini katika jambo hili kwani linaweza kuwauwa wananchi pale waendapo na safari ya reli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari, kuna bandari kavu ambazo zimemilikiwa na watu wa nje, hizi ni nygingi na zimetanda katika Jiji la Dar es Salaam. Walizomiliki ni raia wa Kimali, Waarabu na Waingereza. Bandari hizi zinashughulika na magari yanayotoka bandarini. Serikali inakosa fedha nydingi sana kwa kuwapa watu kutoka nje na hivi ni vianzio nya kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakosa fedha/kupata fedha za kuendesha nchi ni vyema ikawapa wananchi nafasi hii ya kuweka *yards* za magari au kufanya wenyewe Serikali na kukusanya fedha nydingi mno.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, kwa mara zote tangu niwe humu Bungeni nimekuwa nikisemea reli, na bado sitachoka kuendelea kusema juu ya reli kama kichocheo kikubwa cha uchumi wa nchi hii lakini jitahada kidogo sana inayofanywa na hata tunapofikia maamuzi bado utekelezaji wake haupo na hautekelezeki. Usafiri wa gari moshi unaosuasua hasa wa abiria ni mbaya na hakuna mabehewa ya kutosha, uchache wa *engines* na kadhalika lakini pia madai ya wafanyakazi ni ya msingi sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia na mpango ambaao hautekelezeki wa kufufua reli madai ya kifuta jasho bado kama Serikali itapuza kuwalipa wafanyakazi ninayo mashaka mimi binafsi kwamba kadri mgogoro huu ambaao haupati suluhu unachangia kwa njia moja au nydingine kutokuwepo na ufanisi kati ya utekelezaji wa majukumu ya reli na mchango wa watu katika uchumi wa Taifa. Napendekeza kifuta jasho kwa wafanyakazi wa reli walipwe haki zao kama ilivyokuwa kwa taasisi na mashirika mengineyo ambayo yamepitia mchakato kama huu wa *EAR&H/TRC/TRL* na haijulikani baada ya *TRL* ni nini.

Mheshimiwa Spika, hofu nydingine nilyonayo ni mali zilizokuwa za *TRC*. Magenge na nyumba nydinginezo zimetelekezwu na zinahujumiwa kwa kasi ya ajabu hasa magenge, kuna mkakati gani wa kunusuru hali hii, aidha, mali zilizokuwa za *TRC* ambazo zinaendelea kuuzwa naomba ufanuzi wa faida au hasara ya kuuza mataruma hususan kwa kung'oa njia za mchepuo (*siding*) kama ile ya Mwadui na pengine hata ile ya *TPC* na nydinginezo, je, hakuna mpango wa kuimarishwa kwa *siding* zilizopo sanjari na uimarishaji wa reli kuu au umuhimu huo leo haupo tena kama ilivyokuwa wakati ikiengwa? Naomba kupata ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana inajapofikia wananchi kuanza kuchukua hatua kama walivyofanya wafanyakabiashara wa Mpanda kwa kuzuia gari la mizigo lisiondoke ili lipakie mizigo yao, mahitaji ya behewa za mizigo kwa *local customer* ni zaidi ya behewa 100. Kuna mrundukano wa mizigo (nafaka) pale *Mpanda Station*, wafanyakabiashara hawa mizigo yao inaharibika kwa jua na kushuka kwa bei na wanapata hasara kwa kushindwa kusafirishiwa mizigo yao lakini pia Shirika limekosa mapato na kadhalika uchumi wa nchi kuathirika pia. Je, kuna mkakati gani wa kuondoa mizigo hiyo na sambamba kwa kuimarishwa kwa njia ya reli kati ya Mpanda/Kaliua?

Mheshimiwa Spika, kuna upanuzi na ujenzi wa kiwanja cha ndege Mpanda unaendelea na pia umegusa baadhi ya wananchi kuhamishwa na kulipwa fidia lakini yapo malalamiko ya wananchi kupata malipo ambayo hayalingani na thamani halisi ya mali zao na kwa kuwa tathimini imefanywa na wataalamu pekee bila wao kushirikishwa katika hatua za awali na kulipwa kile ambacho hawakushirikishwa katika utayarishaji wake, kwa wale ambaao hawakuridhika watalipwa tofauti ambayo wanaamini wanastahili kulipwa, naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho usafiri katika maziwa yetu, Kampuni ya *MSL* haina mtaji, imerithi meli chakavu, hakuna huduma bora kwa abiria na uchukuzu wa mizigo kwa sababu ya kutokuwepo na ratiba maalum, inafanya wananchi wasafirishe mizigo yao kwa maboti ambayo

wanahatarisha maisha na mali zao hususan katika Ziwa Tanganyika na kwa kusimama kwa muda mrefu kwa Mv. Mwongozo ni lini meli hii itaanza kufanya kazi. Nitapenda kupata maelezo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, *SUMATRA* ni taasisi inayodhibiti vyombo vya baharini na nchi kavu lakini utendaji wake haqidhishi. Ni kawaida vyombo vya abiria vya baharini kubeba au kusafirisha abiria zaidi ya uwezo wa vyombo vyenyewe. Sijasikia vyombo hivyo hukamatwa kwa hali hiyo wakati ni suala la kawaida vyombo hivyo kuchukua abiria zaidi ya uwezo wa vyombo vyenyewe.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa usalama wa vyombo hivyo pia haufanywi kikawaida hali ambayo inaweza kuhatarisha uhai wa abiria wanaosafiri kwa vyombo hivyo vya haranini. *SUMATRA* imeshindwa kudhibiti hali ya ujangili kwenye bahari na hata kwenye maji ya maziwa. Hali sasa inatisha katika bahari yetu na maziwa hasa Ziwa Tanganyika, je, *SUMATRA* imejipanga vipi kuhakiki suala hilo?

Mheshimiwa Spika, kutodhibiti ajali za barabarabni ni ushahidi mwingine wa kiasi gani *SUMATRA* imeshindwa ipasavyo katika Nyanja ya Usafiri Nchi Kavu. Maisha ya wananchi wengi yanapotea kutoptaka na ajali za barabarni. Je, *SUMATRA* imejipanga vipi kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli katika nchi una umuhimu wa pekee katika kuleta maendeleo. Leo kwa kukosa huduma nzuri ya reli barabara zitakufa kwa mizigo mizito inayosafirishwa na gari za mizigo. Pia ukosefu wa huduma nzuri wa reli zile nchi ambazo zimetuzunguka zinazohitaji mizigo yao kusafirishwa kutoka bandari zetu haitowezekana, kwa vyovyote reli ina umuhimu sana kwa maendeleo yetu. Abiria pia wananaufaika sana kama usafiri wa reli upo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa nchi yetu kukosa Shirika la Ndege la Taifa, licha ya kusafirisha abiria wa kawaida pia Shirika la Ndege la Taifa lingewenza kuleta abiria (watalii) kutoka Ulaya, Asia na Marekani. Utalii haukui ipasavyo kwa kukosa Shirika la Ndege la Taifa. Je, Wizara wamejipanga vipi katika kuanzisha shirika jipya. Ahsante.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Uchukuzi, awali ya yote naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa reli, nchi yoyote inayoendelea kiuchumi hutumia usafiri wa reli na hapa kwa kubeba mizigo katika kutumia barabara, lazima Serikali iwekeze zaidi kwenye uimarishaji wa usafiri wa reli kuliko barabara. Tumeshawekeza sana kwenye barabara sasa tugeuke tuiangalie upya eneo hili la reli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa ndege, naomba Serikali ijenge uwanja mpya Njombe, kwenye Mkoa mpya wa Njombe. Baada ya kuimarisha uwanja wa Songwe na baada ya kuamua kuanza kuchimba makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga, eneo hili litahitaji uwanja wa karibu ambao naomba uimarishwe ulio wa Njombe Mjini.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imejenga uwanja mdogo wa llembula kwa ajili ya kuinua utalii eneo la Mpanga. Naomba uwanja huo uliojengwa na *TANAPA* uboreshwe ili uanzu kutumika.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, sekta ya uchukuzi imekuwa na changamoto nyingi hapa nchini na kusababisha kutoa huduma zake chini ya kiwango cha matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie usasfiri wa reli na usafiri wa anga na viwanja vya ndege. Kuhusu usafiri wa reli, kutoptaka na jiografia ya nchi yetu inaonyesha njia pekee inayoweza kutosheleza huduma za usafiri ni kupitia njia ya reli kwa sababu itawafikia wananchi kwenye maeneo mengi na vilevile kutoptaka na pato dogo la Watanzania ambao 85% wanaishi vijijini na kutegemea kilimo cha jembe la mkono, hivyo hawawezi kumudu gharama za usafiri wa ndege au mabasi kwani gharama zake zipo juu ikilinganishwa na gharama za usafiri wa reli.

Mheshimiwa Spika, aidha, usafiri wa reli unasaidia kusafirisha mizigo mizito ambayo kadri inavyoendelea kusafirishwa kwa njia ya barabara inachangia uharibifu mkubwa amba Serikali imetumia fedha nyingi kujenga barabara hizo katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, pendekeso, nashauri kama inavyofanyika kwenye sekta ya ujenzi kutoa *tender* za ujenzi kutoa *tender* za ujenzi wa barabara kwa kilomita, nashauri Serikali itumie mfumo huo katika ujenzi wa reli kutangaza *tender* za ujenzi wa reli, wawekezaji wa ndani hasa kutoka sekta za umma wahamasishwe kuwekeza kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndege Tanzania (*ATC*), kutohana na ushindani wa kibiashara kuwa mkubwa, naushauri *ATCL* iishirikane na *Airlines* zingine duniani badala ya kufanya kazi peke yake. Aidha, ili kuwa na ufanisi katika uendeshaji wa shirika, Serikali ihamasishewewe wawekezaji wa ndani waweze kumiliki hisa na kuongeza mtaji wa kuendesha shirika, mfano Shirika la Ndege la Kenya (68.14%) ya hisa za Shirika ni mali ya Wakenya wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi nashauri Serikali ipunguze urasimu katika uwekezaji kwenye sekta ya uchukuzi ili tuweze kutoka hapa tulipo na kuhakikisha nchi inafungua milango ya biashara Kimataifa kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwenye hotuba yake alipohutubia Bunge kwa mara ya kwanza mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%. Naelewa changamoto nzito zinazoikabilii Wizara hii changa. Nakupongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu wako Mkuu kwa kazi nzuri yenye changamoto kubwa. Jitihada zipo asiyeziona ni ukosefu wa shukrani.

Mheshimiwa Spika, nashauri katika mambo yafuatallyo, kwanza Reli ya Kati, naelewa juhudhi za Serikali katika kufufua na kuimarisha reli ya kati. Umefika wakati kwa Serikali yenye kwenye reli hiyo hata kabla ya kuikodisha. Uzoefu umeonyesha kwamba si rahisi kupata wawekezaji waaminifu watakaowekeza kwenye ujenzi wa reli. Wawekezaji wengi wanapenda kukodisha sio kujenga, ukikodisha miundombinu chakavu mwisho wake ni kurudishiwa miundombinu mibovu zaidi. Nadhani umefika wakati Serikali ikope bila woga ili kujenga reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam – Kigoma na Mwanza. Suala hili linahitaji uamuzi wa haraka na mgumu lakini naamini hiyo ndiyo njia sahihi.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu Reli ya Tanga (Dar es Salaam – Tanga na Tanga – Arusha). Reli hii imesahaaulika kwa muda mrefu. Naomba jitihada zifanyike kufufua reli hiyo. Pia nashauri reli ya kisasa ijengwe katika maeneo hayo. Usafiri wa reli ni rahisi na reli husaidia kukuza uchumi katika maeneo ya reli inakopitia. Kwa reli hii kutofanya kazi maeneo yote yaliyokuwa na maendeleo chanya wakati wa reli ikifanya kazi, kama vile Mnyuzi, Mombo, Ruvu na kadhalika sasa yamerudi nyuma sana.

Mheshimiwa Spika, tatu, mali zilizokuwa za *NTC* (Shirika la Usafirishaji la Taifa), kuna magari makubwa na madogo yaliyokuwa ya Shirika la Usafirishaji la Taifa, magari hayo yametelekezwa katika eneo la Kamata pale Kariakoo. Magari hayo yanaoza na kuibwa vipuri. Nashauri Wizara ifuatilie, kuna tatizo gani maana magari hayo yametelekezwa kuanzia mwaka 2003. Mimi nilikuwa Mwenyekiti wa *NTC*, naelewa msingi wa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, nne, ubinafsishaji wa UDA. Naomba nieleze kwamba mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Usafirishaji la Taifa ambalo lilikuwa likisimamia mashirika yote ya usafirishaji *RETCO's*, UDA na kadhalika nia ya kurekebisha UDA ilikuwa na lengo jema, lakini watekelezaji, viongozi sio waaminifu. Nashauri uteuzi wa viongozi wa Bodi ifanywe kwa uangalifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakutakia kazi njema nakuomba usikate tamaa. Changamoto ni sehemu ya mafanikio kwa kuzitatua.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Spika, kuhusu Bwawa la Kimagai ndani ya Jimbo la Mpwapwa (Mkoani Dodoma) kata ya Kimagai, Bwawa hili limejaa tope nyingi sana kiasi cha kusababisha mafuriko makubwa yanayoleta kero ya mafuriko makubwa katika jimbo jirani la Kilosa (Mkoani Morogoro) na kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara na reli, mafuriko haya yanatokea Jimbo la Kilosa hata kama mvua hazinyeshi Kilosa, hali hii inatokana na maji ya mvua za Jimbo la Mpwapwa na Kongwa zinaponyesha na kusababisha maji kutiritika kuelekeea Kilosa kupitia Bwawa la Kimagai na Kidete. Je, Wizara ina mpango/mkakati gani wa kufufua Bwawa hili muhimu, kwa kuyafanya maji, yatuame pale na kupunguza mafuriko yanayosababisha uharibifu wa miundombinu ya uchukuzi?

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, ni wazi na dhahiri kuwa bila ya kuwa na mikakati thabitii juu ya uchukuzi na usafirishaji hatuwezi kuwa na uchumi endelevu na imara. Leo hii kutohana na kukosekana kwa mbinu sahihi za uchukuzi mfano reli, usafiri wa anga na maji ndiyo chanzo kikubwa cha kupanda kwa gharama za maisha. Usafiri wa barabara umefanikiwa kuwepo lakini si suluhisho la tatizo hili.

Msheshimiwa Spika, katika maisha ya kawaida, ujenzi wa nyumba bora ni suala la msingi, vifaa vya ujenzi vimekuwa ghali sana kiasi kwamba wananchi wengi imekuwa vigumu kujenga. Leo hii mfuko wa saruji kwa bei ya rejareja ni shilingi 20,000/= na ukizingatia uwezo wa viwanda tulivyo hapa nchini, na uzalishaji wake haiji katika fikra za kawaida kununua kwa bei kubwa hivyo. Lakini hii inasababishwa na suala zima la usafirishaji toka Dar es Salaam mpaka Kagera (Biharamulo Magharibi) ambayo ni kwa njia ya barabara, suala ambalo ni ghali sana. Lakini naamini katika hili kama usafiri wa Reli ya Kati ungefanya kazi nzuri na katika Ziwa Victoria meli yetu ya Umoja ingekuwa inafanya safari zake kawaida, bei hii isingekuwa juu kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuboresha meli ili kupunguza makala ya bei hizi na vilevile kurahisisha usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara na hii ingesaidia kuinua kipato na kukuza uchumi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, suala la usafiri wa anga hapa nchini limekuwa la matatizo makubwa, kuna kampuni za kigeni ambazo zinaendesha huduma za usafiri wa anga hapa nchini. Kuna ukiritimba mkubwa sana. Safari za ndege hazitabiriki na bei ya safari kila kukicha inabadilika. Je, Serikali yetu haioni hili? Nauli ya ndege toka Mwanza hadi Dar es Salaam kwa kampuni au mashirika ya ndege ya *Precision* na *Fly 540* ni tofauti kabisa na ukiangalia faida wanayopata ni kubwa mno! Kwa nini Serikali isifanye mkakati wa sharti walau kuangalia suala la nauli kwa wasafiri hawa! Hata kusimamia tu sheria hizi imekuwa ngumu, hapa kuna nini? Nauli ya ndege toka Mwanza hadi Bukoba nauli ya ndege toka Mwanza hadi Kigoma zinashangaza kabisa, kila kampuni inapanga bei kadri inavyoona kwayo inafaa.

Mheshimiwa Spika, naishauri bodi husika ya usafiri wa anga iliangularie suala hili kwa upana na mwelekeo stahili. Tofauti na hili tunaliweka Taifa letu hatarini. Mashirika ya wenzetu kila kukicha wanaongenza ndege kwa kuwa wanapata faida kubwa, hivyo Serikali ijifunze juu ya suala hili.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa afya njema inayoniwezesha kutimiza wajibu wangu wa Kibunge wa kuchangia hoja mbalimbali zinazowasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa utekelezaji wa mpango wa mwaka 2010/2011 iliyopelekea maandalizi ya hotuba hii pamoja na kwamba Wizara hii ni mpya, pamoja na changamoto inayozikabili Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Pwani hususan Wilaya ya Mafia na Bagamoyo, tunaishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Nne kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa ujenzi wa gati Mafia. Kwa kipindi cha miaka 50, Kisiwa cha Mafia kilikuwa na matatizo ya usafiri, hivyo ujenzi wa gati ni mkombozi mkubwa sana. Ni kweli wananchi wa Wilaya ya Mafia tumeshuhudia ujenzi huo umeanza na kipindi cha uchaguzi ujenzi huo ulienda kwa kasi sana, hata hivyo tarehe 22/07/2011, nilifanya ziara ya kikazi Wilaya ya Mafia na kupata malalamiko ya kuwa kazi hiyo imesimama mara baada ya uchaguzi na hivyo kuwafanya baadhi ya wanasiasa kutumia kama ni kigezo kwa ujenzi wa hilo gati la Mafia ni jambo la kisiasa. Nilipotembelea eneo la mradi lilionyesha kabisa kazi imesimama na hata mkandarasi hayupo *site* na baadhi ya vitendea kazi hasa magari yameondolewa pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 26 inaonyesha ujenzi wa gati utakamilika mwezi Desemba, 2011, kwa kweli nina mashaka na ahadi hii kwa vile kazi hiyo imesimama.

Mheshimiwa Spika, pili, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Mafia. Naipongeza sana Serikali kwa kukijenga Kiwanja cha Ndege Mafia ni matarajio yetu kuwa kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012 lengo la ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, tatu, ujenzi wa Bandari mpya Bagamoyo. Kwa niaba ya wananchi wa Bagamoyo tunaishukuru sana Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga bandari mpya Wilayani Bagamoyo na hivyo kukamilisha kazi ya upembuzi. Naiomba Serikali iharakishe taratibu za kutafuta mbia binafsi ili kazi hiyo ianz, ili wananchi wa Bagamayo na Mkoa wa Pwani ambaa ni maskini sana wa kipato waweze kuboresha kipato kwa kuwafungulia njia za uchumi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuulizia ujenzi wa bandari kavu eneo la Mzenga Wilaya ya Kisarwe ambako reli ya TAZARA inapitia lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuna mahali popote pale ambako bandari kavu hii ya Mzenga haijatajwa na wala hakuna mpango wowote ulioainishwa kuhusu bandari hizo kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii hasa baada ya kupokea maelezo ya Serikali kupitia Waziri Mkuu juu ya kuongeza Bajeti ya Wizara hii, pia mkakati wa Serikali wa kushughulikia tatizo la UDA kwa kuziagiza mamlaka husika kufanya uchunguzi juu ya sakata hilo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yanapaswa kuondolewa ili Serikali ikafanye marekebisho ili kiwango cha fedha kwa ajili ya miradi ya uchukuzi kwenye usafiri na uchukuzi wa anga, usafiri na uchukuzi wa reli, usafiri na uchukuzi wa nchi kavu, usafiri na uchukuzi wa majini. Aidha, Serikali ilete maeneo ya kina kuhusu hatua zilizochukuliwa kwa wote walioliingiza Taifa katika hali hiyo kwenye reli, nchi kavu, majini na anga.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza fedha katika Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi ni muhimu kutoa kipaumbele maalum kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (*NIT*). Kwa mujibu wa kitabu cha Bajeti cha Maendeleo fungu 62 - kifungu cha 2006 Kasma 6377 Chuo cha Usafirishaji kimetengewa Bajeti ya shilingi bilioni 1.7 tu kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo. Kiwango hiki ni kidogo sana ukizingatia mahitaji rahisi na ya muhimu ya zaidi ya shilingi bilioni 10 ambayo yaliwasilishwa mapema kwa Serikali. Hii itawezesha kufanya ujenzi na karabati wa madarasa, mabweni, barabara ya ndani ya chuo na uzio. Chuo kina eneo kubwa ambalo uwekezaji ukifanyika utainua elimu, utapanua wigo wa ajira za uchukuzi/usafirishaji na pia utaongeza mapato. Hii itawezesha pia kununua vifaa vya karakana, magari, vitabu na kompyuta. Aidha, Serikali itoe kauli namna ambavyo inashughulikia tuhuma za ujisadi na utawala mbovu katika chuo hicho zilizojitokeza kwenye vyombo vya habari mwaka 2010 na 2011pamoja na matatizo ya wanafunzi wa chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 2005 Kasma 4215 na 4216 kuhusu ujenzi na ukarabati wa njia ya reli, fedha zinapewe ili kuwezesha reli ya kati na reli ya Kaskazini kama sehemu ya kutumia fursa ya kiuchumi, kupunguza matatizo ya usafiri kwa wananchi na pia kulinda barabara kuu zinazoharibika hivi sasa kwa uchukuzi wa mizigo mizito na kupunguza ajali barabarani. Aidha, katika changizo hiyo ya fedha pawepo na mgawo kwa ajili ya matengenezo ya njia ya reli toka Stesheni mpaka Jimbo la Ubungo na kununua mabehewa maalum kwa ajili ya kuanza usafiri wa umma toka Ubungo mpaka Posta ili kupunguza adha ya usafiri wa foleni katika Jiji la Dar es Salaam. Mkakati huu uguse pia njia nydingine za reli katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, kiwango

cha fedha kilichotengwa kwenye Kasma 4261 ya ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali havioneshi dhamira ya Serikali kutekeleza kwa kuweka makubalino (*MOU*) ya Januari, 2009 katika Tanzania, Rwanda na Burundi. Nchi yetu inapanua kutumia maeneo fursa hii ya kiuchumi ya kijiografia.

Mheshimiwa Spika, ujisadi katika Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) ni matokeo ya uzembe wa Serikali kuchukua hatua mapema. Katika michango yangu kwa maandishi kwenye mijadala ya Azimio la kiliongezea muda Shirika hodhi la Mashirika ya Umma (CHC) pamoja na ofisi ya Waziri Mkuu mapema mwezi Juni, 2011 nilitaka kauli ya Serikali na hatma mahususi kuchukuliwa. Hata hivyo Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu katika majumuisho ya hoja husika hawakutoa kauli wala kuchukua hatua stahili. Tarehe 15 Julai, 2011 nikauliza swali Ofisi ya Waziri Mkuu swali la kutaka hatua kuchukuliwa, hata hivyo jibu lisilordhisha lilitolewa na hatua hazikuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, vikao vyta Jiji vilivyoshughulikia suala hili yote ni batili kwa kukosa akidi. Kauli ya sasa ya TAKUKURU, CAG na OC/kufanya uchunguzi ili kuvezesha Kamati ya Miundombinu kuchukua hatua haitawezesha hatua za haraka kuchukuliwa na hajazingatia taratibu. Hivyo Waziria Mkuu na Waziri wa Uchukuzi katika kuhitimisha hoja anapaswa kutoa kauli mbadala ya kusitisha mara moja utekelezaji wa mkataba chini ya kampuni ya *Simion Group*.

Aidha, taratibu za kisheria zifanyike kubadili mchakato wa ubinafsishaji wa UDA na rasilimali zake ziunganishwe mfumo wa usafiri wa umma, Dar es Salaam (*mass transity*) utakaouganishwa na mradi wa mabasi ya Newala (*DARE*) chini ya chombo kimoja. Kamati ndogo ya miudombinu imepoteza uhalali wa kimaadili kwa mjumbe wake kuwa na mgogoro na maslahi. Ihusishwe Kamati ya Mashirika ya Umma.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Spika, baada ya Waziri Mkuu kutatua matatizo yaliyojiteza jana katika Bajeti hii, sasa naiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono nashauri yafuatayo, kwanza ni kuhusu ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Taveta. Kwa kuwa nchi ya Kenya imeamua kuwa na kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro kwa kujenga kiwanja cha kisasa kitakachowezesha ndege kubwa duniani kutua, napendekeza Wizara ya Uchukuzi kuendelea kuimarisha Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, pili, kujenga reli ya Tanga – Moshi – Arusha hadi Taveta Kenya. Reli iliyotajwa hapo juu imechakaa na ikarabatiwe itasaidia sana kuzuia barabara isichakae mapema. Pia njia ya treni inayotoka Arusha kwenda Taveta Kenya inapita katika Jimbo la Vunjo, hivyo wananchi wangu watanufaika sana.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii kuchangia mchango mfupi kwenye Wizara hii lakini mchango muhimu. Kwanza, Reli ya Tanga – Moshi – Arusha. Nimesikitishwa sana kuona kuwa Serikali imeelemea kuendeleza nchi yetu kwa ubaguzi.

Mheshimiwa Spika, mimi enzi zangu nimesafiri kwa treni kutoka Arusha kwenda Korogwe (kusoma). Wanafunzi toka Mikoa ya Kaskazini hawakupata shida ya usafiri. Leo hii wanafunzi wanapata shida ikiwemo kupata ajali na maafa yatokanayo na usafiri wa mabasi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifufue reli hii, siyo tu kwa kusafirisha abiria, bali hata kusafirisha mizigo/mazao mengi yanayolimwa Ukanda wa Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, pili, Uwanja wa Ndege wa Arusha. Wasafiri wote wanaotoka Dar es Salaam kutua *KIA*, either wanachukua usasfiri kwenda Moshi au wengi wao kwenda Arusha. Safari ya kutoka *KIA* kwenda Moshi au Arusha ni muda mrefu kuliko muda unaochukua ndege kuruka toka Dar es Salaam kuja *KIA* (dakika 50).

Mheshimiwa Spika, naomba kujua, ni kwa nini ndege kubwa hajijaweza kutua kwenye Uwanja wa Arusha na hata ndege ndogo ndogo zinatua kwa nadra na kusuasua?

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Uwanja huo wa Arusha usiboreshwre kupunguza muda usio wa lazima kutoka *KIA* kwa *shuttle* kuja Arusha zaidi ya saa moja na nusu.

Mheshimiwa Spika, Arusha ni mji wa Kimataifa, wasafiri toka nje ya nchi kwa *KLM* wanakuja usiku na inawabidi kusafiri usiku huo umbali mrefu kwenda Arusha. Wengi wanavamiwa na majambazi njiani na kuporwa mali zao. Nataka kujua, ni kwa nini Serikali inalifumbia macho hili linalodhalilisha nchi yetu na hata kupotezea mapato.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa haraka iboreshe uwanja wa ndege wa Arusha, ndege zote ziweze kutua pale.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Rukwa. Mji wa Sumbawanga kwa mahitaji ya sasa unatakiwa kuwa na uwanja wa ndege mpya na siyo kutegemea uwanja uliopo, kwa uwanja huo upo katikati ya mji na ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, uwanja uliopo ni mdogo, unatakiwa upatikane uwanja mwingine tena uwekewe lami. Naomba Serikali ijenge uwanja mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu reli, umuhimu mkubwa wa Serikali kufikiria ujenzi wa kuunganisha reli kutoka Mpanda, kuunganisha bandari ya Kipili, Wampembe hadi Bandari ya Kasanga na kuunganisha reli ya Tunduma.

Mheshimiwa Spika, kama maeneo hayo yangeunganishwa ingekuwa ni ukombozi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, usafiri katika Ziwa Rukwa linatakiwa kuwa na maboti ya kisasa kwa ajili ya usafiri wa majini katika Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wawekezaji, Serikali inatakiwa kutafuta wawekezaji katika kuendeleza fursa zilizopo katika Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, suala la udogo wa Bajeti. Bajeti iliyotengwa ni ndogo mno. Linatakiwa iongezwe ili ipate nguvu ya kukabiliana na utatuzi wa matatizo yaliyopo katika Wizara hii. Vinginevyo Wizara hii itakufa. Naomba Serikali ilione hili ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho siungi mkono hoja mpaka baada ya ufanuzi wa kueleweka.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu katika Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli ni muhimu sana katika usafirishaji wa abiria pia mizigo katika kukuza uchumi hapa nchini. Nianze na reli, kwa upande wa Reli ya Kati naona hata aibu kuongelea, kwani Tanzania tumepigwa changa la macho. Tangu Shirika la Reli lilllobinafsishwa hali imegeuka na kuwa mbaya sana kwani reli zimekuwa zikiharibika bila matengenezo ya haraka na hivyo kusababisha taruma za reli kung'oka kwa urahisi kiasi cha kusababisha ajali za hapa na pale hasa kwa behewa za mizigo. Serikali ichukue Shirika hili la Reli ili iweze kuokoa maisha ya Watanzania waweze kusafiri kwa matumaini.

Mheshimiwa Spika, mabehewa yanatia aibu sana kwani yamechakaa na ni machache hayatoshelezi kukidhi wingi wa abiria wanaosafiri. Kila siku ni hivyo kusababisha watu kujazana sana hadi vyooni, kitu ambacho ni hatari hata kwa afya za wasafiri. Tunaomba Serikali iongeze mabehewa ya kutosha. Serikali itengeneze *engine* ile tabia ya kufeli kwa *engine* zikiwa juu ya Mlima Saranda usiwepo tena, ni hatari kwa wasafiri na Serikali izibe ufa kabla haujajenga ukuta.

Mheshimiwa Spika, meli, usafiri wa meli hasa katika Ziwa Tanganyika unaounganisha nchi nne ambazo ni Tanzania, Burundi, Kongo na Zambia. Meli hizi ni za zamani kwa maana ya muda mrefu sasa kama haziwezi kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara ni hatari sijui kwa nini Tanzania hatujifunzi kutokana na makosa kosa litokee ndipo tunashtuka?

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa barabara, Mkoa wa Katavi tuna matatizo sana ya usafiri wa barabara hasa ya kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda. Tuna kampuni moja tu, nayo ni Sumry.

Mheshimiwa Spika, Kampuni hii haitoshelezi, kwani abiria hujazwa kama kuku wanaopelekwa mnadani hubanana humo na kwenda wanalamikia mpaka wafikapo. Hivyo tunaiomba Serikali itusimamie kwa hili ili tupate kumpuni nyingine Mkoa wa Katavi ili tuwe na kampuni hata mbili za kubeba abiria kutoka Sumbawanga hadi Mpanda tofauti na kampuni ya Sumry.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Ndege kama Shirika la Ndege la ATC halifanyi kazi yake na inaonyesha watumishi bado wanaendelea kupata mishahara, je, Tanzania hii tunakokwenda ni wapi? Naomba tusimamie nchi yetu ili tuinusuru katika janga la uchumi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. PROF. MAKAME NYAA MBARAWA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchangia kuhusu huduma za hali ya hewa. Sekta ya hali ya hewa ni muhimu kwa usalama wa maisha, mali na mazingira. Utabiri wa hali ya hewa unaweze kupatikana kwa rada ya hali ya hewa au kwa kutumia *super computers*.

Mheshimiwa Spika, *super computer* inaweza kukupa utabiri wa hali ya hewa kwa muda wa siku tatu mpaka siku kumi. *Dar es Salaam Institute Technology* ipo *super computer facility* ambayo ina uwezo wa kufanya au kutabiri hali ya hewa. Naomba Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa kuitumia ile *facility* pale *DIT*. Hii *super computer* inaweza kufanya kazi na Serikali inaweza ku-save pesa nyingi za kuinunulia hizi rada.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara ihamasishe Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa kuitumia ile *super computer at DIT*.

MHE. ABDALLAH S. AMEIR: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivi sasa niko hai nikiwa katika Ukumbi huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vizuri sana hotuba yake ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imepangwa vizuri sana kiuongozi, lakini haikuwa tayari kusaidia wananchi wa nchi hii kwani kwa upande wa Bandari ya Dar es Salaam ni tegemeo kubwa kwa wananchi wa Zanzibar kwa usafiri wa majini kuja Tanzania Bara. Katika bandari hiyo kuna matagi matatu ambayo moja linatumika kwa kushushia abiria na mizigo kutoka kwenye boti za *Sea Star* na *Sea Gull* na tagi la pili inatumika kwa maboti ya Kilimanjaro na *Sea Bus* lakini tagi la tatu inatumika na boti za *Sea Express* na *Flying Horse*. Tagi hili limejengwa na Serikali kupitia Wizara, lakini hivi sasa tagi hiyo ni mbovu na linahatarisha usalama wa Abiria na mizigo yao, kwani haliko katika hali nzuri kabisa na halifai kutumika kabisa katika kipindi hiki na sikuona hata shilingi moja ambazo zimetengwa ama kufanya matengenezo ama kujengwa lingine.

Mheshimiwa Spika, Je, Mheshimiwa Waziri anaelewa kuwa tagi hilo ni bovu na halifai kutumika? Je, kama ni bovu, Serikali ina mpango gari wa kufanya matengenezo tagi hilo? Kama nayo yote hayapo: Je, ni lini tagi hili litafungwa ili isije kutokea tatizo la msafara hapo bandarini Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Spika, kwanza nampa pole Mheshimiwa Waziri yeye na Watendaji wote wa Wizara ya Uchukuzi. Pili, nakupongeza wewe pamoja na Serikali yote kwa ujumla baada ya kuona michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge, Serikali imeona na kukubali

kuongeza bajeti ya Wizara. Nawapongeza sana. Nimefurahishwa na tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi, kwa kweli nimesikitishwa sana, kwani lawama zote alizopata Waziri zimetokana na Serikali yote kwa maana ya *cabinet* kutojali ufanisi katika upangaji wa bajeti kwa kuzingatia na kutilia maanani maeneo ambayo yataleta tija, ukizingatia umaskini mkubwa unaotukabili Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kama walivyoongea Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Reli ya Kati, Air Tanzania, Viwanja vya Ndege, haya ni maeneo muhimu sana ambayo kama Serikali yetu ikiwajibika na kuboresha maeneo hayo hakika Watanzania wengi watanufaika, na uchumi wetu utaboreka, tutajikwamua kwa kupunguza umaskini. Tunalaumiana, tunawaona wabaya kwa sababu ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wanapokaa kwenye vikao, hasa vikao vya *cabinet* mwabane sana Maafisa Mipango walete mipango ilioiva. Bajeti muiangalie kwa kina kabla ya kuipitisha. Pia mipango yenu iendane na Ilani ya Uchaguzi hasa hii kauli ya Maisha Bora kwa kila Mtanzania. Kauli mbiu hii haiwezi kutekelezeka kama Sekta ya Usafirishaji haitaboreka. Kama kuna watu wanaokwamisha maendeleo, wasimamishwe au waondolewe kabisa, wasiendelee kuleta vikwazo.

Mheshimiwa Spika, ninasema hayo kuhusu kuondelewa wanaokwamisha kwa sababu ya *UDA*. Kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge, inaonyesha wazi kabisa kuwa kuna ufisadi wa wazi kabisa. Nimefarijika na maeleo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nategemea kwa kutumia vizuri bajeti hii baada ya kuongezwa bajeti itakayofuata, mambo yatakuwa mazuri. Nategemea maeleo mazuri yatakayotupa matumaini baada ya marekebisho haya ya bajeti, utanieleza ni kwa namna gani utaboresha Reli ya Kati, Air Tanzania na Viwanja vya Ndege. Kama nitaridhia, sitatoa shilingi, lakini vinginevyo, mh!

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, *ATCL* ina upungufu mkubwa wa Wahandisi. Hata hivyo, wapo vijana wanaosomeshwa nchi za nje na wazazi wao. Kumekuwepo na tabia ya wataalam wanaosomea nje kubaki huko kwa kuajiriwa kutokana na malipo mazuri. Naishauri Serikali ione umuhimu wa kuwafuatilia vijana wetu wanaosoma, nje iweze kuwapa ajira hapa nchini kwa malipo mazuri ili kupunguza gharama za kupeleka ndege zetu nje kwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe makini kuhusu hujuma zinazofanyika katika Shirika la Ndege, Reli na Bandari maana haieleweki kwa Watanzania kwamba Mashirika yote haya yawe na matatizo makubwa kwa kiasi kilichoeleza na Waheshimiwa Wabunge katika michango yao.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maeleo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu asubuhi ya leo na kwa heshima yake, naunga mkiono hoja. Ahsante.

MHE. MARGARET S. SITA: Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii, lakini kwa bahati mbaya sana haifanyi kazi ipasavyo na hivyo kuathiri uchumi wa nchi hasa kwa wananchi wa upande wa Magharibi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha reli hi katika muda mfupi, wa kati na muda mrefu?

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Omari Nundu - Waziri wa Uchukuzi pamoja na Naibu wake, kaka yangu Mheshimiwa Mhandisi Athumanji Mfutakamba kwa kazi nzito ya kusimamia Wizara hii mpya yenye nembo ya matatizo lukuki wakati huo huo ukiwa ndio mhimili mkuu wa uchumi. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu - Ndugu Mhandisi Omar Chombo, pamoja na wote. Nami mnipongeze

kwa kuwa mmepitisha bajeti yenu siku ya kuzaliwa kwangu (*birthday*) ndiyo maana sipendi kabisa hii bajeti ikataliwe. Naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amekalia kaa la moto, Wizara hii ni jicho la watu. Napenda kutoa ushauri kwa Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye kila hali tupate jibu la reli hasa ya kati ambayo haina migogoro ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, katika Ziwa Nyasa, watu wanakufa kila siku. Siku ya bajeti ya Mambo ya Nje nilisema sana. Tafadhali sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ihakikishe maslahi ya wafanyakazi na wastaifu wa Reli yanashugulikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba *UDA* ifanyiwe kazi. Kuna maoni ya Wabunge kwamba watu wasionewe haya kama wamehusika na ubadhirlifu huu. Hata hivyo, siyo sahihi kumchunguza mtu wakati akiwa ofisi, wapewe hata likizo zenyé malipo kama ilivyofanyika kwa Katibu Mkuu wa Nishati. Jiji kuuza viwanja vya taasisi ni mchezo wao.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji mzuri wa *KIA* ni muhimu uangaliwe kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri Mkuu kwa kuinusuru bajeti hii kwa kuiongezea pesa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ila suala la meli Ziwa Nyasa lishughulikiwe.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa O. Nundu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji na viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara yote, kwa kuandaa hotuba nzuri ya bajeti yenye kueleweka na yenye matumaini ya kutekelezwa kwakwe. Baada ya pongezi hizo, nachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile Wizara hii ndiyo inayoshughulikia masuala ya uchukuzi ikiwemo magari, reli, anga, maji na kadhalika, natoa masikitiko yangu kuhusu ukosefu wa mazingira yasiyo rafiki kwa wasafiri wenye ulemavu nchini katika vituo vya usafiri wa aina yote. Kwa mfano, katika "*Airport*" ya Dar es Salaam wenye ulemavu hawana huduma muhimu za vyoo vinavyokidhi mahitaji yao. Huduma za *wheelchair* ni mpaka uhangaike kuulizia ulizia, nyenzo za kupandia na kushuka kwenye ndege ni adha tu.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu mazingira haya yataboreshwa lini? Hivi Serikali inashindwa vipi kuiga mambo mazuri toka nje ambako viongozi nina uhakika wanayaona wanapofanya ziara huko?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara imeeleza mipango mingi katika hotuba yake kuhusu uchukuzi nchini, natoa rai kuwa mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu yazingatiwe kikamilifu katika *programme* zote. Kwa mfano, kuna umuhimu wa kutoa mwongozo kwa wasafirishaji abiria iwe meli, ndege, au magari kuzingatia haki ya kumwezesha mwenye ulemavu kupanda na kushuka katika vyombo hivyo; kuwa na wahudumu maalum wa kuwahudumia na kadhalika. Nashauri hivyo kwa sababu hivi sasa baadhi ya wasafirishaji abiria nchini wanakataa kuchukua abiria wenye ulemavu kwenye vyombo vyao vya usafiri wakidai kuwa ni mizigo.

Mheshimiwa Spika, ifahamike kuwa safari salama na ya raha inahitajika kwa kila binadamu na wenye ulemavu wakiwemo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, nitaunga mkono hoja, baada ya kupata maelezo ya nia ya dhati ya kutekeleza ushauri wangu.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika, Reli ya Tazara iboreshwe. Imesahaulika sana na hivi sasa ufanisi unaotolewa na reli hii umepungua sana. Wizara kwa kushirkiana na uongozi wa Tazara ukae na kufikia muafaka wa namna bora ya kuboresha huduma ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Chindile Wilayani Kilombero hawana njia nyingine yoyote ya usafiri isipokuwa wa reli. Napendekeza huduma za *vischoma* pamoja na viberenge vifanye huduma ya kusafirisha wakazi hao kwa maeneo ya karibu na hapo.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa reli, wanaodai pesa zao za mafao, posho na kadhalika wafanyiwe utaratibu walipwe stahili zao.

Mheshimiwa Spika, ni aibu mpaka leo miaka 50 ya Uhuru Taifa halina ndege hata moja.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la kutoa mizigo bandarini. Hivi sasa kutoa magari imekuwa ni ishu. Wizara itupie macho upya suala hili.

MHE. RAYA I. KHAMIS: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba hii katika maeneo tofauti tofauti katika hotuba hii ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na matatizo mengi katika bandari zetu. Bandari ya Dar es Salaam ina kero kubwa kwa wasafiri wake hususan watoto, wazee, na walemavu na hata wengine kwa kuwa na ngazi nyingi ambazo ni kikwazo kwa wasafiri. Serikali iangalie hili.

Pia ukaguzi/*searching* kwa abiria, leo hii tunajiandaa kusherehekea miaka 50 ya Uhuru lakini cha kusikitisha ni kwamba hakuna teknolojia inayotumika kwa kukagua wasafiri na badala yake kufunguliwa mabegi yao. Hii ni aibu, tunaomba hali hii itafutiwe ufumbuzi kwa haraka.

Pia katika upande wa maziwa, pia kuna usafiri ambaao umechoka, upo toka mkoloni mpaka sasa ambaao ni *MV Liemba*. Naomba Serikali iachane na usafiri huu na kuleta unaostahili kwa sasa. Pia tunataka kujua kuna mpango gani katika kuboresha usafiri huu? Au tunasuburi ajali itokee ndipo tuweke minara ya historia kwa kupoteza roho za Watanzania?

Vile vile tunaiomba Wizara ifikirie abiria wote wanaoelekea Visiwani Unguja na Pemba kwa kuweka boti ambayo itakuwa nafuu ukilinganisha na iliyo sasa, kwani gharama za usafiri ni kubwa kwa kutumia vyombo vya usafiri vya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hii hakuna ndege hata moja ambayo inasafiri kutoka nchini kwetu, lakini cha ajabu na cha kushangaza, watumishi bado wanalipwa mishahara na wanapata huduma zote kana kwamba bado wanawajibika na kazi. Huu ni mpango mbovu ambaao unaonyesha matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa kuwalipa watu ambaao wanafanya kazi hewa. Serikali na Wizara iangalie hili.

Pia napendekeza viwanja vyetu vya ndege viboreshwe na vitumike ili kuongeza pato la Taifa letu, mfano kiwanja cha Mwanza kuwa cha Jumuuya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, *TRC* ililikabidhi *TRL* injini 79 na mabehewa ya abiria 97 na mengi ya mizigo na badala yake kwenda kukodi mengine India kuona yetu hayafai na hatimaye kufilisi na kuiweka pabaya. Lakini lengo la Serikali siyo hivyo, bali lengo lilikuwa ni kuendeleza usafiri huu. Siyo hivyo tu, pia Serikali ilitegemea kuwekeza kwenye *TRL* na baadaye kumilikiwa na *RITES* ambapo ilikuwa na 51% vile vile wafanyakazi wengi waliondolewa kazini.

Mheshimiwa Spika, pia baya zaidi wafanyakazi hao walioondolewa kazini, kuna ambaao wamelipwa kiinua mgongo zaidi ya wenzao, kwani nina ushahidi wa *documents* ambazo zinaonyesha malipo, wengine wamelipwa Shilingi milioni 20 na wengine Shilingi milioni mbili na kidogo, jambo ambalo halionyeshi usawa. Kwani mionganoni mwa walipata kiinua mgongo kidogo ni watumishi wa muda mrefu katika shirika hilo ukilinganisha na walolipwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali kushirikiana na Wizara hii iwapatie haki zao na kuwalipa wanavyostahiki, kwani kutokufanya hivyo hakuonyeshi haki kwa wastaafu/watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, vile vile hakuna reli, lakini cha kushangaza, nao watumishi waliopo wanalipwa na kupata huduma zote kana kwamba bado wanalitumikia Shirika la Reli. Huo pia ni mfumo mbovu wa matumizi mabaya ya pesa kwa kuwalipa watu wanaofanya kazi hewa.

Mheshimiwa Spika, Tunataka kujua hatma ya *UDA*, kwani kwa mahojiano ya Kamati ya Miundombinu na Mkurugenzi wa *UDA* inaonyesha kwamba kuna mali za *UDA* zinauzwa kiholela, yaani bila mpangilio maalum na bila taarifa yoyote kwa Mkurugenzi. Pia hakuna hata gari moja inayotembea *share/hisa* za *UD*, pia hazieleweki ni kwa vipi *malloted share* kuuzwa, yaani *share* za Serikali kuuzwa bila ya watendaji wengine na *CHC* kushirikishwa. Tunaomba hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna kiwanja ambacho kimeuzwa na kina hati tatu za umiliki wa kiwanja hicho, jengo la ghorofa mbili kuuzwa kwa bei ya kutupwa na shirika la *UDA*. Sasa tunaitaka Wizara isimamie mali zote za *UDA* zilizouzwa kiholela zirudishwe na wenyewe kurudishiwa pesa zao, kwani kufanya hivyo kutapelekea kufufua *UDA* na kutokuwa na haja na kubinafsisha. Kwani kuna taarifa ya kuwa shirika hili linadaiwa, lina deni kubwa na hata kufikia kuingiza mamilioni ya pesa katika akaunti ya mtu binafsi badala ya kuingiza katika akaunti ya *UDA*. Je, pesa hizo zimetumika vipi?

Mheshimiwa Spika, tunaomba kujua, lakini kwa kurudisha mali zake kutapelekea kupunguza madeni na kufufuka kwa Shirika la *UDA*.

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Waheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuwasilisha bajeti hii nzuri pamoja na matatizo makubwa ya kifedha yaliyozunguka Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itufikirie sisi wananchi wa Kaliua ambao hatimaye tutakuwa Mkoaa wa Katavi, na kwa hiyo, shughuli zetu nyingi kuelekezwa Mpanda Makao Makuu ya Mkoaa wa Katavi, tuwekewe behewa moja maalum la kwenda Mpanda na kurudi Kaliua. Pia ni muhimu treni ya Mpanda iwe na behewa la *First Class*.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ituongezee urefu wa *air strips* yetu ya Kaliua ili iweze kumudu ndege za ukubwa wa wastani. Kaliua imezungukwa na mbuga za wanyama ambazo kuna vitalu vyta uwindaji kwa hiyo, kiwanja hicho kitakuwa na manufaa kwa uchumi wa nchi na kuvutia watalii na wawindaji.

Mheshimiwa Spika, Kaliua iko karibu na ndege adimu duniani anayeitwa Statonga. Watalii wa kundi la "watazama, ndege" hupenda kuja huku Tanzania ili wawaone. Ndege huyu ni hazina kubwa kwetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuchangia. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumshukuru Mungu kwa neema yake kubwa ya uhai na uzima kwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa maeleo ambayo ametoa asubuhi hii ya tarehe 4 Agosti, 2011. Nampongeza kwa hekima, burasa na ujasiri katika hutuba yake fupi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti hii, pamoja na kuongezwa fedha, lakini bado hazitoshi. Mimi nashauri Serikali iangalie miradi muhimu ambayo kwa sasa haifanyi kazi. Wananchi wanapata taabu sana, Serikali inakosa mapato.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri Serikali iangalie Reli ya Kati kwa kuboresha injini, mabehewa na barabara ya reli. Serikali iboreshe maeneo yote kuondoa usumbufu na kupata usafiri wa hakika.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ipanue bandari zetu hasa Dar es Salaam ili kuondoa msongamano wa mizigo tukiondoa msongamano. Mizigo ikishushwa kwa haraka wateja wengi watapenda kutumia Bandari zetu. Kwa hiyo, tungemudu ushindani wa biashara na Serikali ingepata pato zuri.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo ni muhimu sana, usafiri wa ndege ambao unaonekana unasuasua, Shirika la ndege ambalo limeanza na ndege 14, muda huu ambao nazungumza hakuna ndege hata moja ambayo inafanya kazi. Utakuta hapana ndege, lakini shirika lipo, wafanyakazi wapo na wanalipwa na Serikali. Hii ni hasara.

Mheshimiwa Spika, naomba shirika hili liangaliwe vyema uongozi wake wote. Kama si hivyo itakuwa mara zote ni mizigo kwa Serikali kuongeza fedha kila mara, lakini hamna ufanisi kwa Taifa. Ni hasara.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni lazima uwepo usimamizi mzuri katika nyanja zote za utendaji. Ukitokea uharibifu wa mali, basi wahusika wawajibishwe pasipo ubaguzi wala upendeleo.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza viongozi wa Wizara ya Uchukuzi kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na kuwa na changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo yamenifanya nipunguze nguvu ya mchango wangu wa leo, niunge mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nitaendelea kusitiza juu ya kusimamia Reli ya Kati. Reli ya Kati ni muhimu sana kwa sisi wakazi wa Mpanda na Rukwa. Uwezo wa wananchi wa maeneo hayo ni mdogo, hawawezi kukabiliana na gharama za usafiri wa mabasi, hivyo tunaomba reli ifufuliwe, itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, shirika la reli lifufuliwe. Ni aibu nchi kama Tanzania kukosa hata ndege moja pamoja na madini yote yaliyopo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa niaba ya Serikali Kuu kutoa kauli ya marekebisho juu ya ongezeko la Bajeti ya Wizara hii na hivyo kurejesha kwa kiasi imani ya Waheshimiwa Wabunge juu ya hoja ya Wizara. Pamoja na hayo, sasa napenda Mheshimiwa Waziri asaidie kutoa kauli juu ya ujio wa Mheshimiwa Waziri wa Sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano kutoka Uganda, aliyekuwa mwezi uliopita hapa Tanzania na Bungeni Dodoma juu ya ushirikiano kati ya Tanzania na Uganda juu ya ujenzi na ukarabati wa reli kutoka Tanga – Arusha – Musoma ili kuitisha mizigo ya Uganda kutoka Bandari ya Tanga. Nini kimejadiliwa? Nini kimekubaliwa? Nini mkakati wa utekelezaji wake?

Mheshimiwa Spika, katika mkakati wa kulipia madeni ya Ndege za ATC/ATCL nje ya nchi, tunaomba pia Mheshimiwa Waziri asaidie kutoka mwelekeo ya makakati wa kulipa madeni ya service za ndege nje ya nchi na kuonyesha mkakati wa urejeshwaji haraka wa ndege hizo.

Mheshimiwa Spika, haitoshi kwa Serikali kuchukua madeni na kucheleva kulipa madeni hayo na hivyo kucheleva kurejeshwa ndege hizo na kuzuia riba juu ya madeni yaliyopo. Je, hili linatekelezwa vipi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya China iliyonunua ndege kwa ajili ya ATCL, Mheshimiwa Waziri atueleze Kampuni ya China iliyotununulia ndege na kuwa na makakati wa kuwekeza zaidi, ndege hizo ziko wapi? Je, zile zilizokuwepo kwenye mpango wa Kampuni hiyo sasa zimefutwa au vipi? Nini kimesitisha mpango huo kati ya Tanzania na China/kampuni hiyo ya China.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba mikataba ya ukodishaji ndege imechangia sana kuvuruga mapato na matumizi ya ATCL? Je, ni kweli ATCL inakodisha ndege na kulipia gharama za ukodishwaji pamoja na gharama za service za ndege iliyokodishwa? Je, ni gharama gani ATCL imeingia kwa matengenezo/service za Airbus? Je, gharama hizo zinalingana vipi na Mapato ya Ndege hiyo kwa muda ilipoanza kazi hadi kwenda service?

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa ni mgeni katika Wizara hii mpya, basi atafute na kusoma ripoti ya Kamati ndogo ya Bunge iliyoundwa chini ya Mheshimiwa Kaboyonga (aliyekuwa Mheshimiwa Mbunge wa Tabora mjini) ili kuongeza uelewa wa ukweli wa hali mbaya ya Shirika la ndege Tanzania, Mkataba wake na Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kuomba dua, hoja hii iendelee kuungwa mkono.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi ina umuhimu sana na majukumu yake ni mazito, hivyo Serikali ina wajibu wa kuitengea mafungu ya fedha ya kutosha. Baadhi ya majukumu ya Wizara hii ni:-

- Kuhakikisha reli inaimarika na kufanya kazi vizuri, ili mizigo na abiria waweze kusafiri kwa gharama nafuu. Kutetereka kwa Reli ya Kati, usafirishaji wa bidhaa/mizigo – vifaa nya ujenzi, mafuta ya *diesel, petroli* umekuwa wa shida na kusababisha bei za bidhaa hizo kupanda sana. Aidha, kwa kuwa bidhaa hizo zinasafirishwa kwa barabara, barabara hizo zinaharibika upesi:-

- Kuhakikisha tunakuwa na ndege, Shirika la Taifa lenye ndege imara zinazobeba nembo ya Taifa.

- Kujenga na kusimamia uendeshaji wa viwanja nya ndege. Napongeza mpango wa ujenzi wa viwanja nya ndege, lakini viwanja tu bila ndege inatosha?

Mheshimiwa Spika, tunashukuru uwanja wa ndege wa Bukoba utaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, Wizara ya Uchukuzi itasaidia vipi Manispaa ya Bukoba kujenga barabara mbadala ya ile iliyolazimika kufungwa kupisha upanuzi wa uwanja? Barabara inayotumika sasa kuelekea maeneo ya Kashai hadi Kahororo, Kashai kwenda Nyamukazi ni nyembamba na inapita katikati ya majumba ya watu na kusababisha ajali mara kwa mara.

Mheshimimwa Spika, miaka kadhaa iliyopita, Serikali ilitambua eneo la Kajunguti Wilayani Missenyi kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege, na wananchi wamezuiwa kufanya maendelezo katika eneo hilo pamoja na kwamba Serikali haijawalipa. Wananchi wanaauliza, ni lini atalipwa fidia? Aidha, tunauliza, ujenzi wa uwanja huo utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, *MV Victoria* ni mzee, kwa hiyo, utendaji wake ni wa kususua (*on and off*). Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi aliahidi kwamba meli mpya itanunuliwa ili kuboresha usafiri wa watu na mizigo ukizingatia kwamba *MV Bukoba* iliyozama mwaka 1996 iliacha pengo kubwa. Ni lini meli hiyo itanunuliwa?

Mheshimiwa Spika, tunashukuru maelezo ya Waziri Mkuu na fedha Shilingi bilioni 95 itakayoongezwa bado ni ndogo, haitakidhi, lakini angalau.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na wadau wa uchukuzi kwa kazi ngumu ya kuandaa bajeti. Poleni sana.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa sababu mtihani unaotokea ni matokeo ya matatizo ya muda mrefu ambayo yamelundikana kwa pamoja kwa muda mrefu na matokeo ni kushindikana kwa kuitisha kwa vizuri bajeti yetu leo.

Mheshimiwa Spika, hali ya Shirika la Reli ni tete sana kiasi cha kutia huruma. Shirika la Reli limekuwa tatizo tokea pale walipoweka mbinafishaji wa kwanza ambaye alivuruga sana na mpaka sasa hali ya Shirika la Reli ni tete sana.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati ni kiungo muhimu sana kati ya Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Tabora, Mwanza na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, naomba reli hii iwekewe mkazo sana na pia iendeshwe kibiashara zaidi. Tatizo la kubebesha mzigo Serikali kwa kushindwa kulipa wafanyakazi wake mishahara, hatua hii ni tatizo, wanafilisi Serikali yetu. Ushauri wangu kwa Serikali yangu makini ya Chama cha Mapinduzi, tutafute mwekezaji mzuri wa Kimataifa mwenye uwezo, tuingie naye Ubia wa uendeshaji wa reli hii, tupunguze mzigo kwa Serikali. Hali kadhalika, kwa Kampuni ya Ndege ATC nayo tufanye hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nichangie katika eneo la bandari zetu. Mamlaka ya Bandari nayo bado hajakaa vizuri. Bandari ya Dar es Salaam imejaa mlundikano wa magari na mizigo mbalimbali. Ni vyema basi tukazijengee uwezo Bandari za Lindi, Mtwara, Tanga na Mafia. Kujengewa uwezo kwa Bandari hizi itasaidia sana katika kupanua uwezo wa nchi kibiashara, kukuza uchumi wa nchi na hasa katika Sekta ya Utalii, Madini, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie juu ya Bandari ya Dar es Salaam ambayo iko katika Mkoa wangu.

Mamlaka ya Bandari tunaiomba ipokee ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwa kutufungulia milango ya kuja kuangalia utendaji wa kazi. Bandari ya Dar es Salaam inatoa huduma kwa wananchi ambao sisi wametupigia kura. Tunapopata taarifa yoyote inabidi tuifanyie kazi. Upande wa *Dar es Salaam port* kidogo viongozi wake wanapatikana. Lakini Bandari Makao Makuu ni tatizo, hakuna mapokezi. Sijui kama Mkurugezi anajua kuwa kuna tatizo Makao Makuu?

Mheshimiwa Spika, nikikariri maeneo ya Rais wetu - Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, "Viongozi wote tufanye kazi kwa ushirikiano na tuwe wawazi." Mimi sioni kama kuna ushirikiano kati ya viongozi na jamii inayozunguka Bandari hii.

Mheshimiwa Spika, kama Mbunge anashindwa kuwasiliana na kupokelewa: Je, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Kurasini, Bandari atapokelewa? Mganga Mkuu Kliniki ya Kurasini, Bandari atapokelewa?

Mheshimiwa Spika, naomba watambue Mamlaka ya Bandari iko Wilaya ya Temeke na inalindwa kwa kiasi kikubwa na wananchi wa Temeke – Dar es Salaam. Sina imani kama mamlaka hii ambayo inaingiza mapato makubwa wameshiriki vipi katika kuchangia miradi ya maendeleo ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hatupendi kusema Bungeni, lakini hatuna pa kusemea, wahusika hatuwaoni. Tunaomba ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, Temeke inaathirika kwa shughuli za uchukuzi wa malori ya mizigo na mafuta vyote vinatoka pale, japo mbele vinagawanyika kwenda sehemu mbalimbali, chanzo ni Temeke. Tunaiomba Serikali itujali na ituthamini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yenyeye ufanuzi mzuri juu ya masuala yote yaliyokuwa yanatutatiza, naunga mkono hoja. Yaliyosemwa yafanyike kwa maslahi ya Taifa letu. Ahsante. Naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, uchukuzi ni nyenzo kubwa ya kusafiri na kusafirisha ni jambo la kushangaza kuona usafiri wa reli, Bandari umetengewa fedha kidogo huku Wizara ya Ujenzi ikitengewa fedha nyingi sana. Tanzania ni nchi maskini ambayo wananchi wake wana kipato kidogo sana na kwa historia yetu walitegemea sana usafiri wa reli. Mfano, watu wa Kanda ya Ziwa na Nyanda za juu Kusini ikiwemo Mikoa ya Tabora na Kigoma, walitegemea zaidi

usafiri, kwani ndiyo miundombinu pekee iliyokuwepo ya bei nafuu na inayobeba watu wengi kwa pamoja na mizigo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika ni kukiuka kwa Katiba Ibara ya 17 kuwa kila raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayo haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano. Kama Katiba ambayo ndio sheria mama ya nchi, lakini inakiukwa kwa wananchi kushindwa kusafiri watakako kutokana na vikwazo vyta usafiri huku Serikali ikikusanya kodi.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa TAZARA na TRL wamekuwa wakipata mishahara midogo sana na hata stahili zao, hali iliyopelekea wafanyakazi kugoma mara kwa mara, jambo ambalo linazorotesha tija katika shirika. Pamoja na haya, kumekuwa na ubaguzi mkubwa sana na tofauti kubwa ya mishahara jambo linalowafanya wafanyakazi kuwa na makundi.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kaskazini ya kutokea Tanga hadi Arusha na ile inayoelekeea Voi – Kenya ilikuwepo, lakini cha kushangaza, reli ile ilikufa siku nyangi na matokeo yake mizigo mizito yote, *containers* yamekuwa yakipitishwa katika barabara ambazo zinajengwa kwa gharama kubwa sana, hivyo kuharibika haraka sana wakati reli hizi zingesaidia sana. Kuna viwanda vingi, lakini malighafi hizi zinakwama kutokana na kutokuweko kwa reli.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa ndege ni wa haraka na kutokana na sayansi na teknolojia ni aibu kuona nchi kubwa yenye raslimali nyangi kama Tanzania inashindwa kuwa na ndege ya Taifa. Tuliwahi kuwa na ndege nyangi, lakini uendeshaji umekuwa mbovu sana na wahusika hawakuchukuliwa hatua yoyote. Lakini cha ajabu, watu binafsi wanaendelea kuwa na ndege nyangi sana. Mfano, *Precision Air* ilianza na ndege moja, sasa hivi wana ndege kibao na hata kushirikiana na Kenya *Air ways*. Tunataka Serikali iache siasa na ifanye biashara, vinginevyo waachie wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi yenye bahati kubwa sana kutokana na jiografia yetu ya kuzungukwa na nchi sita zisizo na mlango wa Bahari “*landlocked countries*” ni kwa jinsi gani tunatumia fursa hii kuhakikisha nchi hizi mizigo yake inapitishwa kwetu? Ni kwa jinsi gani reli zetu zitaboreshwa ili watu wetu wasafiri na mizigo yao midogo na mikubwa iweze kusafirishwa?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hoja ya Wizara ya Uchukuzi kwa kuanzia na Bandari ya Dar es Salaam ambayo utendaji kazi wake ni wa kusuasua. *The service rate is just ridiculous*, hali inayoplekekea gharama kubwa kwa wafanyabiashara na wananchi ambaao wanaingiza bidhaa mbalimbali nchini kuititia bandari hii kwa gharama za demurrage ambazo ni kubwa sana na zingweza kuepukika. Ingawa Waziri katika hotuba yake kaeleza kuwa bandari sasa imeboresha huduma na kuwa mizigo, haikai sana bandarini.

Mheshimiwa Spika, ni juzi juzi tu *company* ya Tanzania *liquid storage* ambayo ni kampuni imara ya *Equatatorial Tarading* ya *Mauritius* ambayo inasimamia na *agent* wake ambayo ni *Southcommon East Africa*, waagizaji wa mafuta ya kupikia (*guide Palm Oil*) na *Crude degummed Soyabean oil* kutoka Mauritius na USA ambapo meli hukaa hata zaidi ya mwezi mmoja.

Mfano, meli ilioingia hapa nchini Bandari ya Dar es Salaam Mei, 2011 kueberth mwezi Julai na gharama za *dummarage* baada ya muda ambapo wenyewe meli hutoa baada *arrival/ku-expire* ni zaidi ya dola za kimarekani 20,000 kwa kila saa inayoongezeka. Sasa meli ikikaa zaidi ya mwezi, siku zaidi ya 30 ni sawa na siku 720, sasa ukizidisha na dola 20,000, ni sawa na dola 14,420,000, yaani ni zaidi ya Shilingi bilioni 30 za kitanzania. Hii gharama yote hupelekwa kwa mlaji wa mwisho, kwani waingizaji wa mafuta hawa akina *Murrah Oil*, *G & B Soap*, *Rest Twiga*, *East Coast Oil and Fat* na wengine wadogo wadogo ndio hulipa hii *demurrage* na hivyo kupeleka gharama zote kwa mlaji, kitu ambacho hufanya bei ya kuuzia kuwa juu sababu ya *production cost* kuwa juu vile vile. Cha kushangaza, huyu mwekezaji alijitolea kujenga *berth* kwa makubaliano kuwa wajenge kisha Serikali wawe wanakata katika malipo ya Serikali hadi deni liishe. Lakini cha ajabu walikataa kabisa kuchukua ofa hii na cha ajabu leo wanatafuta hela za mkopo.

Mheshimiwa Spika naomba kuwasilisha.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kusema naunga mkono hoja hii hasa baada ya Serikali kutoa kauli ya kuongeza fedha katika Wizara hii. Aidha, napenda kutoa maoni yafutayo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuondoa vikwazo vya biashara, vitokanavyo na ucheleweshaji wa mizigo iendayo nje, Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Ujenzi na wakala wa uwezeshaji wa biashara na uchukuzi kanda ya kati (*central corridor transit transport facilitation agency*) kuna mpango wa kuanzisha vituo vichache vitatu vya ukaguzi wa magari ya mizigo ya nje ili kuondoa tatizo la magari hayo kupambana na vizuizi vingi mno barabarani (mizani na *traffic check points*). Mipango hii ni muhumu sana lakini: Je, utaanza kutekelezwa lini? Ya fedha za kutekeleza mpango huu zimo katika bajeti ya mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati inao umuhimu wa kipekee katika kukuza uchumi wa nchi hii, kwani inahudumia nusu ya Mikoa ya nchi hii na nchi nne za Uganda, Rwanda, Burundi na *DRC*. Kwa hiyo, uwekezaji katika reli hii ni jambo la kufa na kupona. Bajeti ijayo uwekezaji uwe mkubwa zaidi kuliko bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, reli ya kati inayo michepuo mitatu. Mmojawapo ni mchepuo wa reli ya Manyoni – Singida. Kwa hiyo, matengenezo yafike katika mchepuo (matawi) hii. Katika bajeti hii shilingi milioni 200 zimetengwa kwa tawi hili la reli. Ni fedha kidogo, lakini zinaonyesha nia ya Serikali kuikomboa reli hii. Katika bajeti ijayo ningependa kuona fedha nyingi zaidi ili sehemu hii ya reli ikamilike na itoe mchango katika kuinua uchumi wa Mkoa wa Singida na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kuitakia kheri Wizara hii mpya katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla naunga mkono hoja hii.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza mikakati ya Serikali juu ya kuwezesha shughuli za uchukuzi hapa nchini mwetu. Lakini suala la kibajeti ndio ninaloliona na tatizo kubwa kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha hotuba, sijaona suala la bandari kavu ya Kisarawe. Je, Serikali inasemaje juu ya ujenzi wa bandari hii kavu ambayo itawezesha kupunguza mizigo katika bandari yetu ya Dar es Salaam? Naomba tamko la Serikali katika hili.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Omari Rashid Nundu - Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Athumanji Rashid Mfutakamba, Katibu Mkuu - Ndugu John Thomas Mgodo, Msaidizi wake - Ndugu Alphonse Mwingira kwa hotuba nzuri sana ambayo wameisoma hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naanza mchango wangu kuchangia tatizo kubwa linaloikumba nchi yetu katika Sekta ya Uchukuzi, ni ukosefu wa reli ya uhakika kutoka Dar es Salaam kwenda Bara. Sina uhakika kama kuna njama ya makusudi ya kuiua reli hii inayofanywa na wafanyabiashara wa barabara ili isifanikiwe. Reli ndiyo njia muhimu ambayo inaweza kupunguza gharama za bidhaa kwa Mikoa ya bara, lakini kwa jinsi inavyosuasua, kwa hakika inawafanya watumiaji wa vifaa vya viwanda na kutoka nje walioko Kanda ya Ziwa wawe na maisha ya ghali sana. Lakini pia wananchi au abiria wanaotegemea reli ni wale wanaoishi kwenye maeneo ambapo barabara haifiki. Sasa wafanyeje? Hata hivyo, Reli ya Kati pia inahitajika sana kwa biashara na uchumi wa nchi za ukanda wa Maziwa Makuu. Nasikitika kusema kuwa Tanzania tumeshindwa kabisa kuitumia vyema fursa hii tuliyopewa na Mungu?

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wamechoka kusikia mipango tu ya kwenye karatasi ambaya haitekelezwi kwa vitendo kufufua na kuimarishe reli ya kati.

Mheshimiwa Spika, nahitaji maelezo ya kutosha, kwa nini reli ya kati haiamuliki?

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa matengenezo ya uwanja wa ndege wa Mwanza. Hata hivyo, nashauri uboreshaji wa uwanja uendelezwe hasa katika maeneo yafuatayo:-

- (a) Maegesho ya ndege (*apron*) ili ndege nyingi zipate maegesho ya kutosha;
- (b) Eneo la abiria kupumzikia na kununua vitu mbalimbali na migahawa (*terminal buildings* lenye hadhi ya kimataifa); na
- (c) Eneo la kupitia wageni mashuhuri lenye hadhi ya uwanja wa kimataifa (*ripplounge*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja. Kwa sababu nia ni nzuri ya Serikali kuianzisha Wizara, bila shaka lengo ni kupata nafasi nzuri za kuzishugulikia changamoto, *thrust* hiyo pekee ni mwelekeo wa kuboresha miundombinu yetu ya meli, reli, ndege, bandari zetu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, sasa tuanzie na kiasi kilichopo na kile kitakachoongezwa kwa hutuba ya Waziri Mkuu. Changamoto za usafiri wa reli na matreni mabovu tulionayo, lazima zishughulikiwe. Usafiri wa reli ni rahisi kwa bei na inawasaidia watu wetu wa ngazi ya chini kiuwezo. Kumbe hatuna hiaru katika kushughulikia changamoto zao. *RITES* baada ya kuchukua huduma hii tu wameshuhudia mateso ya kila aina, si kwa watumishi wa Reli tu, lakini huduma sumbu kwa wananchi ilikuwa changamoto kubwa. Tuanze vizuri na lazima pawepo pa kuanzia, sasa Mheshimiwa Rais ameanza kwa kuunda Wizara hii, ni *thrust* njema.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nkasi Kusini takriban nusu ya wakazi wake wanaishi kandokando ya Ziwa Tanganyika, kumbe changamoto za usafiri wa majini zinawakabili kwa kiwango kikubwa. *MV Liemba* imezeeka na sasa inasafiri mara mbili tu kwa mwezi na hakuna chaguo lingine la usafiri na usafirishaji, zaidi ya maboti ambayo mara kadhaa yamegharimu maisha ya wananchi hawa. Kwa hiyo, naiomba Serikali katika mipango yake inunue meli mpya iliyopo, inaweza hata kuleta balaa lingine la ajali kwa uzee wake.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia vituo vya kusimama meli, viongezwe katika Jimbo la Nkasi Kusini eneo la Msamba Kata ya Ninde. Kuna idadi kubwa ya mizigo kwa sababu ni kituo kizuri cha uvuvi, na hapa wakati fulani meli zilikuwa zinatua Msamba, leo haitui wananchi wanaomba ianzie kutua hapo Msamba. Eneo lingine ni Mpasa Kata ya Kala ni Kijiji cha wafanyabiashara, tunaomba meli iwe inatua hapo.

Mheshimiwa Spika, Rukwa ni Mkoa wa wakulima wa mahindi na huzalisha ziada. Mahidi hukosa soko kabisa na huwezi kuyapeleka kwenye soko Dar es Salaam, Mwanza, Shinyanga kwa barabara na upate faida, haiwezekani. La muhimu hapa ni kuunganisha reli toka Mpanda hadi Tunduma. Reli hiyo ingeweza kuongeza sana thamani ya mahindi na ingewezekana kuza mahindi popote nchini ambako mara zote wanahitaji mahindi.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano na kwa kuzingatia uwepo wa Mpango wa *SAGCOT*, itakuwa na maana kubwa kwa ajili ya kuleta huduma za uchukuzi wa uzalishaji mkubwa wa bidhaa zinazotegemewa kuzalishwa kupitia mpango wa *SAGCOT*.

Mheshimiwa Spika, Wabadhirifu wa *UDA* na Ndege, naomba wachukuliwe hatua kali kama ikithibitika kuhusika na uchakachuaji.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Uchukuzi, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kujipanga upya kufanikisha shughuli ya uchukuzi nchini. Hata hivyo, kuna changamoto nyingi zinazoikabili Wizara hii kubwa na muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, siyo jambo baya kujenga Bandari mpya ya Bagamoyo hasa kwa sababu Bandari ya Dar es Salaam tayari ina mlundikano mkubwa wa bidhaa, urasimu mkubwa, lakini kama kupanga ni kuchangua. Kwa nini Serikali isizifufue Bandari za Tanga na Mtwara ili ziisaidie Bandari ya Dar es Salaam? Naamini kuanzisha Bandari mpya ni gharama zaidi kuliko kutengeneza bandari zilizopo.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa Watanzania walio wengi ni wa kutumia reli. Ni usafiri wa wanyonge ambao hapa nchini ndio wengi zaidi. Kwa nini reli hii bado haijafanya kazi vizuri? Tatizo la kubadilisha uongozi kwa kuweka *RITES* halikupata ufumbuzi wa *RITES*, sasa wanaondoka nchini. Lazima tujamini na tuweke viongozi wazalendo ambao watalipwa vizuri na watapewa motisha mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa ndege ni jambo la kusikitisha na kweli ni jambo la aibu kuwa nchi yetu haina ndege yake yenyewe ya abiria ingawa inayo ndege ya Rais. Lakini ni jambo linalotia unyonge zaidi kuwa tumewahi kuwa na ndege 11 zinazoruka na sasa hatuna ndege hata moja inayoruka.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tujiulize ni kwa vipi tumefikia hapa? Nani waliotufikisha hapa? Kama kosa ni la Watendaji, basi tuelezwe wachukuliwe hatua gan?

Mheshimiwa Spika, suala la usafiri katika Jiji la Dar es Salaam ni suala mtambuka, kwani pia unategemea kuwepo kwa barabara nzuri (au tuseme Wizara ya Ujenzi).

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam inahitaji usafirishaji wa abiria wa uhakika kupunguza msongamano wa magari ingawa Serikali haifanyi biashara, lakini inaweka mazingira mazuri ili wawekezaji binafsi wawekeze katika usafiri wa ndani wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Wizara hii inahitaji marekebisho makubwa ya kiutendaji na raslimali fedha ya kutosha ili usafiri wa angalu nchi kavu na baharini ufanye kazi vizuri na hiki kitakuwa ni kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi wetu.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya katika hali ngumu ya bajeti ndogo. Pili, niseme, uchukuzi, kilimo, elimu, nishati, barabara, madini ni sekta *very strategic* kwa uchumi wetu. Hivyo, inahitaji uwekezaji mkubwa na Menejimenti ya mashirika yake. Tatuhili, Tanzania tuna bahati ya kijigrafia ya kuwa na ufukwe (*coastline*) kubwa. Kwa hiyo, bandari ambazo zikiwa *well managed* tutakuwa na biashara nzuri na nchi ambazo ni *Landlocked* kama Zambia, Burundi, Rwanda na Uganda.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ninaloliona ni Menejimenti ya Mashirika ya Uchukuzi - *TPA*, Reli, *Air Tanzania* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mimi siamini *foreign management contracts*, watu hao hawana uchungu na maendeleo yetu. Tuteue vizuri Mameneja wetu kwa kuzingatia sifa, uzoefu na *background* ya mtu *trackrecord* nzuri halafu wapewe *management training* katika uongozi *institute* wapewe msasa wa uzalendo na uadilifu (*tergrity*). Mameneja wetu wanaweza wakipewa maslahi mazuri.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa nchi yetu kutokuwa na ndege zetu. Nchi ya Ethiopia ambayo ilikuwa nchi ya kijamaa nchini ya Menjistu Haile Mariam aliyekuwa Mkomonist lakini alikuwa na msimamo kuhusu *Ethiopian Airlines* alikataza siasa kuingilia Menejimenti ya ndege na sasa *Ethiopian Airlines* ina *compete* na ndege za wakubwa. Nchi ya Rwanda, nchi ndogo sana yenye watu milioni 10 tu, ina ndege tano, kubwa mbili na inazi-manage vizuri.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati imezeeka sana. Ikarabatiwe, ni reli muhimu sana kwa Mikoa mingi na pia kubeba mizigo ya nchi ambazo hazina bandari kama Burundi, Rwanda na Uganda. Reli hii ni muhimu sana kwa uchumi wetu kwa sababu tatu:-

- (i) Nchi itafaidika na kuwa na biashara nzuri na nchi za Burundi na Rwanda;
- (ii) Mikoa ya Shinyanga na Kagera - hasa Wilaya za Kahama, Biharamulo na Ngara zitafaidika sana kiuchumi kutokana na reli ya Isaka kwenda Burundi na Rwanda; na
- (iii) Reli hii ya Isaka itasaidia kubeba mizigo ya mgodi wa Kabanga *Nickel*. Kambanga *Nickel* ni mgodi wa pili kwa ukubwa duniani baada ya mgodi wa Nickel wa Canada. Kabanga *Nickel* ina utajiri mkubwa wa *Nickel*. Kwa hiyo, naomba tuchangamkie utajiri huo kwa kujenga reli ya Isaka – Keza – Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba nieleze kwa nini mimi naamini Watanzania wakiwa na uzalendo na wakapewa maslahi mazuri wanaweza kuwa Mameneja wazuri kuliko wageni ambao hawana uchungu na maendeleo yetu na hawajui mazingira yetu.

- Reli yetu iliwhali kuendeshwa vizuri sana na Marehemu Peter Bakilana;
- *Harbours* iliwhali kuendeshwa vizuri sana na Marehemu Peter Bakilana na Mbunge wa zamani wa Kisarawe;
- Shirika la Ndege la Tanzania iliwhali kuendeshwa vizuri na Bakari mwapachu na *Melixedec Sanare*;
- Shirika la *NBC* liliendeshwa vizuri na Marehemu Amon Nsekela; na
- Shirika la *N/C* liliendeshwa vizuri na Marehemu Mwaikambo wakati huo mimi nilikuwa Katibu wa *Scopo*.

Mheshimiwa Spika, msikimbilie *foreign managements*.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hasa baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutangaza ongezeko la Shilingi bilioni 95, Waheshimiwa Mawaziri nawapongeza, kwani hizo ni Wizara mpya. Natoa mchango wangu kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, tunayo malalamiko ya wananchi jinsi ambavyo wanauziwa tiketi kwa bei ya juu nje ya dirisha la kuuzia. Ombi langu ni kwamba Wizara ikemee tabia hii ya *station* ya Kigoma. Ushauri wangu ni kwamba Wizara isitumie mtindo wa kuridhisha Wabunge wa kila mahali kutengeneza viwanja vya ndege ila ijikite kuangalia vichache vitakavyomaliza kwa manufaa ya nchi yetu. Viwanja vya Tabora na Kigoma ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *UDA*, Uchunguzi ufanywe na Wizara iwajibishe watu watakaobainika na kuhujumu raslimali za *UDA*.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati ni kipaumbele cha Wizara, msifurahishe kila eneo;

Mheshimiwa Spika, mwisho, mawaziri waelewe kwamba mpo hapo kufufua vilivyokufa, hivyo, lazima muwe na kipaumbele cha kuanzia na siyo kufanya vyote.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Uchukuzi kwa hotuba yake. Lakini pia napenda kumpongeza Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa jitihada yao ya kuhakikisha Sekta ya Uchukuzi inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukuaji wa Sekta ya *gas* asili katika Mkoa wa Lindi na Mtwara au kusini mwa Tanzania, naishauri Serikali yetu Tukufu kuhakikisha kuutengeneza Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko ambao kwa sasa ni mdogo na haukidhi haja ya sekta hiyo kuwa kusini mwa Tanzania. Inasikitisha hata bajeti haikupangia matengenezo au upanuzi wa uwanja huo.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Kiwanja cha Kisiwani cha Songsongo kitengenezwe ili kiweze kutumika kwa wageni wanaokwenda kuangalia uchimbaji wa gesi. Pia naomba wananchi wa kisiwa hiki cha Songsongo wawekewe boti ya kisasa ambayo itakidhi mahitaji ya wananchi ambao wanapata taabu sana hasa wagonjwa, akinamama wajawazito na watoto hasa wanapoumwa magonjwa ya ghafla.

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia Serikali iwekeze katika eneo la Kilwa Masoko Kijiji cha Pande na Kilwa Kisiwani ambapo wananchi wa huko wanatumia usafiri wa boti za kienyeji tu ambazo ni mbovu, zinahatarisha maisha ya binadamu. Hivyo, naomba sana Serikali iangalie kuweka boti za kisasa kwenye visiwa hivi.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuishauri Serikali kuhamisha wafanyabiashara kuwekeza katika Bandari ya Tanga – Pemba – Zanzibar – Mombasa ni eneo kubwa na linaweza kuongeza mapato ya nchi na pia kuondolea wananchi usumbufu, kusafiri kwa eneo la masafa marefu kwa kutumia boti za kienyeji au jahazi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara kudhibiti bandari ya panya ndogo ndogo ambazo nydingi zinatumika kwa kupitisha magendo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuvunja mkataba na *RITES* waliokuwa wamewekeza Reli ya Kati. Nawapongeza Mawaziri Nundu na Naibu wake kwa usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwekeze katika reli nchini, Reli ya Kati, Reli ya Voi, Reli ya Tanga – Arusha. Reli inapunguza sana kero za usafiri. Bila usafiri thabiti uchumi hauwezi kukua.

Mheshimiwa Spika, Serikali mwaka 2010 ilitunga sheria ya *PPP* Serikali iangalie ni kwa namna gani *PPP* inaweza kusaidia hata kama kwa kuweka *Trans* katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Malaycia *Trans* zinasaidia sana kupunguza foleni mijini.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la ajali za barabarani kila leo maelfu ya raia wanakufa. Nashauri Serikali iwatakie Sumatra wafanye kazi zaidi. Chuo cha Usafirishaji, wakufunzi wawe *standby*, lakini *SUMATRA* iweke utaratibu kila dereva wa basi aende Chuo cha Usafirishaji kabla hajapewa ruhusa ya kuendesha *bus* la kubeba abiria. Inawezekana ajali zikapungua kwa sababu madereva watakumbushwa majukumu, lakini pia ndiyo wakati wa kujua madereva wanaofaa na wasiofaa, na hivyo kushauri *TRA* na wamiliki wa mabasi wasipewe leseni.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kuangalia upya tatizo la ajali barabarani kwa kupitia upya tatizo la ajali barabarani kwa kupitia upya ratiba za magari ya abiria. Mabasi yalikuwa yanasaferi mchana, yaani kuanzia asubuhi saa 12.00 mpaka saa 4.00 usiku. Sasa hivi Serikali imeruhusu mabasi yatembee usiku, ni hatari. Nashauri ratiba ya magari ya abiria kusafiri mchana, ianze upya. Usiku haushoni nguo.

Mheshimiwa Spika, zilitolewa amri nydingi na Kamanda wa Polisi aliyekuwepo akishughulikia *traffic* – *ACEP* Kombe kuwa magari ya mizigo *scania*, *Layland daf*, *Isuzu* yasibadilishwe kuwa mabasi ya abiria. Mpaka leo bado yanatumika. Nashauri Serikali ivalie njuga, mabasi ya abiria yawe kweli ni gari za abiria.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa amri mabasi yote yaweke milango miwili wa kutokea abiria, lakini kuwe na *emergency door*, mlango wa nyuma.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo, mabasi mengi yana mlango mmoja na hayana mlango wa nyuma (*emergency door*).

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, ili kufuata sheria na kanuni zilizowekwa, tutakuwa hakuna maendeleo. Ifike mahali wenyewe mabasi haya wafuate sheria zilizopo ili iwe salama kwa raia wa Tanzania wanaopanda magari hayo.

Mheshimiwa Spika, kiwanja cha Ndege cha *KIA* ni muhimu kiwe na mkataba mzuri wa kukiendeleza. Mwl. Nyerere aliona umuhimu wa kiwanja hiki. Katika Soko la Afrika Mashariki, *KIA* itatakiwa isiweze kupokea watalii wengi zaidi. Kuna haja Serikali iweke mkakati jinsi ya kuvutia ndege za nchi nyingine zitue *KIA* badala ya kutua Nairobi. Kenya wanajenga Kiwanja cha Ndege Holili mpakani na Wilaya ya Rombo. Nia yao ni kuleta watalii wa kupanda mlima Kilimanjaro na Hifadhi ya Mkomazi Same (Nyati weusi). Kuna haja ya Serikali iweke mkakati ili ushindani wa uwanja wa Holili usiwe mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kiwanja cha ndege cha Arusha pia kuna haja kiwekwe vizuri kibiashara. Ikumbukwe Makao Makuu ya Jumuuya ya Afrika Mashariki yatakuwa Arusha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LOESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii. Nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Wizara hii, yako mambo makubwa matatu ambayo ni ya muhimu sana katika kukuza uchumi wa kitaifa na uchumi wa wananchi wa kawaida. Mambo matatu hayo ni Reli, Bandari na usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, nikianza na usafiri wa reli, ninaweza kusema kwamba ni usafiri muhimu sana na ndiyo maana ukienda hata nchi nyingi zilizoendelea utakuta usafiri unaoaminika kutumika na wenye unafuu zaidi ni usafiri wa reli. Hata hapa Tanzania tukitaka kupunguza msongamano Dar es Salaam ni vyema tukaanzisha usafiri wa treni kutoka Dar es Salaam hadi Kibaha, Dar es Salaam - Bagamoyo kwa kuanza. Usafiri huu unabeba watu wengi kwa mara moja, hiyo kuondoa msongamano wa watu walio wengi wenye kusubiri usafiri. Kwa sasa Dar es Salaam hali ni mbaya sana. Tusipokuwa na maono makubwa ya kuleta mageuzi katika Sekta ya Usafirishaji katika miaka ijayo hali itakuwa mbaya zaidi. Nazidi kusisitiza Reli ya Kati iimarishe. Kupitia Reli ya Kati kutarahisisha usafirishaji wa mizigo mizito kutoka bandarini kwenda Mikoa ya Kati, Kanda ya Ziwa na kanda ya Magharibi na Mikoa ya jirani ya Rwanda, Burundi na Uganda.

Mheshimiwa Spika, katika usafiri wa anga ni vyema ndege ya Taifa *ATCL* ifufuliwe na niombe Menejimenti itakayoteuliwa kuongoza Shirika hili iwe makini. Mimi inanisikitisha sana kuona Shirika la Ndege la Taifa linakuwa halifanikiwi. Wakati wanaofanya kazi katika mashirika yote mawili wanakuwa ni Watanzania. Pengine ipo haja ya kuangalia mfumo mzima wa uendeshaji ndani ya Shirika la Ndege la Taifa. Unatakiwa uwe wa kibiashara zaidi. Kama hakuna (*performance*), uwajibikaji ni muhimu, hatua muhimu zichukuliwe mapema kabisa kabla hali hajawa mbaya zaidi. Uongozi wa juu wapelekwe wakajifunze kwenye mashirika mengine makubwa namna ya kuendesha kwa faida.

Sambamba na hilo, kiwanja cha ndege cha Mwanza naomba kiimarishe kabisa. Kwa miaka iliyopita, kumekuwa na ahadi hewa kwamba Kiwanja cha Ndege kitaimariswa, lakini mpaka sasa hakuna chochote kinachoendelea. Naomba sasa katika bajeti ya mwaka huu Serikali ihakikishe kuwa ahadi inatimia katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Bandari zetu ni vyema Serikali ikaboresha na kuimarishe Bandari zetu zote katika ukanda wa Bahari na Ukanda wa Maziwa. Kwa upande wa Ziwa Victoria ninaomba Bandari ya Mwanza iboreshwe zaidi na kwa sababu meli iliyopo kwa sasa ni *MV Victoria* pekee ambayo inasafirisha abiria Mwanza - Bukoba. Kwa kuwa ni meli moja tu, kumekuwa na tatizo la usafiri na usafirishaji wa mizigo toka Mwanza - Bukoba ambapo pia na watu wa nchi jirani za Uganda walikuwa wakitumia meli hizi. Ni ombi kwa Serikali iangalie uwezekano wa kununua meli mpya ku-replace meli iliyozama ya *MV Bukoba*. Hii pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais katika Mkoa wa Mwanza. Hata kama siyo bajeti hii ya mwaka huu wa fedha inaomba Wizara iweke kwenye mipango yake ya miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache. Naunga mkono hoja.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa sana ya uendeshaji wa Bandari ya Kigoma. Napenda kujua zabuni ya kupata *operator* mpya itatoka lini na kama kwa muda fulani *TPA* wanaweza kuiendesha Bandari hii ili iweze kurejea hadi yake.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bandari ndogo ya Kagunga Mkoani Kigoma umefikia wapi na utakwisha lini? Utaratibu gani utatumika kuiendesha?

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kupata nyongoza ya bajeti. Nawatakia kila la kheri katika kazi.

Mheshimiwa Spika, Chinese *loan to build berth 13 na 14 uangaliwe upya*. Tangaza zabuni *internationally*.

MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naanza kusema kuwa mimi siungi mkono bajeti hii hadi nione utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa tamko la Serikali kuhusu mjadala wa hotuba ya Wizara hii unaoendelea katika Bunge lako Tukufu. Nami napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Usafiri Dar es Salaam (*UDA*) japokuwa Serikali leo imetoa tamko kuwa imemwelekeza CAG kuanza kufanya uchunguzi wa haraka kuhusu shutuma za waziwazi kwa wahusika waliohujumu *UDA* kwa kununua na kuuza hisa kinyume na sheria na kanunua za nchi yetu, lakini nami natoa ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchunguzi huu ukamilike kwa haraka na mrejesho uje Bungeni ili wananchi wa Tanzania walioiweka madarakani Serikali ya CCM waweze kunufaika na raslimali za Tanzania. Siyo akina Mheshimiwa Kapuya, Idd Simba na wenzao wanyonyaji wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *UDA* ni ukombozi mkubwa sana kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakiwemo wanafunzi wanaoteseka kwa huduma za usafiri kila siku wanapokwenda na kurudi kutoka mashulenii na hawa ni watoto wa maskini, sio hao wa vigogo wanaosoma *International School* na nje ya nchi. Tunaiomba Serikali ichukue hatua kama ilivyotuahidi leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa fedha, Shilingi milioni 95 zilizotolewa na Serikali zitumike kama ilivyokusudiwa. Nidhamu ya matumizi ya fedha hizi lazima izingatiwe, vinginevyo mwakani tutahoji tena matumizi ya pesa hizi kama ilivyo kawaida yetu kupita kelele bila utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kujenga magari katika Bandari za Mafia na Lindi yakikamilika yatakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa Watanzania wanyonge, na maskini wanaoishi katika Mikoa ya Pwani na Lindi ili nao wajikwamue kiuchumi na wasiendelee kuitwa maskini wa kujitakia kwa uvivu, kwani Serikali ya CCM imewaacha kwa muda mrefu na ndio imewasababishia umaskini huu uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, Usafiri wa Anga siyo maarufu sana kwa Watanzania walio wengi, kwani unaonekana kwamba una gharama kubwa sana na pili kuna Mikoa michache tu ambayo ina viwanja vichache vilivyo chakaa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye Sekta ya Anga ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ikaribishe wawekezaji zaidi katika eneo hili na hasa yale makampuni ya nje ambayo yana uzoefu mkubwa katika kutoa huduma za haraka kati ya mji na mji (*shuttle service*). Makampuni haya yanatoa huduma za usafiri wa anga kwa gharama nafuu sana kiasi kwamba huduma zao zinavuta wa aina zote wakiwemo na wananchi wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichambue kwa makini gharama za usafirishaji wa anga na hasa bei za mafuta ya ndege kwa nia ya kuangalia jinsi ya kuzifanyia marekebisho yenyenye lengo la kushusha gharama za uendeshaji na kwa abiria. Ahsante.

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii kama nilivyoandika hapo juu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuanza kuchangia kwa kuzungumzia suala la ujenzi wa Viwanja vya Ndege hapa nchini. Kumekuwa na kutokujipanga au kuchagua wapi papewe kipaumbele zaidi kuliko sehemu nyiningine katika ujenzi wa viwanja hivi.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita nililiza swalii la msingi juu ya zao au kilimo cha maua waridi hapa nchini ambacho kinafanya zaidi katika Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Kilimo hiki au zao hili linauzika au soko lake liko nje zaidi katika Jiji la Amsterdam. Kwa hiyo, ni lazima usafiri wa ndege utumike katika kufanikisha mkulima anapata faida. Lakini shida kubwa inakuwa ni usafiri huo ambaa umekuwa kigugumizi, kwani ndege za mizigo kubwa hazitui katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa KIA.

Mheshimiwa Spika, ndege kubwa inayotua KIA ni KLM na ina-deal zaidi na abiria na mizigo yao ya maua haya yanasafrishwa kwa kiwango kidogo sana, kwani siyo ndege ya mizigo. Kutokana na hilo, inabidi mizigo ya maua isafirishwe kuitilia Uwanja wa Ndege wa Jomo Kenyatta nchini Kenya. Hii imekuwa ikiwasumbua sana wafanyaabiashara wa maua na pia hela nyangi imekuwa ikiingia nchini Kenya kwa sababu uwanja wao ndiyo unaotumika kwa kuwa ndege za mizigo nydingi zinatua nchini humo na takribani *cargo flights* 13 kwa siku tofauti na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sababu zinazotolewa na Wizara hii, kwanini ndege kubwa za mizigo hazitui katika uwanja wa KIA? Ni ushuru mkubwa unaotozwa na uwanja huo wakati wa kutua na kuondoka ndege au kulaza pia. Vile vile eti hakuna mizigo ya kutosha ya kuchukua na kushusha kwa kweli kwa sababu hizi ambazo zinaweza kurekebishiwa sidhani kama viwanja vyetu vya ndege vitaendelea na tutaendelea kuachwa nyuma na wenzetu mfano Kenya katika usafirishaji wa anga.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa uwanja wa ndege wa Taveta Kilometra saba, kutoka nchini Kenya unakwenda kuua soko la Uwanja wa KIA kabisa, kwani wageni wote watatumia uwanja huo kwa sababu kutakuwa na ndege nyangi zitakazotua kama ilivyo kwa Jomo Kenyatta na ikiwemo na ndege za mizigo. Hii italeta athari katika soko la utalii hapa nchini, kwa mfano kwa sasa 50% ya wageni toka nje (Ulaya, America, Japan na Asia na Kadhalika) wanatua Jomo Kenyatta na wanalala hoteli za Kenya, kisha wanakuja nchini Tanzania kwa magari. Hii ni kwasababu usafiri wa ndege wa chini ya Kenya ni rahisi, tofauti na Tanzania inasababishwa na tozo za kodi kubwa zinazotozwa katika viwanja vyetu.

Mheshimiwa Spika, naomba ufanyike mkakati maalum wa kufanya KIA iwe competitive. Au kama hatuwezi tufunge mipaka.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa reli ni muhimu sana, mfano reli iliyokuwa inapita Tanga hadi kukutana na Reli ya Kenya ingesaidia sana usafirishaji wa mizigo ikiwemo maua waridi ambayo ni lazima yasafirishwe kwenda Kenya ili yaweze kusafirishwa katika ndege za mizigo kwa kuwa hazitui katika uwanja wa KIA. Vilevile barabara zetu zimekuwa zikiharibika sana kutokana na mizigo mikubwa inayopakiwa katika malori na magari makubwa kuelekea nchi jirani mbalimbali kama Congo, Burundi, Rwanda, Zambia, Malawi na kadhalika. Naomba ujenzi wa reli uanzishwe na upewe kipaumbele ili kunusuru barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, treni hii kutoka Tanga ikipakia cement behewa 15 kupeleka Arusha: Je, huoni ni bora kufufua treni kwani ni sawa na kusafirisha cement hiyo kwa kutumia lori tatu? Hata bei ya cement itapungua kutoka Sh. 12,000/= instead of 12,000/=.

Mheshimiwa Spika, hii inaonekana kama kuna sintofahamu inayoendelea baina ya wenye malori hayo na baadhi ya watu Serikalini na ndio maana azma nzima ya kufufua reli hizi imekuwa

ikikwama au kukwamishwa. Naomba Serikali iliangalie hili kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na siungi mkono hoja.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ofisi kwa mwaka 2011/2012 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Omari Rashidi Nundu – Waziri wa Uchukuzi kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilimu na moyo wa kujitolea sana kiutendaji. Huu ni mfano wa kuigwa kwa maana hachoki na amekuwa mstari wa mbele katika kulitetea Taifa letu. Lakini siachi kumpongeza Naibu Waziri Athumani Mfutakamba kwa uwezo mkubwa aliuonyesha kwa kipindi kifupi tu ambacho ameingia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu, Wizara hii ni kiungo na roho ya uchumi wa nchi yetu katika nyanja ya usafirishaji. Hivyo majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekelezaji. Ni kheri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kurahisisha utendaji wao. Ni vyema ikumbukwe, siyo haki hata kidogo tukawabebesha matatizo waliyoyakuta kwa maana utendaji wao ni kipindi cha mlezi isiyozidi kumi. Tuwape nafasi illi tuje kuwahukumu kwa utendaji wao au kwa mabaya yao maana lawama tu hazijengi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba kubeba karibu kila kitu na kujibu hoja nydingi, napenda nami nitoe mchango wangu katika hotuba husika japo kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, naanza na Bandari. Ipo haja tukamaliza tatizo la Bandari ya Dar es Salaam kwanza kwa kuboresha miundombinu iliyopo maana haitumiki ipasavyo na kumekuwa na urasimu usio na lazima. Tuige mfano kwa maeneo ya nchi jirani ama nchi nyininge duniani kwa kuweka pamoja taasisi zote zinazohusika na utaratibu wa utoaji mizigo kwa mfano, (*TBS, TFDA, TRA, TSCAN, Shipping lines, Mionzi*) kwa kuanzisha *on stop center* ili kurahisisha utoaji shehena bandarini. Izingatiwe taasisi hizi zipo mbali sana na huchukua muda mrefu kukamilisha taratibu zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari, pia naishauri Serikali ifikie haraka uamuzi wa uanzishaji wa bandari Mwambani Tanga kwa maana ni jambo ambalo limekuwa kwa muda mrefu na halijapata majibu. Mradi uanze tu kwa kushirikiana na wawekezaji. Lakini pia lipo tatizo la ucheleweshaji wa upanuzi wa Bandari ya Mtwara ambayo imekaa bila ya kufanya kazi stahiki huku Bandari ya Dar es Salaam ikiwa imezidiwa na mizigo. Kwa nini tusihamishie shughuli nyininge katika bandari hii ambayo itasaidia pia kuinua uchumi wa maeneo ya kusini?

Mheshimiwa Spika, napongeza jitihada zote zinazofanywa na Serikali katika kutatua tatizo la reli pamoja na kuvunja mkataba na mwekezaji (*RITES*), ila nasisitiza Serikali ifike wakati tujiamini na kazi za Shirika hili tufanye wenyewe, tuongeze mtaji na Shirika libaki kwa Wazalendo.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Tazara mara zote imekuwa na matatizo kutokana na ushirikiano mbaya walionao upande wa Zambia. Kwanini tusiimarishe na kujenga reli kuelekea Sumbawanga ambapo tunaweza kusafirisha mizigo ya Congo pia? Lakini kumekuwa na mpango wa kujenga reli kutokana na makaa ya mawe ya Liganga/Mchuchuma, kwani isiunganishwe na Tazara ambayo siyo zaidi la kilometra mia mbili tu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Usafiri wa Dar es Salaam linaweza kupata ufumbuzi kwa kuwekeza katika reli ya mji (*City Railways*) ambapo wananchi wanaweza kupata unafuu kwa kutumia reli hasa maeneo ya Pugu, Ubungo, Tabata na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *ATCL* hali iliyonayo inasikitisha. Naishauri Serikali ichukue jitihada za haraka sana kuondoa tatizo hili. Pamoja na yote, ifanyike jitihada kubaini mali za shirika ambazo kuna watu wamejimilikisha kinyume na sheria.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kitabu cha hotuba pamoja na kumsikiliza Waziri wakati anawasilisha bajeti, sijaona mahali popote ikizungumziwa Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko ambao kuna watu walivunjiwa nyumba zao na kuambiwa uwanja unapanuliwa. Je, wanaambiwa nini wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, umefika wakati wa kuwa na *Urban Transport Act*, Sheria ya Usafirishaji Mijini. Kwa sasa ipo sheria ya Tanzania *Road License Act* ambayo inabeba nchi nzima ambayo kimsingi, haikidhi matatizo ya usafiri mijini. Pamoja na mengine, haijaweka ubora wa mabasi ya mijini yawe ya aina gani. Abiria, hasa wanafunzi, wanalindwa vipi? *Bus linakaa* kituoni kwa muda gani, muda wa kuanza kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki na utekelezaji hawa ukizingatia umahiri wa Mawaziri na Watendaji wa Wizara hii mpya. Nakutakia kila la kheri. Namwomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema, siungi mkono hoja hotuba hii ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kutisha sana, hata baada ya Semina Elekezi, mafunzo, safari za nje na ndani kwa lengo la kujifunza, bado leo hii Waziri, Naibu wake na wataalam wote wameshindwa kuja na mpango wa bajeti ya kusaidia Watanzania hawa masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya Reli, Bandari, Viwanja vya Ndege na hata ndege vilivyoachwa na Serikali na viongozi waliongoza nchi hii badala ya kuendelezwa vimeachwa vife na hakuna mpango wa kuviockoa.

Mheshimiwa Spika, nini *priority* ya Wizara hii kwa mwaka huu? Wataalam tulionao wanatusaidiaje? Kama fedha ni kidogo kwa nini tusiwe na kipaumbele?

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali itueleze ina mpango gani wa uhakika wa kuondoa adha ya wananchi wanaoteseka kwa kukosa huduma ya usafiri wa reli kwa Mikoa ya Singida, Tabora na Kigoma?

Mheshimiwa Spika, treni moja tulionayo ni tatizo kubwa sana. Ratiba ni mara mbili tu kwa wiiki kuja Dodoma na mara mbili tu kwenda Tabora. Ili kupata tiketi ya safari, unatakiwa kufanya *booking* siku tatu kabla. Hata baada ya kupata tiketi, huna uhakika wa safari. Treni inaweza kuwepo au kutokuwepo kwa siku iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi/wasafiri wanakaa na watoto wadogo pale stesheni zaidi ya siku mbili mpaka tatu, hawana chakula na wanaumwa na mbu. Tunataka Serikali ionde tatizo la adha hii kwa hawa masikini.

Mheshimiwa Spika, watumishi wanaofanya kazi kwenye *center* za njia ya treni hawalipwi stahili zao na mishahara yao kwa wakati. Kwanza wapo porini, pia mazingira ni magumu, lakini Serikali haiwaangalii. Naomba Serikali iangalie wafanyakazi wa vituo vyote kuanzia Tabora Mjini hadi Usinge Stesheni wanalalamika sana, wako kwenye hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/2009 iliahidi kutenga fedha kwa ajili ya kutengeneza kwa lami kiwanja cha ndege cha Tabora mwaka 2009/2010 Waziri tena alisema kiwanja hiki kitakamilika na fedha ilitengwa. Hakuna kilichofanyika. Mwaka huu Serikali pamoja na Shirika la *IDA* wametenga Shilingi milioni 16,083.00 kuboresha kiwanja hiki.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali fedha zitoke haraka kwa ajili ya kazi iliyopangwa kutengeneza kiwanja hiki. Pamoja na kiwanja, pia majengo ya kupoakelea na kumpumzika wagensi

ni finyu sana na yanahitaji kupanuliwa. Sambamba na marekebisho ya kiwanja, yafanyike matengenezo ya majengo na kuboresha mashine ya uchunguzi wa mizigo.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa nchi yetu kutokana na ndege hata moja, huku tuna shirika la ndege na watumishi wanalipwa. Haya maneno yanatudhalilisha kama Taifa, hasa ukizingatia utajiri wa Taifa letu na rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, tunategemea sana utalii wetu kuinua uchumi wetu, kukosekana kwa ndege yetu tumekuwa tunanufaisha Kenya, Uganda, Afrika Kusini na nyininge. Matengenezo ya utalii/vipeperushi vyetu kwenye ndege za Kenya haviwekwi/wageni hawapewi, wanatoa vya kwoo na hivyo kuendeleza utalii wao.

Mheshimiwa Spika, nani katufikisha hapa tulipo leo? Tabia ya Serikali kulinda wabadhirifu/wezi/watendaji wasio waaminifu, waliokosa uzalendo ndilo limetufikisha hapa?

Mheshimiwa Spika, mikataba mibovu katika maeneo yote muhimu, mfano bandari, *Railway*, Shirika la Ndege kwa maslahi ya wachache yanaendelea kututafuna na kutumaliza na Serikali imeendelea kuikumbatia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ieleze leo hapa Bungeni kuna mkataba mchafu wa kinyemela kwa miaka 15 zaidi wa kitengo cha Kupakua Mizigo (*TICKS*). Mkataba huu unaleta matatizo mengi sana na kusababisha mlundikano mkubwa wa makontena bandarini. Hili limesababisha wafanyabiashara kuhama Bandari ya Dar es Salaam na kwenda kutumia Bandari ya Mombasa. Sisi tumetulia tu.

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu unaporomoka na Watanzania wanakosa huduma muhimu kwa sababu Serikali imeshindwa kuwajibisha watu wazembe na kukumbatia ubadhirifu.

MHE. MOHAMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Spika, kuhusu Menejimenti ya *ATCL*, tuache kufanya kazi kwa kuoneana haya, tusifanye kazi kwa kulindana, bila ya kushitakiwa Menejimenti ya *ATCL* iliyoساببisha leo hii pasiwepo hata ndege moja na kusababisha hasara kwa Serikali. Hivyo basi, Mheshimiwa Waziri hawezi kufanikiwa kwa kuingiza fedha na kununua ndege moja. Kwa nini hizi za zamani zikashindwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubadhirifu wa bandari zetu hasa Dar es Salaam, kwa utarabibu unoaoendelea katika Bandari ya Dar es Salasam, haitawezekana kuboresha na kufanya mizigo itoke kwa wingi kwa mfumo uliopo hivi sasa. Malalamiko ya bandari hii ni mengi na makubwa sana. Hivi sasa watu wengi wanahama kutoka bandari hii na kwenda bandari nyininge za nchini Mombasa. Watu wanaikimbia bandari. Hata baada ya *release* ya kwamba nenda katoe mizigo wako, bado kuna mlolongo mkubwa sana wa kufuata kiasi kwamba ni lazima uchoke. Ni zaidi ya sehemu 15, bado uende na kugongwa mihuri.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kwanini pasiwe na "One Stop Centre" ili yejote mwenye mzigowake, taratibu zifanywe ofisi moja tu. Kwa mtindo uliopo hivi sasa, ni shida na tumefanya mambo yawe magumu zaidi.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji mizigo na abiria kwa kutumia meli, ukiacha reli inayotumika kusafirisha vitu vizito, usafiri wa baharini (meli) ndiyo usafishaji unaoweza kubeba mizigo mizito zaidi duniani. Hivyo kwa mwambao wa Pwani Dar es Salaam – Bagamoyo, Tanga, maeneo yote haya hayana meli ambaao ndiyo usafiri wa uhakika, lakini hakuna meli yoyote ya Serikali Dar es Salaam – Mtwara. Hivyo, Wizara ya Uchukuzi ni lazima iwe ni meli mbili za abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya mafao ya wastaafu (*TRL*) tofauti na waajiriwa wengine wa Makampuni au Mashirika ya Serikali yaliyobinafishwa, kuna *NMB & NBC* wafanyakazi wa Reli Tanzania wanaacha kazi katika mazingira magumu kwani mafao yao, stahili zao hawapewi kwa mujibu wa Sheria za kustaafu.

Mfano halisi ni wa Mzee Abdul Ibrahim Mtefu aliyekuwa fundi wa matenki ya mafuta *TRC* mpaka *TRL* kwa miaka 40 ya kazi tokea tarehe 3 Septemba, 1969 mpaka mwaka 2009 ameambulia kulipwa Sh. 2,634,751.94

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wakati tunasitisha shughuli kipindi cha asubuhi, tulisema sasa tutanza kuwaita watoa hoja, sasa nitamwita Naibu Waziri wa Uchukuzi aanze. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala*, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai, siha na afya njema katika Mwezi Msharafu wa Ramadhani na kuniwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge unaojadili bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu mkubwa na kudumisha umoja, amani na utulivu tangu wamekabidhiwa madaraka tangu wamekabidhiwa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama, aah! Samahani, limekaa kama Kamati ya Matumizi...

SPIKA: Unajibu hoja, hamna watu kukaa hapa jibu hoja.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, najibu hoja. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu mkubwa na kudumisha umoja, amani na utulivu tangu amekabidhiwa madaraka la kuliongoza Taifa letu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu kwa kunituea kwa mara ya pili kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, awali aliniteua mwaka 2006, kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Iringa, nimejifunza mengi kuhusu Uongozi, Maendeleo na mahusiano katika kazi na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu, kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM Chama Tawala na wakati nikiwa *DC*, naye akiwa Waziri TAMISEMI na kuendelea kama Waziri Mkuu hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa wote waliofiwa na ndugu, jamaa na marafiki. Aidha, natoa pole kwako wewe kwa kufiwa na mama yako mzazi mpandwa Marehemu Emilia Samunyuha, pia Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai kwa kufiwa na bibi mlezi Mwamhama. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Engineer Omar Rashid Nundu, Mbunge kwa ushirikiano wake anaonipatia katika utendaji wangu wa kazi. Aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi wengine wa Wizara akiwemo Katibu Mkuu Engineer Omar Abdallah Chambo, Naibu Katibu Mkuu, Bwana John Thomas Mgodo, Wakurugenzi wa Wizara, Wakuu wa Taasisi zote pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kumshukuru mke wangu mpenzi Remmy Mziray Mfutakamba, kwa kunivumilia na kunitia moyo kwa kipindi cha zaidi ya miezi miwili tangu kuanza Bunge hili la Bajeti. Aidha, nawashukuru watoto wangu Florah Athuman Mfutakamba, Athuman Athuman Mfutakamba, Halima Kakuwa Mfutakamba, na Robert Carlos Abdul Mfutakamba, kwa kuwa karibu nami kwani wamekuwa wakifuatilia kwa karibu wakati Wizara ya Uchukuzi inajibu maswali. Wote nawaahidi nitaungana nao mara baada ya kumalizika kwa shughuli za Bunge mwishoni mwa mwezi huu na wengine kurejea kutoka masomoni.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwaombea *maghfira* wazazi wangu

SPIKA: Naomba, Mheshimiwa jibu, dakika tano, umemaliza na dakika za kwako ni kumi na tano tu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Dakika kumi na tano, ndiyo ndiyo. Naomba pia kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Igalula, lilitoko Wilaya ya Uyui....

SPIKA: Mheshimiwa Mfutakamba, itakupa matatizo anza kujibu, una dakika sasa kumi basi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru pia Katibu wangu Thomas Ngulika. Mwisho, naomba kutoa ufanuzi kwa hoja zilizotolewa Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, hoja zilizolekezwa kwa Wizara ya Uchukuzi ni nyingi na zote ni nzuri na zenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za uchukuzi nchini. Napenda tu kuwahakikisha Waheshimiwa Wabunge kuwa hoja zote hizi zitajibowi kwa ufasaha kwa maandishi na watapatiwa Waheshimiwa Wabunge kabla ya mwisho wa mukutano huu wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na usafiri wa anga, sekta hii imechangiwa na wachangiaji wengi na nitazitolea ufanuzi baadhi ya hoja hizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba, tumechoka na porojo za *BADEA* kuhusu uwanja wa ndege wa Mwanza, miaka sita toka kusikia mradi unaanza, nataka Waziri atamke lini mradi utaanza. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Dokta Charles Tizeba, Mbunge na Mheshimiwa Augustino Masele. Ufanuzi ni kwamba, hadi tarehe ya leo, uchambuzi wa zabuni upo katika hatua za mwisho, uchambuzi wa zabuni upo katika hatua za mwisho, tunatarajia kukamilisha uchambuzi wa zabuni ifikapo mwisho wa Mwezi wa Septemba, 2011. Mkandarasi wa mradi huu atapatikana mwezi Septemba, 2011 baada ya kuridhiwa na mfadhili *BADEA*, pamoja na *OPEC Fund For Infrastructure Development (OFFID)*. Kazi hizi zinatarajiwaa kuanza mwezi Novemba, 2011.

Mheshimiwa Hamoud Abuu Juma alitaka kujua Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanja kipywa Dodoma na ni lini ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe utakamilika. Ufanuzi ni kwamba, kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Dodoma, Serikali tayari imeshatenga eneo jipya huko Msalato kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja kipywa cha Ndege na tayari fidia zilishalipwa kwa wakazi wa eneo hilo. Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Songwe, ujenzi wa kiwanja hiki unatazamiwa kukamilika mwezi Desemba, 2011 na mwishoni mwa wiki nitakwenda kutembelea kuona utekelezaji unaendeleaje.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, ni lini Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga kitajengwa kwa kiwango cha lami na ni lini Serikali itakamilisha malipo ya fidia ya wananchi wa Kipunguni, Gongolamboto ili wapishe upanuzi wa uboreshaji wa Julius Nyerere *International Airport*. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Rahel Mashishanga, Mheshimiwa Josephine Ngezabuke na Mheshimiwa Ismail Aden Rage. Ufanuzi ni kwamba, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetenga kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya matengenezo ya Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga, wiki jana nilikuwa huko na Mheshimiwa Maselle, Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuboresha miundombinu ya kiwanja hicho kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia za wananchi Kipunguni, Serikali inatarajia kukamilisha ulipaji wa fidia hiyo ifikapo mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Stephen Ngonyani, ameuliza Kiwanja cha Ndege cha Mombo, kimesahaulika na hakipo katika orodha ya viwanja viliviyotengewa fedha, ufanuzi kiwanja cha ndege cha Mombo hakijasahaulika, kiwanja hiki kimetengewa fedha na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kuititia kiwanja cha ndege cha Tanga katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kiwanja cha Ndege cha Mombo kimetengewa shilingi milioni sita kwa ajili ya uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijibu kwa ufupi hoja zilizotolewa na Waheshimiwa kuhusu reli. Mheshimiwa Dokta Charles John Tizeba, anaitaka Serikali itoe kipaumbele kuwekeza katika reli kwanza, hata kabla ya barabara. Serikali itazingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na

kwa kweli Serikali imesikia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na kuweza kuongeza bajeti ya Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe, Mbunge, naye anaendelea kusitiza kuwa bajeti iliyotengwa ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji, nami nakiri tu kwamba, ni kweli mahitaji yetu ni makubwa sana lakini uwezo wetu wa kibajeti ni mdogo. Pia aliliza mpango wa ufufuaji wa reli ya Tanga, Via Arusha, haupo na kwamba mipango ya Serikali ni kujenga reli mpya. Niseme kwamba, Serikali ina mipango ya muda mfupi, muda wa ufufuaji na uendelezaji wa reli ya kat, kwa kutumia ufadhili wa Benki ya Dunia, Serikali itafanya matengenezo ya awali ya njia ya treni, sambamba na hilo tathmini ya mahitaji halisi ya kurejesha huduma kwa mitandao yote ya reli itafanyika katika mwaka huu wa fedha. Aidha, Mheshimiwa Mbewe anaendelea kuhoji, haja ya Serikali kuwawajibisha watu walioitungiza katika mikataba mibovu, kama vile *TRL*, *ATCL* na kadhalika. Niseme tu kuwa, ushauri wake umepokelewa na utazingatiwa na wote ambao wamevunja sheria, vyombo vya dola vitachukua mkondo wake ili wachunguzwe na baadaye wakipatikana na hatia hizo, Mahakama itaamua.

Mheshimiwa Angella Jasmin Kairuki, anahoji kwamba, *RITES* bado hajakabidhi nyaraka muhimu. Katika hili namjibu Mheshimiwa Kairuki kuwa, baada ya mikataba wa ukodishaji wa reli ya kat Serikali ya Tanzania na *RITE*, mikataba umevunjwa rasmi, *RITE* wamekabidhi nyaraka zote muhimu kwa Serikali na *TRL*. Mheshimiwa Mbewe anaendelea kuhoji Serikali imejipanga vipi kufufua reli ya Tanga. Ufanuzi, kama nilivyoeleza awali, Serikali ina mpango wa muda mfupi na muda mrefu wa ufufuaji na uendelezaji wa reli ya kat, kwa kutumia ufadhili wa Benki ya Dunia, Serikali itafanya matengenezo ya awali, njia ya huduma ya treni ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni yaliyohamishiwa *RAHCO* iagizwe kuhakikisha kuwa ratiba ya malipo inasambazwa mikoani na siyo Dar es Salaam peke yake, ushauri huo tumeupokea.

Hoja nyingine ya Mheshimiwa Kairuki ilihusu menejimenti ya *TAZARA* ina mamlaka makubwa yaliyoko kwa Mkurugenzi Mtendaji wa *TAZARA* pamoja na ubaguzi katika utoaji wa huduma na matibabu na matatizo ya wafanyakazi. Katika hili nasema kuwa Serikali ilikwishalionia na tayari imeshaunda timu ya wataalam kufanya kazi matatizo yote ya *TAZARA*, ni matarajio ya Serikali kwamba matatizo yote yanayoikabili *TAZARA* yatapatiwa ufumbuzi kutokana na ushauri wa wataalam hao.

Mheshimiwa Salvatory Machemli, anahoji karakana ya Morogoro imekufa, mabehewa yakiharibika yanapelekwa Ulaya, hivyo wafanyakazi wanalipwa bure, kampuni ya *RITES* haiwezi kuendesha reli bila kurekebisha reli na barabara hazitadumu. Katika kujibu hoja hii nimjibu tu Mheshimiwa Machemli kuwa kwanza karakana ya Morogoro hajafa, wiki mbili zilizopita nilikuwa huko, bado ina-repair mabehewa pamoja na engine na bado inafanya kazi. Mabehewa yanayoharibika yote yanatengenezwa pale na hayapelekwi nje ya nchi, inafanywa na wafanyakazi wazawa na hakuna behewa liliopelekwa Ulaya kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kampuni ya *RITES*, mikataba ya uendeshaji ulivunjwa rasmi tarehe 22 Julai, 2011, baada ya kusainiwa kwa *deed of installment*. Kuhusu mizigo mizito kusafiri kwa treni, hii nakubaliana naye kabisa na ndiyo maana katika mipango yetu ya muda mfupi na muda mrefu ni kufufua na kuifanya reli iimarie, reli zote ziimarie na ziweze kutoa huduma stahiki za uchukuzi nchini.

Mheshimiwa Godfrey Zambi, amegusia matatizo ya uongozi wa *TAZARA*, mikataba mibovu kama vile uliofanywa baina ya *ALASZ, Railway system* ya Zambia kama nilivyosemwa, wakati wa kujibu hoja ya Mheshimiwa Angella Kairuki, Serikali tayari imeshachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika sekta hii ya reli ni wengi sana kama nilivyosemwa, wote watapatiwa ufanuzi kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niingie sekta ndogo ya usafiri wa majini na bandari, tatizo la wizi wa mizigo na vifaa vya magari bandarini Dar es Salaam. Hoja hii imechangiwa na

Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Rahel Mashishanga, Mheshimiwa Naomi Mwakyoma Kaihula, na Mheshimiwa Hemed Ali Hemed. Ufafanuzi ni kwamba, mamlaka ya usimamizi wa bandari *TPA* kwa kushirikiana na *TICS* na vyombo vingine vimechukua hatua zaidi kudhibiti ulinzi ikiwa ni pamoja na hatua zifuatazo:-

- (i) Kutenga eneo maalum la kuhifadhi kontena zenye bidhaa hizo, chini ya ulinzi mkali;
- (ii) Kuweka utaratibu maalum wa kupakia na kuhamisha kontena zenye bidhaa hizo;
- (iii) Kuwa na mikutano ya kila mwezi kati ya *TPA*, *TICS* na kuripoti hali ya usalama; na
- (iv) Kuimarisha ulinzi *CCTV* na ukaguzi wa nyaraka za hatua hizo na hakuna tukio la wizi ambalo limetokea toka Machi, 2011.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge walichangia kuhusu mipango ya kuiwezesha bandari kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi na maendeleo ya bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na upatikanaji wa vitendea kazi. Waliochangia hoja hiyo ni Mheshimiwa Rahel Mashishanga, Mheshimiwa Benedict Mgalama, Mheshimiwa Ole Nangoro, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Abia Mhama Nyabakari, Mheshimiwa Augustino Manyanda Maselle, Mheshimiwa Benardeta Kasabago, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau. Ufafanuzi ni kwamba, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*), inatekeleza miradi mingi ya kupanua na ukarabati wa Bandari zote za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kwa kupitilia mpango kabambe wa bandari *port master plan*. Baadhi ya miradi, ni pamoja na ujenzi wa boyla *SDM* na matenki ya kuhifadhi mafuta; Ujenzi wa gati mbili za kuhudumia kontena, yaani gati namba 13 na 14, na kuongeza kina cha lango la Bandari ya Dar es Salaam; Ujenzi wa kituo cha mizigo Kisarawe, *Freight Station*; ujenzi wa Bandari ya Mwambani pamoja na upanuzi wa Bandari ya Mtwara ili kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mboge, alitaka Serikali isaidiwe, *TPA* ipewe maeneo ya Vijibweni na Kurasini. Katika hili napenda tu kulifarifupi Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali tayari imeipatia *TPA* eneo la hekta 112, eneo la Vijibweni na hatua za kuipatia barua la toleo inaendelea ikiwa ni pamoja na kufanya uthamini kwa ajili ya kulipa fidia.

Mheshimiwa Zuberi Zitto Kabwe, anahoji mkopo wa ujenzi wa gati namba 13 na 14, kutoka China ni ghali sana, kitafutufe chanzo kingine cha mkopo. Ufafanuzi, utafiti wa kampuni ya *CPCS* ya Canada ulihusu ujenzi wa gati mbili tu yaani 13 na 14 kwa gharama ya dola milioni 300 za Kimarekani. Kampuni ya Kichina imeunganisha gharama hizo pamoja na kazi ya upanuzi wa kina cha bandari kutoka mita 10.5 mpaka mita 14;, upana wa lango kutoka mita 240 mpaka mita 320 na urefu wa kilomita 2.5. Gharama za upanuzi wa lango na ununuzi wa vifaa ni dola 223.7 milioni. Hali kadhalika ujenzi wa gati utahusisha ujenzi wa *yard* kuhudumia kontena na ununuzi wa vifaa vya kuhudumia kontena. Hivyo gharama za kampuni ya *CPCS* haukujumuisha upanuzi wa lango la ununuzi wa vifaa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kujibu swali alilouliza Mheshimiwa David Ernest Silinde kwamba si kweli kwamba miaka 50 ya uhuru hatujajenga reli. Baada ya uhuru Serikali ya Tanzania ilijenga Reli ya *TAZARA* kilomita 1860, Reli ya Manyoni Singida kilomita 115, Reli ya Mrozi, Ruvu kilomita 188, jumla ni kilomita 2153. Ni muhimu sana aangalie takwimu na *data* zake kwa sababu Mheshimiwa Nundu ni mahiri kwenye Uwaziri wa Uchukuzi, lakini labda kama anataka Uwaziri, hapa hatutayarishi maandamano, tunataka watu makini wa kufanya hilo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kujibu swali la Mheshimiwa James D. Lembeli kuhusu kusafiri kwa njia ya reli. Nimeshasafiri kwa reli, nimezaliwa kwenye Reli ya Kati, nimekwenda kwa Mototroli na pia nimekwenda kwa treni, kwa hiyo, Wizara yangu tunasafiri pia kwa reli na siyo kwa barabara tu.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kuwa hoja ni nyingi sana kama nilivyokwishesa, Waheshimiwa Wabunge wote watajibiwa hoja zao kabla ya kumalizika kwa Mkutano huu wa

Bunge lako Tukufu kwa kuandika kitabu cha majibu na nakala zote tutawapatia Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ufanuzi huu, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa nimwite Waziri, mto hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia hapa tulipo kuhusu mjadala unaoendelea wa Wizara ya Uchukuzi.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyevitii wote kwa jinsi mlivyo simamia majadiliano kwenye Bunge hili. Mmeonyesha kwa vitendo jinsi gani Chama cha Mapinduzi kilivyo hazina ya viongozi wa sasa na siku za usoni katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mizengo Pinda Mbunge wa Katavi, Mtoto wa Mkulima na Waziri Mkuu kwa jinsi alivyosimamia shughuli za Bunge kwa umakini mkubwa sana, busara ya hali ya juu, uzoefu mkubwa na pia ubinadamu usio na kipimo. Nakumbuka alipota machozi hapa miaka miwili illyopita. Wote ni mashuhuda wa hili kwani ameweza leo kutuweka sawa kwa kuagiza Wizara ya Uchukuzi ipewe fedha ya ziada shilingi bilioni 95. Fedha hizi zitatumika kuboresha maeneo ya Reli, Kampuni ya Ndege ya Tanzania na Kampuni ya huduma za Meli. Lengo ni kukidhi mahitaji ya kuwezesha Sekta ya Uchukuzi kufanikisha shughuli nyine za uchumi na kijamii. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mchangano wa bajeti ya nyongeza ni kama ifuatavyo:- Kurudisha huduma za Reli shilingi bilioni 53.07, kuimarisha miundombinu ya Reli shilingi bilioni 18.5, kuboresha huduma za kampuni ya meli shilingi bilioni 6.78 zaidi ya zile ambazo tuliambiwa tuwape mashirika ya meli. Kurejesha na kuimarisha huduma ATCL shilingi bilioni 16.65, hizi fedha tayari zipo katika kasma na ziko katika vifungu.

Mheshimiwa Spika, ni matumani yetu kuwa sekta hii ya uchukuzi itaendelea kutengewa fedha ambazo zinakidhi mahitaji ili iweze kufaidisha shughuli za kiuchumi na kijamii kama ilivyoanishwa katika mpango wa maendeleo wa mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini kwa kuichambua kwa kina bajeti ya Wizara na kwa maoni aliyo yatoa ambayo yameonyesha kwamba anao upeo mkubwa wa ufahamu wa masuala ya sekta ya uchukuzi. Hizi ndiyo hazina za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu ambao kwa ujumla wao tupo nao karibu sana katika kupanga, kujadili na hatimaye kutekeleza masuala ya sekta ya uchukuzi ndiyo maana wamechukua jukumu kubwa kuhakikisha kuwa tunapata angalau cha kuweza kuanzia kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii kwa ujumla wao chini ya Mwenyekiti niliyemtaja wameonyesha ushirikiano mkubwa kwa Wizara, kwangu mimi binafsi pamoja na watumishi wote tumeuona upeo mkubwa wa kisera walikuwa nao Wajumbe wa Kamati hii kuhusu masuala ya sekta ya uchukuzi. Ni Kamati ambayo sisi tumeweza kufanya nao kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, upeo huo pamoja na hekima na busara walizonazo pamoja na ushirikiano waliotupa vimesaidia kwa kiwango kikubwa kufanya mapinduzi kwenye sekta hii na hivyo kuchangia kwa kiwango kikubwa ukuaji mkubwa wa nchi yetu. Napenda kuchukua fursa hii kuihakikisha Kamati hii kuwa tutaendeleza ushirikiano mzuri uliojengeka kati yake na Wizara tukiwa

na lengo moja tu nalo ni kuboresha na kuimarisha sekta hii muhimu kwa uchumi na shughuli za kijamii za Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Sekta ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum kwa maoni na mapendekezo yake kuhusu bajeti hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge ni mingi na yote inalenga katika kuboresha utoaji wa huduma za uchukuzi na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wetu. Wakati wa majadiliano, hotuba ya bajeti ya Serikali Waheshimiwa Wabunge 22 walitoa mchangwo wao kuhusiana na Sekta ya Uchukuzi. Wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge 14 walitoa maoni yao mbalimbali na ushauri kuhusu Sekta ya Uchukuzi. Aidha, waliochangia kwenye hotuba za bajeti za Wizara nyininge ni Waheshimiwa Wabunge 22, hii ina maana kuwa jumla ya wachangiaji walikuwa ni 58. Hata hivyo, Wabunge hao walikuwa na jumla ya hoja 72 kuhusu Sekta ya Uchukuzi kama ifuatavyo:-

Walioongelea usafiri wa reli walikuwa Wabunge 19, usafiri wa anga Waheshimiwa 27, usafiri kwa njia ya maji Waheshimiwa Wabunge 23 na huduma za usafiri kwa njia ya barabara ni Waheshimiwa Wabunge watatu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano ya hoja ya Wizara yangu tulipokea michango ya Waheshimiwa Wabunge waliyooita kwa kuzungumza na kwa maandishi. Michango hii ni mizuri yenye kutoa mwelekeo wa kisera na itatusaidia sana kuratibu na kusimamia utekelezaji wa bajeti hii pamoja na kuweka mweleko mzuri wa siku za usoni. Nawashukuru sana nyote.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, mimi na Naibu Waziri pamoja na viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Uchukuzi na Taasisi zake zote tutazingatia ushauri na maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge. Tayari Mheshimiwa Athumanu Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igala ambaye ni Naibu Waziri wa Uchukuzi ameshaanza kutolea ufanuzi wa baadhi ya masuala yaliyojitekeza, kazi ambayo nitaiendeleza. Tusipopata muda wa kujibu hoja zote hapa leo kwa sababu hoja zilikuwa nyangi na hatukutegemea kwamba hoja zingekuwa nyangi na hatukutegemea kwamba hoja zingekuwa chache, tumeongelea mambo mazito hapa. Tusipopata bahati na muda wa kujibu hoja zote, napenda kuwashakikishia kuwa tutajibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kimaandishi na kuwapa Waheshimiwa Wabunge wote nakala.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza na kwa maandishi hapa Bungeni kama ifuatavyo. Waheshimiwa Wabunge waliochangia Sekta ya Uchukuzi kuititia hotuba ya bajeti ya Serikali ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Augustino L. Mrema, Mbunge wa Vunjo; Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi; Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu; Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe; Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mbunge wa Sumve; Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala; Mheshimiwa Zakhia H. Meghji, Mbunge wa Kuteuliwa; Mheshimiwa Dokta Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni; Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa; Mchungaji Peter S. Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini na Mheshimiwa Nimrod E. Mkono Mbunge wa Musoma Vijijiini. (*Makof*)

Wengine ni Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini; Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini; Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mchungaji Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijiini; Mheshimiwa Ritha L. Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Deo K. Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia Sekta ya Uchukuzi kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mbunge wa Lingido; Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mbunge wa Monduli; Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Jenista J Mhagama, Mbunge wa Peramaho; Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini; Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga; Mheshimiwa Dokta Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Vijijini; Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini; Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Seif Suleiman Rashid, Mbunge wa Rufiji; Mheshimiwa Agness Ellas Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia Sekta ya Uchukuzi kupitia hotuba za Wizara mbalimbali ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole; Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini; Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini; Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mbunge wa Hai; Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro; Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi; Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni; Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mbunge wa Chonga; Mheshimiwa Ramo Mataala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini na Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu; Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini; Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini; Mheshimiwa Mchungaji Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini; Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mbunge wa Sumve na Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu kwa maandishi ni Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini; Mheshimiwa Lucy F. Owenga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini; Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto; Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo; Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa na Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini; Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi; Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki; Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini; Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mbunge wa Meatu; Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Dokta Seif Seleman Rashidi, Mbunge wa Rufiji; Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi; Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari, Mbunge wa Rukwa Vibi Maalum; Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani; Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Magogoni; Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi; Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe; Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni; Mheshimiwa Dokta Fenella Ephraim Mukangara, Mbunge wa Viti

Maalum; Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar Mbunge wa Viti Maalum. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijiji; Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijiji; Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo; Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Mbunge wa Kuteuliwa; Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu; Mheshimiwa Dokta Mary Machuche Mwanjewa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi; Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela; Mheshimiwa Anna MaryStella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde; Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Amer, Mbunge wa Mikumi na Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Mjini; Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Kalenga; Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mbunge wa Siha; Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa; Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mbunge wa Mbarali; Mheshimiwa Angella Jasmine Mbelwa Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Naomi Amy Mwakyoma Kaihula, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Munde Tambwe, Mbunge wa Tabora; Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti maalum na Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mbunge wa Mvomero; Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo, Mbunge wa Chalinze; Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu; Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mbunge wa Sumve; Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime; Mheshimiwa Eugen Elishiringa Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga; Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Jitu Vrajjal Soni, Mbunge wa Babati Vijiji; Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi; Mheshimiwa Amina Clement Andrew, Mbunge wa Koani na Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhammed, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini; Mheshimiwa Kheir Ali Khamis, Mbunge wa Mkoani; Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mbunge wa Njombe Magharibi; Mheshimiwa Sarah Ally, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mbunge wa Lushoto; Mheshimiwa Gregory G. Teu, Mbunge wa Mpwapwa; Mheshimiwa Antony Gervase Mbassa, Mbunge wa Biharamu Magharibi; Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge wa Ubungo na Mheshimiwa Dokta Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Sharia Ameir Abdallah, Mbunge wa Diwani; Mheshimiwa Chiku Aflah Abwao, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Anastasia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Regia E. Mtema, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Raya Ibrahim Hamisi, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Yusuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi; Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza; Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Sussan A.J. Lyimo,

Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki; Mheshimiwa Seleman Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe; Mheshimiwa Esther Lukago Minza Midimu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani; Mheshimiwa Deogratias Aloys Ntukamazina, Mbunge wa Ngara; Mheshimiwa Ntabalila Albert Obama, Mbunge wa Manyovu; Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembesamaki; Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Masele Bukwimba, Mbunge wa Busanda; Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini; Mheshimiwa Kurthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni; Mheshimiwa Haroub Shamis, Mbunge wa Chonga; Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini; Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai; Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mbunge wa Kilindi; Mheshimiwa Zainab Rashidi Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Maua Daftari, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Susan Limbweni Aloyce Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi na Mheshimiwa Salum Khalfan Barway, Mbunge wa Lindi Mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia waliochangia kwa maandishi ambaye sikumtaja hapa ni Mheshimiwa Assumper N. Mshama, Mbunge wa Nkenge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu kwa kuzungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini; Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanywa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Charles John Tizeba, Mbunge wa Buchosa; Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mbunge wa Hai; Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mbunge wa Mafia; Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Machemli Salvatory Naluyaga, Mbunge wa Ukerewe; Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini; Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini; Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mbunge wa Kawe; Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe; Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa; Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini; Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini; Mheshimiwa Donald Kevin Max, Mbunge wa Geita; Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini mara mbili; Mheshimiwa Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Wawi; Mheshimiwa Mbarouk Mohammed Rajab, Mbunge wa Ole na Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwé; Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Conjesto Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mbunge wa Tunduru Kusini; Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini; Mheshimiwa Juma S. Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini; Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi; Mheshimiwa David Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini na Mheshimiwa Athuman Mfutakamba, Mbunge wa Igala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge imejikita kwenye kuthibitisha kwamba miundombinu ya uchukuzi pamoja na huduma zake ni mhimili mkuu wa kuwezesha ukuaji wa uchumi, shughuli za kijamii na mgawanyo stahiki wa pato la Taifa. Kwa Wizara yangu,

miundombinu hiyo ni ya reli, bandari na viwanja vya ndege. Kwa niaba ya Naibu Waziri wa Uchukuzi na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake, tunaahidi kuwa tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa miundombinu hii inaboreshwu ili kukidhi matakwa ya utoaji huduma zilizo bora na salama.

Mheshimiwa Spika, lengo letu ni kuwa na sekta ya uchukuzi ambayo itawezesha ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa shughuli za kijamii bila vikwazo vyovyote. Tutafanya hili kwa kushirikiana na Kamati ya Miundombinu ya Bunge lako Tukufu, kwa ujumla wake na wadau wote wenye nia njema na sekta ya uchukuzi na mustakabali wa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Bunge la bajeti la mwaka 2010, Bunge lako Tukufu, lilipitisha sheria ya ushirikishwaji wa sekta ya umma na sekta binafsi (*Public Private Partnership Act*). Sheria hii pamoja na sera na kanuni zake, zimekuja wakati nchi yetu ina dhamira ya kuboresha na kuendeleza miundombinu ikiwemo ile ya uchukuzi ili ikidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii. Nina imani kubwa sana kuwa sheria hii na kanuni zake, zitatatuwezesha kama nchi kufikia malengo haya.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuongelea hoja zilizoletwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Joseph Serukamba ambaye kwanza alitaka kujua Serikali ina uwezeshaje Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, kuwa *hub* na pia kuviboresha viwanja vingine.

Mheshimiwa Spika, uchukuzi wa anga hauwezi kuendelea kama hatuna viwanja vizuri na kama hatuna uwanja amba ni kitovu cha uchukuzi huo. Sasa hivi tunaongelea Dar es Salaam. Ili Dar es Salaam iwe *hub*, hatua tunazochukua sasa hivi ni kutafuta njia ya kujenga *terminal* ya tatu (*terminal three*) ili uwanja wa Dar es Salaam uweze kuitisha abiria na wasafiri wengi. Pamoja na hilo, lillo kubwa ni kuhakikisha kuwa uchukuzi wa anga unachanganya hapa Tanzania ukichangiwa na makampuni ya nje na Kampuni yetu ya Air Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Serukamba alitaka Mamlaka ya Hali ya Hewa iimarishe kwa kutengewa fedha za kutosha ili kukidhi mahitaji ya mafunzo pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa. Naomba kulieleza Bunge lako hili kwamba, hiki ndicho kinachofanyika katika Mamlaka ya Hali ya Hewa. Mamlaka ya Hali ya Hewa pamoja na kwamba siyo chuo kikuu, ni mamlaka moja pekee hapa Tanzania ambapo tunapeleka watu kuchukua *post doctoral degrees*. Mwaka huu tumempeleka mmoja kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo chuo chetu ambacho kiko Kigoma, kinaimarishwa kila siku ili kiweze kutoa huduma nyngi. Tuliongelea katika bajeti yetu kuwa tuna mpango wa kusambaza rada saba (7) kwa nchi nzima. Tumekwishaweka rada moja pale Dar es Salaam na mwaka huu tunajenga rada nyngine Mwanza. Hivi ni baadhi ya vitu ambavyo tunavifanya kule. Ukamilifu wa jibu la swali hili umo katika kitabu chetu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2011/2012, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 3.481 ikiwa ni mwendelezo wa kufunga *rada* kama nilivyosema. Aidha, Serikali imetenga tena shilingi bilioni 5.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya *Tanzania Meteorological Agency (TMA)*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Serukamba kama Wabunge wengine aliongelea pia suala la *Air Tanzania Corporation Limited (ATCL)*, lakini ye ye hapa alijikita kwenye kuitaka Serikali iimarishe ATCL kwa kulipa madeni ili wafanyakazi wa kampuni wapatao 182 wafanye kazi na kuingizia mapato kampuni.

Mheshimiwa Spika, naomba niliongelee hili la wafanyakazi kwanza. Ni matarajio yetu kuwa Shirika la Ndege litaanza kufanya kazi kwa ndege kuruka na si muda mrefu kutoka sasa. Ni kwa sababu hiyo ndiyo maana unakuta kwamba kwa kipindi ambacho kilikuwa hakieleweki ni lini ndege itarudi, tusingeweza kupunguza wafanyakazi. Ndege zitakaporudi, tukilikabidhi shirika menejementi mpya na bodi, zoezi la kwanza ambalo litafanyika ni kuangalia ni wapi katika ya wafanyakazi waliopo pale wanahitajika ili idadi ya wafanyakazi iendane na idadi ya ndege. Itabidi hapa tutafute fedha za kuwalipa wale wafanyakazi ambao wataondoka ili kusiwe na matatizo. Hata hivyo, hili suala la ATCL nitaliongelea kwa kirefu zaidi baadaye kidogo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Serukamba pia alihoji na kushauri kuwa ili kuendana na ushindani unaotarajiwa kutokana na reli zilizojengwa katika nchi za Angola na Msumbiji, Serikali ihakikishe ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* na pia kuimarisha reli ya TAZARA kwa ajili ya kuhimili ushindani na kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nataka niliongelee hili kidogo. Tunachofanya sasa hivi ni kujaribu kuirudisha reli yetu iweze kufanya kazi kwa kiwango ambacho itatoa huduma zinazokidhi mahitaji tuliyonayo sasa. Hili ni zoezi ambalo tumelianza mwezi wa Novemba wakati kukiwa na ndege moja tu ya abiria, lakini tukalazimisha zikapanda zikawa mbili na mikakati yetu ilikuwa tuwe na ndege tatu, inapofika Juni na itakapofika Disemba mwakani tuwe na ndege tano. Hali kadhalika, turudishe hali ya kubeba mizigo kutoka tani 250,000 ambazo tumefikishwa sasa hivi angalau tuanze kurudi kwenye tani nusu milioni (500,000) na hatimaye tuangalie namna ya kwenda mbele. Hii ndio mikakati tuliyonayo. Tulihitaji dola bilioni sitini na tatu (US\$ 63,000,000,000) kwa kazi hiyo katika *time* ya kwanza. Sasa hivi tumepata fedha za kwanza na tumepata dola bilioni tisini na tano (US\$ 95,000,000,000) na kati ya hizo kama niliviotaja kifungu kikubwa kinakwenda kufanya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli Waheshimiwa Wabunge wameonesha dhamira yao ya kuwa ingebidi tupewe fedha nydingi. Lakini fedha nydingi tulikuwa tuzifanyie nini? Sisi tulikuwa tumepanga tutoe hata *deposits* ya kuweza kuweka akiba ya kupata mabehewa baadaye, kupata injini baadaye, kupata hata vitendea kazi vya kututia tuta la reli kule ambako imejengwa. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba pesa nydingi za kufanyiakazi nydingi ambazo sehemu kubwa ya fedha hizo si ambayo tulikuwa tunaitaka kwa dharura sasa hivi. Tulikuwa tunazihitaji kwa kujitayarisha. Sasa tulichofanya ni kutengua zile ambazo hazina umuhimu sana zikae kando, tupate zile chache za kuanzia kazi. Nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kuwa fedha tulizopewa sasa hivi shilingi bilioni 95 zinaweza kufanya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Serukamba ameuliza kwamba ikiwa wale wenzetu (nchi jirani) wanafanya, sisi tunafanya nini hapa? Kama tulivyosema sisi tuna bahati na tumekwishaweka kanda nne (4) za biashara na kanda nne (4) za uchukuzi. Tunafanya nini? Je, tunaondoka kwenye reli hii ya kisasa twende ya kisasa zaidi au tunabaki kwenye reli hii na kuishia kuboresha tu? Nimeona tunapingana pingana, wengine wamesema aah, tuboreshe haka kareli tuliko nako tu, wengine wamekuwa na mawazo kama yetu sisi kuwa haka kareli hakawesi kukidhi mahitaji yetu ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, inabidi tuubadilisha mfumo wa reli wote. Sasa katika kuubadilisha mfumo wa reli hatuwezi kufanya kazi hiyo kwa bajeti ya Serikali. Hatuwezi! Tunahitaji kati ya US\$ 3.5 - 5.1 bilioni kuboresha reli ya kati na kuweza kuwasafirishia wenzetu wa Rwanda na Burundi mizigo yao. Ni pesa nydingi sana. Tukiangalia reli yetu ya kati tuliyonayo kwa sababu, tuta tunalo, hatuna haja ya kukata miti, hatuna haja ya kufanya chochote cha ziada zaidi ya kuweka reli, tunahitaji US\$ 0.995 bilioni.

SPIKA: *Microphone* Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, hizi ni fedha ambazo tukifanya bidii tunaweza kuwavutia wawekezaji wakaja kutusaidia na hatuongelei uwekezaji wa kubabaisha. Kinachokatisha tamaa ni pale barua zetu tunazowasiliana na watu wengine, zinapokuja hapa na kuoneshwa tu. Hilo itabidi lishughulikiwe kwa njia nydingine. Ndugu zangu tatizo lillipo ni kwamba hamuelewi ni nini tunafanya Wizarani. Mheshimiwa Freeman Mboge, njoo Wizarani, uliza huu mkataba mmeandika *memorandum of understanding* ya kitu gani? Tuulize ili tuwaeleze, kwa sababu hawa tunaowasiliana nao tukifanya hivi wakitusikiliza tunawafukuza. Hapa hatuna *closed session*, hapa dunia nzima inasikia. Kwa hiyo, katika hili tumeweka mikakati hiyo kwamba, reli ya kati tutaiboresha kwa kuijenga kwa kiwango cha *standard gauge*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, alisema Tanga tumeisahau. Reli ya Tanga haijengwi. Ndugu yangu Ngonyani dhima tuliyonayo hapa Bungeni ni kuangalia maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla. Kile kinachoweza kutengenezwa mahali ambapo kuna mahitaji makubwa tunakitengeneza. Hii haimaanishi kuwa kule kwinge hatufanyi. Kuhusu reli tukisema kwa fedha tunazofikiria tuweze kufanya reli ifanye kazi kikamilifu, twende tukaanze kufufua reli ya Tanga sasa, ni kazi kubwa kwa mwaka huu na tuna miaka mitano ya kufanya hii kazi. Kupanga ni kuchagua, wenzetu wa Kigoma wanahitaji reli! Mizigo inayokwenda Burundi kule hata kama italetwa na gari mpaka Isaka inahitaji reli. Ndiyo maana tukasema nguvu zetu sasa tuziweke kule siyo tu kwa kufufua lakini pia kwa kuona umahiri wa menejementi tutakayoiweka. Hiyo menejimenti itakuwa ni ya *TRL* nzima. Tukiweka kule sasa tutageukia Tanga na kuona tufanye nini. Kwa upande wa Tanga sasa hivi tatizo si kubwa sana kwa sababu ukishatoa mizigo bandarini pale unakuja ku-connect reli ya kati unakwenda zako. Tatizo ni usafiri na sana wa abiria na simenti kwenda Arusha na Moshi, lakini barabara za Tanga ni nzuri, malori kule siyo mengi hivyo hatutegemei uharibifu kuwa utatokea.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Tanga. Niliishughulikia Bandari hii nilipoingia tu, si kwa sababu natokea Tanga, hapana! Ile bandari ilikuwa inasababisha hasara ya shilingi bilioni nne (Tsh 4,000,000,000/=) kwa mwaka. Nikasema haiwezekani! Tukaongea na wenzetu wa *TPA* wakatoa pale dola za Marekani bilioni 10.8 (US\$ 10.8 bilioni) kuboresha Bandari ya Tanga. Sasa hivi kila siku muulize Meneja wa Bandari ya Tanga, ananilettea ripoti ya mambo yanakwendaje. Ananiambia Kaka, mambo yanakwenda vizuri huku. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Tanga. Ndugu zangu wengi wameomba viwanja vya ndege na afadhalii umenisaidia kwa hilo kwa sababu wengine sielewi hata nitawaambiae. Kwa sababu tunataka tutengeneze viwanja ambavyo vitasaidia usafiri wa anga uenee nchini, ndijo maana tumechagua hivi viwanja na tukimaliza kazi hiyo tunakwenda katika viwanja vingine. Uwanja wa ndege wa Tanga, una lami, lami imeharibika, ina mabaka mabaka, inahitaji matengenezo ambayo Mamlaka za Viwanja vya Ndege wanaweza wakayayafanya wao wenyewe na watafanya hivyo. Katika fedha zinazokusanya na mamlaka hiyo, tunawaachia *retention* ya bilioni kumi na nane (Tsh 18,000,000,000=) kila siku kwa marekebisho madogo madogo kama hayo. Kwa hiyo, watu wa Tanga wasipewe *impression* kwamba nimekuja huku nimesahau Tanga, sivyo!

SPIKA: Mheshimiwa Waziri shilingi bilioni kumi na nane (18) kila siku?

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI) Mmh?

SPIKA: Shilingi bilioni kumi na nane (18) kila siku?

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI) Mheshimiwa Spika, hapana ni kwa mwaka! Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Miundombinu pia ilishauri usafiri wa reli uanzishwe Jijini Dar es Salaam kati ya stesheni ya Dar es Salaam - Ubungo Maziwa na stesheni ya Mwakanga - stesheni ya *TAZARA*. Naona kama tulikuwa na mawazo ya kufanana. Sisi haya ndijo yalikuwa mawazo yetu kwamba, tutumie reli zote mbili, *TAZARA* na *TRL*. Hatutasubiri mpaka tupate mabehewa ya kutosha, nilikwishawaambia watu wa *RAHCO* karibu wiki mbili au tatu zilizopita kuwa hata wakipata kichwa kimoja na mabehewa mawili, waanzishe ule usafiri wa reli. Wasingoje mpaka tupate vichwa vingi! Tuanze ili tuone utatuzi wa shida ya usafiri utakuwaje. Sasa kama hawakufanya hayo, ndijo hayo mnayotwambia kwamba tuanze kuchukua hatua, lakini tunaomba msije mkalia tu pale tutakapochukua hatua.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri wafanyakazi wataalam waliopo wathaminiwe kwa dhati kwa kuboresha mazingira ya kufanya kazi na kuwapatia vifaa na maslahi ya kutosha. Hizi fedha tulizozitafuta ndijo za kufanya kazi hiyo. Najua pale wameleta malalamiko mengi kuwa alipoingia *RITES* hata zile haki za msingi walizokuwa wakipata, wakawa hawapatiwi. Tutaiambia menejementi tunayoiweka iwashughulikie ndugu zao, iboreshe maslahi yao, hiyo si kazi ya Serikali bali ni kazi yao. Sasa kama hawakuifanya kazi hiyo sasa hapo ndijo tutaulizana masuala mengine.

Mheshimiwa Spika, tuna kazi kubwa ya kufufua reli, sasa ukiunganisha kazi ya kufufua reli na kulipa kifuta jasho, sisi tunasema kwamba tuanze kwanza kuimarisha reli kama alivyowahi kusema John Kennedy. *"Think of what you can do to your country, not what your country can do to you."* Hiyo ndiyo hatua tuliyofikia, watu wa reli wafikirie hivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam eneo lake ni kama takriban hekta 24 na ndiyo maana tukasema Bandari ya Mtwara inajitosheleza kwa kina na kwa eneo. Pale Mtwara Bandari ina hekta 2700 ambazo ni nyingi sana ukilinganisha na hekta 24 za Dar es Salaam. Kwa hiyo, kwa Mtwara hatuna tatizo. Wale wanaosema ni kwa nini Bandari ya Mtwara haishughulikiwi? Niseme tu kwamba Bandari ya Mtwara tutaishughulikia kwa nia moja maalum, kuna watu wanaotafuta mafuta pale. Ndugu zangu hata kama hatukujenga sasa reli ya kwenda kwenye machimbo, mafuta yatakayotoka pale yataifanya Mtwara iwe mahali ambapo pataendelea sana kiuchumi. Sasa sisi tunajikita huko kuhakikisha kwamba uchimbaji wa mafuta na gesi vinapewa kipaumbele ili tufaidike kwa hilo. Pia vitokeo vitakavyotokeza, vyombo hivi nya plastiki na vitu kama hivyo na viwanda kuchanganya kule.

Mheshimiwa Spika, kwa bandari ya Dar es Salaam pamoja na ufinyu wake tumeamua kwamba kama Kamati ilivyoshauri na sisi ndiyo tulikuwa tunafikiria kwamba, tuongeze gati ya 13 na 14 ili zichukue makontena mengi zaidi. Kazi hii itatugharimu kwanza kuongeza kina kwani kama tulivyosema awali kina chake siyo kikubwa sana na pili pia kupanua lango la kuingilia bandarini pale. Suala la kuchukua maeneo kama Vijibweni ni suala ambalo tunalishughulikia kwa lengo la kuona kama tunaweza kupaendeleza.

Mheshimiwa Spika, ilisemwa hapa kwamba tushughulikie Bandari ya Dar es Salaam na tusijikite kutafuta Bandari za Bagamoyo na kwingineko. Ndugu zangu mipango ni lazima iangalie ufinyu wa uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam. Ni mategemeo yetu kuwa reli zetu zitakapochanganya na mizigo ikapita kwa wingi pale katika Bandari ya Dar es Salaam, ni wazi kuwa bandari ya Dar es Salaam haitoshi. Ni lazima twende kwingine na ndiyo maana ya azma ya kuwa na bandari ya Bagamoyo. Hatuwezi kukwepa hilo kama tunataka kufaidika kikamilifu na uchukuzi wa reli kama ambavyo tumekuwa tunasema hapa. Hali kadhalika na Tanga kule wenzetu wa Uganda wanataka washirikiane nasi. Nikiwa hapa hapa Bungeni Mkutano uliopita walikuja tukasaini *memorandum of understanding* (MoU). Nimeulizwa tumefikia wapi? Wao na sisi tunazunguka kutafuta wawekezaji halafu tuje tukae pamoja sasa na kuona ni viperi tutashirikiana kwenye reli hiyo na bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, imeulizwa je, wamehama? Mbona Bandari iko Entebbe, sasa tunaambwa Kampala! Ni kweli! Kwa ajili hii wao wanajenga bandari mpya mahali wanapoita New Kampala. Kwa hiyo, mradi ule tunaosema wa Tanga *line*, ni pamoja na bandari ya Mwambani Tanga, reli ya Tanga – Musoma na bandari ya Kampala Mpya (New Kampala)

Mheshimiwa Spika, kuna mengi ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Serukamba ameyasema hapa na mimi na yeye mara nyingi tunakaa pamoja na kubadilishana mawazo. Kwa hiyo, hayo pamoja na kuwa tunayaongelea lakini pia tutayajibu kimaandishi.

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa Sekta ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mhonga Saidi Ruhwanya, alikuwa na hoja mbalimbali. Kwanza, alihoji kuhusu udhaifu wa miundombinu muhimu katika viwanja vya ndege vya TANAPA na Wizara ya Maliasili chini ya Wanyamapiro. Kila taasisi inayomiliki uwanja wa ndege ina jukumu la kuhakikisha kuwa uwanja husika unafanyiwa matengenezo ili uweze kukidhi matakwa ya utoaji wa huduma za usafiri wa anga. Mamlaka ya Usafiri wa Anga ina jukumu la kuhakikisha kwamba viwanja hivyo vinakidhi viwango. Aidha, mamlaka inahakikisha usalama wa matumizi ya viwanja upo kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, liliulizwa swali kwamba kwa nini tusiwaambie TANAPA wakawekeza? Kwa nini tusiwaambie Watanzania wawekeze? Ndugu zangu tunalifanya hilo. Kuna Watanzania kadha wa kadha tunaoona kwamba kwa uwezo wao sasa wanaweza wakawekeza kwenye

usafiri wa anga na hata kwenye reli, tunaongea nao. Tunaposema wawekezaji hatuongelei wawekezaji wa nje tu. Tatizo ni kuwa uwezo wa Watanzania kuwekeza kwenye miradi hii mikubwa sana ni mdogo, lakini akitokea Mtanzania ambaye anawekeza kwenye miradi mikubwa tutakuwa na faraja kubwa kuwa naye. Haya mashirika yatakapofikia hatua ambayo tutaweza kuwajumuisha Watanzania wote wachukue *shares*, tutakwenda huko. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo yako katika mipangilio.

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ya Kambi ya Upinzani ilikuwa ni Serikali iwezeshe vituo vya kufanya uchunguzi wa hali ya hewa ya anga za juu vifanyi matengenezo. Ushauri huu utazingatiwa na sio tu utazingatiwa, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu tutaboresha vituo hivyo pamoja na studio zake. Hata hivyo Serikali ilianza jitihada za kufufua vituo hivyo na imeshakamilisha kufunga kituo kipyta cha Dar es Salaam katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere na sasa kinafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani alihoji ilipo ndege ya *ATCL* iliyokuwa inafanya kazi zake kati ya Dar es Salaam, Kigoma kupitia Tabora. Kila tunavyosema hapa kuwa tunataka ndege zetu Serikali inatoa fedha, tunataka ndege zetu Serikali inatoa fedha. Niwape mfano tu wa huko tulikofika.

Mheshimiwa Spika, Ndege ya *Dash 8* ilikwenda kutengenezwa Johannesburg kwa thamani ya dola laki mbili na Serikali ikatoa dola laki moja, ilipokamilika tukaambiwa bei ni dola laki nane, Serikali tumetafuta fedha tunarudisha ndege hiyo, mara nne ya bei hiyo ya kwanza. Pametokea watu wengine wanasema wana madai nao. Serikali inatafuta inalipa, kila tukijishinikiza hapa kuwa jie ndege kuna vidudu mtu huko wanatafuta njia za kuchimbua madai. (*Makofi*)

Nilipomjibu ndugu yangu Mbunge alipouliza tunafanya nini kwa watu ambao wametufikisha kwenye matatizo, nilisema sisi Uchukuzi sasa hivi kazi kubwa tunajikita *concentrate* kwenye kubadilisha mambo na kwenda mbele pale ambapo yameharibika. Lakini hilo halimaanishi kuwa mtu ambaye atabainika kuwa amefanya matatizo ataachiwa. Sasa hivi tunatayarisha uchunguzi wa kuangalia nini kimetokea katika sehemu ambazo zimejitozeza na matatizo. *Air Tanzania, KADCO* na *TRL*. Hatuwezi kukurupuka tu kusema tunawashika wote Menejimenti ya *Air Tanzania* tunaichukulia hatua, unawenza ukawachukulia hatua watu ambao hawahusiki. Kazi ni kutafuta uchunguzi kuona nani amehusika halafu anayestahili kuchukuliwa hatua achukuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani alihoji ilipo ndege hiyo ya *Air Tanzania*, nasema sasa hivi ndege ile tuliahidiwa kuwa ingefika hapa tarehe 28 baada ya kupeleka fedha zao za mwisho, baadae tukaambiwa ina matengenezo madogo madogo sasa ahadi iliyopo ni kuwa itafika tarehe 10 Agosti, 2011, kwa hiyo tunaisubiri hiyo ndege jie.

Ndege ya pili bado ipo hapa na tumeitengeneza, katika fedha hizi ambazo zimeongezwa jana ikatengenezwe irudishwe. Zile fedha mchanganuo wake sikuueleza kikamilifu. Kuna fedha pale za *working capital*, kwanza tulikuwa tumeshawatengea shilingi bilioni 1.5 kwa *working capital*, tunawaongezea tena takribani shilingi bilioni sita tuwakabidhi waendeshe hilo Shirika.

Kaka yangu Michael Shirima wengine walisema ameanza na ndege moja, hakuanza hata na ndege moja, alianza ku-spray tu, sasa kama ye ye anafanya hivyo na ni Mtanzania kama wengine kwa nini na Watanzania wengine wasiweze kuendeleza *Air Tanzania* kwa kiwango hicho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani alikuwa ana hoja kuhusu *SUMATRA* inahusika vipi kati ya *TABOA* na *U-Track Africa Limited*. *SUMATRA* ni mtu anayefuatilia na kuangalia masuala ya usafiri wa barabarani, walipokuwa wakijadili mambo ya *U-Track* alikuwepo kwenye kikao sio kama mshiriki ambaye ana upendeleo wowote wa hiyo *U-Track*. Alikuwepo pale kama mdhamini wa usafiri wa barabara kuongelea mazungumzo yanakwendaje.

Mimi nilishawaita watu wa *TABOA* na wengine wote ofisini kwangu nikaongea nao na ilikuwa hatukusaini kitu pale tunaongea tunapatana na kusema mnakwendaje, nendeni

mkakubaliane. Kama pangekuwa na karatasi naona leo pia ingeambiwa Waziri amehusika maana yake amesaini. Tuwe na tahadhari tunapotoa hizi taarifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine ya Msemaji wa Upinzani ilikuwa ni kwa nini *TRL* itozwe tozo ya mafuta kwa ajili ya kuendesha *engine* wakati fedha hizo zinanufaisha Mfuko wa Barabara. Tozo la mafuta linajumuisha mafuta yanayotumika katika *engine* na mitambo ya reli inafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Barabara. Hata hivyo Serikali imeshaanza kulifanya kazi tatizo hilo ili fedha zinazopatikana kwa tozo hizo zitumie kuboresha miundombinu ya reli. (*Makofii*)

Msemaji wa Kambi ya Upinzani alikuwa na maoni kuwa kwa kuwa Serikali imeamua kuchukua hisa zote za *TRL* Serikali haina budi kuiwezesha *TRL* kuwekeza katika miradi muhimu ya maendeleo. Mtaji wa kufanya kazi pamoja na kulipa madeni yote ambayo yameachwa na Menejimenti ya *RITES* napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea na fedha za uwekezaji na kama mlivyoona tumepata zile ambazo sisi kama Wizara tulifikiri pia tuklongezwa zitatusaidia kuweza kuanza na Kamati ya Miundombinu pia ilifikiria hivyo dola za Kimarekani bilioni 95, kwa hiyo kazi hii sasa itafanyika kama inavyoelezwa hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilihoji kuwa Serikali inatumia vigezo gani katika kuingia mikataba na Kampuni mbalimbali za kifedha, kwa mfano mkataba na Kampuni ya *Glasgow International General Trading*. Hatua tulionayo sasa hivi sisi ni kujaribu kuongea na wawekezaji, kukubaliana makubaliano ya mwanzo. Ni viyi tutatoa *tender* hizo inategemea tutakapokaa kama Serikali kwa pamoja tutakapojadiliana tutafikia wapi. Serikali haijaingia mkataba na mwekezaji yeyote, lakini kumekuwa na mazungumzo ya awali kama nilivyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine ilikuwa ni kwamba wakati tumevunja mkataba na *RITES* wakati huo huo tunaenda haraka mbele kutafuta mbia mwininge. Je, Serikali imezingatia mazingira iliyosababisha mkataba na *RITES* kuvunjwa, je, maslahi ya Taifa yanazingatiwa? Kama nilivyoeleza *PPP* ndio njia ya kwenda na sasa tunachofanya ni kutafuta wawekezaji waonyeshe nia yao halafu tuone tutakwenda nao viyi. Suala la kuwa mikataba itaingiwa viyi, hilo ni suala la hatua ambayo tutafikia ya kuingia mikataba nayo. Tutakuwa hapa wadhibiti kabisa kuhalikisha kwa makosa yaliyofanyika nyuma yale ya kama *RITES* hayafanyiki tena. Kwa kuzingatia sera na sheria hiyo tunaendelea kuwakaribisha. Napenda kulithibitishia Bunge lako kuwa Serikali wakati wa mchakato huu itazingatia sera na maslahi ya Taifa kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilihoji Serikali ilishiriki viyi katika kuingiwa kwa mkataba wa *TAZARA* kwa upande wa Zambia na Shirika la Reli la Zambia na je, nini manufaa ya mkataba huu kwa Taifa la Tanzania? Serikali ya Tanzania haikuhusika na uingiaji wa mkataba huu ile ni Kampuni ambayo inajidesha na Menejimenti ipo pale na wanazo kila haki za kuingia mikataba. Lakini mikataba ikiwa mibovu hapo sasa ndio tutakapoingia na kuona nini cha kufanya na kuna dalili hizo, ndio maana tumeweka Kamati ile ya Wachina, Wazambia na wataanza kwa kuliangalia Shirika la *TAZARA* kikamilifu tuone ni mabadiliko gani tunaweza kuyafanya pale. Hatuezi kusema leo kuwa kesho kutwa itakuwa Meneja anaweza kuwa Mtanzania, anaweza kuwa Mzambia tunaanza tuone kutoka katika uchunguzi huo unaofanywa ni mapendekezo gani yale ambayo tunapewa na tuyafanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilitoa mawazo kwa Serikali ijenge gati namba 13 na 14 kwa kushindanisha makandarasi na kutumia mfumo wa *BOT*. Tupo huko na ndio tunatafuta hao watu wa kuwekeza kwenye gati hizo 13 na 14 hivi sasa. Naona hili swali limekuwa ni zuri kwa sababu hata Kamati ya Miundombinu pia imelitoa na sisi wenye tulikuwa tunalishughulikia hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeelezea fedha tulizopata zinakwenda kwenye sehemu zipi, nimeeleza mpango wa muda mfupi na pia dhamira ya mpango wa muda mrefu ambao tunaufanya kazi, sasa nielezee Bajeti. Katika kuhalikisha kuwa kwanza umuhimu tunaouweka ni kuwa Mashirika yetu haya yafanye kazi madeni yale ambayo hakuna dharura ya kuyalipa sasa hivi hatutayalipa. Yale ambayo yana dharura ya kulipwa sasa hivi tumeamua kuyalipa na tumewekeana ratiba ya ulipaji huo.

Sasa hizi fedha tulizoomba zinakwenda pia kulipa madeni ambayo ni ya *AFC* na madeni ambayo tunalipa ya Menejimenti inayoondoka na hapa nataka nitoe ufanuzi. Tunalipa hapa sio *RITES*, tunalipa Menejimenti kwa huduma walizotoa. Hisa zile tulizinunua bure, tulirudisha hisa kutoka *RITES* bila ya kuzilipia hata senti tano. Sasa haya madeni ni madeni ya kazi zilizofanywa na Menejimenti. Kama Menejimenti imefanya kazi mbaya au vipi hilo ni suala lingine lakini lazima myalipe na tumeyalipa kwa *prorate*, sisi tunalipa 49 kwa 100 na *RITES* wanalipa 51 kwa 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema maswali ni mengi, lakini nataka nilirudie swalii la ndugu yangu Mheshimiwa Freeman Mbewe. Hili nalirudia kwa sababu ndugu yangu kwa lugha nyepesi nyepesi amesema nimedanganya, unajua ndugu yangu yaani vitu vingine vinakuwa vina hisia mbaya. Nimweleze tu Mheshimiwa Mbewe na nilihakikishie Bunge lako na wananchi wote kwamba tuliposema kuwa *KADCO* waliwekeza kwenye Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro hatukuwa tunasema uongo. Tunarudia kusema ni kweli waliwekeza, sasa waliwekeza kiasi gani hili ni suala lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1998 Benki ya Dunia iliikopesha Serikali ya Tanzania dola milioni saba sawa sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 10.5. Sasa *KADCO* walilipa baadhi ya fedha hizi, hizi fedha ni za *World Bank* na nyininge zililipwa na Serikali kwa sababu wao ndio walikuwa wamechukua mkopo. Lakini baadae Serikali ilichukua mkopo wa *European Investment Bank*, mkopo ule ukagawanywa baadhi ikawa ilipwe na Serikali na ile ambayo ilikuwa inakwenda kutengeneza *KADCO Kilimanjaro Airport* ikawa ilipwe na *KADCO*. Sasa hizi kiasi cha *Euro* milioni 5.7 ndizo ambazo zilikuwa zilipwe na *KADCO*. Sasa hilo hapa hatuna muda tukipata muda tutakaa nikuelekeze vizuri ni nini ambacho kimetokea kule. Kwa upande wa Kampuni ya Ndege ya Tanzania nimeshasema kuwa hizi fedha tulizopata tutatoa kule tuziridishe. Kwa upande wa usafiri wa majini tunataka Kampuni ya Huduma za Meli iweze kutoa huduma bora zilizo salama na nafuu na nimeshataja hapa tunawapa fedha zaidi ya zile ambazo wameomba.

Mheshimiwa Spika, naomba mwisho kabisa lakini sio kwa umuhimu nachukua fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa mimi binasifi nathamini kwa kiwango kikubwa ushirikiano kati ya sisi wanasiasa ndani ya Wizara na watendaji amba ni wataalam. Nisingeweza kusimama hapa na kuwasilisha hotuba hii bila ya ushirikiano ninaoupata mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri kutoka kwa watendaji wa Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umakini na ufanisi wao unajidihirisha katika namna sisi tunavyowasilisha kwenu masuala ya sekta kwa ufanisi. Ninaomba ushirikiano uliopo kati ya Wizara na Kamati ya Miundombinu pamoja na Bunge lako Tukufu uendelezwe ikiwa ni pamoja na ushirikiano kati ya mimi na Naibu Waziri na watendaji ndani ya Wizara. Tunaweza na nina nia imani kubwa kwamba tutafikia malengo yetu. Sasa yule anayesema ninyongwe aah, ye ye aseme, kama nitanyongwa kwa kujaribu kubadilisha miundombinu ya nchi yangu acha ninyongwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi

Kifungu 1001 – *Administration and General*..... Sh. 1,409,012,000

MWENYEKITI: Waheshimiwa ningewashangaa kabisa kama msingesimama. Wakitaja fedha ndio mnasimama. Sasa nitaanza na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Sasa tunaanza na Mheshimiwa Freeman Mbwe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza.

Wakati nikichangia kwa kuzungumza na baadae kuchangia kwa maandishi nilizungumza kidogo kwa kirefu kuhusiana na suala la Uwanja wa Ndege wa *KADCO* na mojawapo ya mapendekezo niliyokuwa nimezungumza na kushauri ni kwa sababu Serikali imefanya uamuzi wa busara wa kurejesha uwanja huu katika mamlaka yake kwa asilimia mia moja, nilipendekeza kwamba wafanyakazi wote wa iliyokuwa *KADCO* ikiwepo *ANS-KADCO* ambayo ni *Air Navigation Services* warudishwe katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania pamoja na *Tanzania Civil Aviation Authority* ili warudi katika ajira rasmi ya Serikali kama walivyo wafanyakazi wenzao katika viwanja mbalimbali vya ndege vilivyozunguka nchi nzima na nilieleza kwa kifupi kwamba wapo chini ya uongozi wa aliyekuwa Meneja au Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni wa iliyokuwa *KADCO* ya zamani chini ya mkataba wa *KADCO* ya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri hakunijibu katika hili na sikusikia kauli ya Serikali kuhusu rai hii lakini pamoja na yote hayo tangu nimetoa hotuba yangu katika Bunge hili jana kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu baadhi ya wafanyakazi wa *ANS-KADCO* wameshapewa barua ya kusimamishwa kazi kwa tuhuma nzito kwamba wamevujisha taarifa za Shirika au za Kampuni hiyo ambayo kimsingi ni mali ya Serikali na naweza kutoa mfano halisi kwamba aliyekuwa Meneja wa *ANS-KADCO* akijulikana kwa jina la Bwana Riwadi Aman amesimamishwa kazi kwa barua yenye kumbukumbu namba ADM/02/01/053/ ya tarehe 3 Agosti, 2011 ambayo amepewa jana mchana kufuatia hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko kwamba hatutawadhalilisha wafanyakazi kwa ajili ya mambo ya hisia na kwamba wafanyakazi hawa watarejeshwa kwenye mamlaka za Serikali ili waweze kufanana na wenzao kwenye viwanja vingine ili kuoanisha ajira nzima ya watumishi katika sekta ya ndege.

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala lake la msingi *KADCO* kwa kuwa imerudi Serikalini, *KADCO* kwa mantiki zote, *KADCO* sasa ni *parastatal organisation*. Kilichobaki ni kuangalia tu inawezaeje kurudi tena kwenye mfumo wa *parastatal organisation* kabla hatujafanya mengine. Kuhusu menejimenti iliyoko pale taarifa ni kuwa menejimenti ile ni kwenda kwenye mchananuo kwa kugombea kazi ile. Walikuwa watano akapatikana mmoja, sasa cha kufanya sisi ni kuangalia mikataba ya hiyo menejimenti na hizi tuhuma nydingi ambazo zimetolewa hapa zinakwenda kwendaje tufanye marekebisho. Kuhusu wafanyakazi, suala la Watanzania kudhalilishwa kama hakuna sababu sisi hatulikubali na tutalifanya kazi. (*Makof*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilieleza kadhia ya Bandari ya Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri hajataja au hajazungumzia kuhusu menejimenti au namna gani ataboresha Bandari ya Dar es Salaam namna inavyolalamikiwa na hasa katika utoaji wa mizigo na urasimu mkubwa kiasi kufikia watu wengi wanakimbia na wengine wanapitishia mizigo yao Mombasa. (*Makof*)

Moja katika sababu kubwa kwamba hata unapopata *release* bado una ofisi 15 za kuzunguka tena masafa marefu. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kututolea ufanuzi kwamba hiyo menejimenti mpya au *reshuffling* ya Bandari ya Dar es Salaam ili kufanya kazi kileo nayo utaifanya au bado itaendelea katika mfumo uleule?

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar es Salaam wazungu wanasema ndio *cash caw* yetu kama alivyoona katika mashirika yote yaliyo chini ya Wizara ya Uchukuzi lile ndilo ambalo linatengeneza faida. Linafika mpaka bilioni 64 na tunategemea zinaweza kuwa zaidi ya hivyo. Ni kweli kumejitokeza matatizo machache na linafanyiwa kazi kwa mbinu mbili. Mimi mwenyewe kwa kufuatana tu na suala la kuwa *storage charges* ni kweli kila mtu anayetao mizigo pale asifaidike na zile siku saba za *storage*

charges na kwa kulifuatilia hilo nimewatuma watu kwenda kudadisi kupita kwenye *ICD's*; nataka niunganishe *ICD's* sio tatizo nitakapojibu hilo kama litaulizwa tena nitasema.

Kwa hiyo, tunafanya utafiti wa kuona tutaboreshaje bandari yetu ili *charges* wanazochajiwa wawe wanachajiwa kwa sababu wamechelewa. Lakini kuitisha mizigo bandarini kuna watu wengi ambao wako *involved*. Sasa tumesema bandari iwe inafanya saa 24. Tumesema tuanzishe kituo cha shughuli zote za ku-clear mizigo zinafanyika palepale bandarini pamoja na benki kuwekwa pale Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa ni *cash caw* haiwezi kudorora. Kama kuna ubadhilifu au matatizo ya watu binafsi hatutasita kuyachukulia hatua tusije tukalaumiana. Ahsante. (*Makofii*)

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipatia nafasi. Kwanza niishukuru Serikali kwa kusikiliza ombi langu la kuongeza pesa katika hii Wizara. Sasa katika mchango wangu wa kuzungumza nilitaka kujua ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa reli ya Kimataifa kutoka Dar es Salaam mpaka Isaka mpaka Rwanda na Burundi itaanza? (*Makofii*)

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati natoa maelezo, suala la kuibadilisha reli ni kubwa. Suala la kuiboresha tuna mkakati wa muda mfupi wa kuboresha na kubadilisha ili iwe *standard gage* ni kubwa. Hilo tuko katika hatua sasa hivi za kutafuta wawekezaji sambamba na kufanya usanifu wa kina. Wanaita *details design*, tumeshamaliza *feasibility study* ndiyo maana tunaweza kuongea pesa zinazohitajika. Tukipata mwekezaji tunafikiria kuanza mpaka kumaliza kujenga reli ile itakuwa kama miaka mitatu. Lakini suala ni kwamba tupate kwanza mwekezaji, kwa hiyo mtutie imani tunapotafuta wawekezaji badala ya kutuvunja nguvu. (*Makofii*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na shukrani zangu kwa Serikali kuitia Waziri Mkuu na Waziri mwenye dhamana kwa uamuzi wa kuongeza fedha katika Bajeti hii. (*Makofii*)

Sasa swali langu linakuja kwenye mchango wangu nilipokuwa nachangia Bajeti ya Waziri Mkuu na kwenye mchango wangu wa maandishi kwamba kwa kuwa mashirika yetu haya ya umma yamekuwa yakifikishwa mahala pabaya na watu wasiokuwa waaminifu; na kwa kuwa Serikali imetenga fedha nyngi katika Bajeti hii kwa ajili ya kufufua mashirika haya ya umma ambayo yanafanya kazi chini yako Mheshimiwa Waziri ambaye nina imani kubwa sana juu ya uzalendo wako. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya watu watakapewa kuongoza mashirika haya ambayo watakuwa ni watu wapya na menejimenti mpya itakayotoa matumaini kwa Watanzania ili tusifike tena mahala hapa ambapo tulikuwa tumefika au tulipofikishwa na wale wasiokuwa waaminifu? (*Makofii*)

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nilijibu hili kwa kutoa mifano maalum. Nichukue mfano wa *Air Tanzania*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Air Tanzania* ilivyo sasa hivi haina Mkurugenzi Mkuu. Mkurugenzi aliyopo pale anakaimu. Kazi tullyonayo sasa hivi ni kutafuta *management team* nzima. Wale ambao tutaona wanaweza kuendelea nasi tuiswakatishe tamaa ambao wapo mle tutaendelea nao. Lakini wale ambao tutawatilia wasiwasi hatutaendelea nao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TRL* tumeweka menejimenti ya mpito na ni menejimenti ya mpito na nilishaongea nao wala sio leo tangu Januari niliwaambia tutawaangalia mmoja mmoja. Wale ambao tutaenda nao tutaendelea nao na wale ambao tutaona hatuwawesi kuendelea nao hatutakwenda nao na sio kwa menejimenti tu, hata kwa Bodi tunazoziweka ni hivyo hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki mbili zilizopita nilizindua Bodi mbili, Bodi ya *TMA* na Bodi ya *TAA* pale Dar es Salaam ambao walinisikiliza nilivyokuwa naongea nao wataelewa nilikuwa nawaambia nini. Nilisema tutawekeana vigezo. Bodi inatakiwa itusaidie Serikali, Bodi ambayo mara nne haitatusaidia mpaka mimi niende nikatatue matatizo huko haitufai. Tukifika huko mimi

sitasita kumshauri Mheshimiwa Rais kuivunja kwa vile zile Bodi anachagua Wenyeviti na zile ambazo mimi nina madaraka ya kuzivunja nitazivunja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waziri ameamua kwamba hafi peke yake. Mheshimiwa Maria Hewa.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimechangia kwa kuzungumza suala la reli kuukuu ambayo inatoka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Fedha imepatikana je, kazi itanza lini katika kuikarabati ili tuweze kupata treni? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za ukarabati wa reli yetu ya Dar es Salaam mpaka Mwanza itanza mara moja fedha zitakapoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu jana pamoja na mambo mengine niligusia kidogo suala la usafiri wa majini hasa katika Ziwa Victoria. Zipo meli nyngi ambazo zinamiliikiwa na Kampuni ya Meli lakini sasa hivi hazifanyi kazi. Sasa kwa sababu leo imeonyesha nia ya dhati ya kuondokana na tatizo hili kwa kuongeza Bajeti leo asubuhi. Naomba kujua endapo meli ya Mv. Serengeti itakapofanyiwa ukarabati kama itatoa huduma katika vituo vyote vya awali ambavyo ilikuwa inatoa huduma ikiwemo na sehemu ya Luhama ndani ya Ziwa Victoria katika Kata ya Katu?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, hii meli mara baada pesa zitakapoidhinishwa matengenezo yataanza ili ianze kutoa huduma Ziwa Victoria. (*Makofii*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa niaba ya Kamati yetu kwa kusikiliza na kutambua matatizo haya ambayo wameamua ktuongezea pesa. Mimi la kwangu ni dogo tu, naomba tu Mheshimiwa Waziri kwenye hizi fedha ambazo zimetoka kwa ajili ya reli kwa manufaa ya Watanzania tungependa tujue zitafanya shughuli gani hasa?

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, hela ambazo tunazipeleka kwenye reli zinakwenda kwa makundi matatu. Hii itakuwa ndefu kidogo ngoja nisome upesi upesi tu. Tutaimarisha tuta la reli kati ya stesheni ya Kilosa na Gulwe, ununuvi wa vifaa vya karakana vya kunyooshea mataluma ya reli yaliyopinda. Kutandika njia ya reli kwa paundi nane kwa *yard* urefu wa kilomita 80 ili kupunguza ajali na kuongeza mwendo wa treni, kukarabati mashine za kuchimbia kokoto kwa ajili ya njia ya reli. Hii ni kwa matengenezo madogo madogo. Kazi inayofanyika ni malipo kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa injini sita za aina ya 88 ili tuongeze injini zetu. Kununua seti moja ya mitambo ya kunyanyulia mabehewa wakati wa ajali, malipo ya awali ya kununulia mashine ya kutengeneza kokoto, kukarabati mabehewa 82 ya mizigo, kununua vipuli kwa ajili ya kutengeneza injini tano za treni ambazo ni mbovu ili kuongeza idadi za treni, kukarabati mabehewa 31 ya abiria ili idadi ya treni za abiria kufikia tatu kwa wiki, kutoka mbili. Novemba tulikuwa moja, tukaja mbili sasa tunaenda tatu, kukarabati mashine nne za kushindia kokoto kwenye njia za reli, kujenga magenge matano ya wafanyakazi ya reli yaliyobomolewa kwa ajili ya wakaguzi na watengenezaji njia, kukarabati mitambo ya ishara kati ya Dar es Salaam na Ngerengere ili kuepusha ajali, matengenezo ya kawaida ya njia, kukarabati majengo ya karakana ya Dar es Salaam, Morogoro na Tabora. Pia tutalipa madeni tuliyonayo ambao tutayalipa kwa awamu. (*Makofii*)

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nataka kuulizia upande wa ndege na ukizingatia kwamba ni jambo la aibu kidogo kutokuwa na *airline* ya Taifa. Labda niseme wenzetu Ethiopia mwaka 2005 walikuwa na maono kwamba mwaka 2005 mpaka 2010 tunataka kuzalisha bilioni moja na kusafirisha watu milioni tatu na wakaanza kazi. Mwaka 2007 mpaka 2008 wakawa wameweza kusafirisha watu milioni 2.5 faida ni *USD* milioni 900, *net profit* wakatengeneza *USD* 56 milioni nisiongee sana lakini nia yangu ni kwamba sisi kama tumetoa hizi fedha kwa upande wa ndege. Mheshimiwa Waziri mmelenga kusafirisha watu wangapi kwa mwaka na mnategemea kupata faida kiasi gani ili tuone kwamba faida inapatikana na inaonekana kwa usafiri wa ndege? (*Makofii*)

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutenganishe mambo mawili hapa. Kuna suala la mmiliki wa Shirika la Ndege, kuna suala la menejimenti na kuna suala la Bodi na mimi nataka tuwe tunafanya kazi hivyo. Katika masuala ya usafiri wa anga kuna masuala ya mwenye hisa, kuna masuala ya Bodi na masuala ya Menejimenti. Kazi yetu sisi kama Serikali ni kutafuta Bodi imara tuiweke pale. Bodi pamoja na sisi tutafute menejimenti imara tuiweke pale. Masuala ya kuwa watabeba abiria wangapi, watakwenda kukodisha ndege wapi sio masuala yetu sisi ya kujibu hapa, ni masuala ya menejimenti. Tunapoanza kufanya hivyo na hatuna uwezo wa kufanya hivyo ndiyo tunaingia kwenye matatizo. (*Makofi*)

Ethiopian Airlines tangu mwanzo na najua historia mimi nilifanya kazi kwenye mashirika ya ndege miaka mingi tu. Wale walikuwa na Bodi ya watu watatu Kapteni Mohamed walikwenda kumchukua America kuja kulishughulikia shirika lile la ndege na Kapteni Mohamed alikuwa anauwezo wa kufanya maamuzi ya kizalendo. Walifika mahali tunaiita *moment of truth*, hata ukifika kwa yule mtoa huduma pale uwanja wa ndege anayekukatia tiketi yeye ana mamlaka kamili ya kuchukua maamuzi pale. Lakini anakuwa na maamuzi kwa sababu anakuwa na uzalendo na analionea huruma shirika lake. Hawezi kuchukua maamuzi ya kupandisha mizigo yako halafu hela akatia tumboni hapana. Sasa sisi tunataka shirika liende huko. Tukiliwezesha hivyo na watu ambao tunawafikiria wanaweza kurudi pale ndugu zangu lile shirika litaanza kuendelea. Nakubaliana na ninyi ni aibu Tanzania kutokuwa na shirika la ndege. Kule Air Navigation Commission naambiwa wewe *President* wa Air Navigation Commission nchi yake haina ndege. Unatafuta mahali pa kujificha hupaoni. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali yake kwa kusikiliza kilio cha Wabunge, jana tumepiga kelele humu ndani na kuongeza fedha kwenye Bajeti ya Wizara hii, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati ninachangia hapa kwenye hotuba yangu niliweka msimamo wangu bayana kabisa kwamba kwa niaba ya wananchi wa Ludewa siwezi kuunga mkono Bajeti hii mpaka hapo Shirika la Meli ambalo wananchi wa Ludewa kule Ziwa Nyasa watakapotengewa fedha. Je, Mheshimiwa Waziri umetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya Shirika la Huduma za Meli kule Ziwa Nyasa ambalo linahudumia wananchi wa Lumbila, Kilondo, Makonde, Lifuma, Lupingu na Manda kule Ziwa Nyasa. Naomba thabiti umetenga kiasi gani ili tukuunge mkono? Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Hasa ukizingatia kwamba alinusurika kufa. (*Kicheko*)

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la ndugu yangu Deo Filikunjombe...

MWENYEKITI: Naomba utumie *microphone* vizuri.

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, inapofika saa hizi sisi na mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani sauti pia kidogo zinapotea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapa tulikuwa tunaongelea kulipa Shirika la Meli shilingi bilioni nne, sisi tunaangalia kwa mapana yake ndiyo maana tumeitengea shirika hili pesa nyingi kuliko zile ambazo tunazijadili jana hapa, tumeitenga fedha shilingi bilioni 6.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ni kwamba kila meli zinazoweza kufanyiwa ukarabati upesi zifanye kazi, kazi hiyo tunawaachia kampuni hiyo ya meli itufanyie. Suala la meli alilosema Mheshimiwa Filikunjombe hapa itabidi tuwaambie wenzetu wanaoshughulika na shirika hili tulitilie maanani sana. (*Makofi*)

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa asubuhi nilimuuliza Waziri kwamba ni lini watapeleka mabehewa ya abiria katika njia ya reli ya Mpanda - Tabora. Naomba majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali pesa ambazo Bunge lako Tukufu litatuidhinishia zitalenga pia kuongeza mabehewa yale ambayo yatakarabatiwa haraka na Wizara yangu itahakikisha kwamba wasafiri wa Mpanda nao wanaongezewa mabehewa, hilo ndilo lengo letu. (*Makofii*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo tulioletewa na Wizara hii.

Wizara ilikuwa imependekeza matumizi kwa ajili ya maendeleo ya shilingi bilioni 167 na baki na mchana huu tumeletewa *addendum* inayoonesa kwamba Wizara hii imeongezewa kama shilingi bilioni 95 kwa ajili ya hizi shughuli za maendeleo, katika kuangalia *addendum* yenye we inaelekea kwamba hizi shilingi bilioni 95 zimetolewa kutoka kwenye fungu la miradi maalum ya barabara ambalo liliipigia sana kelele jana la shilingi bilioni mia tatu arobaini na nane zimechotwa bilioni tisini na tano pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nifafanuliwe, kama Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ilishapitishwa mafungu yote yalisshapitishwa, hii bilioni 95 iliyochotwa kutoka fungu la miradi maalum ya barabara na kuletwala kwenye miradi ya maendeleo ya Wizara ya Uchukuzi ambayo ni *Vote tofauti kabisa* zimechotwa kwa idhini ya Kanuni ipi, mimi naomba nipewe angalau msingi wa Kikanuni au wa kisheria wa kuchota fedha ambazo tayari zimeshatengwa na Bunge hili bila kupata *authorization* ya Bunge hili. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni kweli kwamba jana tulioletewa na Makadirio ya Wizara ya Ujenzi, lakini chini ya utaratibu wa sheria za fedha tunaweza kupendekeza **viament** na ni juu ya Bunge kuidhinisha au la. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu alichokisema Mheshimiwa Tundu Lissu kipo ukurasa 276, Kifungu kidogo cha 4168. Hizi ni fedha ambazo zimewekwa katika Kifungu hiki katika Bajeti hii ya ujenzi lakini ni mfuko maalum, hela hizi hazijawa *committed* kama unavyoziona. Ukiangalia miradi yote iliyomo katika kifungu hiki ina barabara tayari. Fedha hizi ziliwekwa maalum kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya miundombinu hasa katika maeneo ambayo ipo miradi kadhaa ambayo tuna uzoefu, imekuwa inachangiwa inatolewa na wafadhili, lakini hii tulifikiri sehemu nydingine miradi hii imekwama kwa sababu sisi tulikuwa hatujajitarisha kuweka *counterpart fund*. Kwa hiyo, hizi fedha zimewekwa hapa kwa ajili hiyo, miradi yote ambayo Serikali ya Tanzania itafanya kutoka kwenye fedha za wafadhili hizi ni fedha ambazo zimewekwa, ni fungu ambalo haliko *committed*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hizi fedha zimechukuliwa hapa zimepelekwa ujenzi kwa maana ya kwamba ni fedha ambazo ziliwekwa kwa ajili ya mfuko wa miundombinu. Zimekuwa *voted* lakini Mheshimiwa Tundu Lissu atakuja kupata ukweli wa mambo haya yote wakati wa *Appropriation Bill*. (*Makofii*)

TAARIFA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwa...

MWENYEKITI: Na iwe taarifa kweli kweli, mimi najua hii...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Waziri aliymaliza kuzungumza...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge ngoja kidogo, kwa sababu sasa hivi hatuna kuongeza muda. Hiki kilichofanyika kinaruhusiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 102, unaweza kuhamisha fungu moja ukapeleka fungu lingine na mwisho tutakuwa na *Appropriation Bill*.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu niendelee kutoa taarifa fupi sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Kwa kifupi sana maana yake nina tatizo la muda. Tuendelee.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 100 na Kanuni ya 102 zinahusu kuhamisha vifungu, hapa tumehamisha kutoka fungu moja kwa maana ya fungu la Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ambalo ni Fungu 98 kwenda Fungu la Bajeti ya Uchukuzi ambalo ni Fungu 62. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tarehe mbili tulishafanya maamuzi, Kanuni za Bunge za 54, 60 na Kanuni ya 64 zinakataza siyo tu kujadili na kupidisha suala ambalo lilihaamuliwa, ukitaka kuliamua tofauti ni lazima iletwe hoja tofauti ya kubadilisha uamuzi jambo ambalo kwenye hoja hii iliyowasilishwa mezani hivi sasa *addendum halijafanyika*.

Kwa hiyo, naomba kutoa taarifa ili utaratibu huu wa Kikanuni uweze kuzingatiwa na Bunge letu liweze kuendeshwa kwa mujibu wa Kanuni. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mwanasheria.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nillelewa kwamba jana Waheshimiwa Wabunge wote toka sehemu zote hizi walifanya *specific reference* kwenye fedha hizi na wakashauri kwamba Serikali ione uwezekano wa kuzihamisha na kuzileta kwenye matumizi haya. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali yenyeewe ahsante. (*Makofii*)

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mwaka 2007 Serikali ilikuja na mpango kabambe kabisa na kuliarifu Bunge kwamba tutakuwa na menejimenti mpya na lengo kubwa lilikuwa ni kulibin afsisha shirika letu la reli na tukaambiya kwamba menejimenti mpya ya *RITES* italiboresha Shirika, italicifanya liwe la kisasa na matokeo yake sasa limekufa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeingia hasara ya shilingi bilioni 63.68 katika kufidia kuvunjwa kwa mkataba huu kati ya *RITES* na *TRC*, je, Serikali inawachukulia hatua gani wale wote waliosababisha tuingie katika Mkataba huu mbovu ili iwe fundisho *next time* tusiingizwe katika mikataba ya aina hii.

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwishesemwa kwamba kwa matatizo ambayo yanajitokeza, sasa itabidi tuunde Kamati ya kuangalia kumetokea nini huko na wale ambao watakuwa wamehusika Serikali itawachukulia hatua zinazostahili, ahsante.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kumuuliza Waziri swali moja. Hivi karibuni tumeshuhudia wafanyakazi wa Shirika la Reli wakiomba kitu kinachoitwa kifuta jasho na kwa kuwa wanamalamako makubwa sana na kwa kuwa katika mazingira ya kawaida katika *ku-run business entity* ye yeyote *human resource, capital* ni muhimu sana kuweza kuthaminiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunasema tunaboresha reli lakini tukiboresha reli bila kuangalia pia maslahi ya hawa watu itakuwa ni kazi bure, naomba kauli ya Serikali inazungumza nini kuhusiana na madai haya, ni kwa nini isifanye kama ilivyofanya kwa waliokuwa wafanyakazi wa *NBC, NMB* pamoja na Mashirika mengine hapa nchini, kwa nini wao wasilipwe? Naomba kauli ya Serikali.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, niseme yale aliyosema Waziri wakati akiwasilisha hotuba yake ya majumuisho. Jithada yetu hapa ni kupata pesa ambazo zitaliweka hili shirika katika hali ya kuweza

kuzalisha kikamilifu, *balance sheet zi-improve*, wale wafanyakazi waweze pia kukopesheka kwa mabenki na kadhalika. Sasa nafikiri kwa kiasi hiki tulichopata mimi nafikiri watuvumilie, tuendeleze hili shirika halafu baadaye hayo tumeyapokea yanazungumzika, nashukuru. (*Makofi*)

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nimemwomba Waziri aangalie kile kitisho kinachotokea karibu na Jimbo la Vunjo upande wa Kenya, pale wanataka kujenga uwanja mkubwa wa kisasa na tunaambiwa ni mkubwa kuliko viwanja vyote vya Afrika Mashariki, Afrika ya Kati na Kusini, ili waweze kuleta ndege kubwa na wanajenga *ma-godown* pale, lengo ni kuteka biashara ya utalii katika Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Arusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nililiza mpango wa kukipanua na kukiendeleza kiwanja cha *KIA* ili huo mpango wa Kenya usije ukaua kiwanja chetu hasa ikizingatiwa Wizara ya Ujenzi tunatengeneza barabara kuanzia Arusha mpaka Holili tena barabara mbili mbili, kwa hiyo, ina maana tunawarahisishia wale watu wa Kenya waweze kuja kwenye mbuga zetu waweze kuleta wasafiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumejiandaaje katika wakati huu wa ushindani ili kiwanja chetu cha *KIA* kisije kikafa au na biashara ya utalii isije ikauawa katika nchi yetu?

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la kaka yangu Dokta Mrema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulipata taarifa hizo kuwa kuna kiwanja kinajengwa karibu na mpaka wetu tukapeleka watu kutafiti wakauliza na wenzetu wa Kenya wakakana wakasema hawana jitihada hizo, lakini inawezekana wakawa wamekana tu lakini wanafanya. Kwa hiyo, kwa taarifa za kiofisi ni kwamba wamesema hawana jitihada hizo. (*Makofi*)

Lakini kuhusu kiwanja chetu cha Kilimanjaro, nilisema tunataka Dar es Salaam iwe kitovu lakini pia tunataka Kilimanjaro iwe kitovu. Sasa baadhi ya mikakati ni kuangalia tutavutia vipi mashirika ya ndege yaje pale Kilimanjaro kama ambavyo yalikuwa yanakuja huku zamani, ikibidi tupunguze *landing fee* tutapunguza, ikibidi tupunguze *parking fee* tutapunguza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Mbowe ana *interest* pale na mimi nina *interest* pale, nimetumia miaka yangu ya ujana pale kujenga karakana, kwa hiyo, kile ni kiwanja ambacho ni lazima kifanyi kazi ambayo imepangiwa. (*Makofi*)

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini pia naishukuru Serikali sikuvi kwa kuongeza fedha ambazo jana katika michango yetu tuliomba ziongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa jana moja ya vitu ambavyo nilizungumzia ni juu ya viwanja vya ndege ikiwemo Njombe Mkoa mpya na Iringa uwanja wa Nduli. Katika majumuisho ya Waziri sijaona akizungumzia kauli ya viwanja hivi viwili Njombe na Iringa. Ni nini sasa baada ya kupata fedha, tunaomba kauli ya Serikali. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, naomba nimjibu swalii Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha tumepata shilingi bilioni 18 zikishapitishwa na Bunge lako Tukufu tutashukuru tutaielekeza *TAA* ivitazame hivi viwanja viwili na siyo viwili tu hivi kwa Mkoa wa Iringa na Mkoa mpya wa Njombe lakini mimi nafanya safari pia kwenda kukagua uwanja wa Masasi pale *Ludewa Air Strip* ili Mheshimiwa Deo Filikunjombe asije akatunyonga. (*Kicheko*)

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Katika mchango wangu jana hapa Bungeni pamoja na masuala mengine nilizungumzia suala la kifuta jasho, pamoja na kwamba Mheshimiwa Moses Machali ameliongelea kwa namna yake,

ningependa kufahamu ni lini malipo haya yatalipwa kwani Waziri ameomba wafanyakazi wawe wavumilivu, kwa kweli walishakuwa wavumilivu kwa muda wa kutosha, ni wakati sasa umefika wanahitaji malipo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kauli ya Serikali ni lini? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angella Kairuki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa sisi tuna nia na azma ya kuwalipa kifuta jasho hawa ndugu zetu lakini itategemea kabisa na uwezo wa kifedha wa Serikali. Lakini mpaka hapo tutakopokuwa tumejua uwezo wetu wa kifedha ukoje ndiyo tunaweza kutoa tamko ni lini tutawalipa na siyo vinginevyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wafanyakazi wa reli waongeze bidii, tufunge mikanda ili shirika tulibadilishe, sasa menejimenti mpya ni ya wazalendo, *RITES* wameondoka tunataka tuwaoneshe kwamba Watanzania tunaweza na mimi ninaamini *TRL* inaweza kabisa. (*Makof*)

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Miiongoni mwa mambo niliyochangia kwa maandishi nilipenda kujua ni lini Serikali itatoa fidia kwa wananchi ambao katika eneo la Kajunguti Wilaya ya Misenyi ambalo lilitambuliwa kwa ajili ya kujenga uwanja wa ndege, lakini kwa zaidi ya miaka mitatu sasa hawajalipwa lakini pia wamezuiliwa kufanya shughuli zozote za kimaendeleo ikiwa ni pamoja na kulima.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Batenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mimi nimetoka wiki jana Bukoba na *TAA* pamoja na Wizara tutaangalia utaratibu wa malipo haya kwa hiyo tunalipokea hilo na kulifanyia kazi, nashukuru. (*Makof*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kuniona. Katika mchango wangu wa kuongea pamoja na wa maandishi, moja ya jambo ambalo nilikuwa nimependekeza ni ule msongamano wa magari Tunduma na maeneo mengine, ni kwa nini sasa kama moja ya chanzo cha Serikali kupata mapato wasianzishe bandari ya nchi kavu pale, sijamsikia Waziri akilizungumzia suala hili, maana yake hili siyo tu kwa maslahi ya watu wa Tunduma na Mbozi Magharibi kwa ujumla itakuwa ni kwa Taifa, kwa hiyo, ningependa kupata maelezo na ufanuzi katika hili.

Hivi sasa kama moja ya chanzo cha Serikali kupata mapato wasianzishe bandari ya nchi kavu pale, sijamsikia Mheshimiwa Waziri akilizungumzia hili maana hii si tu kwa maslahi ya watu wa Tunduma na Mbozi Magharibi kwa ujumla itakuwa ni kwa Taifa kwa hiyo, ningependa maelezo katika hili Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa nataka ufanuzi. (*Makof*)

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa David Silinde kama ufuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miaka mitano ya kutekeleza kwanza llani ya Chama cha Mapinduzi halifu na kazi nyininge. Huu ni mwaka wa kwanza hatuwezi tukajenga bandari kavu za kila mahali ambapo tunaona zinahitajika kwa mwaka huu. Nikijibu hivi ni pamoja na Korogwe kule. Kwa hiyo, hilo tutaliangalia katika mpangilio unaokwenda tutakopoona kuwa kuna tija ya kutosha kufanya hivyo tutajenga. Lakini si kwa mwaka huu ambao tunao sasa hivi. (*Makof*)

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka ufanuzi katika huduma za bandari ukurasa 51 mapato ya *TPA* yameainishwa hapa ni shilingi 219,776,000 lakini sijaona mapato ya *TCTS* wala mgawanyo wa *ICD* sasa nataka

kujuu Waziri hii shilingi 219,779,000 ni pamoja na *TICTS* na mapato ya *ICD* na pia nijue asilimia ngapi mnapata kutoka kwenye *ICD*?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Amina Abdallah Amour kuhusu mapato ya Shirika la Bandari, *TICTS* na *MASS* hizi ni kampuni binafsi kwa hiyo, haziwezi kuonyeshwa kwenye Mapato au Matumizi ya Serikali. Lakini pia kwa ridhaa yako jana aliuliza kuhusu wale wanaomiliki hizi *ICD's*, hizi *ICD's* hawa ni Watanzania lakini wengine wameshirikiana na wageni kwa hiyo, asiwe na wasiwasi Watanzania pia wanafaidika kwenye hizi *ICD's*.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, lakini naomba nichukue nafasi hii kumpungeza Waziri Mkuu kwa kuliona suala hili na kulipa uzito wake, tatu naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na maelezo yake mazuri. Lakini hata hivyo ningependa kupata ufanuzi au maelezo kutoka kwa Waziri ni lini Uwanja wa Sumbawanga Mjini utaanza kujengwa kwa kiwango cha lami pamoja na upanuzi wa kiwanja hicho? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa pongezi za Mheshimiwa Mbunge. Napenda kusema kwamba Uwanja wa Sumbawanga umetengewa fedha za *European Investment Bank* milioni 360. Kwa hiyo, mara fedha zitakapokuwa tayari na wakandarasi wameanza kutathiminiwa ili kazi ile iweze kuanza mara moja. (*Makof*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Waziri na pengine *cabinet* kushindwa kufuata taratibu za kuitisha au kuhamisha mafungu na Mwanasheria Mkuu kushabikia ni kielezo cha wazi kabisa kwamba kuna tatizo la kuchoka. (*Makof*)

Nina suala moja tu, wakati nachangia nilichangia sana kwamba ni muhimu sana mipango hii ya uchukuzi kwa sababu inagusa masuala ya kisayansi na uchumi tuzingatie maoni ya kisayansi na kiuchumi. Kwa mujibu wa mpango wa miaka mitano ambao umesainiwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, eneo la reli, bandari na anga kwa mwaka wa kwanza kwa maana mwaka huu lilipaswa kupata takribani shilingi bilioni 468. Siyo hapo tu, ukisoma ukurasa wa tatu wa maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu uchukuzi eneo la anga, bandari pamoja na reli taarifa waliyopewa na Waziri huyu huyu ilionyesha kwamba zingehitajika shilingi bilioni 492 kuweza kufikia malengo.

Lakini wakati Waziri huyu huyu anafanya majumuisho pengine baada ya Kikao cha CCM kule nje anatuambia kwamba takribani nyongeza ya shilingi bilioni 95 kwenye miradi ya maendeleo kwenye shilingi bilioni 167.9 ambayo jumla inatengeneza shilingi bilioni 262 anasisitiza kwamba inatosha sana na wala hahitaji ziada. Naomba maelezo. (*Makof*)

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunapanga mambo kisayansi, tunapanga mambo kuangalia *opportunity costs*. Suala la *planning* ni suala ambalo linendelea, unakwenda unajipanga unaona kipi ambacho kinawezekana. Hatuwezi hapa kwa sababu kuna vitu tutaweza kuvifanya tukapiga hatua sisi tusisitize tu kuwa lazima tupangiwe fedha fulani wakati fedha zile zinahitajika mahali kwingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardh, Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya zote zinahitaji fedha. Sasa kwetu sisi kikubwa hivi sasa ni kuboresha hizi taasisi zetu zianze kufanya kazi. Hizi fedha tunazosema itafika wakati hapa tuombe Mungu tu labda tukisema Bajeti tutakuta kwenye uchukuzi tuna Bajeti kubwa kuliko ambavyo tungeweza kupanga wenywewe kwa kutumia *PPP* huko ndio tunakotaka kwenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuhalikishia Bunge lako, fedha ambazo Wizara hii zimepangiwa sisi tunaweza kuzifanya kazi tukaanza kupiga hatua. Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipochangia kwa maandishi niliongelea tatizo la vyombo nya bahari na nikasema kwamba vyombo kama meli, boti,

jahazi ambavyo vinafanya safari kutoka Dar es Salaam, Unguja, Pemba, Tanga baadhi ni vibovu vinahatarisha maisha ya abiria. Sasa nilitaka kupewa ufanuzi hapa kwamba je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuvichunguza vyombo hivi yaani kila wakati ili kuona tatizo hili linatatuka ili kuwaondoa wasiwasni abiria ili waweze kusafiri kwa usalama? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar swali lake kuhusu usalama wa vyombo baharini, *SUMATRA* inaendelea kujizatiti ili kukagua hivi vyombo na sisi usalama wa abiria ni suala letu muhimu katika utendaji wetu wa kazi. Kwa hiyo, nimthibitishie tu kwamba tutaendelea kusisitiza kwamba hivi vyombo vikaguliwe na visibebe abiria kuliko kiasi cha uwezo wa vyombo hivi. (*Makofii*)

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka jana Rais Kikwete akiwa Bukoba kule aliahidi kutuletea meli mpya pale Ziwa Victoria kusaidia usafiri wa abiria na mizigo hasa baada ya meli kupinduka. Naomba kupata ufanuzi mipango hiyo imefikia wapi ya kupata meli hiyo mpya Ziwa Victoria? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rais aliahidi na hii ipo katika llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala. Sasa hivi Kampuni ya Denmark inafanya upembuzi yakinifu na ukikamilika tukijua ni meli ya ukubwa gani ya kwenda kwa kasi gani Serikali itaanza utaratibu wa ujenzi wa meli hiyo. Ziwa Tanganyika ni meli moja, Ziwa Victoria meli moja na Ziwa Nyasa meli moja. (*Makofii*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuongezea Bajeti Wizara ya Uchukuzi. Lakini kama nilivyokuwa nimechangia katika mchango wangu wa maandishi kuhusiana na malalamiko na tuhuma inakabiliwa Bandari ya Dar es Salaam katika eneo la kushusha kontena wakati meli zinapotia nanga bandarini. Kumekuwa na malalamiko kwamba baadhi ya meli ambazo zinapaswa kuwahi kushusha makontena zimekuwa zikidaiwa rushwa dola laki moja na kiwango hicho meli nydingi zinashindwa *ku-afford* na mizigo mzima unabaki kwa mfanyakishara ambaye ni mzawa kwa kuendelea kulipa dola 70 kwa kila kontena inayoendelea kubaki kwenye meli. Lakini pia meli nydingi sasa hivi zimehama na kwenda kushusha kontena katika Bandari jirani hivyo kuendelea kukoshesha Serikali yetu mapato. Je, Serikali ina taarifa hii na kama ina taarifa imechukua hatua gani? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ester Bulaya kwanza rushwa ni adui wa haki na kama kuna mtu yule ameombwa rushwa sisi tunaomba taarifa hizo tupeleke kwa vyombo vyaa dola ili waweze kushughulikiwa lakini wiki mbili zilizopita mimi nilitembelea pale Bandari ya Dar es Salaam tumezungumza na wadau wote kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza, tuna *one stop centre*, lakini tunaanzisha pia *port community system* ambayo itahakikisha taasisi zote zinazohusika na kutoa kontena na mizigo pale *TRA*, mabenki yamekubali kuanzisha *facility* pale na tunataka kufanya shughuli hizo saa 24 kwa siku pamoja na mageti. Kwa hiyo, taarifa hizi tutazifanyia kazi na kama lipo suala lote la rushwa vyombo vyaa dola tutavihakikisha vifanye wajibu wake. (*Makofii*)

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana katika mchango wangu wa maandishi niliaishwa juu ya umuhimu wa kuboresha usafiri wa majini katika kata zangu tatu, Kata ya Wampembe, Kata ya Ninde na Kata ya Kala na kwamba katika eneo lote hilo hakuna mahali ambapo ni salama kwa kutua meli. Nikaainisha umuhimu wa kujenga bandari katika Kijiji cha Wampembe ambacho pia ni Makao Makuu ya Tarafa nataka kupata majibu. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo tumeyapokea kwa sababu ni lazima upembuzi unaohusu *hydro graphic survey* kuona kina cha maji pale, watalaam wetu wa *TPA* tumepokea watachukua na kwenda kufanya vipimo hivi na tuone maeneo gani yanafaa kwa ajili ya kujenga hizi bandari. (*Makofii*)

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu niliuliza kwamba katika Bandari yetu ya Dar es Salaam kwa kuelekea Zanzibar kwamba abiria wetu ambao wanasaifiri wanakaguliwa kana kwamba nchi inatawaliwa na mkoloni kwa kufunguliwa zipu mabegi na kupekuliwa ndani ya mabegi, nje na utaratibu ambao upo. Kwa hiyo, nilikuwa nataka maelezo kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alisema wanatumia sayansi katika Wizara yao, basi huu utaratibu uweze kuondolewa katika Bandari yetu ya kuwadhalilisha wasafiri. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Utaondoka lini huo utaratibu wa kuwadhalilisha wasafiri. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ukaguzi wowote wa msafiri kama ni mama anayepaswa kumkagua ni mama kama ni baba akaguliwe na baba. Kama inakwenda kinyume chake hilo ni kosa na totalishughulikia. Lakini napenda tu kumweleza Mheshimiwa Mbunge, tunafanya utaratibu sasa hivi katika bandari yetu hapa kuweka vipimo vyta kisasa ambavyo vitakuwa vinatumia *x-ray* na scanner ili pia tuweze kuepuka na watu ambao labda wanaweza kuingia na vyombo vyta hatari katika boti zetu hizi. Kwa hiyo, atuvumilia tu kidogo lakini namuomba radhi sana kama kuna watu wamedhalilisha kwa utaratibu kama huo na tutaukemea kwa nguvu zote na hatua za kisheria zitachukuliwa. (*Makofii*)

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi maswali yangu ni mawili tu ya pongezi kwanza kuipongeza sana Serikali kwa kuongeza fedha kwenye Wizara hii lakini kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kwa tamko ambalo alilitoa asubuhi kuhusu tatizo lililojitokeza kwenye kampuni ya usafiri ya UDA pale Dar es Salaam. Nampongeza sana kwa hatua alizochukua ili vile vyombo viweze kufanya kazi, isipokuwa jambo dogo tu labda Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa sababu uchunguzi unafanyika wale wahusika wote walijotajwa wako kazini na ile kampuni iliyotajwa na yenyewe imeshaanza kufanya kazi na kukusanya mapato. Wasiwasi wasije wakafanya kitu kibaya. Serikali haioni haja ya kuzuia ile kampuni isifanye kazi na wale waliohusika nao wasimamishwe ili kupitisha uchunguzi? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya TAMISEMI ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa kwa wasiwasi ambao anao Mheshimiwa Iddi Azzan. Kwa hiyo, tutawasiliana na Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika ili kuona kama hiyo haitokei mapema iwezekanavyo. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoelekeza na alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa tunac consider haya yote yanayosemwa hapa kwamba ni *package* moja sasa. Tayari hatua zimeshachukuliwa kuelekeza vile vyombo vinavyohusika kwa maana ya CAG pamoja na TAKUKURU na wale wengine wote wanaohusika, matokeo yale ndio yatakayoonyesha kwamba sasa ni hatua za namna gani zichukuliwe. Maelekezo haya yametekelezwa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema. (*Makofii*)

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba mionganoni mwa sababu zilizopelekeza hapo miaka ya nyuma katika ajali ya Msagali na Igandu watu wengi walifariki kutokana na wingi wa mizigo kwenye treni zetu. Je, Serikali siku ni lini itatatua tatizo la kuchanganya abiria, shehena ya mizigo, mende na panya? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Hiyo umeongeza mchuzi kwa kweli. (*Kicheko*)

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuombe radhi sana Mheshimiwa Sungura kama alipoingia kwenye treni hizo mende walikuwa wakitembea, nafikiri tunachosema sasa hivi tunataka kutoka huko kama kulikuwa na mende basi mende wasiwepo tena, sasa hiyo kazi tunawaachia menejimenti ambayo katika maboresho yao hayo ni mambo ambayo watazidi kuyashughulikia. (*Makofii*)

MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nianze kwa kuipongeza Serikali kwanza kwa kuongeza shilingi bilioni 95 kwenye Bajeti ya Wizara hii. Hii ni *testimony* kwamba Serikali ya CCM kweli ni siku. Mimi la kwangu ni dogo tu kwamba Serikali siku ya CCM inatuambia nini kuhusiana na Uwanja wa Ndege uliojengwa na Kampuni ya *Resolve* wakati kuna uwanja mwagine wa Serikali ambaa upo katika Wilaya ya Nzega? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja kama havitumiwi kwa njia ambazo ni kinyume cha sheria kuwa na viwanja viwili sioni kama ni tatizo. Lakini ninalipokea hili na mimi nitazungumza naye ili anielezee kwa undani halafu sisi tuchukue hatua husika, labda kiwanja kimoja kifungwe kimoja kiwe kinatumika, TAA watafanya hilo. Lakini viwili nafikiri si haba kwa sababu wenyewe mashavu mawili hawaungui uji ndio methali ya kule Nzega. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, bahati mbaya wale wote ambaa waliandikwa waweze kuchangia muda umekwisha tunaingia kwenye *guillotine*. (*Makofii*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 496,386,200
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh. 555,302,500
Kifungu 1004 – <i>Information Education and Comm. Unit</i>	Sh. 277,541,500
Kifungu 1005 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 173,314,100
Kifungu 1006 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 132,005,000
Kifungu 1007 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 112,576,900
Kifungu 1008 – <i>Information and Comm. Tech. Unit</i> ...	Sh. 118,885,200
Kifungu 2005 - <i>Transport Infrastructure Division</i> ...	Sh. 362,355,300
Kifungu 2006 – <i>Transport Services Division</i>	Sh. 65,698,293,300
Kifungu 5002 – <i>Transport Safety and Enviroment Division</i>	Sh. 250,000,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapa juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MPANGO WA MAENDELEO

Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi

Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Sh. 28,004,901,000
Kifungu 2005 – <i>Transport Infrastructure Div</i>	Sh. 220,374,489,000
Kifungu 2006 – <i>Transport Services Division</i>	Sh. 262,978,130,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapa vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake*)

(*Bunge lilirudia*)

TAARIFA

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2011/2012 kifungu kwa kifungu na kupitisha pamoja na mabadiliko hivyo naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2011/2012. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofii*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2011/2012 yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Makadirio ya Wizara ya Uchukuzi yameweza kupidishwa na Bunge lakini pia tunaomba tuwapongeze kwa kazi mtakayokuwa mnafanya. Maana leo ni mwanzo Bunge litakalokuja msipofanya mambo itakuwa mambo mazito. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hicho mllichokifanya leo mjue kwamba yale yote yaliyozungumzwa pale ni fundisho. Kwa hiyo, mchukulie *serious* na mashirika haya ni roho ya nchi hasa. Kwa hiyo, nadhani watendaji wenu ninyi wenye kweli msimamie mtakapofika mwaka mwingine Mungu atupitishie mbali, itakuwa siyo hivi itakuwa zaidi ya hapo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nachukua nafasi hii pia kuwapongeza watendaji wetu wote wajisikie ni nchi yetu maana hakuna mahali pengine pa kukimbilia kwa hiyo, mimi naamini kabisa Waheshimiwa Wabunge kauli zene zote ni maonyo kwa Wizara husika, si kwamba yamekwenda bure, yamekwenda vizuri kabisa. Kwa hiyo, naamini mmesikia na mtatekeleza ipasavyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kwa sababu watu wanawahi kwenye shughuli nyingine nimemuona Waziri sauti ilikuwa haitoshi, mwishoni imetoka. Kwa hiyo, ni dalili kwamba amefurahi. Jamani nawatachia kufuturu kwema. Naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.27 jioni Bunge lillahirisha mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 5 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi)